

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Thelathini na Tisa - Tarehe 5 Agosti, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009

**MHE. AL- SHYMAA JOHN KWEGYIR (K.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2008/2009.

**MHE. MGENI J. KADIKA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Hitaji la Kuzigawa Kata za Kipanga na Tutuo**

**MHE. MGANA I. MSINDAI (K.n.y. MHE. SAID JUMA NKUMBA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa kupitia vikao husika, Kata za Kipanga na Tutuo Wilayani Sikonge ziliombewa ili zigawanywe kutokana na ukubwa wa maeneo ya kata hizo na kwa kuwa ni muda mrefu sasa maombi hayo yako TAMISEMI:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saidi Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Halmashauri zote kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa nchini mwaka mmoja kabla ya kufanyika kwa uchaguzi wa Serikali za Mitaa Februari, 2003 zilielekezwa kuwasilisha TAMISEMI taarifa za idadi za majina ya vitongoji, vijiji mitaa na Kata. Mwisho wa utekelezaji wa agizo hilo lilikuwa ni mwezi Machi, 2004.

Baadhi ya Halmashauri ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge hazikuweza kutumia vema muda huo kuyashughulikia mahitaji yake ya kuanzisha kata upya.

Kwa mujibu wa kumbukumbu za Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ni kweli Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge iliwasilisha maombi ya kuzigawa kata za Kipanga na Tutuo na kuanzisha kata nyingine mbili mpya yaani Kata ya Usunga na Kata ya Ibunda. Taarifa ya maombi hayo iliwasilishwa ofisini kwangu tarehe 20 Desemba, 2004, muda ambao tayari ofisi yangu ilikuwa imekamilisha maandalizi ya upatikanaji wa taarifa muhimu kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao nao ulikuwa umekwishafanyika mwezi Oktoba, 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchaguzi wa mwaka 2009 ofisi yangu inayashughulikia kikamilifu maombi ya Halmashauri mbalimbali nchini yakiwemo ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala na uratibu wa zoezi hili karibu unakamilika. Napenda kutoa wito kwa mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi za Halmashauri za Wilaya na Miji, kwamba katika mchakato mzima wa kuandaa na kutekeleza mapendekezo ya kuanzisha maeneo hayo mapya ni muhimu na lazima kushirikisha wananchi wa maeneo husika kupitia vikao vyao vya kisheria na mamlaka zao ambazo husimamia na kutekeleza maamuzi mbalimbali kwa Maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa nchini kote utakaofanyika mwaka 2009 ofisi yangu inatarajia kuzifahamisha Halmashauri zote

juu ya uamuzi wa Serikali kuhusu maombi ya kuanzisha vijiji, Vitongoji, Mitaa na Kata katika maeneo yao husika.

Namshauri Mheshimiwa Nkumba kuvuta subira ili tuweze kukamilisha zoezi hili kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na hatimaye kufanya maamuzi juu ya maombi hayo.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge Said Nkumba na wananchi wa Kipanga na Tutuo na Sikonge nzima wameridhika na majibu ya Waziri.

(a)Je, Waziri tayari kupokea ahsante kutoka kwao?

(b)Kwa sababu wananchi wa Iramba nao wameomba kugawanya Kata za Mwanga na Irunda na masharti yote aliyoyasema Waziri wametimiza. Je, nao watafikiriwa ili waweze kupata Kata mpya? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa ahsante sana yake lakini naomba nitoe angalizo kwamba ili kuanzisha Kata au vijiji kuna vigezo maalum. Kwa hiyo, kwa Kata moja imetimiza vigezo vinavyotakiwa lakini kwa kata nyingine tumewarudishia kwamba ili waweze kupata Kata inabidi wagawe tena vijiji vingine kwa hiyo, tumewarushia wafanye kazi hiyo haraka ili tuweze kuunganisha katika uchaguzi wa mwaka 2009.

Kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ni kweli wameleta mapendekezo yao mbalimbali ofisini kwetu na yamo katika mapendekezo ya kuanzishwa Kata ya Mwanga pamoja na Irunda. Lakini kwa Halmashauri nyingine zote nchini nitoe wito kwamba tunaomba wafikishe maombi hayo kabla ya mwezi Desemba ili tuweze kuyashughulikia kikamilifu. Baada ya mwezi Desemba haitakuwa rahisi kushughulikia maombi mbalimbali kwa sababu tutakuwa tumeshaingia kwenye mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri huyu mzoefu kwenye sekta hiyo ya *Local Authority* na mimi nilikuwa naomba tu kupata uhakika tatizo la Kata ya Magagula ambayo imekidhi vigezo vyote na taarifa zake zilishapelekwa kwenye Wizara yake kwa muda mrefu pamoja na Kata nyingine za Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Je, taarifa hizo anazo na mgao huo wa Kata ya Magagula utazingatiwa katika awamu hii anayoifanyia kazi sasa hivi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI mbona hata mimi nimeleta? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama alinipa nakala ya ugawaji wa Kata katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Kata ya Magagula ni kati ya Kata ambazo ni kubwa sana katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Kwa hiyo, maombi yake tumeyapokea tumeyafanyia kazi na Kata ya Magagula imo katika mgawanyo.

Na. 338

### **Taarifa ya Kutuma Fedha Mikoani**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa siku za nyuma Serikali ilikuwa na utaratibu wa kuwapa Wabunge taarifa kila ilipotuma fedha mikoani, ili Wabunge wa maeneo husika waweze kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha hizo na kwa kuwa taarifa hizo zilikuwa zikibainisha wazi kiasi cha fedha na aina ya miradi iliyokuwa imekusudiwa jambo lililowarahisishia Wabunge kuafuatilia fedha hizo na matumizi yake.

(a) Je, kwa nini Serikali ilisitisha utaratibu huo mzuri?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kutoziweka fedha hizo wazi kwa Wabunge kunatoa mwanya kwa baadhi ya watendaji wakuu wa idara wasio waadilifu watumie fedha hizo kinyume na malengo yaliyokusudiwa bila kugundulika mapema?

(c) Je, Serikali iko tayari sasa kuzielekeza Wizara zote zianzishe na kuendeleza tena utaratibu huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mbunge wa Jimbo la Kwimba, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuwapatia taarifa za mgao wa fedha Waheshimiwa Wabunge, Viongozi mbalimbali na wananchi mara zinapotumwa kwenye Halmashauri, kwa lengo la kufahamu na kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha hizo hupitia kwa Afisa Masuuli haujasitishwa. Afisa Masuuli anapaswa kuziandikia Halmashauri zake juu ya upatikanaji wa mgao wa fedha na kuzitaka zitangaze upokeaji wa fedha hizo kupitia kwenye vikao vya Madiwani ambamo Waheshimiwa Wabunge ni wajumbe.

Aidha, Halmashauri hutakiwa kuwajulisha wananchi kwa kutoa taarifa kupitia kwenye ubao wao wa matangazo. Na kama kuna Halmashauri hazitoi taarifa, nawaomba watoe taarifa hizo mapema iwezekanavyo.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoieleza kuwa utaratibu haujasitishwa, Serikali inaweka wazi fedha zote kwa Waheshimiwa Wabunge, kulingana na utaratibu uliopo. Ni muhimu kwa Serikali kushirikiana kwa karibu zaidi na Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla, kufanya hivyo kutasaidia kutotoa mwanya wa ubadhirifu na udanganyika wa mali za umma kwa mtumishi wa Serikali.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa utaratibu huu ni mzuri, Wizara na Idara za Serikali zinatakiwa kuzingatia kwa ukamilifu utaratibu wa kutoa taarifa za matumizi ya fedha, kutoa taarifa za fedha ni hatua muhimu ya kuendeleza na kukuza utawala bora pamoja na kuleta uwajibikaji mzuri katika matumizi ya fedha za umma. (*Makofi*)

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri akubali kupokea shukrani zangu kwa Serikali kwa kutoa maelekezo mazuri sana kwa Halmashauri na sehemu zinazohusika kuhakikisha kwamba Wabunge na Madiwani pamoja na wananchi wanapata taarifa hizi muhimu.

(a)Je, Serikali inao utaratibu mahususi wa kufuatilia utekelezaji wa maelekezo hayo mazuri kuhakikisha kwamba Madiwani na Wananchi katika kata zao wanapata hizi taarifa muhimu?

(b)Kabla ya kumalizika mkutano huu je, Serikali itakuwa tayari kutupatia taarifa za fedha hizi zilizotumwa katika mwaka wa fedha uliopita pamoja na fedha zilizotumwa kwa ajili ya matumizi ya ofisi za Waheshimiwa Wabunge katika ofisi zao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napokea shukrani zake kwa dhati kabisa. Pili, Serikali inao utaratibu wa kufuatilia juu ya utoaji wa taarifa hizi na kama mahali au kuna eneo au kuna Halmashauri hazitoi taarifa hizo basi naomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane ili tuweze kuona ni sababu zipi msingi zilizofanya Halmashauri hizo zisitoe taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tutawapatia Waheshimiwa Wabunge, taarifa za matumizi katika mwaka uliopita kwa ile miradi ambayo iliyokwenda katika maeneo yao. (*Makofi*)

Na. 339

### **Malambo ya Maji**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, maeneo mengi ya nchi yetu ni kame na mara nyingi maji yanapokauka wananchi na wanyama huwa wanapata matatizo makubwa sana ya kukosa maji:-

(a)Je, ni malambo mangapi yaliyopo nchini yatajwe kwa kila Mkoa?

(b)Je, ni malambo mangapi huchimbwa kila mwaka na huzingatia vigezo gani hasa?

(c)Kwa kuwa Wilaya ya Nkasi inahitaji malambo angalau matatu; je, Serikali itasaidiaje Wilaya kuchimba malambo ili kupunguza shida na adha ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya malambo na mabwawa yaliyokwishajengwa nchini na Serikali, watu binafsi, mashirika na taasisi mbalimbali, hususan kwa matumizi ya wananchi na mifugo ni 1225. Hata hivyo, ni malambo na mabwawa 825 tu kati ya 1225 ndiyo yanayofanya kazi.

Baadhi ya vikwazo vinavyosababisha malambo na mabwawa 373 kutokufanya kazi ni pamoja na kujaa tope na mchanga kunakosababishwa na uharibifu wa mazingira. Aidha, baadhi ya malambo na mabwawa yalijengwa zamani hata kabla ya Uhuru, hivyo yanahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa orodha na majina ya mabwawa na malambo 1225 anayotaka Mheshimiwa Mbunge ni ndefu sana, nitamwandalia orodha hiyo na kumkabidhi kabla ya Mkutano huu wa 12 wa Bunge haujaahirishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mgawanyo wa malambo na mabwawa katika Mikoa ni kama ifuatavyo:-

Arusha, 143, Dar es Salaam 1, Dodoma 81, Iringa 94, Kagera 16, Kigoma 3, Kilimanjaro 45, Lindi 23, Mara 126, Mbeya 13, Manyara 88, Morogoro 45, Mtwara 20, Mwanza 103, Pwani 97, Rukwa 3, Ruvuma 0, Shinyanga 104, Singida 103, Tabora 85 na Tanga 32.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajenga mabwawa kwa kutumia fedha zake yenyewe na kwa kushirikiana na Washirika mbalimbali kama *TASAF* baada ya maombi kupitishwa na Halmashauri husika.

Vigezo vingine vya kitaalam kama vile hali ya mazingira, upatikanaji wa maji na kuwapo kwa mpango bora wa matumizi ya ardhi vinafuata wakati wa uchunguzi baada ya mradi kuibuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, ujenzi na ukarabati wa mabwawa 11 ulifikia hatua mbalimbali za utekelezaji. Mabwawa saba ya Ugunga (Urambo), Kinyambwiga (Bunda), Moita na Indamuriak (Monduli), Emboret (Simanjiro) Amasatwa (Kiteto) na Katoro (Geita) yamekamilika .

Aidha, ujenzi wa Bwawa la Mugumu (Serengeti) umefikia asilimia 90, Bwawa la Nyambele (Bunda) asilimia 50, Bwawa la Nyashitanda (Misungwi) asilimia 80 na ukarabati wa Bwawa la *New Sola* (Maswa) uko katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2008/2009, Wizara yangu itajenga mabwawa 19 yakiwemo mabwawa mpaya na miradi-viporo ya miaka ya nyuma. Mabwawa manne ya Mugumu (Serengeti), Nyambele (Bunda), *New Sola* (Maswa) na Nyashitanda (Misungwi) yatakamilishwa. Mabwawa 14 mapya yatajengwa katika maeneo ya Iguluba (Iringa Vijijini), Matwiga (Chunya), Sasajila (Chamwino), Masuguru (Bagamoyo), Habiya (Bariadi), Seke Ididi (Kishapu), Nyambori (Rorya), Mwanjoro (Meatu), Wegero (Musoma Vijijini), Ngodin (Longido), Mti mmoja (Monduli), Salama Kati (Bunda), Kantawa (Nkasi) na Loonderkes (Simanjiro).

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na upungufu wa maji kwa matumizi ya watu na mifugo katika Wilaya ya Nkasi, Serikali inaendelea kuchukua hatua.

Kwa mfano, katika mwaka 2007/2008, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ilitenga shilingi 105,629,000/=, kupitia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo (*DADPS*) wa Wilaya ya Nkasi. Kazi inayoendelea hivi sasa ni mchakato wa kumpata mkandarasi wa ujenzi wa Bwawa la Kacheche.

Aidha, Serikali katika mwaka 2008/2009 imetenga tena shilingi 64,960,000/= kupitia *DADPS* kwa ajili ya kujenga lambo katika kijiji cha Ipanda. Katika mwaka wa 2008/2009, Wizara yangu imepanga kujenga Bwawa la Kantawa katika Wilaya ya Nkasi. Kwa taarifa hii, namwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane kufuatilia utekelezaji wa miradi niliyotaja.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huwa ni uungwana ukijibiwa vizuri unapaswa kushukuru.

(a)Je, pamoja na kazi hiyo nzuri inayotegemewa kufanyiwa katika Wilaya ya Nkasi kwa kuchimba hayo malambo na mengine kuyachunguza. Je, Mheshimiwa Waziri atanikubalia kwa ushauri wangu kwamba ni vizuri hawa watalaam watakapokuja washirikiane na watalaam waliopo pale Nkasi kwa sababu baadhi ya maeneo aliyoyataja nafikiri itakuwa ni vigumu sana kuchimba hayo malambo?

(b)Kwa kuwa Mkoa wa Rukwa unayo hayo malambo mawili na Bwawa moja la Milala na maeneo mengi ya Mkoa wa Rukwa kwa kweli ni makame na kuna mifugo mingi ambayo imetoka Shinyanga inapata shida pamoja na wananchi kwa mito kukauka. Je, ili kusaidia wananchi pamoja na mifugo hiyo isije ikahangaika zaidi Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa anapaswa kuweka mpango mahususi wa kuchimba mabwawa katika eneo la Sumbawanga, maeneo ya Kalambo na maeneo ya Kwela? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu wa kawaida kabisa kwa watalaam, kushirikiana na watalaam walioko katika Halmashauri husika.

Naomba nitumie nafasi hii tena kumkumbusha Mheshimiwa Nyami na watalaam wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kwamba watalaam hawa ambao karibu watakuja washirikiane nao na watalaam wa Wilayani ndiyo watakaosaidia kumwonyesha mtalaam atakayekuja kusaidia kutathimini miradi ile na kuisanifu.

Jana, mimi mwenyewe nimeongea na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Nkasi Mama Christina Ndallu na nikamwelekeza hivyo kwamba mtalaam atakapofika basi Wilaya iwe mstari wa mbele kumwonyesha ni miradi ipi ambayo ni ya kipaumbele.

Swali la Sumbawanga nadhani tofauti siyo kubwa wakati tunaeleza katika Hotuba ya Bajeti, tulieleza mipango tuliyonayo kwa ajili ya Wilaya ya Sumbawanga na utaratibu ni huo huo. Naomba watalaam wakifika Sumbawanga kama vipaumbele ni mabwawa basi watalaam hao waonyeshwe.

**NAIBU SPIKA:** Tumetumia muda mwingi sana katika swali hili. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 340

### **Sera ya Maji ya Taifa Vijijini**

**MHE. BENSON M. MPESYA (K.n.y. MHE. YONO S. KEVELA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sera ya Maji ya Taifa inatoa msisitizo uwakilishi wa wanawake kwa kutumia maji kwenye maeneo ya vijijini:-

- (a) Je, Serikali inatekeleza vipi Sera hiyo?
- (b) Je, ni vigezo vipi vinavyoweza kutumika ili wanawake washirikishwe kwenye maamuzi na usimamizi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la msingi la Wizara yangu ni pamoja na kutunga sera, miongozo na ufuatiliaji wa utekelezaji katika sekta ya maji. Baada ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 kupitishwa na Serikali, Wizara iliandaa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Maji unaotoa Mwongozo wa Utekelezaji wa Sera hiyo. Mkakati huo ndio unaotuongoza katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji WSDP, 2006 – 2025.



Sera inatambua kuwa wananchi, kwa kushirikiana na wataalamu katika sekta ya maji wanaelimishwa kuhusu matakwa ya Sera, si tu katika utekelezaji wa miradi bali, vilevile katika kuiendesha miradi ya maji. Kwa sababu hiyo, miongozo imeweka kuhakikisha kwamba:-

(i) Unakuwepo uwakilishi wa jinsia zote katika vyombo vyote vya watumiaji maji, zikiwemo Kamati za Maji Vijijini.

(ii) Asilimia isiyopungua 50 ya wajumbe katika Kamati za Maji Vijijini inakuwa ni wanawake.

(iii) Kupitia *WSDP* kuhamasisha na kutoa mafunzo ili kuwezesha wanawake na wanaume kushiriki kikamilifu katika hatua zote za utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Programu ndogo ya Uboreshaji wa Huduma za Maji Vijijini, ambao unasimamiwa na Halmashauri za Wilaya, ndio umebeba dhima hii ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maji. Serikali inafanya jitihada mbalimbali za uelimishaji wa wananchi zikiwemo zile za usambazaji wa vitabu vya Sera ya Maji (2002), Mkakati wa Taifa wa Kutekeleza Sera ya Maji (2006 -2015) na *WSDP* (2006-2025).

Aidha, Serikali inatumia vyombo vya habari, hasa nyakati za maadhimisho ya Wiki ya Maji, kuwaelimisha wananchi kuhusu majukumu yao. Kwa sasa Serikali imekamilisha vijitabu vya Sera ya Taifa ya Maji, katika lugha nyepesi ya Kiswahili ambavyo vitaeleweka kirahisi zaidi na wananchi. Hii itawasaidia kuelimika kuhusu mchango wao unaotakiwa katika utekelezaji wa miradi ya maji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vigezo kadhaa ambavyo hutumika, kufuatana na Sera ya Taifa ya Maji, kuhakikisha kwamba wanawake wanshirikishwa kikamilifu katika masuala ya maji. Suala muhimu ni nafasi waliyonayo wanawake katika jamii kwa kutambua yafuatayo:-

(i) Mzigo mkubwa walionao wanawake ambao, katika maeneo mengi ya nchi, ndio husumbuka kutembea umbali mrefu kutafuta maji;

(ii) Mzigo mkubwa wa wanawake katika kutunza mazingira ya nyumba; na

(iii) Mzigo mkubwa wa wanawake katika kulinda afya za wanafamilia (kupika, kutafuta maji ya kunywa na kadhalika.)

Nyenzo kubwa ni kujua kusoma na kuandika ili kushiriki kikamilifu katika maamuzi kwa kutumia Sera ya Maji na miongozi mingine. Serikali inaamini kwamba endapo wanawake watashirikishwa kikamilifu, kwa kuwekwa mbele katika maamuzi kuhusu utoaji wa huduma endelevu ya maji safi na salama karibu na wanapoishi, mzigo wanaoubeba katika kushughulikia upatikanaji wa maji utapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Sera ya Maji, Wizara yangu inazingatia pia Sera ya Wanawake na Jinsia ya Mwaka 2000 na Mkakati wa Taifa ya Maendeleo ya Jinsia. Aidha, Wizara inatekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inayoelekeza kuhusu wanawake kama ifuatavyo:- Naomba kunukuu:-

*“120 (a) Kuongeza Ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi kwa lengo la kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2010 kama ilivyokwishaazimiwa na Umoja wa Afrika.*

*120 (d) Kuendelea kupanua na kuongeza nafasi za Viti Maalum katika Chaguzi za mitaa, vijiji, vitongoji, Kamati ya Shule, Kamati ya Maji, Kamati za Zahanati, Kamati mbalimbali za Bunge na za Taifa, Ubunge na Uwakilishi na kadhalika.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya kati ya Bodi 21 za maji, ni asilimia 20 tu ambazo zina wajumbe wanawake mpaka sasa; wanaume ni asilimia 80.

Bila kuathiri Sheria ya Maji Na. 8 ya mwaka 1997, nazishauri Mamlaka zinazopendekeza majina ya wajumbe wa Bodi kwa Waziri Mwenye dhamana ya maji, wakiwemo Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, *Tanzania Chamber ya Commerce (TCCIA)*, na wahusika wengine, wazingatie jinsia katika mapendekezo yao. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa, katika Bodi nyingi hapa nchini takriban Bodi 21 ni asilimia 20 tu ya Wajumbe wake ni Wanawake. Je, Serikali kwa kuliona hilo itachukua hatua gani za dharura za kuhakikisha Bodi hizo angalau zinafikia asilimia 50 ya wajumbe wake ni wanawake ? *(Makofi)*

La pili, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha uwiano huo wa uwakilishi hauathiri katika vyombo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema asilimia ni 20 tu na katika sehemu yangu ya mwisho kabisa ya jibu langu nimewaomba na nimewaasa mamlaka zote zile ambazo zinapeleka mapendekezo yao kuhusu Wajumbe ambayo inawahusu Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya, Wawakilishi mbalimbali wa Tume ya Maji, basi wafanye kwa makusudi kabisa kuhakikisha kwamba wanawake nao wanakuwemo katika uwakilishi huo. Kitakachoweza kufanyika hapa ni kuendelea kuwashawishi ili waweze kuona umuhimu wa jinsia katika Bodi hizi.

## Usambazaji wa Pembejeo za kilimo

**MHE. RAYNALD A. MROPE (K.n.y. MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa suala la pembejeo ni muhimu sana katika kuimarisha kilimo chetu na kwa kuwa bado usambazaji wa mbolea una matatizo kiasi cha kushindwa kuwafikia wakulima wetu kwa wakati:-

- (a) Je, Serikali inalifahamu kwa kiasi gani tatizo hilo na kama inalifahamu vilivyo, inachukua hatua gani kulitatua ili wakulima wapatiwe pembejeo hizo kwa urahisi na kwa wakati?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kujenga viwanda vya pembejeo hapa nchini kama vile vya *sulphur* ili iweze kupatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI) (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA)** alijibu:-

Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchanya, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa pembejeo ni muhimu katika kuimarisha kilimo, kuongeza uzalishaji wa mazao na tija na kuwa usambazaji wa pembejeo hasa mbolea umekuwa na matatizo kiasi cha kutokuwafikia wakulima wetu kwa wakati. (*Makofi*)

Matatizo haya ni pamoja na bei ya pembejeo kuwa juu, kutotekelezwa vizuri kwa Waraka wa Serikali wa usimamizi na usambazaji wa pembejeo zenye ruzuku. Makampuni ya pembejeo kushindwa kufikisha pembejeo kwenye vituo vikuu mapema kama ilivyoainishwa kwenye mikataba.

Uteuzi wa mawakala ambao aidha hawana uwezo wa kusambaza pembejeo au wasio waaminifu. Baadhi ya Mikoa kutokuwa na takwimu sahihi za mahitaji halisi ya pembejeo. Kuwepo kwa bei mbili za mbolea katika soko na kutokuwa na mawakala wa kutosha hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za kupunguza matatizo hayo na kuhakikisha kuwa wakulima wanapatiwa pembejeo kwa urahisi, kwa bei nafuu na kwa wakati, Serikali inatekeleza yafuatayo:-

Kwanza kutoa mwongozo wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku kupitia Waraka wa mkakati wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya pembejeo kwa mikoa, Wilaya na Kata.

Serikali inaandaa mawakala wa pembejeo vijijini kwa kuwapa mafunzo ya kuwawezesha kupata mikopo ili kupitia kwao, pembejeo ziweze kuwafikia wakulima na Serikali inaandaa mfumo utakaotumika kusambaza pembejeo zenye ruzuku kwa kutumia vocha ambapo ruzuku itatolewa moja kwa moja kwa mkulima badala ya kutoa ruzuku kwa makampuni inayoagiza na kusambaza mbolea na mbegu bora.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekwishaona haja ya kujengwa viwanda vya pembejeo za kilimo nchini. Serikali inaendelea kuwahamasisha wawekezaji kujenga viwanda vya mbolea kwa kutumia malighafi zilizoko hapa nchini ili kukidhi ongezeko la matumizi ya mbolea katika kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Hivi sasa kuna kiwanda kilichopo Minjingu Mkoani Arusha kinachozalisha mbolea aina ya Minjingu fosfeti katika mfumo wa chenga chenga na unga na jitihada zinafanywa ili kizalishe mbolea zenye virutubisho zaidi ya fosfeti. Pia Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na kampuni mbalimbali zilizoonyesha nia ya kujenga viwanda vya kuzalisha mbolea aina ya *Urea* kwa kutumia gesi ya asili inayopatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *sulphur* Serikali inaendelea kushawishi wawekezaji katika sekta ya viwanda ili wazalishe pembejeo hiyo hapa nchini. Hata hivyo wakati juhudi hizo zinaendelea na ili kuhakikisha kwamba upatikanaji zaidi wa pembejeo hiyo unaongezeka, Serikali inahamasisha makampuni mengi zaidi ili yaweze kujihusisha na uagizaji na usambazaji wa *sulphur*. Kampuni ya mbolea ya Tanzania *TFC* imeshaonyesha utayari wa kuingiza na kusambaza *sulphur* nchini.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza kwamba kwa kuwa matatizo haya kama alivyoyajibu Mheshimiwa Waziri yalikuwa makubwa sana kiasi kwamba *sulphur* ilichelewa sana kwa wakulima na tulipata mfano kwa pale Tandahimba, wananchi waliandamana wakaweka magogo

**NAIBU SPIKA:** Naomba uulize maswali, usitupe hotuba, tafadhali.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Sawa sawa! Wakaweka magogo barabarani. Je, sasa Serikali inasema nini ikiwa mwaka huu kutakuwa na upungufu mkubwa wa zao hili la korosho itawalipa fidia hawa wananchi waliokosa kupata fedha zao kutokana na kuchelewa kwa hii *sulphur*?

Swali la pili, kwa kuwa pia yeye ni Naibu Waziri wa Fedha na Serikali iliahidi kulipa asilimia 6.5 kwa wakulima kwa kupitia Halmashauri zao. Je, anaweza kuahidi hapa sasa hivi fedha hizi zitatolewa lini ili ziweze kusaidia pembejeo hii ya *sulphur*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI) (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hatutegemei kwamba kutakuwa na ucheleweshaji wa

kufikisha pembejeo ama madawa haya ya *sulphur* kwenye Wilaya za Mkoani Mtwara, Tandahimba, Newala na Mtwara yenyewe.

Kwa hiyo, kutokana na mipango ambayo na mikakati ambayo Serikali tayari imeshaiweka na kwa hiyo hatutegemei kwamba kutakuwa na suala la fidia.

Lakini swali la pili, kuhusu asilimia 6.50 siyo suala la tangazo ni suala la Sheria kwamba kuwe na makato haya na kwamba makato haya 6.50 yaende moja kwa moja kwenye Wilaya ambazo zinauza korosho nje na tayari utaratibu umeshawekwa. Tayari Mamlaka ya Mapato nchini ya kodi yanakusanya mapato haya kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zinalipwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na Mfuko Mkuu unalipa moja kwa moja kwenye Wilaya hizi. Tunajua kwamba zinalipwa. Kwa hiyo, hatutegemei kwamba vile vile malipo haya yatachelewa.

Na. 342

### **Fidia kwa wananchi waliopokea wakimbizi**

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuingia kwa wakimbizi katika Wilaya ya Ngara kulisababisha matatizo mengi makubwa hasa uharibifu wa mazingira na miundombinu.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwapa fidia wananchi wa Wilaya ya Ngara kwa ukarimu waliouonyesha katika mapokezi ya wakimbizi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Feetham Philipo Banyikwa, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ujio wa wakimbizi hapa nchini ulisababisha matatizo mengi na uharibifu mkubwa wa mazingira na miundombinu katika maeneo mbalimbali waliyofikia wakimbizi ikiwemo Wilaya ya Ngara.

Hata hivyo ni vyema ikafahamika kwamba pamoja na matatizo hayo ya uharibifu wa mazingira na miundombinu, Serikali haina mpango wowote wa kuwalipa fidia wananchi ambao maeneo yao yameathiriwa na ujio wa wakimbizi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kuhifadhi wakimbizi ni jukumu linalofanywa na nchi yetu kwa niaba ya Umoja wa Mataifa. Serikali, Taasisi za Umoja wa Mataifa na nchi wahisani kwa kuelewa changamoto zitokanazo na ujio wa wakimbizi hapa nchini, zimekuwa zikifanya jitihada za makusudi kusaidia wananchi wa maeneo

yaliyoathirika katika sekta za Afya, Maji, Miundombinu, Elimu, Mazingira, Elimu ya Ufundi, miradi midogo midogo ya kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi hiyo yote pamoja na misaada mingine ni kielelezo tosha kwamba Serikali, Jumuiya za Kimataifa na Nchi Wahisani zinatambua na kuthamini mchango mkubwa wa wananchi wa maeneo yaliyowapokea wakimbizi hapa nchini ikiwemo Wilaya ya Ngara.

Serikali pia inaendelea kufanya juhudi za kupata wafadhili wa kuanzisha miradi mingine mikubwa ya Maendeleo kwa ajili ya kukabiliana na athari zilizotokana na ujio wa wakimbizi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii, kuwaomba wananchi wote kwa ujumla na wale waliopo katika maeneo yaliyoathirika kwa ujio wa wakimbizi waache tabia ya kuharibu mazingira ya asili na yale yanayorejeshwa kwa kuendelea kukata miti na kuchoma moto, kuharibu vyanzo vya maji na rasilimali zilizopo. Sote tujitahidi kutunza mazingira yetu kwani mazingira ni uhai.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ujio wa wakimbizi uliambatana na ongezeko la ujambazi katika Wilaya ya Ngara na baada ya wakimbizi hao kuondoka Ofisi ya *UNHCR* imepunguziwa majukumu, lakini wanauza magari ambayo hawahitaji kwa mnada.

Je, isingekuwa busara Serikali kuyaomba hayo magari wapewe polisi wa Wilaya ya Ngara ambao wanakabiliwa na matatizo makubwa ya ujambazi? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakika mambo anayoyasema ni kweli na utaratibu upo kwamba *UNHCR* wanafunga Ofisi yao pale. Ningependa kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli pia Serikali msimamo wake si kuchukua magari au kununua magari ambayo yamekwishatumika.

Lakini kwa hali iliyopo pale Ngara tumefanya mazungumzo, tumekwishaanza mazungumzo na Uongozi wa *UNHCR* kuona kama tunaweza wakatusaidia tukapata ili kwa sababu hili ni tatizo ambalo niliwahi kulizungumza na Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, mazungumzo yapo na nitamweleza jinsi yanavyokwenda na kama tutakuwa tumefanikiwa basi tutaweza kupata haya magari.

Na. 343

**Mabasi ya Abiria kuzuiwa kutembea usiku  
Kwa hofu ya majambazi**

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa mabasi ya abiria yanapaswa kutembea kuanzia saa 12.00 asubuhi na kusimamisha safari zao ifikapo saa 1.00 jioni kwa kukwepa uvamizi wa majambazi:-

Je, Serikali kuendelea na mfumo huo haioni kuwa ni sawa na kuwafanya hao majambazi kuwa ndio wenye utawala wa nchi hii kwa nyakati za usiku?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruksa yako naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ilitoa agizo kwamba mabasi yote ya abiria yataanza safari saa 12.00 asubuhi na kusitisha safari zake ifikapo saa 4.00 usiku na sio saa 1.00 usiku kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Aidha, kabla ya agizo hilo mabasi ya abiria yalikuwa yanatembea kwa saa ishirini na nne (mchana na usiku wote).

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za msingi zilizopelekea kuweka muda huo ni baada ya kubaini kwamba ajali nyingi za mabasi zinazotokea usiku zinatokana na uchovu wa madereva, uzembe wa baadhi ya madereva kutofuata sheria za usalama barabarani na kutoa tahadhari, ubovu wa magari na sababu nyingine zinatokana na hali halisi ya barabara zetu kwa wakati ule. Kwa misingi hiyo, inaonekana kwamba muda sahihi wa kusitisha safari iwe saa nne (4) kamili usiku pamoja na kuwaagiza wamiliki wa mabasi hayo wahakikishe mabasi yaendayo safari za masafa marefu yanakuwa na madereva wawili watakaopokezana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo hivi karibuni Serikali imeruhusu mabasi ya abiria kutembea mpaka saa 6.00 usiku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uamzi huo Jeshi la Polisi wakati wote, usiku na mchana limekuwa likidhibiti vitendo vya ukiukaji wa Sheria za usalama barabarani na vitendo vyote vya uhalifu hapa nchini. Usalama wa Raia na mali zao ni jukumu la Serikali. Tahadhari ya Serikali kwa usalama na uhai wa raia wake na mali zao naomba isipewe tafsiri ya kwamba majambazi ndio wenye utawala wa nchi hii wakati wa usiku. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameweka bayana sababu zilizosababisha magari yasitembee usiku, si kuwakimbia majambazi. Je, anaelewa ajali nyingi zinatokana mchana kuliko usiku? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa huo ndio ukweli, ajali nyingi zinatokea mchana kuliko usiku. Kwa mtaji huu Mheshimiwa Waziri si atafungia magari kutotembea mchana? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi. Maana yake swali limeshakuwa na maneno mengi basi inakuwa na maneno mengi. Kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la msingi lilisema kwamba shabaha ya kutosafiri usiku ilikuwa ni kwa sababu ya utawala wa majambazi. Mimi nimesema la hasha hiyo haikuwa sababu na kubwa zaidi ni kwamba wakati ule barabara zilikuwa mbaya na mambo mengine ya usalama wa ajali barabarani yalikuwa bado.

Lakini nafikiri kweli ajali zinatokea mchana, lakini kwa udhibiti ambao tumekuwa nao na tahadhari ambazo tunajaribu kuzichukua nadhani hiyo isimtie sana hofu Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Na. 344

### **Upatikanaji wa jenereta Mbinga**

**MHE. GAUDANCE C. KAYOMBO (K.n.y. MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2007 Serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI iliwaarifu Wabunge wa Wilaya ya Mbinga kuwa imetoa shilingi bilioni 5.0 kwa ajili ya kununua jenereta za umeme na kwa kuwa hadi sasa ni mwaka mmoja umepita bila utekelezaji:-

- (a) Je, ni hatua gani imefikiwa hadi sasa kuhusu upatikanaji wa jenereta hizo?
- (b) Kwa kuwa jenereta inayotumika sasa katika mji wa Mbinga ni ndogo na haikidhi mahitaji. Je, Serikali haioni haja ya kuharakisha upatikanaji wa jenereta hizo ili umeme wa Mbinga uwe wa uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mbunge, Mheshimiwa John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilitoa shilingi bilioni 5.0 kwa ajili ya kununua jenereta za umeme. Aidha, Serikali kupitia Shirika la Umeme *TANESCO* iliingia mkataba na kampuni ya *ZWART TECHNIEK B.V.* ya Ubelgiji tarehe 17 Aprili, 2007 kwa ajili ya usanifu, ununuzi, usafirishaji na ufungaji wa jenereta hizo mjini Mbinga.



Mheshimiwa Naibu Spika, jenereta mbili ziliwasili katika bandari ya Dar es Salaam mwezi Mei, 2008 na kusafirishwa kwenda Mbinga ambapo ziliwasili mjini Mbinga tarehe 19 Juni, 2008. Kazi ya kufunga jenereta mjini Mbinga ilianza tarehe 18 Julai, 2008 na inategemewa kukamilika mwanzoni mwa mwezi Septemba, 2008 yaani mwezi ujao. Jenereta hizi mpya zikikamilika zitakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme MW moja (1) kila moja.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa jenereta ndogo za Halmashauri ya Mbinga pamoja na njia za umeme ulikamilika mwezi Septemba, 2007 na umeme ulianza kuzalishwa rasmi mwezi Septemba, 2007. Jenereta hizi zina uwezo wa kuzalisha umeme wa kWh 250 na kwa sasa zinafanya kazi vizuri ambapo wakazi wa mji wa Mbinga wanapata umeme kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 6 usiku. Ni matumaini ya Serikali kuwa mara baada ya jenereta hizi mpya kukamilika na kuanza kuzalisha umeme, mji wa Mbinga utakuwa unapata umeme kwa muda wote kila siku na hata viwanda vya kahawa vikubwa vitapatiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho la kudumu la kuupatia mji wa Mbinga na viunga vyake umeme wa uhakikisha na ulio bora ni kupitia mradi wa umeme wa Makambako – Songea ambao unahusisha pia kufikisha na kusambaza umeme Wilaya ya Mbinga pamoja na maeneo ya Ludewa, Peramiho na Namtumbo.

**MHE. GAUDANCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza niipongeze Serikali kwa kazi kubwa waliotufanyia kutoka wakati ambapo Mheshimiwa Lowassa alikuwa Waziri Mkuu alifuatilia kwa karibu sana jambo hili. (*Makofi*)

Maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kazi ya usambazaji umeme umekwisha. Taarifa nilizonazo ni kwamba hiyo kazi haijaisha na kithibitisho ni kwamba hata pale ambapo wamefunga zile jenereta mbili hazitaweza kufanya kazi kwa sababu ule usambazaji wa nyaya haujafika kwenye zile mashine zinazofungwa sasa.

Serikali inafanya juhudi gani kuhakikisha kwamba usambazaji wa umeme mji wa Mbinga unafanyika kama ambavyo Naibu Waziri aliyekuwepo Mheshimiwa Membe alivyojibu mwaka 2006 kwamba zimetolewa shilingi milioni 5 kwa ajili ya kazi hiyo?

Swali la pili kwa vile katika Mkoa wa Ruvuma umeme upo katika Makao Makuu ya mji wa Songea na Wilaya sasa ya Mbinga na Tunduru ukiiondoa Namtumbo. Je, Serikali iko tayari sasa kulipeleka lile jenereta dogo la Halmashauri katika mji mdogo wa Maguu ili kiwe kijiji cha kwanza katika Mkoa wa Ruvuma kupata umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya usambazaji umeme Mbinga imeanza mwaka jana. Kwa hiyo, kuna kasma iliyotolewa kwa ajili ya kusambaza umeme pale kwa kuweka maandalizi ya jenereta hizi ambazo tulikuwa tunajua kwamba zingefika mwaka huu wa fedha.

Sasa kazi hiyo imeshaanza na sasa hivi kazi anayosema Mheshimiwa Kaka yangu Mbunge Kayombo ni kazi ambayo ni ya kupeleka umeme kwenye eneo la Lusaka ambapo ndiyo ipo hiyo mitambo.

Taarifa ambazo tunazo ambazo amesema na kwa taarifa ambayo tunayo sisi, ni kwamba *TANESCO* Mbinga wameshaanza kazi ya ujenzi wa njia ya umeme kwa ajili ya kuunganisha kutoka jimboni kwenda eneo la Lusaka ambako ipo mitambo hiyo. Ndiyo tukasema kazi hizo zinajumuisha ujumla wa kazi wa kuunganisha mitambo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili la Kijiji cha Maguhu, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapotoa mitambo kwenda maeneo mengine, tunaangalia mahitaji ya jumla mengi na kuangalia mahitaji ya umeme yanayohitajika pale na upatikanaji na maeneo mengine na masuala ni mengi.

Kwa hiyo, ninachooomba nimwahidi ni kwamba tutalifanyia kazi. Lakini pia azingatie kwamba kama tulivyosema kuna mradi mkubwa wa Makambako-Songea ambao utaleta umeme wa gridi kwenye Mkoa wa Ruvuma ukitokea Makambako kwenda Songea na umeme huu kwa sababu utakuwa ni mwingi utawezekana na utakwenda ukifipitia kwenye vijiji mbalimbali nadhani utakuwa ni suluhisho zaidi kwa maeneo haya ya Maguu na maeneo mengine. (*Makofi*)

Na. 345

### **Huduma za umeme vijijini**

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi wa vijijini ndio wazalishaji wakuu katika kilimo na ufugaji na kwa kuwa mapinduzi ya kilimo yanahitaji miundombinu ya kisasa kama umeme na tekinolojia:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa huduma za umeme zinawafikia walengwa vijijini kwa bei nafuu?

(b) Kwa kuwa *EWURA* ndio chombo kinachodhibiti bei ya nishati ya umeme. Je, kwa upande wa Zanzibar chombo hiki kina mkakati gani wa kuona kuwa hakiathiri uhusiano wa Shirika la Umeme Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba asilimia 75% ya wananchi wa Tanzania wanaishi vijijini, pia ni kweli kwamba kilimo ndiyo mwajiri mkuu wa wananchi.

Hivyo kadri wananchi watakvoweza kujumuisha mbinu za kisasa za uzalishaji ndani ya Sekta ya Kilimo ambayo inamaanisha kuingiza sekta hiyo kwenye mfumo wa uzalishaji wa kutumia mashine kama vile matrekta na mashine za kubangua, kusindika mazao, na kuzingatia matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za mbolea, pembejeo na mbegu bora, pamoja na matumizi ya umeme kwenye viwanda vya mazao ya kilimo, ndivyo tutakavyofungua milango mingi ya kujikomboa kiuchumi kwa kutegemea ubunifu wa miradi na namna ambavyo wananchi watatumia umeme huo kuboresha uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo ya utangulizi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mipango ya kuwafikishia umeme wananchi wanaoishi vijijini kupitia programu mbalimbali zinazogharamiwa na fedha za hapa nchini na zenye kutegemea ushirikiano wa wahisani na wabia wa maendeleo (*Development Partners*) kama MCC kwenye mikoa ya Dodoma, Mwanza, Tanga, Morogoro, Iringa na Mbeya, Benki ya Dunia kwenye maeneo ya (Pwani, Lindi na Dar es Salaam (Temeke). Benki ya Maendeleo ya Afrika kwenye mikoa Mikoa ya Arusha, Shinyanga na Mwanza na *Tanzania Energy Development and Expansion Project (TEDAP)* kwa Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Iringa na Rukwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwafikishia walengwa huduma hii kwa bei nafuu, gharama za huduma za kusambaza umeme zimepanda sana kutokana na kupanda kwa bei za malighafi muhimu kama shaba, transform pamoja na nguzo za umeme. Kutokana na haya *TANESCO* wamelazimika kupandisha bei za huduma za usambazaji umeme.

Hata hivyo Serikali inawasiliana na *TANESCO* na kuwaomba wafikirie njia za kuwapatia wananchi huduma hii kwa njia yenye unafuu ikiwa ni pamoja na kulipa kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha Wakala wa Nishati Vijijini kwa lengo la kuwezesha uwekezaji katika miradi ya aina hiyo kwa kutoa ruzuku kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini. Ruzuku inayotolewa na Mfuko wa Nishati Vijijini inakusudiwa kulipia sehemu ya gharama za mradi ili kuwawezesha wananchi kumudu bei ya umeme utakaosambazwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya majukumu ya *EWURA* ni kudhibiti bei za umeme kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa maslahi ya mteja na mtoaji huduma yanazingatiwa.

Kisheria, *EWURA* majukumu yake yanaishia Tanzania Bara na kwa sababu hiyo utendaji wa *EWURA* hauwezi kuathiri moja kwa moja mahusiano kati ya *TANESCO* na *ZECO*.

Hata hivyo, *TANESCO* na *ZECO* wana mahusiano mapana ya biashara na wote wawili wana dhamana ya kufikisha huduma ya umeme kwa Watanzania kwa viwango na ufanisi unaokubalika. Katika hali hiyo masuala mbalimbali ya kiutendaji yanaweza kuathiri upande mwingine kwa namna isiyo ya moja kwa moja.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa *TANESCO* na *ZECO* wana uhusiano mzuri na mpana na Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara bei za umeme zinalingana na kama hazilingani kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza katika kutathmini bei za umeme lazima tufahamu kwamba umeme wenyewe ile huduma inatokana na gharama na lazima tufahamu kwamba umeme wenyewe ile huduma inatokana na gharama ambayo inaingizwa katika uzalishaji wake.

Sasa kwa maana hiyo hadi pale umeme unapofika kwenye mamlaka ya *ZECO* unakuwa umeingia gharama ambayo ni tofauti na tuseme gharama ambayo inazalishwa umeme unaofika Dar es Salaam au umeme unaofika Morogoro.

Kwa hiyo, kwa maana hiyo gharama za umeme zinavyokwenda kwenye maeneo yote ya nchi kusema kweli yanatofautiana kutokana na vigezo vingi. *EWURA* najua swali lake linapokwenda ni kwamba bei zinafanana.

Kusema kweli bei haziwezi kufanana isipokuwa viwango vya kupanga bei hiyo, palikuwa na mgogoro hapa katikati na viwango vya Zanzibar vilionekana vipande kwa asilimia kubwa zaidi kuliko viwango vya Tanzania Bara.

Lakini *EWURA* walishauri hiyo katika sehemu ya ushauri wao na kazi yao kama *Regulatory Authority* na ulikuwa ni ushauri wa kibiashara.

Hata hivyo, Serikali tumekaa na wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na tumefikia makubaliano kwamba kupanda kule kupanda kwa bei kuzingatia pia mambo mengine ya ziada ambayo yanaathiri maisha ya wananchi wa Zanzibar na uwezo pia wa kumudu ongezeko hilo la bei.

Kwa hiyo, naomba niwaambie kwamba bei hazifanani lakini pia gharama za kuzalisha umeme huo ni kubwa zaidi kwa upande wa Zanzibar kuliko ilivyo kwa Bara. Lakini ongezeko hilo linazingatiwa na sisi wasimamizi wakuu wa Serikali zote mbili.

## **Serikali Kuongeza Watumishi wa Vituo vya Afya**

**MHE. AZIZA S. ALLY K.n.y. MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni nia ya Serikali kuhakikisha kuwa, vituo vya afya na zahanati vinajengwa kwa kila kijiji na Kata ili kusogeza huduma kwa wananchi; na kwa kuwa kuna upungufu wa watumishi kwenye vituo na zahanati hizo:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza waganga na waiguzi sehemu hizo?
- (b) Je, ni lini Serikali itatembelea kilichokuwa chuo cha *MCH* – Kibondo, ili kukifungua rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII (MHE. DR. AISHA O. KIGODA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, kwamba kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi, Serikali ina mpango wa kuwa na zahanati katika kila kijiji na kuwa na Kituo cha Afya kwa kila Kata ili kusogeza huduma za Afya kwa wananchi ili walau wasitembee zaidi ya kilometa tano kutafuta huduma.

Aidha, nakubaliana naye kuwa Serikali inakabiliwa na tatizo la upungufu wa watumishi wa afya katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za Afya vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga kikamilifu kukabiliana na tatizo la upungufu wa watumishi wa Afya kwa vituo vilivyopo na vitakavyoanzishwa kwa kuweka mikakati ifuatayo:-

1. Kubadilisha matumizi ya vyuo sita vilivyokuwa vya mafunzo ya kujiendeleza kwa waganga wasaidizi vijijini, *RMA* na vyuo tisa vya wahudumu wa Mama na Mtoto, *MCHA*, ili kuchukua wanafunzi watarajali ngazi ya cheti. Kwa kufanya hivyo Serikali imeongeza wanafunzi watarajali 885. Hii inafanya ongezeko la wanafunzi kuwa 1,002 ambalo ni ongezeko la 44%.

2. Serikali imepunguza muda wa mafunzo ya uiguzi ngazi ya cheti kuwa miaka miwili badala ya miaka mitatu na Stashahada kuwa miaka mitatu badala ya miaka minne bila kuathiri ubora wa mafunzo yanayotolewa. Hivyo, kuongeza upatikanaji wa wahitimu wengi zaidi kwa muda mfupi.

3. Kufufua vyuo vitano vya Kibondo, Nachingwea, Nzega, Tunduru na Mpanda vilivyofungwa mwaka 1995.

4. Serikali imeongeza Bajeti ya mafunzo yanayoendeshwa kwa njia ya masafa ambapo Kanda nane za mafunzo zitaanza kuendesha mafunzo hayo. Kwa kufanya hivyo idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa itaongezeka kwa kiasi kikubwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007/2008 wataalamu wa Wizara walitembelea chuo cha Kibondo kilichokuwa cha *MCHA* pamoja na vyuo vingine nilivyovitaja katika kipengele cha tatu hapo juu ili kutathmini hali yake kabla ya kuvifungua. Taarifa ya tathmini hiyo inaonyesha kuwa majengo ya chuo cha Kibondo yamechakaa na mifumo ya maji safi na taka pamoja na umeme vimeharibika. Hivyo, chuo kinahitaji ukarabati mkubwa kabla ya kufunguliwa rasmi. Katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 Wizara imetenga fedha kwa ajili ya hatua za awali za ukarabati wa chuo hicho. Baada ya kukamilika kwa ukarabati chuo hicho kitafunguliwa rasmi.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, imeshakuwa ni muda mrefu katika zahanati nyingi ambazo zilijengwa na nyingine ambazo mpaka sasa bado hazijafunguliwa kutokana na tatizo la waganga;

Je, Serikali ina utaratibu gani wa hivi sasa kuwapatia Wabunge wa Majimbo yote idadi ya waganga na wauguzi ambao wanahitajika katika majimbo yao ili iweze kufahamika vizuri idadi ya waganga ambao wanahitajika kabla hawajaondoka hapa Bungeni? (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna mkakati wa kujenga zahanati na vituo vya afya wa muda mrefu. Je, kuna mikakati gani ambayo imeandaliwa mizuri na myepesi ambayo itatekelezeka kwa haraka zaidi? (*Makofi*).

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII (MHE. DR. AISHA O. KIGODA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya uhaba wa wafanyakazi ambao wanapatikana katika majimbo inapatikana katika Halmashauri. Lakini nimeahidi kwamba Wizara ya Afya kwasababu tumefanya sensa ya wafanyakazi wote ambao wapo na ambao wanahitajika. Kwa hiyo, kabla ya Bunge lako Tukufu halijaisha tutatoa hapa kila wilaya, hatuwezi tukatoa kila jimbo, tutatoa kila wilaya ina upungufu wa kiasi gani na mahitajio kiasi gani ili Wabunge, wenyewe watapata sasa kwa wilaya nzima sio kwa kila jimbo kwasababu hatuwezi kujua jimbo na vituo vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, mikakati ambayo tumeifanya kwa haraka ni kwamba ni kweli kabisa kwamba kuna zahanati ambazo zimefunguliwa na nyingine tunaziongezea. Mikakati ya haraka ambayo tunaifanya, tumezungumza kwamba tunaongeza udahili wa wanafunzi, hilo ni

moja. Lakini vilevile Bajeti yetu imeongezeka kuhakikisha kwamba dawa na vitendea kazi vinapatikana katika zahanati ili wananchi waweze kupata dawa hizi katika maeneo ambayo wanaishi pungufu ya kilometa tano kupata hizi huduma.

Lakini vilevile tumesema hapa kwamba tunafanya ukarabati wa vyuo lakini vilevile tumebadilisha matumizi ya vyuo kutoka vyuo vilivyokuwa vya *RMA* na *MCHA* ili kuweza kuhakikisha kwamba tunapata wadhili wengi na wengi watachukua mafunzo haya ya *Clinical Officers* na *Nurses* vilevile watachukua. Kwa hiyo, tutapata wahitimu wa Stashahada na Shahada katika upande huu wa Uuguzi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo kulikuwa na maswali 11 lengo letu lilikuwa kujaribu kama tunayaweza 11, Imeonekana haiwezekani Kwa hiyo, hili swali litaonekana kesho kwenye *Order Paper*. Kwa hiyo, muda wa maswali umekwisha na muda wa maswali 10 ya kawaida umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni. Kwanza ninao wageni asubuhi hii wageni wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, hawa ni Ndugu Yared Mkasanga, Katibu wa *CCM* Kata ya Kimagai na yuko Ndugu Lawrance Makuya, Katibu wa *CCM* tawi la Makutupa. Ahsanteni na karibuni sana. Tuna wageni wa Mheshimiwa Margareth Sitta, Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto. Moja ni kaka yake Ndugu Enock Simwanza, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kata ya Visiga Kibaha. Yuko wapi? Yupo mtoto wake, Benjamin Sitta, yuko wapi? Yupo *Mr. Maurice S. Mwaffisi*, mume wa Katibu Mkuu, yuko wapi? Ahsante, yupo Ndugu Ismail Suleiman, Mkurugenzi wa nafikiri ni *NGO* ya *Watoto Salama Trust*, yuko wapi huyu? Halafu yupo na Ndugu Anastazia Mpeka, Katibu wa *UWT* Morogoro Vijijini, sijui yuko wapi? Na yuko Ndugu Pili Bagwere, Katibu wa Wazazi Morogoro. (*Makofi*)

Halafu Waziri pia ameongozana na maafisa 77 kutoka Wizarani kwake wakiongozwa na Katibu Mkuu, Mariam Mwaffisi, sitawatawataja wote hao wako wengi. Halafu nina wageni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii pamoja na wajumbe wa Kamati hiyo ambao ni walezi wa Baraza la Watoto wa Mkoa wa Dodoma. Hao walezi ni Cosmas Donald, Mwenyekiti, yuko wapi? Yuko Faustina Robogast, Katibu, yuko Prince Antonio, Mshauri. Kwa hiyo hilo ni Walezi wa Baraza la Watoto Mkoa wa Dodoma.

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Ezekiel Maige, Naibu Waziri Maliasili na Utalii. Hawa ni Robert Wilason, Mkurugenzi wa *READ International*, hili shirika lisilo la kiserikali linalojishughulisha na utoaji wa msaada wa vitabu mashuleni. Yuko wapi huyu *Mr. Robert Wilson*? Karibu sana. Halafu nina wageni wa Mheshimiwa Mossy Mussa, hawa ni Ndugu Meshack Abdi Kear, Mkurugenzi wa *TANZAMENT*, yuko Ndugu Kisia Omary Almasi, Mkurugenzi wa *ACROSS AFRIKA INVESTIMENT*, yuko Ndugu Takdir Abdulatif, Mkurugenzi wa *ACROSS AFRICA INVESTIMENT*, nadhani. Halafu yuko Ndugu Hilary Ngowi, Mkurugenzi wa *NEBETA MINING*.

Pamoja na hao wageni wa Mheshimiwa Mossy Mussa, anao wageni ambao ni wawekezaji wa viwanda vikubwa kutoka China. Hapa ndio mutapata matatizo majina ya

Kichina hapa, yuko Ndugu Wang Zhen Fang, bila shaka sikutaja maana hajijui. Ndugu Auquer Qiang James, halafu yuko Ndugu Daniel Kibona, yuko na mpwa wake Mossy ambaye anasoma *China University, Computer Science*, yuko wapi mpwa wake? Aah, ndio nawafahamu hawa wageni, Kwa hiyo, hawa ni wageni wawekezaji ambao Mheshimiwa Mossy amekuwa anajishughulisha sana kuwatafuta na ninasema matarajio ya mwanzo wanatafuta kujenga kiwanda cha kopa pale Chalinze na mambo mengine kama hayo. Nadhani mnaweza kuongea naye huko nje mkimpata. (*Makofi/Kicheko*).

Halafu tuna wageni kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, ambao wamekuja kutembelea Bunge kwa ziara ya mafunzo. Ni vizuri wakaja wenzetu kuliko wanatoka mabunge mengine wale wa Baraza la Wawakilishi hawajaja. Yuko Ndugu Saleh Ally Salim, yeye yuko katika utawala Pemba na Unguja, yuko Ndugu Moza Abdulla Jabir, Sekretari wa Katibu wa Baraza, Yuko Ndugu Hamida Ibuni Saleh, *Hansard Reporter*, yuko Ndugu Khamis Khamis Juma, Mpambe wa Baraza, *Sergeant at Arms*, yuko Ndugu Hindu Muhammed Abdulrahman, mwangalizi wa bustani, yuko Khamis Iddi Khamis, yeye ni dereva. Tunawakaribisha sana huu ni utaratibu ambao huwa unafanyika na Bunge letu kukaribisha mabunge mengine hapa na sisi tunakwenda kwa wenzetu. Kwa hiyo, tunawakaribisha sana na tunamshukuru Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar kwa kuwaruhusu kuja huku. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, ambao ni wajasiriamali waliokuja kutoka Fuoni, Zanzibar, kwa ajili ya maonesho ya nane nane. Hawa ni Mheshimiwa Asha Maulid, asimame. Mheshimiwa Mwanaharusi Mwinchum, yuko Mheshimiwa Mafunda Kombo na Mheshimiwa Fatuma Kombo. Karibuni sana nadhani mmefanya jambo zuri kujifunza mambo ya watu wengine.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma. Hawa ni Viongozi wa CCM Kata ya Chamwino, wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani wa Kata hiyo, Jumanne Ngede. Karibuni sana wenyeji wetu. (*Makofi*).

Waheshimiwa Wabunge, tunazo shughuli za kazi. Kwanza kabisa kuna tangazo la Kikao, linasema kwa niaba ya Alhaji Mohamed Misanga, Mbunge Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Miundombinu, sijui ni kwanini kwa niaba? *Okay*, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge, wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe tano kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo saa 7.00 mchana katika Ukumbi Namba 432, ghorofa ya nne jengo la Utawala.

Halafu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo saa 5.30 asubuhi katika Ukumbi Namba 231, ghorofa ya pili jengo la Utawala.

Baada ya matangazo hayo, Katibu endelea na *Order Paper*.

## **MAELEZO BINAFSI YA WABUNGE**



**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maelezo binafsi ya Mbunge Kkuhusu Ujumbe wa Bunge, ulioliwakilisha Bunge kwenye mazishi ya Mheshimiwa Marehemu Chacha Zakayo Wangwe. Maelezo haya nayatoa chini ya Kanuni ya 50 (1) na (2).

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa baada ya kifo cha aliyekuwa Mbunge, wa Tarime, Marehemu Chacha Wangwe, tarehe 29 Julai, 2008 na kwa mujibu wa Kanuni ya 149 ya Kanuni za Bunge inayoelekeza mambo ya kufanywa na Bunge hili anapofariki Mbunge wakati Bunge likiwa katika shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lilituwa ujumbe wa Wabunge 20, kwenda Wilayani Tarime Mkoani Mara, kushiriki kwenye mazishi ya Mpendwa wetu, Marehemu Chacha Zakayo Wangwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi William Hezekiah Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, niliteuliwa na Mheshimiwa Spika, kuwa kiongozi wa ujumbe huo wa Bunge, na Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, aliiwakilisha serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwataje wajumbe wengine wa msafara huo ambao ni hawa wafuatao. Mheshimiwa James Wanyancha, Mbunge na pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Nimrodi Mkono, Mheshimiwa Hassan Rajabu, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa *Professor* Philemon Sarungi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge na Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Mheshimiwa *Engineer* Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa *Dr.* Wilbroad Slaa, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Rosemery Kirigini, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Gaudensia Kabaka, Mbunge na Naibu Waziri, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Janeth Masaburi, Mheshimiwa Eliatta Switi, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa *Dr.* James Nsekela, Mbunge na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe wetu uliondoka Dodoma tarehe 31 Julai, 2008 kwa kutumia ndege ndogo mbili zilizokodishwa na Ofisi ya Bunge, kwa madhumuni hayo. Safari ilianza saa 2.30 asubuhi na kuwasili katika Uwanja wa ndege wa Musoma saa 5.00 asubuhi.

Ujumbe ulipokelewa mkoani Mara na Kanali Machibya ambaye ni Mkuu wa Mkoa huo akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wa Serikali pamoja na vyama vya siasa. Msafara wa ujumbe wetu uliondoka mjini Musoma saa 6.00 mchana kwa kutumia magari ya serikali na kuwasili Wilayani Tarime katika kijiji cha Kemakorere, nyumbani kwa Marehemu mnamo saa 7.20 mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe ulipofika eneo la shughuli za mazishi ulibaini mara moja kwamba mambo sio shwari. Walionekana vijana wengi wakiranda randa, wakiwa na mabango yaliyoandikwa maneno yaliyoonesha kwamba kuna mtafaruku,

Kwa mfano bango moja liliandikwa tuko tayari kwenda jela. Tulipodadisi kuna nini, tulielezwa na viongozi wa Wilaya ya Tarime wa Serikali na Ndugu wa Marehemu kwamba mazishi yasingefanyika siku hiyo ya tarehe 31 Julai, 2008 kwa sababu Ndugu hao walikuwa na wasiwasi na ajali hiyo ya gari inayoelezwa kuwa ndiyo iliyosababisha kifo cha ndugu yao. Kwa hiyo walitaka ufanyike uchunguzi mwingine wa kujitegemea kwa kiingereza, *Independent Autopsy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata maelezo ya azma ya wafiwa ya kutaka uchunguzi mwingine ufanyike tulijadiliana nao tukiwa na Mkuu wa Mkoa wa mara na kuafikiana kwamba kwa kuwa, Bunge, lilikwisha kutoa heshima za mwisho hapa Dodoma, na ujumbe uliotumwa ulikuwa na kazi ya kusoma risala ya Mheshimiwa Spika, kukabidhi mchango wa rambirambi na kushiriki katika mazishi, basi zifanyike kazi za kusoma risala na kukabidhi mchango wa rambirambi wa 5,000,000/= na ujumbe wa Bunge uondoke kwa kuwa tarehe 31 Julai, 2008 mazishi yasingefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutekeleza maafikiano yaliyofikiwa mnamo saa 8:30 hali ilibadilika na mtafaruku mkubwa kutokea na maneno mazito mazito kutamkwa. Mfano, tutamchagua mwingine mukamuue, vivyo hivyo utulivu ulikosekana kabisa na juhudi za kuwatuliza vijana wengi waliovamia eneo la kufanyia shughuli ya mazishi hazikufanikiwa. Katika hali tuliyoiona hatukuweza kufanya jambo lolote zaidi ya kuamua kuwa ujumbe ulitumwa kuliwakilisha Bunge hili Tukufu, uondoke eneo la shughuli za mazishi na kupanda magari na kuelekea mjini Musoma na hatimaye kupanda ndege ambazo zilikuwa zinatusubiri kwenye uwanja wa ndege ili kurejea Dodoma. Na tuliondoka uwanja wa ndege saa 10.10 jioni na ujumbe uliwasili uwanja wa ndege wa Dodoma saa 12:20 jioni salama salimini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha maelezo haya humu Bungeni, tulipata taarifa za uhakika kutoka kwa viongozi wa Serikali wa Mkoa wa Mara na Wilaya ya Tarime kuwa uchunguzi wa pili ulifanyika tarehe 1 Agosti, 2008 na matokeo yake kuafikiwa na Ndugu wa Marehemu na baadaye Marehemu kuzikwa. Tunazidi kumwomba Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya Marehemu, mpendwa wetu, Marehemu Chacha Zakayo Wangwe, mahali Pema Peponi, amina. Kwa kuwa mazishi yalikwishafanyika lakini risala ambayo ilisomwa na Mheshimiwa Spika, hapa Dodoma haijawafikia wafiwa, ikiwa ni pamoja na mchango wa rambirambi wa ofisi ya Bunge na Wabunge, utaratibu mwingine unaandaliwa wa kuwasilisha mchango huo kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Chacha Wangwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wabunge wenzangu waliotumwa kuliwakilisha Bunge kwenye mazishi ya Mheshimiwa Wangwe, tunapenda kukushukuru wewe binafsi na Bunge zima kwa kutupa heshima hii kubwa ya kuliwakilisha. Jukumu tulilopewa lilikuwa zito, nyeti na lenye utata mkubwa au kwa lugha ya kingereza jina lake lingekuwa ni "*Mission Impossible*."

Mwisho kwa niaba ya Wajumbe wenzangu, napenda kuushukuru kwa dhahti uongozi wa Serikali Mkoani Mara, chini ya uongozi wa Kanali Machibya, kwa

ushirikiano waliotupatia tangu kufika uwanja wa ndege Musoma hadi nyumbani kwa Marehemu, katika kijiji cha Kemakorere na kurejea hapa Dodoma salama. (*Makofi*)

Kwa upande wangu napenda kuwashukuru wajumbe wenzangu kwa ushirikiano, uadilifu na utulivu waliouonyesha kwa siku nzima ya tarehe 31 Julai, 2008 tulipokuwa tunatekeleza jukumu tulilopewa. Aidha namshukuru Mheshimiwa Spika, Samuel Sitta, kwa maandalizi yote yakiwemo yale ya kuviwezesha vyombo vya habari, hasa *Tanzania Broadcasting Corporation, TBC*, kushiriki shughuli za mazishi ya mpendwa wetu Marehemu Chacha Wangwe, ambayo ilionesha shughuli za mazishi hayo, hai, au *live* kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa taarifa hiyo. Kama alivyosema utaratibu utafanywa wa kuweza kupeleka rambirambi zetu kwa familia ya marehemu. Katibu shuguli inayoendelea.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi yz Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai hadi siku ya leo na pia kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, na baada ya kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kuanza kwa masikitiko kutoa pole nyingi kwa familia, ndugu, jamaa, Waheshimiwa Wabunge, wananchi wa Tarime na wanachi wote wa Tanzania kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe. Aidha, natoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Salome Joseph Mbatia, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, aliyefariki dunia mwisho wa mwaka jana. Mchango wake katika Wizara utakumbukwa daima. Nitumie nafasi hii pia kutoa rambirambi kwa familia ya Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto. Natoa pole nyingi kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamefiwa na wapendwa wao hivi karibuni. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia Bunge lako tukufu, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteuliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika.

Aidha nampongeza pia kwa kuwa mwenyeji na kuwezesha kwa ufanisi mkubwa Mkutano wa Nane (8) wa *Leon H. Sullivan*, uliofanyika mjini Arusha hivi karibuni. Matukio hayo yameendelea kuchangia katika kufanya Tanzania itambulike na kuheshimika na mataifa mengine duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.) kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawapongeza Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira (Mb.) Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika; Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani (Mb.) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa (Mb.) Waziri wa Miundombinu; Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla (Mb.) Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa Dr. Lucy Sawere Nkya (Mb.) Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje (Mb.) Naibu Waziri wa Miundombinu; Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga (Mb.) Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana na Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri (Mb.) Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuongoza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naahidi kufanya kazi hii kwa bidii katika kufanikisha malengo ya Wizara.

Aidha, nawashukuru wafanyakazi wa Tanzania ambao bila wao nisingekuwa katika nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Spika kwa kuonyesha uhodari katika kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge kwa ufanisi. Aidha, nakupongeza wewe mwenyewe na Waheshimiwa Wenyeviti, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb), Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb) na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid (Mb) kwa kusaidia kuliongoza Bunge letu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo imekuwa dira ya mjadala wetu hapa Bungeni. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mustafa Haid Mkulo (Mb.), Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba yake iliyofafanua mwelekeo wa uchumi wa nchi yetu na bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kwa namna ya pekee kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, (Mb.) na Makamu wake Mheshimiwa Haroub Said Masoud (Mb.) kwa kuchambua na kuijadili bajeti ya Wizara yangu. Ushauri na maelekezo ya Kamati hiyo yameiwezesha Wizara kukamilisha bajeti yake katika muda muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mbunge wa Kiteto Mhe. Benedict Ngalama Ole-Nangoro, kwa kuchaguliwa kwake kwa kishindo. Pia nawapongeza Mheshimiwa Getrude Lwakatare (Mb.), Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma (Mb.) na mwanafunzi wangu mpendwa Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo, napenda kuchukua nafasi hii kufanya mapitio ya utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara yangu kwa mwaka 2007/2008 na makadirio ya bajeti kwa mwaka 2008/2009, kwanza kwa kutaja majukumu ya Wizara kama yalivyoelezwa katika ukurasa wa tano wa kitabu cha bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Wizara. Yafuatayo ni majukumu ya Wizara yangu:-

- Kuandaa Sera za Wizara, kuzisimamia, kuziratibu na kutathmini utekelezaji wake;
- Kueneza na kuendeleza dhana ya Maendeleo ya Jamii kwa kuwashirikisha wananchi wote;
- Kutayarisha mikakati na mifumo ya utekelezaji ili kuchochea maendeleo ya jamii;
- Kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili waweze kushiriki katika ngazi zote za utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo na kufaidika sawa katika maendeleo hayo;
- Kuendeleza, kuhamasisha na kuwezesha jamii kuwapatia watoto haki ya kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kutobaguliwa na kushiriki katika maendeleo ya Taifa;
- Kuratibu shughuli za mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na kuyawezesha kufanya kazi kwa uwazi na ufanisi zaidi;

- Kusimamia utendaji kazi Wizarani kwa misingi ya uadilifu, haki na utawala bora; na

- Kusimamia utoaji wa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na mafunzo ya maarifa, ujuzi na stadi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (MTC).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia na kutekeleza majukumu yake Wizara inaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2005 pamoja na Sera za Wizara ambazo ni:

- Sera ya Maendeleo ya Jamii 1996;
- Sera ya Maendeleo ya Mtoto 1996 – 2008;
- Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia 2000; na
- Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mpango na Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika kipindi cha 2007/2008 utekelezaji wa majukumu ulifanyika kupitia Idara na Vitengo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Maendeleo ya Jamii. Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wanazo stadi maalumu za uraghibishi na uhamasishaji wa jamii ili ziweze kuwa tayari kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kujiletea maendeleo. Licha ya umuhimu wa wataalamu hao bado kuna upungufu mkubwa katika ngazi ya Kata ambako wanahitajika sana. Ni asilimia 39 tu ya Kata zote nchini zenye wataalamu hao. Katika kukabiliana na upungufu huo, Wizara yangu kati ya 2006/2007 na 2008 imetoa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii kwa jumla ya wanachuo 1,498 wakiwemo Wanachuo 721 wa ngazi ya Stashahada ya Juu wakiwemo wanawake 494 na wanaume 227 na kwa wanachuo 777 wakiwemo wanawake 591 na wanaume 186 katika ngazi ya Cheti. (Jedwali Na.1(a) na(b)) la kitabu cha hotuba.

Aidha, Wizara imeongeza idadi ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kutoka vinne hadi tisa. Vyuo vitano vilivyooongezwa ni vilivyokuwa vyuo vya Mafunzo ya Maendeleo Vijijini yaani Mlale mkoa wa Ruvuma, Mabughai mkoa wa Tanga, Ruaha Mkoa wa Iringa, Uyole mkoa wa Mbeya na Monduli. Ukitoa Chuo cha Monduli mkoa wa Arusha kitakachojumuishwa na Vyuo vya Buhare Mkoa wa Mara, Missungwi Mkoa wa Mwanza na Rungemba Mkoa wa Iringa katika kutoa mafunzo ya ngazi ya Stashahada. Vilivyobaki vitatoa mafunzo katika ngazi ya cheti cha msingi na cheti. Aidha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru katika Mkoa wa Arusha kwa ajili ya mafunzo katika ngazi ya shahada ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendesha mafunzo ya rejea kwa wataalam wa Maendeleo ya Jamii na Mafundi Sanifu wa Maendeleo ya Jamii 147. Mafunzo hayo yalihusu mbinu bora za uhamasishaji, ushawishi, uandishi wa miradi shirikishi, ujasiriamali na matumizi ya teknolojia sahihi. Aidha, Wizara imeendelea kutoa kipaumbele cha kuwaendeleza kitaaluma wataalam wa maendeleo ya jamii wenye sifa ya cheti kwa kuwatengea asilimia 60 ya nafasi kwa wanaojiunga na mafunzo ya stahhada ya juu inayotolewa katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuvo vya Maendeleo ya Wananchi ni muhimu sana katika kukuza ajira nchini. Hadi Juni, 2008 jumla ya wananchi 31,493 wakiwemo wanawake 13,571 na wanaume 17,922 walipata mafunzo ya stadi za kazi ya muda mrefu na ya muda mfupi kupitia Vyuvo vyetu, kama inavyooneshwa katika Jedwali Na.2 la kitabu cha hotuba. Mafunzo ya muda mrefu yalihusu utoaji wa maarifa na stadi hususan, useremala, uashi, udereva, umekanika, umeme wa majumbani, kilimo, mifugo na somo la uraia. Mafunzo ya muda mfupi yalihusu utatuzi wa matatizo yanayokabili jamii katika mazingira yao mfano unasihi kuhusu maambukizi ya virusi vya UKIMWI, ujasiriamali, hifadhi ya mazingira, lishe na malezi ya mtoto, haki za mtoto na stadi za maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta ufanisi wa utendaji kazi katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Wizara yangu iliendesha Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida tarehe 17 hadi 21 Septemba, 2007. Washiriki 275 waliohudhuria walipitisha maazimio yaliyolenga kuimarisha utendaji wao na uboreshaji wa mazingira yao ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora inapatikana katika mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia. Katika kuhakikisha hili, jumla ya watumishi 52, wakiwemo wanaume 32 na wanawake 20 wa Vyuvo vya Maendeleo ya Wananchi wamepata mafunzo ya unasihi, falsafa ya Vyuvo vya Maendeleo ya Wananchi na utafiti shirikishi wa mahitaji ya mafunzo vyaoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika mwaka 2007/2008 imejenga na kukarabati majengo na miundombinu katika vyuo 28 kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 3 la kitabu cha hotuba. Aidha, Wizara imewezesha upimaji wa maeneo ya Vyuvo vya Bariadi, Chisalu, Handeni na Njombe ili kudhibiti uvamizi wa maeneo ya Vyuvo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu uliowekwa na Serikali ya Awamu ya Nne katika hifadhi ya mazingira, katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu, kupitia Vyuvo inavyovisimamia, imeendelea kuhamasisha jamii inayozunguka Vyuvo hivyo kuhusu matumizi bora na endelevu ya mazingira, kutayarisha vitalu na kupanda

miti ya mbao, matunda na kivuli kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 4 la kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Maendeleo ya Jinsia. Ili kuhakikisha kuwepo kwa usawa wa kijinsia na upatikanaji wa fursa sawa kwa wote, uingizwaji wa masuala ya jinsia katika Sera, Mikakati na Mipango mbali mbali ya maendeleo ni muhimu. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara yangu ikishirikiana na wadau imewapatia mafunzo waratibu 78 wa dawati la jinsia katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali. (Jedwali Na. 5) la kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, na kuendeleza Ulingo wa Beijing kuhusu uwezeshaji wa wanawake kumekuwepo na jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (WDF) katika ngazi ya Halmashauri. Jumla ya Halmashauri 23 zilikopesha fedha kiasi cha shilingi 152 milioni kwa ajili ya vikundi vya wanawake wajasiriamali (Jedwali Na.6) la kitabu cha hotuba. Vile vile, wanawake 190 walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali na walihamasishwa kuunda na kujiunga na Vyama vya Akiba na Mikopo kama njia mojawapo ya kujipatia mikopo yenye masharti nafuu (Jedwali Na.7) la kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu iliendelea na mchakato wa kuwezesha uanzishwaji wa Benki ya Wanawake. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imeahidi kutoa kiasi cha shilingi bilioni mbili na milioni mia moja (2.1 bilioni) ili kuwezesha upatikanaji wa leseni itakayoiwezesha kuanza kuuza hisa zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwezesha upatikanaji wa Haki za Binadamu kwa kuzingatia uwiano wa kijinsia, ni dhahiri kwamba wanawake na wanaume wanayo haki sawa mbele ya sheria. Katika kuhakikisha hili, Wizara yangu iliendesha warsha ya wadau 73 ambao ni Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka kwenye Sekretarieti za Mikoja na Halmashauri, *NGOs*, Asasi za Kiraia (*CSOs*), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Kurekebisha Sheria ili kuibua vipengele vya sheria vinavyohitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ukatili dhidi ya wanawake na watoto limekithiri hapa nchini likihusisha mauaji, ubakaji, vipigo, kuumizwa na mengine mengi. Katika kutokomeza vitendo hivyo katika jamii yetu, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau iliandaa uzinduzi wa kampeni ya kitaifa kuhusu utokomezaji wa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Kampeni hiyo ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 24 Mei 2008 ikibeba ujumbe usemao “Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto”. Aidha, Wizara yangu imekuwa ikitoa mafunzo juu ya utokomezaji wa vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto. Mafunzo hayo yalitolewa kwa Maafisa wa Serikali wanaosimamia utekelezaji wa sheria wakiwemo Polisi 29 na Askari Magereza 29 (Jedwali Na.8) la kitabu cha hotuba. Vile vile, Mafunzo yalitolewa kwa wanawake 200 toka Mikoja ya Pwani, Lindi, Mtwara,



Tanga na Dar es Salaam kuhusu uelewa wa haki zao na masuala ya jinsia (Jedwali Na. 9) la kitabu cha hotuba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005; Ibara ya 120 (a) kuhusu kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi na maamuzi ifikapo 2010, Wizara yangu imeandaa mkakati wa kuwezesha utekelezaji wa azma hiyo. Mkakati huu utawasilishwa katika vikao mbalimbali vya maamuzi. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuzidi kuongeza nafasi za ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 10 la kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa nchi yetu katika Mikutano ya Kimataifa na Kikanda ni muhimu kwa ajili ya kupeana taarifa, kubadilishana uzoefu, kupitisha maazimio na kuweka mikakati ya utekelezaji. Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu imeshiriki mikutano hiyo ukiwemo wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa kuhusu Hali ya Wanawake (*Commission on the Status of Women - CSW*) huko New York Marekani uliohusu Mgawanyo wa Rasilimali Fedha Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake: Msingi wa Maendeleo. Mikutano ya Kikanda ya SADC iliyofanyika mwezi Aprili 2008 Mauritius na Mei 2008 Namibia ilihusu Umaskini na Maendeleo na Itifaki ya Jinsia katika Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kama kawaida yaliadhimishwa kimkoa tarehe 8 Machi, 2008. Kaulimbiu ya Mwaka huu 2008 ilikuwa Mgawanyo wa Rasilimali Fedha Kijinsia: Msingi wa Maendeleo. Ujumbe huu ulikuwa ukiikumbusha jamii yetu kutenga rasilimali za kutosha ili kuleta uwiano wa Maendeleo Kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Maendeleo ya Mtoto. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliandaa na kuwa mwenyeji wa mkutano wa Mawaziri wanaoshughulikia Masuala ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Watoto Kanda ya Kusini na Mashariki mwa Afrika uliofanyika Arusha mwezi Februari, 2008. Mkutano huo ulijadili utekelezaji wa Ripoti ya Dunia ya Elimu kwa Wote (*Education for All Global Monitoring Report*) ya mwaka 2007, na kutoa maazimio yanayohusu maendeleo ya awali ya watoto. Aidha, Wizara tatu husika zinapaswa kwa pamoja kuandaa Sera na Programu za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu imeendelea kuelimisha jamii kuhusu mila zenye madhara kwa wanawake na watoto. Wizara yangu kwa kushirikiana na muungano wa taasisi zinazojihusisha na kupambana na madhara ya ukeketaji wa wanawake hapa nchini, iliendesha semina kwa Waheshimiwa Wabunge 25 kutoka mikoa 14 yenye mila ya ukeketaji kwa lengo la kuweka mikakati ya kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika mwaka 2007/2008 imeendesha mafunzo ya Haki za Mtoto kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii 41 ngazi ya Halmashauri

katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuwawezesha Maafisa hao kufikisha elimu hiyo kwa familia na jamii wanazozihudumia. Aidha, Wizara yangu imetoa mafunzo na kusambaza zana za ushirikishwaji wa watoto (*child participatory kit*) kuhusu mbinu shirikishi kwa Maafisa Elimu, Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii kutoka Wilaya za Hai, Magu, Temeke, Bagamoyo, Makete na Mtwara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 Mei 2008, Wizara yangu iliratibu maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani. Kaulimbu ya maadhimisho hayo ilikuwa, Kina Baba na Familia: Majukumu na Changamoto. Madhumuni ya kaulimbiu hii yalikuwa ni kuhamasisha, kushawishi na kuhimiza jamii, kwa kuwalenga wazazi/walezi hususan akina baba kuwajibika zaidi katika kutunza familia ipasavyo na malezi bora ya watoto ambayo yatawafanya kuwa na ustawi bora na tabia njema.

Aidha, Wizara yangu imeratibu maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo huadhimishwa tarehe 16 Juni ya kila mwaka. Kaulimbiu ya mwaka 2008 ni Jamii Iwajibike: Isitelekeze Watoto. Madhumuni ya kaulimbiu hii ni kuwataka wazazi, walezi na jamii nzima kuwajibika ipasavyo katika malezi na makuzi ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Wizara yangu iliendelea kuimarisha uratibu na usajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*) nchini kwa kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii 150 katika Mikoa yote na Wilaya zote Tanzania Bara. Mafunzo hayo yalihusu taratibu za usajili wa *NGOs*, Sera ya Taifa ya *NGOs*, Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002, ufuatiliaji, tathmini na uchambuzi wa taarifa za *NGOs*. Aidha, mafunzo hayo yalilenga katika kuimarisha uhusiano kati ya sekta ya *NGOs* na Halmashauri kwa kuanzisha mchakato wa kuwateua Maafisa Maendeleo ya Jamii kuwa Wasajili Wasaidizi wa *NGOs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2007/2008, Wizara yangu iliwezesha uteuzi wa wajumbe wapya wa Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* iliyoinduliwa rasmi tarehe 10 Desemba, 2007. Bodi hii iliweza kufanya vikao 4 vya kisheria, kutembelea na kukagua shughuli za *NGOs* mkoa wa Tanga. Hadi kufikia mwezi Juni 2008, Bodi imepitisha, imehakiki na kuidhinisha usajili wa *NGOs* 431, kati ya hizi 357 ni usajili mpya na 74 zimepatiwa Cheti cha Ukubalifu. Aidha, Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* imepitisha Kanuni za Maadili ya *NGOs* zilizotayarishwa na Baraza la Taifa la *NGOs*. Kanuni hizi zitatangazwa kwenye Gazeti la Serikali. (Jedwali Na. 11) la kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeandaa mfumo wa kukusanya, kufuatilia na kutathmini taarifa za kazi za mwaka na taarifa za fedha za *NGOs*. Takwimu kuhusu taarifa za *NGOs* 250 zimefanyiwa uchambuzi tayari kuingizwa kwenye Tovuti ya *NGOs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano kati ya sekta ya *NGOs* na Waheshimiwa Wabunge katika uendeshaji shughuli zao, Wizara yangu kwa kushirikiana na Taasisi ya *'Foundation for Civil Society'* iliandaa semina kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ambayo ilifanyika mjini Dodoma kuanzia tarehe 7 – 9 Agosti, 2007. Semina hiyo ilitoa fursa nzuri kwa Waheshimiwa Wabunge kujifunza mambo mengi kuhusu sekta ya *NGOs* nchini na kubaini kwamba sekta hii inahitaji kupewa msukumo zaidi. Changamoto iliyopo ni kuwa na mkakati ambao utasaidia sekta hii kutoa mchango wake zaidi ndani ya jamii katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Sera na Mipango. Katika kipindi cha 2007/2008 Wizara imeendelea kuandaa na kuzifanyia marekebisho Sera zake ili ziende na wakati. Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya 1996 imedurusuwa na kupitishwa na Baraza la Mawaziri. Sera ya Maendeleo ya Familia imeandaliwa na kuwasilishwa ngazi za juu kwa maamuzi. Aidha, kazi ya kudurusu Sera ya Maendeleo ya Jamii inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika harakati za kuhakikisha taarifa na takwimu mbalimbali zinazohusu masuala ya jinsia, watoto na maendeleo ya jamii zinapatikana kwa wadau wake, Wizara imeandaa mkakati wa ukusanyaji wa takwimu hizo. Mkakati huo tayari umewasilishwa Ofisi ya Takwimu ya Taifa ili kuhakiki ubora wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Utawala na Utumishi. Suala la kuboresha utendaji kazi linahitaji mipango mizuri ya kuendeleza rasilimali watu hususan watumishi wa Wizara. Wizara yangu katika mwaka 2007/2008 imekamilisha tathmini ya mahitaji ya mafunzo na imeandaa mpango wa mafunzo kwa watumishi wa Wizara. Aidha, Wizara yangu imewapeleka mafunzoni watumishi 18 ndani na nje ya nchi ili kuongeza ujuzi na kuwa na upeo mpana zaidi wa kumudu majukumu yao. (Jedwali Na.12) la kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanisi wa watumishi unategemea kwa kiwango kikubwa ubora wa vitendea kazi pamoja na mazingira mazuri ya kazi. Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu imekamilisha awamu ya tatu ya ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu ya Wizara na kuwezesha upatikanaji wa vyumba vya ofisi 51 pamoja na Ukumbi wa Mikutano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imekuwa ikisisitiza utoaji huduma kwa wananchi kwa kiwango cha juu kwa wakati. Katika kufanikisha azma hii, Wizara katika mwaka wa fedha 2007/2008 ilizindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Mkataba huu ni ahadi ya maandishi inayotolewa na Wizara kwa wateja wake kuhusiana na viwango pamoja na ubora wa huduma zitolewazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara yangu imefanya vikao viwili vya ushirikiano kati yake na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Vikao hivi vimekuwa na matokeo mazuri hususan ya kubadilishana taarifa na mbinu za kukabili changamoto mbalimbali za kuleta maendeleo kwa wanawake, watoto na jamii kwa jumla.

Aidha, kumefanyika vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi wa Wizara kwa mujibu wa sheria ya mabaraza ya wafanyakazi vikiwa na lengo la kuhimiza kazi na kuboresha uhusiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto. Katika kutekeleza majukumu yetu kupitia mpango wa mwaka 2007/2008, Wizara ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Mahitaji makubwa ya raslimali fedha kukidhi ukarabati wa majengo na miundo mbinu chakavu katika vyuo; hali inayosababisha mazingira magumu ya utendaji kazi na kuathiri lengo la Serikali la kukuza ajira;
- Uwezo mdogo wa kukidhi mahitaji ya vifaa na nyenzo za kufanyia kazi vikiwemo vifaa vya kufundishia, vyombo vya usafiri kwa ajili ya vyuo na Wizara;
- Mila, Desturi na Imani potofu zinazoathiri haki za wanawake, watoto, baadhi ya watu wenye ulemavu na jamii kwa ujumla;
- Kutokuwapo na takwimu sahihi zilizochambuliwa kijinsia kuhusu masuala ya wanawake na watoto; na
- Athari za VVU/UKIMWI katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2008/2009. Katika mambo muhimu yatakayoshughulikiwa na Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009 maeneo matatu yafuatayo yamepewa kipaumbele:-

- Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, kisiasa na kijamii;
- Ukarabati wa majengo na miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; na
- Ufuatiliaji wa Haki na ustawi wa mtoto.

Maeneo haya kwa pamoja yametengewa asilimia 76.88 ya bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Jamii. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 17 kama inavyooneshwa katika Jedwali na 13 la kitabu cha hotuba. Mbali na ukarabati, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi Chilala, Sofi, Chala na Karumo vitapatiwa nishati inayotokana na nguvu za jua.

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinategemea kunufaika kutokana na Mpango wa Kuboresha Elimu Nchini (*Education Sector Development Programme*) kwa kupata fedha za kuwaendeleza watumishi 159 na za kununulia vifaa na nyenzo za kufundishia na

kujifunzia kama majora ya nguo na nyuzi, vifaa vya uashi, useremala, ufundi magari, na ufundi umeme. Aidha, Vyuho vitaendelea kunufaika na misaada ya mafunzo ya mawasiliano, ukusanyaji taarifa na kumbukumbu za kazi zao kutoka UNESCO na Taasisi nyingine za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza idadi ya wataalamu wa Maendeleo ya Jamii ambao ni muhimu katika kuhamasisha wananchi kushiriki katika kujiletea maendeleo, Wizara yangu katika mwaka 2008/2009 itaendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Cheti cha Msingi na Cheti, kwa wanachuo 547 katika Vyuho vya Maendeleo ya Jamii vya Mabughai, Mlale, Ruaha, Uyole na Buhare. Katika ngazi ya Stashahada kutakuwepo wanachuo 489 katika Vyuho vya Buhare, Misungwi, Monduli na Rungemba. Vile vile watakuwepo wanachuo 472 wa Stashahada ya Juu na wanachuo 210 wa Shahada katika Chuo cha Tengeru. (Jedwali Na.14) la kitabu cha hotuba.

Aidha, tutaendelea kuimarisha taaluma ya Maendeleo ya Jamii kwa kutoa mafunzo ya rejea kwa wataalamu 200 wa ngazi ya Kata kwa kuanzia na Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro na Mbeya. Mafunzo hayo yatalenga katika kuwapa wataalamu hao elimu na mbinu za uandishi wa miradi shirikishi, uhamasishaji na matumizi ya teknolojia sahihi ambazo zitapunguza uzito wa kazi kwenye jamii. Vile vile tutaendelea kuratibu utoaji wa mafunzo ya stadi mbalimbali za kazi kwa wananchi wapatao 29,000 kupitia Vyuho vya Maendeleo ya Wananchi 53.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika mwaka 2008/2009 itadurusu Mkakati wa Kijamii wa Kuwakinga Wanawake na Watoto dhidi ya Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) uliotolewa na Wizara mwaka 2002 kwa lengo la kuuboresha ili uendane na matakwa ya kitaifa. Mkakati huu unaonesha kwamba jamii ina mchango mkubwa katika kufanikisha mapambano dhidi ya janga la UKIMWI. Kwa kuwa UKIMWI hauna tiba, mafanikio ya vita dhidi ya UKIMWI yatatokana zaidi na mabadiliko ya tabia na hulka za jamii husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kuvihimiza Vyuho vyote 62 kuongeza jitihada za kuandaa vitalu vya miti ya aina mbali mbali, kwa kutumia fedha za Elimu ya Kujitegemea, ili kuchangia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaanza uhamasishaji wa matumizi ya teknolojia zitakazowawezesha wananchi kuongeza tija na kupunguza mzigo wa kazi hususan kwa wanawake katika Vyuho vya Maendeleo ya Wananchi vya Bigwa, Mamtukuna na Handeni. Aidha, Wizara itaandaa mradi utakaotekelezwa kwa ushirikiano na wadau wengine ili kuzisambaza katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 tutaendesha Mkutano Mkuu wa mwaka kama njia mojawapo ya kujadili utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya

Maendeleo ya Jamii. Mkutano huu unajumuisha Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri, Wakuu wa Vyuo vilivyo chini ya Wizara na wadau wa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Jinsia. Wizara inaendelea na mchakato wa kuwezesha Benki ya Wanawake. Aidha, Serikali itatoa kiasi cha shilingi bilioni 2.1 ili kupata leseni itakayoiwezesha Benki kuuza hisa kwa lengo la kupata shilingi bilioni sita (6) za kuanzisha shughuli zake rasmi katika mwaka huu wa fedha.

Aidha, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na wadau ili kuwawezesha wanawake wajasiriamali 80 wadogo na wa kati kushiriki katika maonesho ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake kupitia Halmashauri. Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri kuhusu uendeshaji wa mfuko, kupitia Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS), ili kurahisisha utoaji na urejeshwaji wa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendeleza mchakato wa uwezesaji wa ushiriki wa wanawake kufikia asilimia 50 katika ngazi mbalimbali za maamuzi na utendaji. Ili kutekeleza azma hii, shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

- Kukamilisha Mkakati wa kufikia asilimia 50 ya ushiriki wa wanawake kwa kushirikisha wadau mbalimbali; na
- Kuhamasisha jamii na viongozi katika ngazi mbalimbali ili kujenga uelewa kuhusu dhana ya ushiriki sawa katika maamuzi na uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo ya uchambuzi wa masuala ya jinsia katika mipango na bajeti kwa watendaji 47 wa Dawati la Jinsia na Maafisa 45 wa Bajeti na Mipango katika Kanda ya Kusini ambayo inajumuisha mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara na Kanda ya Ziwa inayojumuisha mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera zilizokuwa zimebakia. Wizara kwa kushirikiana na Sekta nyingine ina mpango wa kupitia na kuona kama masuala ya jinsia yamezingatiwa katika Sera za sekta hizo. Aidha, Wizara itaendesha vikao vya kikazi kwa ajili ya kujenga uelewa wa masuala ya Jinsia kwa Kamati 15 za Jinsia katika Wizara na Taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itashirikiana na wadau katika kuhakikisha kuwa ukatili dhidi ya wanawake na watoto unatokomezwa kwa kuhamasisha jamii hususan mikoa ya Mara, Mbeya, Mwanza na Shinyanga ambayo vitendo hivi vimekuwa vikitolewa taarifa. Uhamasishaji huu utawezesha viongozi katika ngazi za Mikoa na Wilaya pamoja na vyombo vya habari na usalama kuandaa mikakati ya maeneo yao itakayotekeleza Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuzuia Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 Wizara itaendelea kuratibu, kushiriki na kuiwakilisha Tanzania katika mikutano ya Kimataifa na Kikanda ili kuweza kutathimini utekelezaji wa maamuzi yanayotolewa kuhusu maendeleo ya wanawake na jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Mtoto. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na wadau wengine itaandaa Sera ya Malezi, Makuzi, na Maendeleo ya Awali ya Watoto. Lengo la Sera hiyo ni kuhakikisha kuwa watoto wa umri wa miaka 0-8 wanapatiwa haki zao za msingi ambazo ni kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kushiriki na kutobaguliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itahamasisha jamii kuhusu elimu ya idadi ya watu na maisha ya familia kupitia vipindi 4 vya radio na televisheni. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayoshughulikia kutokomeza mila zenye madhara kwa wanawake na watoto hususan ukeketaji, itaendelea kuelimisha jamii na wasimamizi wa sheria kuhusu madhara ya mila hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kuratibu uandaaji wa taarifa za nchi kuhusu utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda ya haki na ustawi wa mtoto. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaratibu ushiriki wa Serikali yetu katika kutetea taarifa za utekelezaji wa Itifaki za Nyongeza za Mkataba wa Haki za Mtoto (*Convention on the Rights of the Child - CRC*) katika Kamati ya Umoja wa Mataifa (*UN*) huko Geneva-Uswiss mwezi Septemba 2008. Itifaki hizo zinahusu kuwahusisha watoto katika migogoro ya kivita pamoja na uuzaji wa watoto, ukahaba wa watoto na upigaji picha za udhalilishaji watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine, taasisi, NGOs, mkoa, wilaya, madhehebu ya dini na watu binafsi ambao wanajishughulisha na masuala ya watoto, itaandaa Mkakati wa Kitaifa wa kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili na unyanyasaji. Aidha, Wizara yangu itafuatilia sheria zinazolinda haki za watoto ili kubaini upungufu katika utekelezaji wa sheria hizo na kushawishi marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2008/2009 Wizara yangu itahakikisha kuwa Baraza la Taifa la Watoto linasajiliwa kisheria ili kuwa chombo chenye nguvu kisheria katika kuijenga Tanzania imfaayo mtoto. Aidha, Wizara yangu itashirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo mikoani na wilayani pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ili kuhakikisha kuwa Wilaya 27 zinaanzisha Mabaraza ya Watoto ya Wilaya kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na.15 la kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Serikali imedhamiria kuimarisha ushirikiano kwa kufanya kazi kwa karibu na sekta ya NGOs nchini. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kuhimiza kuundwa kwa mitandao ya NGOs kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilaya na kujenga mahusiano mazuri na wadau mbalimbali katika maeneo yao ya kazi. Aidha, msukumo utakuwa katika kuhakikisha

kwamba mipango yao ya kazi inazingatia mipango ya Halmashauri na hivyo kuongeza uwazi na uwajibikaji wa sekta hii si kwa wafadhili tu bali hata kwa wananchi na wadau wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta uelewa mzuri miongoni mwa wadau wa sekta ya NGOs nchini, Bodi ya Taifa ya Uratibu wa NGOs itaendelea kukutana na wadau wa sekta hii ili kubadilishana uzoefu, kutoa ufafanuzi na maelekezo kuhusu utekelezaji wa Sheria ya NGOs. Aidha, Bodi itatembelea na kufanya ukaguzi wa shughuli za NGOs katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upashanaji habari na utoaji taarifa kwa wadau ni muhimu katika kuongeza uelewa na kuondoa migongano katika utekelezaji majukumu mbalimbali. Kwa kutambua umuhimu huo Wizara yangu itazindua rasmi Tovuti ya NGOs ambayo itatumika kurahisisha usajili wa NGOs na kupata tarifa zao sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Mipango. Wizara yangu katika mwaka 2008/2009 itaratibu maandalizi ya Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto. Aidha, kwa kuzingatia ugumu wa upatikanaji wa haki za mtoto, Mkakati huu utazingatia mahitaji ya watoto wote kwa ujumla yakiwemo makundi maalum ya watoto kama vile wenye ulemavu, yatima, na wanaoishi katika mazingira hatarishi. Vile vile, Wizara itaandaa Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Familia mara baada ya Sera hiyo kupitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha ufanisi wa utendaji kazi, Wizara katika kipindi cha mwaka 2008/2009 itawapatia mafunzo ya wiki moja Maafisa wa bajeti 23 wa Wizara ili kuwajengea uwezo zaidi wa uandaaji wa mpango wa Bajeti. Kati ya maafisa hao, 10 watapatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwawezesha wadau wa sekta ya Maendeleo ya Jamii kupata habari na taarifa mbalimbali zinazohusu wanawake, watoto, jinsia na maendeleo ya jamii, Wizara yangu itaandaa mfumo wa kompyuta wa ukusanyaji, uchambuzi, uhifadhi na usambazaji wa takwimu zilizochambuliwa kijinsia. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika harakati za kupambana na maambukizi ya VVU na UKIMWI sehemu za kazi, Wizara itajenga uwezo wa watumishi 210 wa Makao Makuu ya Wizara na kutoka Vyuoni kuhusu uingizaji (*mainstreaming*) wa masuala ya UKIMWI katika mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara yangu itaendelea kusimamia utendaji kazi kwa misingi ya Utawala Bora. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa kila mtumishi anapangiwa kazi za kutosha kulingana na majukumu ya Wizara na kufanya tathmini ya utendaji wake. Aidha, Wizara yangu itatoa mafunzo ya OPRAS (*Open Performance Review Appraisal System*) kwa viongozi na maafisa wakuu 40 wa Makao Makuu ya Wizara ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya



Mpango wa Kuboresha Sekta ya Umma. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kwa watumishi 130 wa kada ya kawaida kutoka Makao Makuu ya Wizara na Vyuoni ili waweze kupata elimu na maarifa ya kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Wizara yangu pia itaendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wake walioko Makao Makuu ya Wizara na vyuoni. Mafunzo haya ni pamoja na mafunzo ya Menejimenti kwa Wakuu wote wa Vyuoni 62 vya Wizara, Mafunzo ya Uongozi kwa watumishi 10, Mafunzo ya taratibu za manunuzi na ugavi kwa watumishi 25 na mafunzo ya Utunzaji Kumbukumbu kwa watumishi 10 wa Masjala kutoka Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara yangu itaendelea na dhamira yake ya kupiga vita rushwa kwa kutoa elimu kuhusu Sheria Na. 11 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini ya mwaka 2004 kwa watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara itaendelea na awamu ya nne ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara sambamba na ununuzi wa samani za ofisi na mitambo ya mawasiliano na nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara yangu itaratibu vikao viwili vya ushirikiano kati yake na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Zanzibar. Vikao hivi vitafanyika kimoja Tanzania Bara na kingine Zanzibar.

Aidha, Wizara itaendesha vikao viwili kwa wajumbe 34 wa Baraza la Wafanyakazi kwa lengo la kuwashirikisha wafanyakazi katika masuala muhimu yanayowahusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kukiimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Umma kwa kuwapa watumishi wawili wa kitengo hicho mafunzo ya uandishi wa habari ya muda mfupi na kukiongezea vitendea kazi ili kumudu majukumu yake kikamilifu ya kutangaza shughuli za Wizara. Aidha, Wizara itaendesha vipindi vya televisheni na radio kwa kushirikiana na wadau ili kuifahamisha jamii mambo muhimu ya maendeleo na shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, majukumu ya Wizara yangu ni mtambuka na hivyo kuhitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali ili kufanikisha malengo. Kwa msingi huo, pamoja na kwamba tuna vipaumbele vitatu ambavyo ni: Uwezesaji wa wanawake kiuchumi, kijamii na kisiasa; Ukarabati wa majengo na miundombinu katika Vyuoni vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuoni vya Maendeleo ya Jamii na ufuatiliaji wa haki na ustawi wa mtoto, yapo maeneo mengine tutakayoyatekeleza kwa kushirikiana kwa karibu zaidi na wadau kama ifuatavyo:-

- Kwa kushirikiana na Halmashauri kuangalia uwezekano wa kuwa na eneo maalum la kufanyia biashara wanawake wajasiriamali Jijini Dar es Salaam;

- Kutekeleza Mpango Kazi wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto; (*Makofi*)
- Kufanya utafiti kuhusu watoto wa mitaani ili kubaini ukubwa wa tatizo na kuweka mikakati ya kukabiliana nalo; (*Makofi*)
- Kuwezesha urushaji wa vipindi vya *TV/Radio* kwa ajili ya kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu maendeleo; na
- Kuendeleza matumizi ya teknolojia sahihi ili kupunguza mzigo wa kazi kwa wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanikisha mipango na malengo haya, Wizara itakuwa inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Malengo ya Ilani ni pamoja na kuwawezesha wananchi wengi kujijajiri na kuboresha maisha yao na pia kuchangia uchumi wa Taifa na kupambana dhidi ya ajira za watoto. Lengo lingine ni kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa inayohusu haki na ustawi wa mtoto, kuheshimu nafasi za wanawake na maendeleo ya nchi kwa kuweka bayana shabaha za kujiendeleza kijamii, kisiasa na kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kuongeza ushiriki wao katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na katika nafasi za maamuzi, kwa lengo la kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, namshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya, kwa ushirikiano, ushauri na usaidizi mkubwa anaonipa katika kuongoza Wizara hii. Natoa shukrani za dhati kwa Bibi Mariam J. Mwaffisi, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu wa ngazi zote na waliopo kwenye taasisi zetu zote, kwa jitihada zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Bila ya mchango wao muhimu ingekuwa vigumu kupiga hatua katika majukumu tuliyonayo ya kuendeleza sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kupitia Bunge lako tukufu, kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao: Asasi ya Wanawake na Maendeleo (*WAMA*), Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*), Mtandao wa Jinsia Tanzania (*TGNP*), Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (*TAWLA*), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (*TAMWA*), Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (*FAWETA*), *Plan* Tanzania, Mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali pamoja na wale wanaofanya kazi kwa maslahi ya jamii kwa namna moja au nyingine. (*Makofi*)

Napenda pia kuzishukuru Serikali za nchi rafiki ambazo kwa kupitia Mashirika yake zinaendelea kutusaidia. Nchi hizo ni pamoja na Marekani (*USAID*), Denmark (*DANIDA*) na Canada (*CIDA*). Aidha, Mashirika ya Kimataifa ambayo ni: *UNICEF*, *UNDP*, *UNFPA*, *UNESCO*, Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Maendeleo ya Wanawake (*UNIFEM*), pamoja na mashirika mengine ya ndani na nje nayo pia nayashukuru kwa misaada yake. Aidha, napenda kuwashukuru Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*), *ILO* na Ubalizi wa Uingereza kwa kuwa tayari kushirikiana nasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kukubali kuanzisha ruzuku ya Sh. 3.6m/= kwa Idara ya Maendeleo ya Jamii katika kila Halmashauri. Ni imani yangu kuwa fedha hizi zitawafikia walengwa. Aidha, naishukuru Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara yangu kutoka Sh. 10.9bn/= hadi kufikia 14.6bn/= na kukubali kuongeza Sh. 2.1bn/= kwa ajili ya kuwezesha uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania. Ni matumaini yangu kuwa bajeti ya Wizara itaendelea kuongezwa mwaka hadi mwaka ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niishukuru familia yangu hasa Mheshimiwa Samuel Sitta, mume wangu na watoto wangu John, Caroline, Agness, Samuel, Benjamin na wakwe zangu wote kwa misaada mbalimbali wanayonipa. Aidha, nawashukuru pia ndugu zangu kaka zangu, dada zangu na jamaa na marafiki ambao wamenipa moyo katika kutimiza majukumu yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, navishukuru Vyama vya Wafanyakazi kwa ushirikiano wanaonipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya bajeti ya Wizara mwaka 2008/2009. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2008/2009, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinisha matumizi ya Sh. 14,665,870,000/=. Kati ya hizo Sh. 7,820,393,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Sh. 3,053,887,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 4,766,506,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (*other charges*). Aidha, Sh. 6,845,477,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo Sh. 4,923,977,000/= ni fedha za hapa nchini na Sh. 1,921,500,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**NAIBU SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono, namshukuru Mheshimiwa mtoa hoja. Sasa nitamwita Msemaji wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii, naona ni Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir. (*Makofi*)

**MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR (K.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA-MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kunipa uzima na afya na kuweza kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya

Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, majukumu ya Kamati hii pamoja na mambo mengine imefanya kazi ya kuchambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Tarehe 4 Juni, 2008, Mjini Dar - es Salaam, Kamati ilifanya kikao na Wizara, katika kikao hicho tulipata maelezo ya Bajeti ya Wizara toka kwa Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu akisaidiana na wataalam wa Wizara hiyo. Timu hiyo ilieleza kwa kina kuhusu dira, dhima, majukumu ya Wizara na utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008.

Aidha, tarehe 13 Juni, 2008, Mjini Dodoma, Kamati ilifanya kikao tena na Wizara kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambaye pia ni Mwalimu wangu, kuhusu utekelezaji wa mpango wa maendeleo, mapato na matumizi kwa mwaka 2007/2008, makadirio ya mapato na matumizi ya fedha pamoja na kazi zilizopangwa kufanywa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Kamati yangu ilikutana tena na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto tarehe 4 Julai, 2008 Mjini Dodoma kupata maelezo zaidi kuhusu mikakati iliyowekwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo inayokusudiwa kufanywa na wizara kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati, napenda kwanza kuwatambulisha Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti; Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Fatma O. Ally, Mjumbe; Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mjumbe; Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mjumbe; Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mjumbe; Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mjumbe; Mheshimiwa Zuleikha Y. Haji, Mjumbe; Mheshimiwa Salim A. Khalfan, Mjumbe; Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mjumbe; Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt Gertrude P. Rwakatare, Mjumbe; Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mjumbe; Mheshimiwa Elietha N. Switi, Mjumbe; Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mjumbe; Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mjumbe; Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mjumbe; Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mjumbe; Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mjumbe na Mheshimiwa Mohamed A. Said, Mjumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha uliopita Kamati yangu ilitoa maoni na maagizo katika maeneo mbalimbali na hasa yanayohusu:-

- Kuboresha sekta ya maendeleo ya jamii;
- Teknolojia rahisi katika kuhamasisha wanaume kufanya kazi ya kusaidia wanawake;

- Kufufua na kuimarisha vyuo vya maendeleo ya wananchi;
- Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*) kupelekwa katika *SACCOS* zinazotambulika;
- Uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Wanawake;
- Mkakati wa kufikia asilimia 50:50;
- Maendeleo ya mtoto nchini;
- Serikali kudhibiti na kufuatilia utendaji kazi wa *NGOs* hapa nchini; na
- Wizara kurekebisha mapungufu yote ili isiendelee kupata hati ya mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi baadhi ya maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika itaendelea kushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara iliidhinishiwa na Bunge matumizi ya Sh. 10.9bn/=. Kamati ilielezwa kwa undani kuhusu matumizi katika kutekeleza bajeti ya Mwaka 2007/2008. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na mafanikio yake ni kama ilivyoorodheshwa hapa chini:-

- Wizara imetoa mafunzo rejea ya uandishi wa miradi shirikishi na matumizi ya teknolojia sahihi kwa jumla ya wataalam 147 wakiwemo maafisa maendeleo ya jamii na mafundisanifu;
- Mkutano Mkuu wa mwaka wa sekta ya maendeleo ya jamii ulifanyika katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida;
- Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ulifanyika katika vyuo vya Rungemba, Misungwi, Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 25;
- Kuvipatia hati miliki Vyuo 8 vya Malya, Chisalu, Handeni, Munguri, Ikwiriri, Mwanva, Bariadi na Njombe;
- Mafunzo kuhusu jinsia na jinsi ya kuingiza masuala ya jinsia katika sera, mikakati na mipango, waratibu 80 wa dawati la jinsia katika ngazi ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali walipatiwa mafunzo;
- Wizara imeweza kuratibu na kutekeleza shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake katika Halmashauri 133 ili ziweze kutoa mikopo katika vikundi vya wanawake wajasiriamali;

- Kuwawezesha wanawake kushiriki katika maonesho, wanawake 54 walishiriki katika banda la Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote, zaidi ya wanawake 300 walishiriki kupitia *SIDO* na *FAWETA*;
- Baraza la Mawaziri limeupitisha Waraka wa Uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania;
- Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria na Katiba imeibua mapungufu yaliyopo katika Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, pamoja na sheria ya mirathi na matunzo ya watoto;
- Mafunzo yametolewa kwa Maafisa 400 wa Serikali ambao wanasimamia utekelezaji wa Sheria ambao ni Askari Magereza, Polisi, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa na Wilaya;
- Sera ya Maendeleo ya Mtoto imekamilika na kupitishwa na Baraza la Mawaziri na rasimu ya sera ya maendeleo ya familia imewasilishwa katika Sekretariati ya Baraza la Mawaziri na kujadiliwa;
- Kuelimisha jamii kuhusu kupiga vita mila na desturi zenye madhara hususan kwa wanawake na watoto wa kike;
- Mafunzo kuhusu ushirikishwaji wa watoto yalitolewa kwa maafisa maendeleo ya jamii;
- Baraza la Taifa la *NGOs* kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya *NGOs* tayari wamekamilisha rasimu ya kanuni za maadili ya *NGOs* na kuwasilishwa kwa Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs*;
- Mafunzo kwa wataalam wa maendeleo ya jamii na kuwateua rasmi kuwa wasajili wasaidizi wa *NGOs* yalifanyika Mkoani Dodoma;
- Kuhimiza na kuhamasisha taasisi, asasi na wafadhili mbalimbali kujikita katika kuwajengea uwezo sekta ya *NGOs* ilifanyika;
- Kuendesha mafunzo kwa watumishi kuhusu jinsia katika sera na masuala ya Ukimwi;
- Wizara inaendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara;
- Wizara inaendelea na utoaji wa mafunzo kwa Watumishi kwa kuzingatia mpango wa kuendeleza rasilimali watu. Aidha, Wizara imeidhinishiwa nafasi tisa za ajira mpya; na
- Mkataba wa Huduma kwa Mteja ulizinduliwa na Waziri Oktoba, 2007. Mikakati ya kuelimisha watumishi, wananchi na wadau wote kwa ujumla imeandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza bajeti ya Wizara kwa mwaka 2007/2008, changamoto hizo ni:-

- Uhaba wa vifaa/nyenzo za kufanyia kazi hii iliathiri sana utendaji kazi na utoaji wa huduma;
- Ucheleweshwaji wa utoaji wa fedha hasa za maendeleo kutoka katika Wizara ya Fedha na Uchumi;
- Uhaba wa ofisi hasa katika Mikoa na Wilaya; na
- Uhaba wa wafanyakazi na bajeti ndogo inayotolewa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2008/2009 imeomba kiasi cha Sh. 14,665,870,000/=. Ongezeko la Bajeti ya Wizara kutoka Sh 10.9bn/= ya mwaka wa fedha 2007/08 hadi Sh. 14.66bn/= linatokana na juhudi za Wizara kuainisha maeneo ya kipaumbele ambayo yameonekana kuwa ni muhimu. Maeneo hayo ni pamoja na:-

- Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi ambapo ni pamoja na Uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania;
- Ukarabati wa vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vitano kati ya vyuo 58 ambavyo vimekuwa kwenye hali mbaya kwa muda mrefu; na
- Uimarishaji wa dawati la jinsia katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata taarifa na maelezo ya malengo na kazi zilizopangwa kufanywa kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Kamati ilijadili kwa undani masuala mbalimbali na kuipitisha bajeti ya Wizara hii. Kamati yangu inaunga mkono maombi ya Wizara hii, hata hivyo Kamati inatoa maoni na ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna dhana potofu iliyojengeka miongoni mwa wataalam na watayarishaji wa Bajeti hasa Wizara ya Fedha na Uchumi kuona baadhi ya Wizara ni duni na hazina umuhimu wa kupata bajeti ya kutosha, ikiwemo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ukweli ni kwamba Wizara hii ni muhimu sana na pengine kuliko Wizara zingine zote katika kuleta maendeleo ya jamii, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

- (a) Wataalam wa Wizara ya Fedha na Uchumi iwe na mtazamo wa pekee katika kuangalia majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mtazamo huo uwe na lengo la kuona umuhimu wa Wizara hii kuongezewa bajeti yake.

(b) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ikamilishe mapema Mpango Mkakati wa Wizara na kuweka mikakati katika maeneo muhimu yenye kujenga msingi wa kuongeza bajeti ya Wizara. Maeneo mahsusi yaainishwe mapema na yajadiliwe na kuihusisha Kamati ya Maendeleo ya Jamii kabla ya kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikakati ya Kuboresha Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Malya. Kamati ilipotembelea Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Malya na kujadili katika bajeti Mjini, Dar- es Salaam na Dodoma, Kamati ilibaini kwamba hali ya Chuo cha Malya ni mbaya sana, hakuna walimu na matatizo mengine mengi. Kamati inaipongeza Wizara kwa kutenga fedha za kutatua matatizo sugu yaliyopo katika Chuo cha Malya katika mwaka wa fedha 2008/2009. Hata hivyo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ielimishe Wakuu wa Vyuo vyote ili wawe wabunifu katika kujiendesha na kuendeleza vyuo vyao;

(b) Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi viwe vinatembelewa mara kwa mara na Uongozi wa Mkoa au Wizara kujionea mafanikio na matatizo ya Chuo na hatua muhimu zichukuliwe mapema katika kutatua matatizo yao; na

(c) Wizara iendeele na mikakati ya kupunguza au kumaliza kabisa matatizo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Malya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufufua na Kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kwa kuwa kuna Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 53 ambavyo vimekuwa kwenye hali mbaya kwa muda mrefu na kwa kuwa Vyuo hivyo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Jamii vikifanyiwa ukarabati mkubwa vinaweza kuleta mageuzi makubwa sana katika kuwaletea maendeleo wananchi. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za kutosha katika kufanya ukarabati mkubwa, fedha zinazotolewa zitumike kukarabati vyuo vichache kuliko kugawanya fedha hizo katika vyuo vyote kwani hazitaleta mabadiliko makubwa (*impact*);

(b) Kwa kuwa mwaka wa fedha 2007/2008 fedha nyingi sana zilitolewa katika kukarabati vyuo vya VETA. Serikali ione sasa umuhimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kama ilivyoona umuhimu wa vyuo vya VETA mwaka uliopita; na

(c) Serikali iwe makini katika utoaji wa tenda za kufanya ukarabati wa Vyuo vilivyopendekezwa (Vyuo vya Ifakara, Muheza, Urambo, Mtwara na Kilosa) ili fedha zilizotengwa zifanye kazi iliyokusudiwa na hatua kali zichukuliwe kwa wale wote watakaokiuka matumizi ya fedha hizo.

(d) Serikali itenge fedha za kujenga uwezo wa watumishi hasa Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika kubuni na kuibua miradi itakayosaidia vyuo kujiendesha badala ya kutegemea fedha toka Serikalini tu;



(e) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Kamati ya Maendeleo ya Jamii wakae pamoja kujadili kwa kina jinsi ya kuvitumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kufundisha stadi za kazi zitakazosaidia wananchi kujajiri ili kuunga mkono azma ya Rais wetu katika kuongeza ajira milioni moja ifikapo mwaka 2010;

(f) Wizara iandae makisio yanayohitajika katika kufanya ukarabati mkubwa katika kila Chuo cha Maendeleo ya Wananchi nchini na majadiliano ya kina yafanyike; na

(g) Serikali ione uwezekano wa kuingiza mafunzo juu ya UKIMWI (VVU) katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na mawasiliano yafanyike ya kuiomba TACAIDS kuona jinsi itakavyosaidia

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu teknolojia rahisi katika kuhamasisha wanaume kufanya kazi za kumsaidia mwanamke. Kwa kuwa teknolojia rahisi mfano, teknolojia ya kutengeneza mikokoteni au matoroli ya kubebea mizigo au majiko ingehamasisha sana wanaume katika masuala ya ubebaji wa mizigo na kupika katika Vijiji na Mijini hali ambayo ingemsaidia sana Mwanamke. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Wizara iweke mikakati madhubuti ya kuibua na kuandaa kitini cha teknolojia rahisi kwa lengo la kuomba fedha katika mwaka wa fedha ujao. Fedha hizo zilenge kuanza na Wilaya chache kwa ajili ya kuendeleza teknolojia hiyo rahisi; na

(b) Wizara iweke mikakati ya kupata fedha za wafadhili kama vile *SIDO* ilivyopata fedha za kutekeleza *MKUKUTA* kutoka kwa wafadhili mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*) kupelekwa katika *SACCOS* zinazotambulika, kwa muda mrefu fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake zilikuwa zinapelekwa katika Halmashauri zetu ili waweze kuzikopesha katika vikundi vya wanawake, lakini utaratibu huo umekuwa na manufaa kidogo sana. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iandae waraka ili fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*) zipelekwe kwenye *SACCOS* zinazotambulika.

(b) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto waweke utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa fedha hizo ili ziweze kukopeshwa na kurejeshwa na kuendelea kukopeshwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania. Kamati ilibaini kwamba bado wananchi wengi hawajaelewa kabisa mikakati iliyowekwa katika uanzishwaji wa Benki ya Wanawake hali ambayo inarudisha nyuma zoezi la ununuzi wa hisa. Kamati inashauri kwamba:-

(a) Wizara iweke mikakati ya kutosha kwa kuwaelimisha wananchi hasa wanawake kuhusu umuhimu wa uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania;

(b) Kabla ya Benki kuanzishwa ni muhimu mafunzo yatolewe kwa wale watakaokuwa katika uendeshaji wa benki, kuhamasisha wateja kuweka akiba katika benki hiyo na masuala ya Uongozi na Utawala wa Benki; na

(c) Serikali iweke wazi namna itakavyoisaidia Benki ya Wanawake, mfano kutoa fedha za kulipia gharama za uanzishwaji na kuona umuhimu wa kutoa fedha za uwezeshaji wa kiuchumi kwa wananchi (Mfuko wa JK) kupelekwa katika Benki ya Wanawake Tanzania pale itakapoanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mchakato wa kufikia asilimia 50:50. Kwa kuwa mchakato wa kufikia asilimia 50:50 katika ngazi zote za maamuzi unaonekana kusuasua hii ni dalili kwamba hatuwezi kufikia lengo hilo kama ilivyokubalika. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Mchakato wa kufikia asilimia 50:50 usionekane tu katika ngazi ya Ubunge na Udiwani bali uwe katika ngazi zote za maamuzi;

(b) Kwa kuwa Kamati ya Maendeleo ya Jamii haikushirikishwa kikamilifu katika Kamati ya Mchakato huo; na kwa kuwa Kamati ya Maendeleo ya Jamii haijapata taarifa ya mchakato, Kamati inashauri Wizara kuleta mchakato kwa lengo la kujadili na kuboresha baadhi ya maeneo; na

(c) Serikali iandae kongamano litakalohusisha Makatibu Wakuu wote kujadili jinsi Wizara zao zitakavyohusika katika kufikia asilimia 50:50 na kuteua wahusika wa *gender focal point* ambao wanaweza kushiriki kikamilifu katika ngazi za maamuzi katika Wizara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Mtoto Nchini. Kwa kuwa malezi na makuzi ya mtoto ni muhimu sana katika kujenga tabia bora kwa vijana wetu. Utafiti unaonyesha kwamba karibu asilimia 80 ya ubongo wa mtoto unakua katika umri kati ya miaka 0-5 na asilimia ishirini iliyobaki ni katika maisha yake yote. Na kwa kuwa sio Wizara moja inayoshughulika na maendeleo ya mtoto hapa nchini. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa shule za kulelea watoto wadogo (chekechea) zinafunguliwa kwa wingi na watu binafsi, Serikali ione umuhimu wa kufungua shule zake za kulelea watoto wadogo kuliko kuwachia sekta binafsi pekee;

(b) Kwa kuwa Muswada wa Sheria ya mtoto hautaletwa tena Bungeni kujadiliwa, imependekezwa kwamba Serikali ifanye marekebisho katika sheria mbalimbali zinazomhusu mtoto;

(c) Kwa kuwa protokali nyingi za Kimataifa zinaitaka nchi kuwa na sheria ya mtoto, Serikali iangalie namna bora ya kutekeleza suala hili kwani kutokuwa na sheria ya mtoto inaweza kuleta matatizo makubwa zaidi;

(d) Kwa kuwa wWizara huwa inaandaa sera ya mtoto lakini watekelezaji wa sera hizo ni wizara zingine (Elimu, Afya, *TAMISEMI*, Mambo ya Ndani, Sheria n.k.) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto waweke mikakati ya ufuatiliaji wa utekelezaji wake;

(e) Serikali ikamilishe mapema iwezekanavyo Sera ya Mtoto kuhusu malezi na makuzi ya mtoto na sera ya familia;

(f) Wizara ione umuhimu wa kuwa na kikao maalum cha kujadili suala la mtoto kwa kina hasa mtoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, mtoto wa shule, mtoto yatima, haki za mtoto na kadhalika;

(g) Serikali iweke mikakati ya kusaidia uanzishwaji wa mabaraza ya Watoto, Kamati ipate taarifa ya utekelezaji wake;

(h) Suala la mimba kwa watoto wa shule, tatizo hili ni kubwa, kwa nini Serikali haifanyi maamuzi ya kuwasaidia ili wakijifungua wapate haki zao za kimsingi za elimu; na

(i) Vifo kwa maalbino tunaomba tamko rasmi la Serikali la kukomesha tatizo hili kama kuna sheria mbovu zinazowalinda wahalifu hao ziletwe kwetu tuzirekebishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikakati ya kurekebisha Sheria zinazohusu haki za Wanawake na Watoto. Kwa kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ina jukumu la kuandaa sera zinazohusu wanawake na watoto, na kwa kuwa Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi ina upungufu mkubwa. Ili kuwa na sheria zenye heshima na kamilifu katika nchi yetu lazima mambo mbalimbali ya mila na desturi yachambuliwe kwa kina ili kuiwezesha Wizara ya Sheria na Katiba kuleta marekebisho ya sheria hizo. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa sheria nyingi zinazohusu haki za mwanamke na watoto zimepitwa na wakati. Serikali iweke mikakati ya kujadili sheria ya ndoa na sheria ya mirathi ili marekebisho ya sheria hizo yaweze kufanyika haraka iwezekanavyo kabla ya Bunge hili kumalizika (2005 - 2010);

(b) Kwa kuwa Protokali na Itifaki za Kimataifa zinazohusu haki za wanawake na watoto ni muhimu sana kufahamika kwa wananchi na kutungiwa sheria ya kutekeleza. Kamati inashauri Serikali kuwa na mikakati ya kutoa elimu na mafunzo ya protokali na itifaki hizo; na

(c) Vifo vya wanawake wakati wa kujifungua, tatizo hili ni kubwa na hata malengo ya kimilenia hayatafikiwa kama tatizo hili halitapatiwa ufumbuzi. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara zingine zikae pamoja kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikakati ya Kuboresha Utendaji kazi wa Taasisi Zisizo za Kiserikali (*NGOs*) hapa nchini. Kwa kuwa utendaji kazi bora wa *NGOs* ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi, na kwa kuwa Baraza la Taifa la *NGOs* kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya *NGOs* tayari wamekamilisha rasimu ya kanuni za maadili ya *NGOs*. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Kanuni za maadili ya *NGOs* zijadiliwe kwa kina ili kuboresha ufanisi kwa lengo la kuondoa migongano katika utekelezaji wa kazi zao hapa nchini;

(b) Wizara iandae mfumo bora wa kukusanya na kuchambua takwimu za utekelezaji wa miradi inayoendeshwa na *NGOs* hapa nchini;

(c) Kwa kuwa sheria ya *NGOs* inaitaka kila *NGO* kutoa taarifa ya utendaji kazi na hesabu zilizokaguliwa kila mwaka, lakini *NGOs* hizo hazifanyi hivyo kwa kisingizio cha kutokuwa na fedha, kamwe kisingizio cha kutokuwa na fedha isiwe sababu ya kuvunja sheria;

(d) Kwa kuwa Kamati imebaini kwamba kuna sheria 3 zinazotumika katika kusajili *NGOs* hapa nchini, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuunganisha sheria hizo ili kuleta ufanisi katika kusimamia utendaji kazi wa *NGOs*;

(e) Kwa kuwa ufuatiliaji katika utendaji kazi wa *NGOs* unahitaji muda na rasilimali mbalimbali. Kamati inashauri Wizara kuboresha mazingira katika Idara ya *NGOs* ili waweze kuwa na uwezo wa kufuatilia utendaji kazi wa *NGOs* kwa ufanisi; na

(f) Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya na Mikoa waendeleo kupewa kazi zingine nyingi ikiwa ni pamoja na uandikishaji wa *NGOs* na kufuatilia utekelezaji wa *NGOs* katika Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikakati ya Kuboresha Sekta ya Maendeleo ya Jamii nchini. Kwa kuwa siku za nyuma Maafisa wa Maendeleo ya Jamii walikuwa ni muhimu sana katika kuleta maendeleo hasa Vijijini kwa sababu wao wanajua mila na desturi za sehemu wanazokaa. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iweke mikakati ya kutoa mafunzo kwa wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya na Mikoa na kuwateua rasmi kuwa Wasajili Wasaidizi wa *NGOs*;

(b) Kuona umuhimu wa kurudisha uteuzi wa maafisa maendeleo ya Jamii wa Mikoa na Wilaya kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto badala ya kuteuliwa na *TAMISEMI*. Wizara iweke mazingira mazuri mfano ofisi, kompyuta na vifaa muhimu vya kufanyia kazi watalaam hao; na

(c) Serikali iweke mikakati ya kupata fedha kwa ajili ya mafunzo kwa maafisa maendeleo wa Wilaya na Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mikataba ya Huduma Bora kwa Wateja. Kwa kuwa Waziri alizindua Mikataba wa Huduma kwa Mteja Oktoba, 2007, ambao ni muhimu sana katika kuboresha utendaji kazi. Kamati inashauri Serikali iweke mikakati ya kutekeleza mkataba huo hasa kwa kutoa mafunzo na elimu kwa wahusika. Aidha Wizara ichapishe majarida ya kutosha na kuwagawia wahusika

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Kwa niaba ya Wanakamati wenzangu naomba kukushukuru wewe binafsi, kwanza kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu, na pia namshukuru Mheshimiwa Spika na Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kufanya kazi ya kuchambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge Mwenyekiti wa Kamati hii na Mheshimiwa Haroub Said Masoud Mbunge Makamu Mwenyekiti, pamoja na Wajumbe wenzangu kwa michango yao katika kuboresha mijadala, Maoni na Mapendekezo ya Kamati, nawashukuru sana. Ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, mwalimu wangu mpendwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Mbunge, Katibu Mkuu Mariam Mwafisi na Watumishi wote wa Wizara na Mashirika yaliyochini ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatakiya mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Kamati Ndugu Lawrence Robert Makigi na Ndugu Brown Mwangoka kwa kazi nzito katika kuihudumia Kamati hii ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa hii kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kuwasilisha taarifa vizuri. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Maulidah Anna Komu.

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU – MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu Na. 99(7) Toleo la Mwaka 2007, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na amani kwa kutujalia kukutana kwetu leo hii tukiwa wazima wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa hayati Chacha Zakayo Wangwe. Marehemu alikuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya Watanzania kwa ujumla na alikuwa miongoni mwa watu shupavu na wasiogopa kusema ukweli na kusimamia alichokiamini muda wote. Namwomba Mwenyezi Mungu ampokee na amlaze mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Savelina Mwijage kwa kupoteza mwanawe, na pia napenda kukupa wewe pole kwa kupoteza mtoto wa dada yako. Pia bila ya kusahau naomba nitoe pole kwa wazazi wa watoto waliokufa jana kwenye ajali ya gari kule Muheza Tanga, Mungu azilaze roho za watoto hao mahali pema peponi na pia Mwenyezi Mungu asimame na wale ambao wameumia ili waweze kupona na kurudi haraka kuendelea na masomo yao. Pia bila ya kusahau kutoa agizo tena kwa madereva wanaochukua watoto, nawaomba sana wajitahidi kuendesha magari taratibu wanapochukua watoto wadogo katika magari yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitakishukuru chama changu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (*CHADEMA*). Chama makini kinachojikita katika kutetea Uhuru wa demokrasia nchini. Nami naendelea kuwaahidi kuwa nitafanya kila lililo ndani ya uwezo wangu kutimiza majukumu niliyopewa na chama changu na Watanzania wote kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa nimetenda haki kama sitatoa shukrani zangu za dhiti kwa Kambi ya Upinzani, chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa Mbunge wa Karatu. Namshukuru Mungu kuwa Kambi ya Upinzani Bungeni ni imara, thabiti na inayofanya kazi kwa ufanisi mkubwa. Naishukuru kwa kuwa imeendelea kuniamini na kunipa nafasi hii ya kuiwakilisha Kambi katika Wizara hii nyeti kwa mara nyingine tena. Pamoja na hilo pia napenda kuwashukuru Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wanaonipa ndani na nje ya Bunge. Bila kumsahau Naibu Waziri kivuli Wizara hii, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika kwa msaada wake wa mawazo na hekima katika hotuba hii. Pamoja na hao pia sijamsahau mume wangu mpenzi Valerian Alley Komu na watoto wangu wote, kwa kunivumulia wakati wote kwa upendo na uvumilivu mkubwa wakati wote ninapokuwa katika shughuli zangu za kisiasa toka mwaka 1992 hadi leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa Wizara. Wizara ya maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni moja kati ya Wizara muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wote kwa ujumla. Ndio maana dhana nzima na dira ya Wizara hii inalenga katika kuhakikisha

Wizara hii inakuwa ni kitu ambacho kitakuza jamii yenye mwamko, kujiamini, kujituma na kuwa na Utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii katika kujiletea maisha bora kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na haki za watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua kama kweli Wizara hii ina jukumu la kuleta maendeleo kwa jamii ya Watanzania? Na kama kweli je, ni kwa nini haipewi kipaumbele na Serikali? Hii imejidhihirisha hata hapa Bungeni imepewa siku moja tu kwenye mjadala wa kuwasilisha mapato na matumizi ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kuwa mgawanyo wa kazi huleta ufanisi yaani “*specialization leads to efficiency*” na wahenga walisema mikono mingi huharibu mapishi. Kambi ya Upinzani inauliza, kwa nini tunakuwa na Wizara zaidi ya moja katika kushughulikia suala moja (hili linaitwa jambo mtambuka). Hii kwa maana nyingine ni kigezo cha kukwepa majukumu ya msingi ya Wizara husika, kwani unaambiwa kazi zake zingine ziko Wizara nyingine na kasma ya shughuli iko kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhihirisha hili naomba nitoe mfano mdogo ambao ni moja ya vitu vinavyosababisha mkanganyiko huo wa majukumu. Suala la watoto, Idara zinazojikita katika kushughulikia masuala ya watoto ziko katika Wizara tatu tofauti. Nazo ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inatupa taabu kujua hasa mwenye mamlaka ya kufuatilia masuala ya watoto hasa ni nani? Moja kati ya masuala mazito ambayo yanaisumbua nchi yetu kwa sasa ni suala la ongezeko la mimba kwa watoto wa shule (*teenage pregnancy*). Hili tatizo limezidi kuwa tata, na ni vyema ieleweke kuwa hili ni suala la kijamii, na wataalam ambao wanastahiki kushughulikia suala hili ni wataalam wa masuala ya sayansi ya jamii. Lakini je, ni wizara ipi yenye jukumu la kushughulikia suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa Wizara hii ndio yenye jukumu la kuangalia maendeleo ya watoto. Inakuwaje vituo vya kulelea watoto viko chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii? Pamoja na hayo kitengo cha Wanawake ndio moja kati ya mihimili mikuu ya Wizara hii, na moja kati ya majukumu yake ni kulinda na kutetea haki za Wanawake. Je, inakuwaje Idara ya Ustawi wa Jamii inakuwa Wizara ya Afya? Ilhali ndio yenye mamlaka ya kusaidia Wanawake na watoto wanaopatwa na matatizo baada ya wanandoa kutalakiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza tofauti iliyopo kati ya Idara ya Maendeleo ya Jamii na Idara ya Ustawi wa Jamii? Na utofauti wa kazi zao uko wapi? Mahusiano ya Idara hizo linasababisha Idara husika na watumishi

wake kushidwa kuwajibika kutokana na kushindwa kufanya kazi ipasavyo na hivyo kubakia kutupiana lawama pasipo na kujua hasa mwajibikaji ni nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais anaunda Wizara ya Mifugo na Uvuvi alisema kuwa hivyo vyote ni ‘vitoweo’ yaani nyama na samaki na ndio maana aliunganisha maeneo hayo mawili kuwa chini ya Wizara moja. Inakuwaje majukumu ya Wizara yanayofanana hayawekwi chini ya Wizara moja? Hii inasababisha mikanganyiko isiyokuwa na sababu ya msingi. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inapenda kutoa wito kwa Wizara husika kuachana na usemi wa kuwa Wizara hii ni Wizara mtambuka kwa sababu kama hatutaachana na usemi huu ufanisi utabakia kuwa ni njozi zisizoweza kufikiwa hata kidogo. Hivyo basi, tunaitaka Serikali kuaangalia upya suala zima la muundo wa Wizara husika na kama inawezekana Wizara hii iwe na jukumu moja la kuangalia Maendeleo ya Jamii kwa ujumla na Wizara nyingine yeyote isipewe majukumu hayo hayo tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jinsia, malengo ya kufikia usawa wa Jinsia ni moja kati ya malengo muhimu sana kwa maendeleo ya jamii nzima. Na kwa nafasi ya kipekee napenda kuipongeza Serikali kwa kuweka bayana mkakati wa kufikia 2010 uwakilishi katika ngazi zote za Uongozi utakuwa wa mlingano wa kijinsia. Hili ni jambo jema na linalostahili pongezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kutambua jitihada za Mheshimiwa Rais kuongeza nafasi za Wanawake Bungeni kufuatana na maamuzi mbalimbali ya vyombo vya Kimataifa kama vile uamuzi wa Asilimia 30 wa Wakuu wa Nchi za SADC uliofanyika Blantyre, Malawi. Tanzania kwa kuzingatia uamuzi huo, imeongeza nafasi za Wanawake angalau mara mbili zaidi ya Serikali ya Awamu ya Tatu. Sasa hivi nafasi ya Wanawake Bungeni ni asilimia 30.28%, na lengo ni asilimia 50% katika mwaka 2010 kwa mujibu wa uamuzi wa Wakuu wa Umoja wa Africa (AU). Mgawanyo wa Wabunge Kijinsia Katika Bunge la Mwaka 2000 - 2005 na Bunge la Mwaka 2005 – 2010

<b>Bunge la 2000 – 2005</b>			<b>Bunge la 2005 – 2010</b>			
Jinsia	Jumla	Asilimia	Jinsia	Jumla	Asilimia	
Wanawake	63		21.35%	Wanawake	98	30.81%
Wanaume	232		78.65%	Wanaume	220	68.18%
Jumla	295		100%			
		318	100%			Jumla

Chanzo: [www.parliament.go.tz](http://www.parliament.go.tz) (Tovuti ya Bunge la Tanzania).



Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lengo la 50% haliishii tu Bungeni. Hili napenda kuliweka bayana kwa sababu ili kufikia Dira ya Maendeleo ya 2025 ambayo inaweka lengo la kuwapatia watu wake hali ya juu ya maisha, kufanikiwa katika kupata utawala bora wa kuheshimu sheria pamoja na kuendeleza uchumi imara na wa ushindani. Ili kuleta usawa wa jinsia na kuwapa uwezo wanawake katika maeneo ya jamii, uchumi, uhusiano wa siasa na utamaduni lazima yatiliwe maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokuwa tunamtayarisha mwanamke kwa kumjengea uwezo kusudi aweze kuhamasika na kujenga uwezo wa kusimamia imani yake ili aweze kugombea ni lazima tuwe wazi tunamtayarisha vipi? Ni lazima tuweke wazi ni mchakato gani unaendelea kumuandaa mwanamke huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifarijika sana niliposoma kwenye Vyombo vya Habari kuwa Wizara hii imeunda Tume Maalum itakayosimamia utekelezaji wa mkakati wa kufikia asilimia hamsini ya uwakilishi wa wanawake katika ngazi zote za uongozi wa maamuzi ifikapo 2010. Ama kweli hili lilinifurahisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu wa tume hii kwa maendeleo ya jamii yote kwa ujumla, haikupewa fedha hata kidogo. Hii ni aibu hasa kwa Serikali ambayo imeweka wazi kuboresha maisha ya Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara ilieleze Bunge lako Tukufu ni nini hasa hadidu za rejea za Tume hiyo Maalum, wajumbe wake ni kina nani na wanatashirikisha vipi Wadau wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maalbino. Maalbino ni binadamu kama wengine, hatupaswi kabisa kuwatenga wala kuwanyanyasa kwa njia yoyote. Lakini la kusikitisha, vifo vya maalbino ambao wanakamatwa na kuuawa vimekuwa vikindelea katika maeneo mengi nchini kwa imani ya kishirikina ati kwa kujipatia utajiri hasa kwenye madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano unosikitisha zaidi, hivi karibuni tuu, tarehe kumi mwezi wa saba (10/7/2008) Mkoani Shinyanga, mtoto wa miezi saba aliuawa kwa kukatwa mikono yake yote miwili. Hii inaonyesha dhahiri unyanyasaji unaoendelea katika jamii zetu.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua jitihada za makusudi kukomesha jambo hili kwa sababu tukikusudia tunaweza. Ikiwa mtu binafsi aliweza kufika mpaka kwa mganga wa kienyeji, inakuwaje Serikali kushindwa na isiweze? Ndiyo maana Kambi ya Upinzani kila siku inasema ‘Porojo za kisiasa tu hazijengi, kinachotakiwa ni vitendo. Kwa namna ya pekee Kambi ya Upinzani inapenda kumpongeza kwa dhati kabisa shujaa Vicky Mtetema, wa *BBC* kwa ujasiri wake kwa kufungua macho ya ulimwengu mzima. Kambi ya Upinzani bado inaishangaa Serikali na hasa Polisi na Usalama wa Taifa wanafanya nini kumlinda mtu kama huyu aliyefanya kazi ambaye ilitakiwa kufanywa na Serikali na sasa anaitishiwa maisha yake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanawake. Moja kati ya njia za kihalali za kumsaidia mwanamke ni kuunda sheria ambazo zitamlinda na mila zenye madhara kwa upande huu wa Jinsia. Mwaka jana niliainisha jumla ya mikataba ya Kimataifa 17 ambayo Tanzania imeridhia, na kwa unyenyekevu nikaiomba Serikali iilete hiyo Mikataba Bungeni ili iweze kurithiwa na Bunge na baadae Serikali iwasilishe Bungeni Miswada ili iwe sheria kamili. Sheria hizi zingewasaidia Wanawake kuweza kuwafikisha mahakamani watu wowote ambao watakuwa wamekiuka sheria kwa njia yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya CCM sura ya 104 Ibara ndogo ya (a) inasema: -

*“Kuendelea kupiga vita mila, desturi na sheria zinazowabagua Wanawake pamoja na kuisimamia sheria na Mikataba ya Kimataifa inayohusu haki na ustawi wa Wanawake”.*

Hivi kweli Serikali inakwenda sambamba na yale ambayo yameainishwa katika Ilani ya uchaguzi? Au ilikuwa ni njia ya kuomba msaada na kuwatumia wanawake tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne ndani ya miaka miwili na nusu tuu ameweza kutia sainsi Miswada zaidi ya 26 na hivyo kuwa sheria. Lakini kati ya sheria hizo zinazogusa matatizo yanayowakumba Wanawake hakuna hata moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Mheshimiwa Rais kaisha tuhakikishia kuwa kusaini Miswada iliyokwishapitishwa na Bunge kwa ajili ya kuanza kutumika kama sheria sio tatizo. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge na wanawake wote ni sababu gani za msingi zinazopelekea hadi sasa mikataba hiyo ibakie tu kwenye maandishi bila kuridhiwa na hailetwi Bungeni ili iweze kuwa sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, Watoto. Serikali kwa kushirikana na Shirika la Kazi la Kimataifa (*ILO*) wameweza kuokoa maisha ya watoto 35,000 waliokuwa katika ajira mbaya. Lakini katika Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2007 inaonyesha kuwa bado kuna idadi ya watoto 22,731 ambao walikuwa tayari wameshajiingiza katika ajira hiyo katika Wilaya 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo Kambi ya Upinzani inapenda Mheshimiwa Waziri husika kutoa taarifa sahihi juu ya jinsi gani imejiandaa katika kuweka mchakato wa kusaidia watoto hao ambao bado wanataabika ilhali taarifa juu yao ipo Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana wakati natoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, kwa makusudi kabisa tuliweka kipaumbele kumzungumzia mtoto wa kike, na kiundani tulizungumzia juu ya sheria ambazo zinamnyanyapaa mtoto wa kike.

Niliweka bayana ni kwa kiasi gani sheria zetu zilivyo na mapungufu katika kumlinda mtoto wa kike. Tulidokeza juu ya sheria ya ndoa ya mwaka 1971. Ambayo inaruhusu mtoto wa miaka 15 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaikumbusha Wizara juu ya azma ya Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotusihia tuwaache watoto wa kike wasome. Kambi ya Upinzani ikaishauri Serikali kuwa wakati sasa umefika wa kuangalia tena uwezekano wa kuboresha sheria hiyo. Lakini mpaka leo mambo hayaeleweki yanaendaje je, hiyo ndiyo ari mpya? Inakwenda mbele au inarudi nyuma? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka wizara husika kutoa tamko kama italeti hiyo sheria Bungeni ama la! Kwa maana muda wa kubembelezana umekwisha. Tunataka jibu moja tu ni ndio ama hapana? Na kama ndio mtupe tarehe. Mambo ya kusadikika sasa mwisho kwani hata uvumilivu una mwisho hasa inapohusu haki za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatia fedheha kuona pamoja na kelele nyingi zinazopigwa na wanaharakati wa fani tofauti na jamii kwa ujumla leo Wizara husika kupitia Bunge lako Tukufu linatoa kauli kuwa litapitisha kura za maoni kukusanya fikra za Watanzania wote. Miaka yote tulikuwa wapi leo ndiyo tunakumbuka kukusanya maoni ya wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuikumbusha tu Serikali, mnamo mwaka wa 1992, Serikali ilipotaka kupitisha sheria ya kuwepo kwa vyama vingi ilipitisha kura za maoni. Walio kataa kuwepo mfumo wa vyama vingi vya siasa ni wengi kuliko waliokubali. Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa demokrasia nchini ilikubaliana na mfumo wa vyama vingi ingawaje wengi walikataa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na historia hiyo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tamko moja kama ina nia njema na wasichana wa nchi hii na wanawake wote kwa ujumla. Watafiti wa fani mbali mbali wamebainisha wazi matatizo yanayosababishwa na sheria hii. Ni muda muafaka sasa Serikali ikaweka nia yake bayana katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusubiri kura za maoni, je Serikali ambayo inajisifu kwa kuweka malengo ya kufikia uwiano mlingano kijinsia ifikapo mwaka 2010, kweli itafikiwa iwapo sheria zetu wenyewe zinaendelea kumdidimiza mtoto wa kike. Hivi huku sio kutwaga maji kwenye kinu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kwa nafasi ya kipekee napenda kuongelea tatizo la mimba mashuleni. Mimba kwa watoto imekuwa kama gonjwa la mlipuko. Ongezeko kubwa la hizi mimba inadhihirisha wazi kuwa elimu ya *UKIMWI* kwa vijana wetu pia ni ndogo. Sote tunafahamu kuwa watoto wetu wanarubuniwa kutokana na sababu nyingi sana zikiwemo za kiuchumi na kijinsia. Pamoja na ukweli huo hili ni tatizo letu sote sisi kama wazazi, jambo la kujiuliza ni je, kama mtoto akichafua mkono wa mzazi huwa tunaukata? Kwa muda mrefu tumekuwa tukiweka bayana kuwa

pindi watoto watakapo patikana na mimba wanasimamishwa shule na kurudishwa majumbani mpaka watakapojifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na kuwasimamisha watoto hawa shule kwa muda, nia na madhuminu yalikuwa ni kuzuia watoto wengine wasijiingize kwenye tatizo kama hilo. Lakini tatizo hilo bado linaendelea kuwa kubwa. Tafiti zimeonyesha kuwa ndani ya miaka mitano tu, watoto waliopata mimba mashuleni ni 18,000, na ndani ya mwaka mmoja tu, Mkoa wa Lindi pekee, watoto walipata mimba ni jumla ya 149, na kati ya hao ni 29 ndio waliotoka katika shule za Sekondari waliobakia ni wanafunzi wa shule za msingi. Ni muda muafaka sasa kuruhusu watoto wanaopata mimba waendeleo na shule kwa sababu tafiti zinaonyesha kuwa watoto wakisha simamishwa shule, wengi wao huacha shule na hawarudi tena. Lakini suala hili linazidisha mlingano wa kijinsia katika masuala ya elimu kwa watoto wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuweka Mpango Mkakati kuhakikisha waathirika wa mimba za mashuleni wanapata nafasi ya kumaliza elimu yao ya msingi au Sekondari. Tusiache tu hao ambao wanatuharibia watoto waendeleo kutuharibia watoto na kuangalia watoto wa kike hawaendelei mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sanjari na hilo, pamoja na Serikali kuwa kimya sana siku hizi kuhusiana na tatizo la ukeketaji katika baadhi ya maeneo nchini mwetu. Kambi ya Upinzani inapenda kuitaarifu Serikali kuwa wanaokeketwa siku hizi si wasichana wenye umri mkubwa ni wasichana wadogo na ambao hawawezi kujitetea wala kukimbia, hivyo iboreshe mbinu na kuweka mtandao makini ili kuwabana wahusika wakuu wa ukeketaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoionba Serikali kuongeza bidii mwaka jana, leo tunaomba kuikumbusha kuwa hili tatizo halijaisha bado lipo na linaendelea. Na ile sheria tulivyoionba mwaka jana ambayo ingesaidia kuweka adhabu kali kwa wanaojihusisha na ukeketaji ipo wapi? Maana bila kuileta Bungeni na kupewa baraka zake haya mambo yataendelea kuendeshwa kimzaha mzaha. Wizara husika naomba itoe majibu ya kina hasa kwa kuzingatia ukweli kuwa Idara ya Maendeleo ya mtoto imeomba kuidhinishwa fedha 172, 695,000 kwa ajili ya utetezi na upembuzi wa sera.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hayo tu, bali, moja ya majukumu ya msingi ya Wizara hii ni kupitia mikataba ya kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia na kuandaa mkakati wa kuifikisha Bungeni ili kuridhiwa na kuwa sheria. Mwaka jana niliorodhesha mikataba takriban tisa ambayo inamhusu mtoto, ambayo Tanzania imeridhia lakini bado haijaja kama Miswada ya Kisheria Bungeni. Hivi tatizo ni nini? Je, Tanzania ni kutia saini kutafuta sifa tu mbele za wenzetu ilhali nia zetu ni tofauti? Fedheha hii sio ndogo, mikataba mingine ilitiwa saini toka mwaka 1985 na Serikali haijabadilika, ni ile ile inayoongozwa na CCM. Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara husika kufanya shughuli zake kwa haraka kufikisha kero hizi Bungeni ili kunusuru maisha ya vijana wetu hawa, Malaika wa Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Kwa nafasi ya kipekee kabisa, nataka nigusie suala la Maafisa Maendeleo wa Wilaya. Dhana nzima ya maendeleo ya jamii inalenga kuwawezesha watu kutambua uwezo walionao wa kubaini matatizo na kutumia fursa na rasilimali zilizopo ili kujipatia na kujiongezea kipato, hivyo kujiletea maisha bora. Kazi yote hii inatakiwa kufanywa na Maafisa Maendeleo ambao wanatakiwa kujenga uwezo wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri imeeleza kuwa Tanzania ina jumla ya washauri wa maendeleo ya jamii 14 katika ngazi ya Mikoa ikilinganishwa na mahitaji kamili 21. Katika ngazi ya Wilaya/Miji/Manispaa Tanzania ina wataalamu 967 ikilinganishwa na mahitaji kamili 2,487. Hii inaonyesha kuwa nchi ina upungufu wa wataalamu hawa ambao unazidi aslimia 61. Hali ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mtaalamu ambaye yuko katika ngazi ya Wilaya ndiye aliye na jukumu la kuangalia Wilaya nzima na ndiye aliye katika ngazi ya chini. Hivi huyu mtaalamu anasaidiana na nani kuhakikisha kuwa anaweza kutimiza majukumu yake kwa wakati? Sote tunafahamu ukubwa wa Wilaya zetu na uwingi wa vijiji pamoja na uwingi wa wananchi ambao wanahitaji kujengewa uwezo na mtaalamu huyu. Wala hana usafiri wa aina yoyote anabaki kuwa ombaomba kwa Idara nyingine za Halmashauri.

Kambi ya Upinzani Kwa kuzingatia mzigo mkubwa wa kazi ambayo anavikwa mtaalamu huyu, leo tunataka kupata taarifa sahihi juu ya majukumu ya Maafisa hawa wa Maendeleo katika ngazi ya Wilaya. Ni vyema tukatoa rai kuwa ili kufikia malengo ya kujenga maendeleo kwenye jamii zetu, ni vyema Afisa Maendeleo wa Wilaya awe na wawakilishi katika vijiji. Hii itasaidia kutambua viashiria vya matatizo kabla ya kusubiri yawe matatizo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha uliopita, Kambi ya Upinzani ilitoa rai kuhusiana na vyuo vya maendeleo ya jamii na vyuo vya maendeleo ya wananchi. Katika maoni yale, Kambi ilitanabaisha kuwa, jamii yetu inakua kwa kasi kubwa, inahitaji Vyuo vya Maendeleo vinavyolandana na ongezeko hilo la watu, hivyo jamii yetu inatakiwa iwekeze thabiti kabisa katika vyuo vya elimu ya maendeleo. Kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu nchini ni asilimia 2.9 (*population growth rate*). Hivyo kiwango cha wahitimu kinatakiwa kilandane na idadi ya ongezeko la watu kama kweli tunayo nia ya kujiletea maendeleo yetu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu umuhimu wa vyuo hivi kwa maendeleo ya jamii yetu. Tukiboresha vyuo hivi, ni wazi kuwa tatizo la elimu ndogo linalowapata wataalamu wetu wa Maendeleo ya Jamii na walio wengi litaweza kwisha kwa haraka zaidi. Pindi watumishi hawa watakapoendelezwa ni wazi kuwa ufanisi wao wa kazi utakuwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina vyuo vinne vya maendeleo ya jamii, navyo ni Chuo cha Tengeru, Buhare, Rugemba na Misungwi. Hivi vyuo vilivyotajwa vina kero nyingi kuliko sana. Sote sisi hupiga kelele juu ya mazingira mabovu

wanayosomea wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na vyuo vingine lakini ni wazi kuwa hatufahamu juu ya mazingira ya vyuo hivi vya Maendeleo ya Jamii. Kwa mfano Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rugemba hakina umeme tangu mwaka 1973 na Chuo hiki kiko Wilaya ya Mufindi na hutegemea umeme wa Jenereta ama *Solar*.

Chuo hiki pamoja na umuhimu wake kina *Computer* moja tu huku idadi ya wanafunzi ambao wanasoma somo hilo wakiwa ni 86. Chuo hiki kimekuwa kikitegemea umeme wa Jenereta ambao umekuwa ghali na hivyo kulazimisha uongozi wa Chuo kuwa na utaratibu wa kuzima umeme saa nne usiku na hivyo kuwafanya wanafunzi hawa washindwe kupata muda wa kutosha kwa ajili ya kusoma. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri kutolea kauli hali hii ya kusikitisha ambayo inakikumba Chuo hiki, pia tunaitaka Wizara iwe na mpango madhubuti wa kuwapatia ajira wataalam wa vyuo hivi mara wamalizapo masomo yao ili kuhakikisha kuwa utaalamu wao unatumika kuendeleza maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na uchakavu wa majengo ambao unadhihirika wazi kwani majengo mengine ya vyuo yalijengwa hata kabla ya Uhuru, lakini pamoja na uchakavu huo bado majengo yaliyopo ni finyu sana na hayawatoshi wanafunzi. Kwa mfano, Chuo cha Tengeru kina jumla ya wanafunzi 640 wakati maktaba yake ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 tu. Hii ni asilimia 7.8% ya wanafunzi wote. Hii haitoshi! Bado kuna matatizo ya upungufu wa wakufunzi kwa mfano Chuo cha Tengeru kina wakufunzi 14 ilhali mahitaji ni Wakufunzi 35; Vyuo vya Buhare, Misungwi na Rungemba vina wakufunzi 45 ilhali mahitaji wakufunzi 92.

Kambi ya Upinzani imechoshwa na kero za vyuo hivi. Haiwezekani kila mwaka tuwe tunaitumbuiza Serikali na kelele zetu juu ya jambo hili. Sasa tunataka mkakati wa kusaidia vyuo hivi? Wekeni nyongeza ya mishahara ili ivutie wasomi wengi kuweza kukubali kufundisha ndani ya vyuo hivi. Kwani wanafunzi wanaohitimu shahada ya Uzamini inayotolewa katika taasisi ya maendeleo ya jamii (*masters in development studies*) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni wengi. Wekeni vivutio kuvutia vijana hawa ili kutatua tatizo la wakufunzi. Kwa kufanya hivyo, suala la elimu finyu kwa wakufunzi litakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kuwa vyuo hivi ni urithi tulioachiwa na Mwalimu Nyerere, ambaye alijua umuhimu wa kujitelea maendeleo wenyewe na umuhimu wa kujitegemea. Ni vyema Serikali endelevu yenye kila jitihada ya kuenzi mafunzo ya Mwalimu yakavienzi vyuo hivi ambavyo sasa ni vinyonge kama vifaranga waliokosa mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, pia vyuo hivi hivi vya Maendeleo ya Jamii katika ripoti ya Wizara iliyotolewa Januari, 2007, ukurasa wa sita, sehemu ya 2.2 Vyuo vya Maendeleo ya Jamii inasema, nanukuu: “Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto ina jumla ya vyuo vinne vya Maendeleo ya Jamii ambavyo ni Buhare, Misungwi, Rungemba na Tengeru”

Lakini katika ripoti ya Wizara hii iliyotolewa Juni, 2008 ikionyesha maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa 2008/2009, katika fedha za maendeleo, kifungu 2002 - Maendeleo ya Jamii, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. 723,100,000/= kwa ajili ya kukarabati majengo na miundombinu katika vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii. Hii linatupa taabu Kambi ya Upinzani, kwani ni lini Wizara hii imeongeza vyuo vya Maendeleo ya Jamii? Maana ndani ya mwaka mmoja Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vimeongezeka mara mbili zaidi ikiwa tulivyo navyo viko katika hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kabla sijachangia katika vyuo hivi kwanza napenda nitoe pongezi kwa waendeshaji wa vyuo hivi pamoja na Wizara kwa ujumla kwa kuweza kuongeza idadi kubwa ya wanafunzi katika vyuo hivi vya wananchi kwa muda mchache sana. Hii ni faraja kubwa na inadhihirisha ni kwa kiasi gani wananchi wameamka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia katika vyuo hivi, kwanza napenda nitoe pongezi kwa wanaoendesha vyuo hivi pamoja na Wizara kwa ujumla kwa kuweza kuongeza idadi kubwa ya wanafunzi katika vyuo hivi. Wizara hii ina Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi jumla 58 ambavyo vimeenea kila Mkoa Tanzania Bara. Vyuo hivi vinatoa elimu na stadi za kuwajengea uwezo wananchi wa kuweza kujiajiri, kujitegemea na kujiletea maendeleo yao na ya Taifa kwa ujumla. Hivyo ni vyuo muhimu sana kwa maendeleo ya jamii yote kwa ujumla. Lakini pamoja na umuhimu wake, matatizo yanayovipata vyuo hivi hayatofautiani sana na vile vya Maendeleo ya Jamii kwani kero ni zile zile ambazo ni :-

- (a) Uchakavu wa majengo na miundombinu;
- (b) Uhaba wa wakufunzi na watumishi wa kada zingine;
- (c) Ukosefu wa umeme wa uhakika na vyanzo vya maji;
- (d) Kiwango kidogo cha elimu kwa watumishi walio wengi;
- (e) Ukosefu wa vitendea kazi ; na
- (f) Uhaba wa nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na kero zote hizo, Wizara husika katika bajeti ya mwaka huu imeomba kuindhinishiwa fedha kwa ajili ya kuboresha majengo ya vyuo hivyo tu. Hili ni zuri, nasi tunakubaliana nalo. Lakini kwa kutambua ongezeko kubwa la wanafunzi katika vyuo hivi: Je, matatizo mengine kama vile uhaba wa wakufunzi utakwisha lini? Kwa maana hata kama wana majengo mazuri, lakini kama hawana walimu maana yake hakuna vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa pendekezo kuwa, kwa kuwa nia ya Serikali ni kuboresha vyuo hivi, ni bora sasa Wizara husika kutoa taarifa sahihi juu ya mipango madhubuti iliyowekwa na Wizara kutatua matatizo ya

Vyuo, hasa kwa kuzingatia kuwa hivi ni vyuo tunavyotegemea kutoa elimu ya uraia kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto yatima katika nafasi kubwa wanalelewa katika asasi zisizo za kiserikali, yaani *Non Governmental Organisations (NGO's)*. Asasi hizi zimeundwa kwa mujibu wa Sheria Na. 24 ya mwaka 2002. Asasi hizi zote zimesajiliwa na Msajili wa Asasi hizi chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za mwaka wa 2007 zinaonyesha kwamba hadi Desemba, 2007, asasi zisizo za kiserikali zilizosajiliwa zilikuwa ni 2,165. Kati ya hizo zilizopata vyeti vya usajili ni asasi 1,659 ikiwa 99 ni katika ngazi za kimataifa, 919 kitaifa, 243 kimkoa na 398 kiwilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ugonjwa wa Ukimwi katika nchi yetu ni moja ya vyanzo vikubwa vya ongezeko la tatizo la watoto yatima nchini. Lakini ni wazi kuwa hilo sio sababu pekee, bado kuna maradhi mengine kama vifo vya akina mama wakati wa kujifungua (*maternal mortality*) ambao sasa limekuwa sugu kwa sababu takwimu zinaonyesha kuwa katika kila wakinamama 100,000, kati yao 578 hufa wakati wa kujifungua. Wazazi wengi wanafariki kutokana na sababu zinazotofautiana hasa ukizingatia ugumu wa maisha ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, tumeshuhudia watoto wakigoma katika siku za hivi karibuni, tumeshuhudia watoto wakigoma katika vituo vyao vya kulelea yatima na kutuhumu uongozi wa vituo hivyo kwa ubadhirifu wa michango na zawadi ambazo zinazotolewa kwa lengo la kusaidia watoto hawa. Hili ni suala ambalo Wizara hii inatakiwa kutolea tamko kwani asasi zote ziko chini ya Wizara hii. Kama lengo la asasi linakuwa tofauti na matarajio, ni wazi kuwa Wizara husika hutakiwa kuchukua hatua. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu: Je, Wizara imefanya nini mpaka sasa katika kunusuru misaada inayotolewa na wazalendo kwenda kwa watoto hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, Kambi ya Upinzani, ilishtushwa na tamko la Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ambaye alitaarifu wananchi kuwa msimamo wa Serikali wa sasa ni kutaka kuviondoa vituo vya kulelea watoto yatima na badala yake itahakikisha yatima hao wanalelewa katika mazingira ya kifamilia kama ilivyo kwa watoto wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukatai kuwa nia ya Serikali ni njema, lakini itakuwaje? Kwani ni kwenye familia hizo hizo watoto hukimbia kutokana na manyanyaso na kunyang'anywa mali zinazoachwa na Marehemu wazazi wao. Kambi ya Upinzani inapenda kuhoji kuwa hatma ya watoto hawa itakuwaje, kama watarudishwa walikokimbia na kurudishwa kwa waliowatesa. Kama jukumu la asasi hizi liko chini ya Wizara hii na si Afya na Ustawi wa Jamii: Je, Waziri huyo anawezaje kutoa msimamo wa Serikali juu ya kufuta asasi ambazo zimeundwa kwa mujibu wa sheria, ambazo pamoja na mapungufu yake bado zina faida kubwa zaidi katika kusaidia watoto hawa. Kambi ya Upinzani inaonelea ni bora kuongezea nguvu katika vituo vilivyopo pamoja na kutupia macho mara kwa mara ili watoto hawa waweze kupata haki zao za msingi. Kwani kwa



utaratibu mzazi anaposhidwa kutoa malezi kwa watoto anayechukua jukumu hilo ni Serikali. Watoto ni Taifa la baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kumaliza naomba kuikumbusha Serikali kuwa maisha bora kwa Mtanzania hayawezi kufikiwa kwa kuvumilia shida, bali ni kwa uwekezaji thabiti katika maendeleo ya jamii kwa ujumla. Hivyo tuache sasa maneno na matendo yatawale zaidi na Bunge lako Tukufu liwe makini katika kusimamia utendaji kazi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naomba nikushukuru sana kwa mawasilisho hayo. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema, kuanzia jana hii ni Wizara ambayo tunaijadili kwa siku moja tu. Walioomba kuchangia hapa wanapata karibu 20 hivi. Kwa hiyo basi, asubuhi hapa tutakuwa na wachangiaji watatu tu. Mchana tukirudi tutakuwa na wachangiaji wanne tu, kusudi saa 12.00 aanze kutoa Naibu Waziri na Waziri mwenyewe atakuwa na dakika 75. Kwa hiyo, Kamati ya Matumizi itakuwa ni saa moja tu.

Sasa kwa sababu mnazungumzia habari ya *fifty fifty* waliojaza hapa ni akinamama tu. Sasa watakochangia basi ni Mheshimiwa Switi, atafuata Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare, atafuata Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa asubuhi hii. Tukirudi mchana atakuwa Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Haroub Masoud, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Bujiku Sakila, ndio wanaotosha. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Switi.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote napende kusema kwamba naunga mkono hoja, lakini pamoja na kuunga mkono hoja, ninayo yafuatayo ya kusema kwamba maendeleo sio ya vitu, ni ya watu na maendeleo yanaletwa na wananchi wenyewe kwa kufanya kazi. Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni mtambuka kama ilivyosemwa. Ni mtambuka kwa sababu inaingia katika kila Wizara kwa namna fulani. Tunapozungumza maendeleo ya watoto tunazungumzia malezi, sio tiba na masuala mengine na hatuzungumzii elimu lakini tunazungumzia malezi kwa ujumla kwamba wanapashwa kupata elimu, wanapashwa kutibiwa na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote pia naipongeza Serikali kwa sababu inaonekana kwamba sasa tunakwenda kwenye mtindo wa kujitegemea katika bajeti kwa sababu, naomba ninukuu: “Mwaka huu nchi za nje zinatusaidia tu Sh. 1,921,500,000/= na bajeti nyingine yote tunajitegemea.” Lakini niseme tu kwamba shilingi bilioni 14.6 kwa Wizara hii ni fedha ndogo sana kwa sababu Wizara hii ukiwaangalia watendaji wake huko kijijini hawana hata baiskeli ya kufikishwa yale wanayopashwa kufikishwa kwa wananchi. Kwa hiyo basi, hawa watu hawafikishi ile dhana ya kazi yao kwa wananchi ili kuleta maendeleo.

Lakini pia niseme kwamba kipaumbele cha Wizara hii cha kuweka *desk* la jinsia ni cha muhimu sana, kwa sababu masuala ya jinsia yamekuwa hayaeleweki eleweki, hakuna mtu anayeshughulikia hasa, lakini kwa kuweka *desk* la jinsia, ina maana masuala haya yatashughulikiwa kuanzia juu mpaka vijijini. Niseme tu kwamba Wizara hii ina changamoto nyingi. Changamoto ya kwanza ni chekechea. Tunasema kwamba watoto wetu hawana maadili, lakini tunasahau kwamba hawa watoto kuanzia umri *zero* mpaka miaka mitano hata hawaeleweki wanatunzwaje.

Katika nchi nyingine chekechea ni muhimu, Serikali inathibitisha kwamba kuna chekechea ili akinamama na akinababa wanapokwenda kufanya kazi watoto wawe na mahali wanapolelewa, wanakula, wanafundishwa wanapewa maadili mema. Lakini watoto wetu mtu akitaka kwenda kazini anamkabidhi jirani au anawakabidhi watoto wenzake kulea watoto wenzake. Hii haiwezekani, naiomba Serikali iangalie umuhimu huu wa kuwa na chekechea ambazo zitatumza watoto wa aina zote.

Sio hilo tu. Dawati hili litatusaidia sisi wanawake na wanaume pia kupunguza umaskini kwa sababu kama alivyoelezea Mheshimiwa Waziri ni kwamba watashughulikia masuala ya umaskini na umaskini sio wanawake wala wanaume peke yao. Zamani hizo tulikuwa na majumba ya maendeleo ambayo yalitusaidia sana katika kuleta maendeleo ya wananchi na haswa kwa akina mama, masuala ya mapishi, masuala ya kutengeneza nguo na kadhalika. Leo akinamama wengi hasa vijijini hawawezi kufanya kazi hizo maana hawana ujuzi, wameamua tu kulima, lakini kama wangukuwa na majumba ya maendeleo wangukwenda kujifunza masuala hayo na kuweza kujitea maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Maendeleo nchini humu kwa kweli vina hali mbaya sana. Tunaposema eti tunavikarabati, hatuvikarabati inavyostahili. Vinapashwa kukarabatiwa katika mfumo wa kuleta maendeleo ya kisasa, sio kuvipaka tu rangi au kuvipiga ripu au kutengeneza vitu vingine ili vionekane vipo. Vinapashwa kuwa na vifaa vya kisasa ambavyo kweli vitaleta maendeleo kwa wananchi. Kwa hiyo basi, hii bilioni 14.6 ikitawanywa kwenye vyuo vyote vya nchi hii na pamoja na mishahara na kazi nyingine iliyoipangiwa Wizara kwa kweli haitoshi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimba za utotoni imekuwa ni tatizo kubwa katika nchi hii. Ili kuleta usawa, kama tulivyoongelea katika bajeti nyingi haiwezekani kabisa kama watoto wa kike watakuwa hawaendi darasani, wanapata mimba hiyo *fifty fifty* tunayoongelea haitafika hata siku moja. Kwa sababu watakuwa wakifikia umri wa miaka 15 wana mimba na kama mlivyoona wengi wanaopewa mimba ni wale ambao wako eti *Primary* hawa akina baba wanaowapa watoto wa *Primary* mimba wana maana kwamba sisi wanawake tuwe ni ndoto ya kupata maendeleo na sisi tunahitaji kupata uwakilishi wa hamsini kwa hamsini katika kila nafasi ya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifo vya wanawake na watoto vimekithiri. Watu wengine watafikiri kwamba tunapoongelea hivi, tunapashwa kupeleka kwenye Wizara ya Afya? Hapana, haya ni maisha ya mtu na maisha ya mtu ni wajibu wa Wizara hii kwamba tunaendelea kuishi, licha ya kuishi, tunapaswa kuishi vizuri na kuifanya

Tanzania yetu iwe ni mahali pema pa kuishi. Kumbe basi vifo vya wanawake vinatokana na wanawake wenyewe, kwanza kutokufahamu wajiweke katika hali gani wakiwa wajawazito ili wanapofika hospitali Madaktari wasiwe na kazi kubwa ya kukuta mwanamke huyu hayupo katika afya nzuri ya kuweza kujifungua salama. Hivyo basi, Wizara hii ina wajibu kabisa wa kutoa elimu kwa wanawake kwa jinsi gani ya kula chakula bora na hatimaye kuwa tayari kwenda kujifungua salama na kuhakikisha kwamba watoto wanazaliwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendea kazi vya Wizara navyo pia havitoshi. Ukiangalia jengo lenyewe la Wizara linatisha, halionyeshi kwamba hii ndiyo Wizara mtambuka inayopashwa kuleta maendeleo kwa Watanzania. Naiomba Serikali iangalie upya bajeti ya Wizara hii ili angalau jengo lile lionyeshe hadhi ya Wizara moja ambayo inapashwa kuwahudumia Watanzania wote bila ya kubagua. Pia wafanyakazi wao waweze kupata vitendea kazi wawafikie wananchi wote na kufikisha yale yaliyopashwa kuwafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji ya maalbino na wakongwe imekuwa ni tishio, imefikia mahali ambapo mtoto anakatwa mikono miwili au miguu au mtu mzima anavamiwa akiwa anasafiri. Mtu anasimamisha gari anam-*hijack Albino* anampeleka anakojua eti kwenda kujipatia utajiri. Hii yote ni ukosefu wa elimu. Wizara hii inapashwa kuhakikisha kwamba watu wanafikiwa kuambiwa kwamba albino au vikongwe ni watu kama watu wengine, hawana kitu chochote tofauti na mimi Switi au na mtu mwingine yoyote. Hii elimu bado haijafikia jamii ndiyo maana wanafanya wafanyayo na Wizara bila kupata fedha ya kutosha itashindwa kuifikia jamii na kufikisha ujumbe huu ili tuweze kuondokana na fikra potofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Hapa nchini ukatili huu kwa kweli unatisha na kuanzia hasa na ukeketaji. Ukeketaji ni mila potofu inayotumika kwa watu wengi hapa Tanzania hasa tukitaja Mara. Tunayo Sheria ya Kuzuia Ukeketaji ya mwaka 1998 lakini hii haijafikishwa kwa wananchi inavyostahili. Kumbe bila Wizara kupewa fedha za kutosha itashindwa kabisa kwenda kufikisha mambo haya kwa wananchi wake kwa sababu fedha hazitoshi. Lakini pia sababu hizi za watu kutokujua wafanye nini inawasababisha wafikiri kwamba kukeketwa kwa mwanamke basi ndio aolewe kwa kuwa amekeketwa kwa sababu sasa anapunguza masuala yake ya ndoa. Sio kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, umaskini wa wanawake hauwezi kuondokana bila ya kupewa elimu ya kutosha. Hivyo basi, Wizara inapashwa kuhakikishwa kwamba wanawake wanapewa mikopo kama ilivyoeleza katika usemi wake wa Wizara lakini pia Benki ya Wanawake ambayo imetajwa hapa kama ikiweza kuwezesha itatuwezesha sisi wanawake wote kuondokana na umaskini na pia itatuwezesha sisi kuwa katika nafasi zile ambazo tunastahili kufanya kazi kwa sababu tuna uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la Ofisi ya Wizara nalo ni lingine. Ukiangalia Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii ofisi yake haifanani kabisa na jengo la Wizara

ambayo inapashwa kuwahudumia wananchi wote wa nchi hii. Kwa hiyo, ninaomba sana Wizara hii ipewe nguvu ya kutosha ili ilingane na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizingumzie Chuo cha Maendeleo ya Jamii. Chuo kile kwa kweli tangu nianze kukiona hakina maendeleo makubwa. Ninaomba sana Serikali iongeze nguvu katika kukiboresha kile Chuo cha Maendeleo Chala, kifananefanane na vyo vyingine nilivyokwisha viona Tanzania hii. Kwa kumalizia, ninaomba sana Serikali iongeze nguvu katika elimu ya wanawake ili waweze kuingia katika nafasi mbalimbali za maendeleo na kuingia katika nafasi mbalimbali za maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MCHUNGAJI DR. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi ya kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuingia Bungeni. Sifa na Utukufu zimrudie yeye. Amen.

Naomba tena nichukue nafasi nyingine nikishukuru Chama changu cha CCM kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuwakilisha Watanzania wenzangu hasa wanawake katika Bunge lako Tukufu. Naomba pia nitoe heshima kubwa kwa Jumuiya yangu ya *UWT* kwa kuweza kunipendekeza kuanzia Morogoro mpaka Taifa mpaka nikaweza kupata nafasi niliyonayo. Mungu awabariki kwa upendo wao.

Mwisho kabisa, niishukuru familia yangu, Kanisa langu, marafiki walioniombea, walionitia moyo mpaka nimeweza kusimama katika Bunge lako Tukufu. Wengi wamekuwa wakisema: “Mama Mchungaji, mbona wewe umekuwa ukisema katikati ya umati wa watu wengi, lakini Bungeni husemi? Nikawaambia najifunza, hakuna haraka. Waswahili wanasema haraka haraka haina baraka. Leo nimeamua kuchangia kwenye Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Wizara ambayo ninaiona ni Wizara nyeti, Wizara ambayo wote tunatoka katika Wizara hii akina mama, watoto wote tunatoka katika Wizara hii. Kwa hiyo, ni Wizara muhimu ambayo inatoa msingi au chachu ya maendeleo yetu kuanzia familia, kaya, kijiji na hata katika Taifa zima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii pia kwa heshima kubwa imeweza kututolea Katibu Mkuu Msaidizi wa *UN*, Dr. Asha-Rose Migiro, tunajivunia, tunafurahi na sisi tunajisikia Watanzania tumo. Wataalamu wa ulimwengu wameweka siku tatu maalum kwa ajili ya kuisitiza majukumu ya Wizara hii. Kuna tarehe 8 Machi, ambayo ni Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani, siku hii imewekwa ili kuimarisha, kuweka malengo makali, kudhibiti unyanyasaji wa wanawake na vile vile kuwaenzi akinamama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nimekwenda kwenye sherehe ya nchi fulani nikakuta kwamba wanaume, viongozi wa Serikali, viongozi wa Makampuni wamekwenda kuwaenzi akinamama, wakiwatia moyo na kuwa-*appreciate* kwa kazi nzuri ambazo akinamama wanafanya. Hakika kabisa hakuna asiyejua kazi ya mwanamke!

Mahali pale waliosha masufuria mengi wakayatandaza uwanjani wakasema mwanamke huyu; je, kama angeosha sufuria zote alizopikia akatandaza, hakika zingefika Dar es Salaam. Nguo alizofua tangu labda pengine aolewe au tangu awe mtu mzima

mpaka akiwa umri wa sasa hivi, nguo hizi zinaweza kufika Bukoba kamba yake. Kwa sababu hakika wanawake ni madaktari, wanawake ni madobi wanawake ni wapishi, wanawake wanafanya kazi bila ya malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ungekula kwa mama ntilie au mama lische lazima ungelipa. Lakini mama huyu hakudai hela. Siku zote anapika kwa furaha akihakikisha familia yake iko salama. Hivyo basi, nilikuwa nimeona katika siku hii, Siku ya Kimataifa ya Wanawake tumeipuuza kidogo hata sisi wenyewe, kwa sababu ukienda unakuta ni watoto na akinamama wana mabango na *T-shirt*. Tunaishia *T-shirt* na mabango, lakini ukweli ingetakiwa hata viongozi wetu wa Serikali wote wanaume na wanawake waje ili waweze kuwaenzi akinamama. Tutunge sheria kali za kusimamia haki za wanawake, wengi wamekuwa wakisema hawa bwana mnadanganyana, mnakwenda Beijing hatuendi Beijing hii ni siku imeteuliwa Kimataifa. Kwa hiyo, na sisi tupewe pongezi kama wenzetu wanavyopewa pongezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna siku ya tarehe 15 Mei, siku hii pia ni ya Kimataifa ya Familia Ulimwenguni. Ni siku muhimu sana lakini wengi hatuelewi umuhimu wake au hatuitili maanani na mimi nilikuwa nasema, jamani tuangalie hizi siku tatu ambazo zimeteuliwa kwa mtazamo wa tofauti. Mnajua kwamba familia ndio chimbuko la kila maendeleo, familia ndiko anakotoka baba, mama na hata watoto. Kama familia itasimamiwa, itasaidiwa, hakika kabisa tutakuwa na Watanzania bora. Lakini Siku ya familia, wengi hata hawaifahamu, hata Mkanisa mengi hawawezi kusema habari ya Siku ya Akina mama. Lakini nilikwenda kwenye Kanisa fulani Marekani, niliona siku hiyo hakika ilikuwa ni siku ya shamrashamra, siku kubwa zaidi ya *X-mas*. Kwa sababu familia ni msingi mkubwa wa kila Taifa, tukizisimamia ndoa, tukikemea mambo ya talaka zisizokuwa na msingi hakika hatutakuwa na watoto wengi wa mitaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena niweke ushauri wangu pamoja na mengi lakini nisisahau kutoa ushauri wangu kabla sijamalizia. Nilikuwa natoa ushauri ufuatao.

Moja, siku hii ya familia duniani iwe siku ya kuweka malengo ya kupunguza watoto wa mitaani, kwa maana chimbuko la watoto wa mitaani ni familia mbovu na misingi mibaya. Talaka zikiingia, watoto wanakuwa hawana malezi bora, wanajikuta wako mitaani. Kuachana kusikokuwa na sababu kuna sababisha watoto wengi wa mitaani. Ndoa zisizokuwa na uaminifu zinaleta watoto wengi wa mitaani kwa sababu wazazi wanakufa na UKIMWI mwisho unakuta watoto hawana matunzo. Hivyo basi, ninaomba kwa pamoja tuweze sio kuachia Wizara tu lakini kwa pamoja tuweze kabisa kuweka malengo na sheria ambazo zitaweza kudhibiti mambo kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ningesema kwamba ingekuwa vizuri tushirikishe dini na madhehebu mbalimbali ili waweze kutokomeza mila potofu, desturi zenye madhara na mambo kama hayo kwa mfano, uchawi. Dini zikikemea uchawi, hakika kabisa kutakuwa na ahueni. Ushirikina umekithiri kila mahali mitaani! Kama tutakemea sisi watu wa dini, hakika Watanzania watapata elimu na vilevile itapungua. Ni aibu kuona *Al-Jazira* anatangaza Tanzania eti wachawi wanapata pesa kwa njia ya uchawi, au unasikia *BBC* wanatangaza habari zetu mbaya, ni aibu! Kwa pamoja tuchukie na kukemea. Nchi yetu ijulikane kwa mambo mengine lakini sio kwa mambo mabaya.

Unamuua mwanadamu mwenzio ili eti upate utajiri! Kwanini usifanye kazi kwa bidii? Kwanini usisome ukaelewa ili uweze kufanya kwa ufasaha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa tatu, ningesema tuweke mkazo katika mipango mizuri ya Wizara ya kumwezesha mwanamke kiuchumi. Ukimwezesha mwanamke kiuchumi tuna uhakika kwamba watoto watasoma, chakula kitakuwepo mezani kwa sababu wanawake ni waaminifu. Hivyo hii michango ya kutunisha hiyo Benki ya wanawake hata wanaume mnunue hisa, sio kuwaachia wanawake tu. Wanaume wengi wakisikia mambo ya wanawake wanadharau. Lakini kumbuka ya kwamba kila nyuma ya mwanamme aliyefaulu yupo mwanamke na wanawake ndiyo sisi. Hivyo mtuchangie na kututia moyo kwa kutusaidia. Tumieni ujuzi wenu ili na hii Benki iweze kufanikiwa kama zilivyofanikiwa *CRDB* au *NMB*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisafiri kwenda Ghana, nilipokwenda Ghana na kikundi cha wanawake wafanyabiashara, mahali pale tuliona yule Rais Rawlings wakati wake alivyowawezesha wanawake. Mtaa mzima ukienda unaambiwa huu Mtaa na maghorofa haya ni ya wanawake. Tukaenda kwenye vituo vya mabasi yanayokwenda Mikoani na sehemu mbalimbali. Unaambiwa unaona haya mabasi 20, ni ya akina mama. Haya mabasi matano ni ya mwanamke fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasi tukahamasika, tukaja Tanzania na kuwa na moyo wa kuweza kuanzisha biashara mbalimbali. Ninasema pamoja na kwamba hayo mengi yote yanafanywa ya kuwawezesha kuwa na Benki na nini lakini, pia waende nje, tuwapeleke wanawake wa kitanzania wakajifunze kwa kuona. Kwa njia hiyo na wao wakirudi watakuwa na wivu mtakatifu, watataka kujiendeleza.

Suala lingine ni ile siku ya watoto. Nilikuwa nawaza na kusema kwamba siku zote ya kwamba watoto wetu tumewapuza mara nyingi, lakini kama kwa pamoja tungeweza kupata haki zao, hata zile za kusikilizwa; mara nyingi hatuwasilizi watoto. “Toka nje! Nenda kacheze!” Ukiwa na wageni ndiyo kabisa! Atalala sakafuni, wageni wako walale kwenye kitanda. Hili sio vizuri. Hatuwatendei haki watoto wetu. Unaweza ukamwuliza mume wako: “Mume wangu, leo utakula nini?” Lakini watoto hawaulizwi leo mtakula nini! Kama ni maharage, mbele kwa mbele. Watoto pia wana vitu vya kula aina fulani wanavyopendelea. Tukiwauliza na wao watajisikia hakika ni sehemu ya familia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wanaotelekezwa, watoto wanaoachwa kwamba mimi simtaki huyu simjui. Kama inathibitika kwamba huyu ndiye aliyempa mimba, huyu mama na mtoto huyu kweli ana damu yake, huyu baba ashitakiwe na amtunze mtoto. Kwanini alimzaa? Kwa sababu sio sahihi umuache mtoto anakaa Mtaani na wewe mwenyewe unakula vizuri eti kwa sababu ulimzaa nje ya ndoa. Tuangalie hata watoto wetu walioko nje ya ndoa. Wapewe haki sawa sawa na wale ambao wako ndani ya ndoa zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria za Ndoa zimekuwa za siku nyingi. Tunaomba basi hizo Sheria mpya ziletwe mara moja Bungeni ili tuweze kuzipitisha tuwe na sheria

mpya ambayo itamlinda mwanamke na mtoto, ama sivyo tunawaachiw watu wanaendelea kufanya uhalifu na kunyanyasa na kutesa wengine. Lakini mimi ninasisitiza tu kwamba hizi siku tatu za muhimu sana katika Wizara hii, lakini ziwe muhimu sana kwa Taifa letu kwa maana ni siku ambazo zinathibitisha au zinasisitiza malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kama hiyo *made speech* ni *speech* kweli! Kwa hiyo, ninamwita Mheshimiwa Jenista Mhagama na nitakuwa na dakika chache kwa mtu atakayefuata kama hatajali nitamwita. Mheshimiwa Mhagama karibu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nichukue nafasi hii na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Lakini niichukue nafasi hii niipongeze siku yenyewe ya leo ilivyokaa kwa sababu kikao kimeongozwa na wewe mwanamke, Waziri mwanamke, Naibu Waziri mwanamke, Katibu Mkuu wa Wizara hii, ni mwanamke sasa Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Haroub Masoud walipoomba kuchangia mada hii, nimejisikia faraja kubwa sana kwamba kwa kweli wanaume wanatupa *support* katika shughuli zetu kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi pia nimpongeze Mheshimiwa Mchangaji Getrude Rwakatale, kwa kweli leo ni mara yake ya kwanza kuchangia humu ndani, lakini amechangia mchango mzuri sana. Niseme yafuatayo: Kwanza, nichukue nafasi ya pekee kumpongeza sana Mama Margaret Sitta na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mawaziri hawa mimi labda ni-*declare interest* yangu kama Mwenyekiti wa Kamati hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; kwa kweli toka wameingia katika Wizara hii wameanza na Mkakati ule ambao tunafikiri utupeleke kwenye hii dhana maalum ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nisipowapongeza na timu yake ya wataalam nitakuwa sijawatendea haki kwa kweli. Naomba wachukue pongezi hizi kwa Niaba yangu mimi mwenyewe, wananchi wa Jimbo la Peramiho na Wajumbe wa Kamati nzima. Ninachotaka kusema ni nini? Mara nyingi na mara zote watu wengi wamekuwa wakidhani hii ni Wizara ambayo kwa kweli haina uzito katika suala zima la kujenga maendeleo halisi katika nchi yetu ya Tanzania. Sitaki kurudia, lakini nasema, haya yanajionyesha katika mlolongo wa majukumu yenyewe ya kila siku. Bajeti kidogo, yaani mambo mengi ambayo ukienda Wizara ya Fedha unaona kabisa wanapopanga vipaumbele vya Bajeti hii watapunguza na hatimaye kila siku Bajeti inaishia: Kwa mfano bajeti ya maendeleo itaishia kukarabati tu vyuo vyetu vya Maendeleo ya Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Jamii na kadha wa kadha.

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba msingi wa maisha wa binadamu yoyote utaanza kwenye familia, utakuja kwenye suala zima la mahusiano katika ya mwanamke na mwanaume na utakuja kwenye wazo zima la watoto. Watoto hawatapatikana bila familia kwa maana ya baba na mama. Lakini baba na mama pia wasipokuwa na mahusiano bora hakuna maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema kwamba suala la maendeleo katika nchi hii kupitia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii ni suala la kimsingi ingawa Wizara hii imekuwa ikiingiliana kwa kiasi kikubwa na Sekta mbalimbali. Mfano, mwaka jana wakati tunapitisha bajeti ya Maendeleo ya Serikali yetu, Wizara ya Elimu kwenye suala la kuimarisha *Vocational Education and Training* katika nchi yetu, Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara hiyo fedha ya ndani ilitengwa shilingi milioni 590, lakini fedha ya nje kwenye Wizara hiyo hiyo ilitenga shilingi bilioni 18. Wizara ya Maendeleo ya Jamii katika kipengele kinachohusiana na vyuo hivyo hivyo ambavyo vinatoa *study* na *skills* mbalimbali kwa wananchi na hasa kule vijijini ambako dhana ya maendeleo inaanzia.

Fedha ya ndani ilitengwa shilingi milioni 799 lakini fedha ya nje haikutengwa fedha hata senti tano. Sasa kwa mwaka huu Wizara ya Elimu, fedha ya ndani imetengwa shilingi milioni 590 na fedha za nje imetengwa shilingi bilioni saba kwenye kifungu cha *VETA* na Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii ambayo ina vyuo muhimu sana katika kuleta Maendeleo ya Jamii na hasa vijijini kule ambako vipo imetengwa shilingi bilioni mbili tu. Shilingi bilioni mbili kati ya shilingi bilioni saba na shilingi milioni 590 kwa Wizara ya Elimu na Bajeti ya mwaka jana; kila siku tunaposema maendeleo ya nchi ya Tanzania uchangiaji mkubwa wa pato la Taifa kwa takribani asilimia 80 zinatokana na wavuja jasho ambao wako vijijini. Wanahitaji elimu, wanahitaji kuboreshewa zana zao, wanahitaji kuwekewa mazingira muafaka kabisa ya kuwaletea maendeleo. Lakini nani ambaye angaweza kufanya kazi hii vizuri kama sio Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani iko haja ya kubadilisha mwelekeo na kuangalia umuhimu. Kipindi cha nyuma Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Maafisa wake katika maeneo tuliyokuwa tunaishi walikuwa wana heshima kubwa sana. Ukikutana na Afisa Maendeleo ya Jamii akikueleza kitu, unaamini kabisa hiki ndicho chenyewe hasa kitakachokupeleka kwenye mafanikio. Lakini Maafisa Maendeleo ya Jamii sasa hivi kwanza hawapo, ni wachache na hivyo kule vijijini suala zima la maendeleo, elimu sahihi ya maendeleo haipo na mtu wa kusimamia suala hilo la maendeleo kule vijijini pia hayupo, ni kwa sababu Wizara hii inaitwa tu ni Wazira ambayo ni mtambuka na mambo mengi yanafanyiwa kazi na Wizara nyingine na hii ni Wizara ya wanawake.

Suala la jinsia ni mahusiano kati ya mwanamke na mwanaume na sio mwanamke peke yake. Kwa hiyo, lazima tubadilishe mtazamo na mimi nafikiri hebu kwanza ibadilishe. Ikiwezekana Waziri ikiwa mwanamke, Naibu Waziri awe mwanaume labda tutapata uelekeo ulio sahihi. Katibu Mkuu awekwe mwanaume. Tunapozungumza suala la jinsia ni mahusiano kati ya mwanamke na mwanaume na mahusiano haya hayatajengwa kwa mtazamo finyu ambao unaendelea kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza hapa kila siku kwamba wanawake wananyanyasika vijijini, ndio wanaolima, ndio wanaotunza watoto, Mama Rwakatale amesema mambo mazito sana hapa. Lakini Wizara hii kwenye *development budget* hawa wangeongezewa fedha, wakatengeneza zana za teknolojia rahisi za kumsaidia mwanamke



kufanya kazi kule vijijini. Wanaume wangeshirikiana na wanawake *automatically* katika kuleta maendeleo.

Kwa mfano, hivi kweli kama kweli kungetengenezwa jembe la kukokotwa na ng'ombe kukatengenezwa labda toroli la kubebea kuni akapewa mama kwenye familia, nakwambia baba angejisikia fahari sana kuburuza lile toroli na hapo angekuwa amemsaidia mwanamke kubeba kuni. Lakini kwa sababu tunaona haya mambo ni jinsia ni wanawake tu, kwa hiyo, hakuna mtu anayeguswa na kuona kwamba uko msingi madhubuti ya kufanya Wizara hii ipate nguvu. Yupo mtu aliniambia leo akasema, sasa kama hii Wizara masuala yake na inaonekana imebakiwa na kazi ya kutunga sera ikiingia kwenye afya Mheshimiwa Dr. Kigoda jirani yangu hapa karibu atashughulikia afya lakini sera itatungwa na Wizara hii ya wanawake kama ni ya watoto au akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nafikiri ipo haja ya kugawanya haya madaraka ipasavyo. Leo tunalalamika hapa kwamba wanawake wengi wanakufa wakati wa kujifungua, lakini kwa sababu anakufa mwanamke mmoja mmoja, hakuna anayeelewa tatizo hili ukubwa wake ni kiasi gani. Kama wangukuwa wanakufa wanawake 100 kwa siku, basi kila mtu angeshtuka na angesema hapa pana tatizo la kufanyiwa kazi. Bajeti zetu kwenye hizo sekta ambazo sera zinatungwa na Wizara hii na kutekelezwa na Wizara nyingine utakuta kwamba Bajeti zile ni kweli zinaonyesha picha ya kusaidia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya mwanamke na watoto. Lakini ukichambua huduma moja baada ya nyingine na ukaangalia hivi bajeti ile inalenga kwa kiasi gani usawa wa kijinsia, utakuta kwamba bado kwa kweli tunahitajika kufanya kazi ya kutosha.

Nampongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika suala la wanawake, suala la usawa wa kijinsia, amekuwa ni Kamanda imara akiongoza mapambano haya kwenda mbele. Hiyo sisi wanawake tunamshukuru, tunaamini hata ajenda hii ya 50/50 anaisimamia. Lakini tunahitaji *support*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha ione umuhimu, wadau wengine wote waone umuhimu, viko vyama vingi vinasema kila siku na kutoa maelekezo lakini kwa kweli inanisitika sana kuona kwamba mkakati mzima wa kuweza kuipa nguvu bado hauko imara. Kwa kweli mimi naamini kabisa Wizara hii ikisaidiwa italeti mabadiliko makubwa kama nilivyokuwa nimesema na kuyataja hapo mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kusema kwamba, pamoja na kwamba kuna mazingira magumu kabisa ya utekelezaji wa shughuli hizi, lakini nichukue nafasi ya pekee kumwamba Mheshimiwa Waziri wetu wa Wizara aone sasa iko sababu ya makusudi ya kuzileta sheria zote ambazo zimekuwa zikiwanyanyasa watoto, zikiwanyanyasa wanawake ili ziweze kufanyiwa mabadiliko ya haraka. Iko mikataba mingi na wenzangu wameshasema na tumesharidhia na yapo mambo mengi ambayo tunatakiwa tuyafanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, dada yetu Dr. Asha-Rose Migiro alipokuwa anahutubia Bunge hapa, alituambia kwamba iko mikataba tumeridhia lakini sheria bado hatujazitunga. Ni wakati muafaka tuzilete na kutunga sheria

hizi ili kweli ziweze kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. Naipongeza sana Serikali kwa mwaka huu kutoa ruzuku ya milioni tatu kwa kila Halmashauri ili kuimarisha madawati ya jinsia. Fedha ile itasaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kuomba kwamba, suala la kuhusisha nguvu ya baba na mama katika kuleta maendeleo iwe ni ajenda ya kubebea bango kwa sasa. Miaka iliyopita tumekuwa tukizingatia sana maazimio ya Beijing na ile ilikuwa ni kupandisha sauti ya wanawake isikike. Sauti ya wanawake imesikika kiasi cha kutosha. Sasa kinachopiganiwa ni mahusiano kati ya baba na mama, mwanaume na mwanamke katika kufanya kazi, kukuza uchumi na kulea familia. Hapo tukiweza, hao wanawake na wanaume wataweza na nchi nzima ya Tanzania itakwenda kwa *speed*.

Yupo mtu mmoja alikuwa ananiuliza akisema: “Nyie akina mama siku hizi mnasema akinamama mbele, nyuma!” Tunasema: “Mbele!” “Akina baba je?” Mwingine akasema: “Nyuma.” Nikasema sio utaratibu. Akina baba bega kwa bega. Kwa hiyo, kama akina baba bega kwa bega, akina mama nao wakiwa mstari wa mbele hakika safari hii ya kuleta maendeleo kwa nchi ya Tanzania itawezekana. Lakini haitawezekana kama hii Wizara haitapewa nguvu au haitaongezewa bajeti na Wizara yenyewe haitasimama kidete sasa kuona inajitahidi kutengeneza mipango, sera na kuhakikisha kwamba inasimamia vizuri yale yote ambayo wanafikiri kwamba yataleta heshima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa ajenda za mimba mashuleni. Kumekuwa na mjadala wa muda mrefu kuhusu haki ya kupata elimu ni haki ya kimsingi ya mwanadamu yoyote katika dunia nzima na nchi ya Tanzania. Wako majogoo mengi katika nchi, kazi yao ni kuwika na kuchafua kwa watoto wa kike wadogo. Watoto hao wanarubuniwa bila wao wenyewe kuwa tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Najua majogoo yamesikia. Sasa namwita Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika kwa dakika zilizobaki.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii japo ni finyu, lakini nitatumia kadiri nitakavyoweza. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema leo hii na kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri pamoja na timu yake kwa kushirikiana na kuandaa hotuba hii nzuri. Wizara hii ni kubwa na ni Wizara pana na ni Wizara ambayo huwa inabeba Wizara nyingi ndani yake, kwa mfano Wizara hii inabeba Wizara hii, inabeba Wizara nyingine ndani yake, kama Wizara ya Afya, Katiba na Sheria, Kilimo Elimu na Wizara nyingine. Kwa hiyo, ni Wizara mama. Lakini inavyoonekana ni kama Wizara ambayo ni ndogo tu kwa vile ni Wizara ya jinsia. Lakini inagota kwenye jinsia zote. Kwa hiyo, japo bajeti yake imeongezwa wakati huu, lakini tunaomba iongezewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimzungumzie mwanamke. Mwanamke ana majukumu mengi ya kifamilia kama wenzangu walivyosema. Mfano, mwanamke uzazi na malezi yote yanamgusa. Mwanamke ana majukumu mengi katika nyumba, usafi wa mazingira, kupikia watoto, kumtunza mume na mengine mengi, yote haya yanamgusa mwanamke. Majukumu haya yanapelekea baadhi ya wanawake kukosa majukumu mengine ya kujiletea maendeleo na hata kukosa haki zake za msingi kama vile elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke huyu anapofiwa na mume hujikuta yeye yupo katika mazingira magumu mno hasa wakati mwanamke yule anapoachiwa watoto. Kulea watoto ni kazi, watoto wanataka suna na kuhudumia. Lakini kuna baadhi ya familia zinazogota kwa wanaume huwanyanyasa wanawake wale kwa kuwanyang'anya haki zao za watoto na haki zao binafsi na hata kuwanyanyasa kijinsia kwa baadhi ya familia eti kuwatakasana na wanawake hao hupelekewa kupata gonjwa la UKIMWI. Hii ni mila potofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama ya Kadhi. Tunaiomba Serikali iharakishe kuanzisha Mahakama ya Kadhi katika nchi hii kwani ni muda mrefu mchakato haumaliziki. Sijui Serikali ina kigugumizi gani? Tunaiomba Serikali iharakishe kwa sababu hiki chombo ni chombo kinachosimamia haki za ndoa, talaka pamoja na mirathi hasa kwa mwanamke wa Kiislam. Vilevile inamtetea mwanamke kupata haki zake kama vile za urithi juu ya watoto wake na mambo mengine. Kwa hiyo, tunaomba Serikali suala hili sio kwetu tu, nchi nyingi zinazo Mahakama ya kadhi, kama vile Zanzibar, Kenya na nchi nyingine na zina dini tofauti na kila mtu haibugudhi dini ya mwenzake. Hiki ni chombo cha kusimamia haki za wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakuja kwa watoto yatima. Watoto yatima wanahitaji kulelewa na sio kwa watoto yatima tu, watoto wa kwenye mazingira magumu, walemavu na wengine wanahitaji kulelewa hasa pale wanapofiwa na watoto wao na kwenye hili tusijali dini wala rangi wala kabila. Tuwalee kama watoto wetu tuliozaa wenyewe, tusiwabague. Lakini la kushangaza, kuna wazazi wengine wanachukua watoto kama hao hawawasomeshi wala hawawapi malezi bora. Kazi yao ni kuwanyanyasa wale watoto. Mfano hai ni hivi karibuni kule Mbeya, kulikuwa na mtoto yatima alikuwa tayari ameuzwa kwa mfanyakazi wa hoteli ili achunwe ngozi kwa ajili ya kupata utajiri wa shilingi milioni tano. Je, huo sio unyanyasaji wa mtoto? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hilo tushirikiane bega kwa bega, wazazi pamoja na Serikali itoe msisitizo. Nije kwa wazee kwa sababu watoto peke yake hawawezi kuishi bila kuwa na wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wenzangu wote mnanisikia, tupunguze hasira juu ya watoto wetu na wanapotukosea makosa madogo madogo tuwahukumu adhabu ndogo ndogo, tusiwapige na hatimaye kuwafanya vilema na katika maisha yao wakawa hawana raha. Baadhi ya watoto huwatoroka wazazi wao na kuwa watoto wa Mitaani kutokana na adhabu kwenye majumba yetu. Mfano mmoja, hivi karibuni, hata juzi tu

nilisoma gezeti hili. Mzazi mmoja alimpiga mwanawe wa kike mwenye umri wa miaka 18, eti kaiba Sh. 500/= za mdogo wake.

Mtoto huyu alipigwa fimbo ya kichwa na akawekwa ndani bila ya kupelekwa hospitali kwa kuogopa vyombo vya sheria kumchukulia hatua; siku ya tatu baadaye mtoto yule alifariki na kuzikwa. Lakini palepale wasamaria wema walipeleka taarifa kwa vyombo vya habari akafukuliwa ili afanyiwe uchunguzi zaidi. Je, ni hasara gani aliyoipata mzazi hapo? Kakosa mwanawe na kakosa kuitunza familia yake. Kwa hiyo, hasira ni hasara hivyo tuzichunge nyumba zetu na watoto wetu. Mtoto unavyomlea kwa imani, basi na yeye mwenyewe atakavyokuwa atakuwa na imani ya kukulea wewe kwa sababu leo tupo wazazi na kesho tunakuwa watoto kwa maana ya kusaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie tatizo la wasichana kubeba mimba na tatizo hili linamgusa kila mmoja na linamuumiza kwa kiasi fulani. Tatizo hili limekuwa linawakumba watoto wa kike wanafunzi kwa kubeba mimba na kushindwa kuendelea kusoma kwa sababu wana mimba. La kusikitisha, hivi karibuni idadi ya wanafunzi waliobeba ujauzito kwa miaka mitano iliyopita ni 18,000. Idadi hii inatisha! Lakini la kusikitisha, sio idadi hiyo ya waliobeba mimba, kuna wengine waliokufa na ndiyo wengi kwa sababu wanabeba mimba katika umri mdogo. Wanapobeba mimba katika umri mdogo watoto hawa hawafikishwi Kliniki na wakati wa kujifunguwa hawapelekwi hospitali kwa sababu wazee wanaona aibu kuwapeleka hospitali na kusababisha vifo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ichukue mkakati wa makusudi kukomesha wimbi hili kama alivyosema Mheshimiwa Rais tushirikiane na sisi wazazi kwa pamoja na viongozi wa dini mbalimbali. Kama vile Mapadri Masheikh tukae pamoja kwenye Halmashauri zetu ili kuwakanya watoto hao na kuwapa malezo bora ili wasiendelee kubeba mimba hovyoyote na wapate nafasi zaidi ya kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maalbino. Maalbino ni binadamu kama binadamu wengine. Lakini sasa hivi inakuwa ni tatizo sugu la kuwanyanyasa maalbino hawa kama sio binadamu kwa kukatwa viungo vyao eti kwa kupata utajiri. Serikali hii iweke mkakati mkubwa zaidi ili kuwakamata waganga wa kienyeji wanaofanya matendo hayo na watakaobainika na wale walioshirikiana na waganga wapewe adhabu kama ni ya kifungo afungwe maisha, wapigwe viboko kabla ya kuingia jela ili iwe fundisho kwa wenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kukubali kutumia chini ya muda ambao tumekubaliana, lakini tumeutumia vizuri muda ule. Kwa hiyo, uliyoyasema ni mazito kabisa tena sana na umejiandaa vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, tukirudi jioni hapa watakaozungumza ni Mheshimiwa Haroub Masoud halafu Mheshimiwa Maghimbi, atafuatia na Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Bujiku Sakila, ndiyo

watakaozungumza jioni. Kwa kuwa hatuna tangazo lingine, napenda kusitisha shughuli za Bunge mpaka Saa kumi na moja jioni.

(Saa 07.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitamke kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Napenda kuwapongeza Watendaji wote, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, labda nirejee nyuma wakati ambapo Mheshimiwa Rais alipomteua Mheshimiwa Waziri kwenda Wizara hii, mimi sikumpongeza. Mimi nilimpa pole kwa sababu ni Wizara ambayo tangu nimeingia Bungeni 1995 ilikuwa iko chini ya Kamati yangu na mimi ni Mbunge pekee ambaye nimedumu katika Kamati hii kwa miaka mingi. Kwa hiyo, naifahamu vilivyo, ni Wizara ambayo inaonewa, ni Wizara ambayo wanaohusika hawajajali, watu wa Hazina, hasa imefanywa kama kitambaa cha mtoto mdogo, ndio maana nikampa pole.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimpa pongezi Mheshimiwa Sophia Simba kwa sababu ameondoka katika janga lile gumu. Lakini hata hivyo, tunaishukuru Serikali kwa mara hii wameongezea bajeti yao. Mategemeo yangu na Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii ni kwamba itafanya jicho la huruma, vile vile kwa sababu Waziri wa Fedha aliendewa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, akamwongezea kitu ambacho inafurahisha. Tunampa pongezi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumzia katika bashrafu, tunazungumzia suala hili la *fifty fifty* kwa akina mama. Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sisemi kwamba Serikali haina nia, sisemi kwamba Rais hajatupa jicho la huruma kwa suala hili la *fifty fifty*. Najua Serikali inalisimamia vizuri na ndio maana utasikia miongoni mwa nchi 20 bora duniani kuhusu *gender* ni Tanzania yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ikiwa mtu anapochangia au anaposema, ndani ya gazeti kwamba aah, Tanzania haiwajali wanawake, nasema sio kweli kwa sababu miongoni mwa nchi 20 ni kitu kikubwa sana hicho!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile hata hapa ndani ya Bunge tuliona mwezi uliopita wewe mwenyewe shahidi, nilipochungulia katika *screen* pale nilikuona wewe unaongozwa na Mkamata Rungu lile Mwanamama na wewe ukakaa. Mwanamama na Makatibu wako wawili walikuwa vile vile Wanawake wanaoku-*escort* wewe pale, nikasema huu ndio mwanzo na Mungu atajalia yatakuwa kuliko vile. Kwa hiyo, nakupongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nawaomba na wale wengine, Mawaziri wafanye mfano wako wewe kama leo alivyozungumza Mwenyekiti wangu kwamba wewe Mwanamke uko hapo, aliyetoa Taarifa Naibu Waziri Mwanamke, aliyesoma hotuba ya Wizara Mwanamke, aliyesoma hotuba ya Kamati Mwanamke, aliyesoma hotuba ya upande wa Upinzani Mwanamke na wakachangia wanawake. Lakini baadaye tumo katika orodha wale watu wanaowajali wanawake nikiwemo mimi na Mheshimiwa Sakila. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa twende katika Vyuo vya Wananchi. Kuna Vyuo 58 ambavyo vinaendeshwa na Wizara hii katika nchi nzima. Vyuo vya Wananchi 58 ndivyo Vyuo vya Walalahoi, ndio Vyuo vya Wanyonge Vijijini, ni Vyuo vya wale watu ambao hawana uwezo kwenda katika Miji Mikuu kujisomea katika VETA au Vyuo vyote vingine. Lakini cha kusikitisha, kwa mwaka wa pili huu wa fedha, fedha zote zinapelekwa VETA ambayo iko chini ya Wizara ya Elimu. Hatukatai fedha zipelekwe VETA, lakini tuangalie VETA na Vyuo vya Wananchi hivi 58 ambavyo viko chini ya Wizara hii ni kipi muhimu zaidi kama kweli tunawajali wananchi wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema Wizara ya Maendeleo ya Jamii inafanya makisio yake, inapeleka, wanapewa shilingi bilioni mbili. Shilingi bilioni mbili zile zitapotea bure kwa sababu hujui ujenge chuo gani, hujui ufanye kazi gani. Lakini laiti Serikali ingekaa kitako katika Vyuo 58 vile wakagawa kwa awamu nne; mwaka huu wakafanya nusu, robo, robo tena mpaka vikamalizika. Tunaiomba Serikali na nimemwona Waziri wa Fedha yuko pale na ninamjua ni mtu mwenye huruma na ni imani yangu kwamba kuanzia leo atakuwa na mkakati wa bajeti ijayo kuona Vyuo hivi vinakarabatiwa vyote kwa pamoja au angalau robo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokwenda kutembelea baadhi ya Vyuo, tumewakuta walimu wako hoi. Walimu wamesoma, wana elimu yao, lakini kutokana na mazingira yaliyopo katika eneo la chuo, utawaonea huruma, utadhandia wale ni wapagazi, siyo walimu. Kamati yetu ikasikitishwa sana na ikasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia suala la Baraza la Watoto. Mwezi Aprili, 2001, Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapu pale Dar es Salaam alizindua Mabaraza ya Watoto haya na akatoa agizo kwamba Mikoa yote iunde Mabaraza ya Watoto pamoja na Wilaya zake. Sasa kwa takwimu za haraka haraka ambazo ninazo hapa, kuna Mikoa miwili hadi hii leo hawajaunda Mabaraza ya Watoto ikiwemo Mtwara na Rukwa. Hatujui sababu ni nini. Agizo limetolewa na Rais na wasimamizi wakuu ni Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Lakini Wilaya ziko nyingi bado hazijaanzisha Mabaraza ya Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Dodoma tunashukuru na leo asubuhi, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii amesema wapo vijana nane wako juu hapa, inatia moyo. Hii labda wanadhania baadhi ya Wakuu wa Mikoa watawanyang'anya madaraka, hawawanyang'anyi madaraka, ni watoto chini ya miaka 18 wanajizoesha ili wawe na wao miongoni mwa watu ambao, labda ninukuu tu kwa ruhusa yako ili tujue lengo kuu la taasisi hii. Inasema: "Lengo kuu la mtandao huo ni kuhakikisha kuwa

masuala ya watoto hapa nchini yanapewa kipaumbele cha kutosha na ikiwezekana yawe mojawapo ya ajenda kuu za kitaifa; Wigo wa utendaji kwa watoto ikiwa ni pamoja na kutekeleza kwa vitendo Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto na ule wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto.” Sasa kigugumizi kiko wapi? Mkuu wa Wilaya anakaa kimya na mambo yote yako wazi kabisa!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninakwenda katika masuala ya ukatili dhidi ya wanawake. Yamezungumzwa mengi, yamesemwa mengi Bungeni na nje ya Bunge, majarida mbali mbali, Umoja wa Mataifa umesema, lakini bado Watanzania hatujataka kubadilika, tunadhani mapenzi hayaji mpaka kwa ngumi, tunadhani wawili ninyi hamwendi mpaka kwa ngumi au kwa magongo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke hapigwi! Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena, mwanaume yeyote anayempiga mkewe au hata msichana, mwanamke, basi huyo ni adui wa Mwenyezi Mungu. Anayetaka pepo ya Mwenyezi Mungu, pepo ya Mwenyezi Mungu haiwezi kuipata mtu. Mpaka yule ambaye kama ni lazima ampige mkewe, basi ampige kwa ncha ya kanga. Mwanamke hapigwi kwa bakora! Nani kasema hivyo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, hapa kuna mambo manne ambayo nitayasoma, labda wenzangu na waliopo nje watayasikia. “Kumdharirisha mwanamke siyo ufumbuzi; ukatili hauna nafasi nyumbani kwangu mimi na kwako wewe iwe hivyo hivyo; mimi mwenyewe binafsi nasaidia kufanya kazi za nyumbani kwa sababu ni nyumba yangu na yenu hivyo hivyo na kama lazima mke kupigwa, basi hupigwa kwa ncha ya kanga! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakwenda Benki ya Wanawake. Nimesema nimeingia Bungeni mwaka 1995, akina Mheshimiwa Mary Nagu walikuwepo hapa Mawaziri walianzisha mchakato wa Benki ya Wanawake. Lakini imekuwa kama ndoto isiyoagulika, tangu mwaka 1995 mpaka mwaka huu, tatizo liko wapi? Michakato yote, kazi nzuri yote imeishafanywa na Wizara. Ninachokikumbuka mimi mwaka uliopita, Serikali ilikubali, Baraza la Mawaziri lilikubali kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii wapewe shilingi bilioni 2.1 ili wakizipata zile waanzishe Benki hii. Cha kusikitisha, siku ya hotuba ya Waziri ya Waziri Mkuu, lakini kwa bahati mbaya ilikuwa mwisho wa mwezi wa Juni, fedha zile hazijatolewa. Lakini, nimefurahi kuona Wizara ya Fedha imeji-*commit* kwamba italipa fedha zile kipindi hiki na vile vile italipa fedha ambazo zimepangwa kulipwa katika awamu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nje katika suala la mauaji ya Albino. Mheshimiwa, inashangaza sana, mimi sidhani kama hao ni waganga na kama kweli ni waganga, waje niwaonyeshe uganga mimi. Mganga hata siku moja hakwambii anataka kiungo cha binadamu mwenzake ili akupatie utajiri wewe au akupatie jambo lolote lingine. Hao ni wababaishaji na tunataka lazima tutoe taaluma kubwa kwa wananchi wetu kwamba wasikubali kudanganywa. Hakuna mwenye uwezo yeyote anayeweza kubadilisha amri ya Mwenzi Mungu. Mwenyezi Mungu anachokipanga ndio kile ambacho anakipanga

mwenyewe. Hakuna yeyote mwenye uwezo wa kukipangua cha Mwenyezi Mungu. Lakini chako wewe kinaweza kupanguliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mchungaji hapa alizungumzia siku ya familia na siku ya wanawake duniani. Siku hizi mbili ni muhimu sana na kama kweli Wizara ya Maendeleo ya Jamii itanisikiliza agizo langu, itasikiliza ushauri wangu, sherehe za miaka inayofuata wasikubali kufanya sherehe, hotuba, nini, anatakiwa kila anayekuja pale aje na mkewe, afanye kazi pamoja na mkewe na mwakamke aliye na mumewe ili tuonyeshe mwaume vipi anafanya kazi pamoja na mwenzake. Yale mambo sio ya mtu mmoja peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikwenda katika sherehe za siku ya familia Kigoma miaka minne iliyopita wakati ule Mheshimiwa Asha-Rose alikuwa ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii. Nilipewa nafasi kuzungumza, mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais. Nilipewa nafasi ya kuzungumza, nikasema leo mimi na Waziri tumefanya dhambi kubwa sana, siku ya familia bahati nzuri mgeni rasmi, Makamu wa Rais amekwenda na mkewe pale, mimi nilikwenda peke yangu, Waziri Asha-Rose kaenda peke yake. Nikawaambia, una dhima kwa Mwenyezi Mungu Mheshimiwa Asha-Rose, sherehe hii haikukamilika na tutakapoifanya tena kila mmoja ahakikishe anakuja aidha na mumewe au na mkewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia suala la mwisho kabla sijapigiwa kengele, suala la ukeketaji. Suala la ukeketaji halijazungumzwa leo kabisa, wala sijalisikia. Suala la ukeketaji mimi nasema kama kweli takwimu zitatolewa, suala la ukeketaji linazidi. Kuna mmoja hapa amesema kwamba sasa wanakeketa watoto wadogo kabisa. Ni kweli, kwa sababu mtoto mdogo hajui kusema, hawezi kukimbia, anajua kulia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliangalia filamu hapa hapa, katika Kamati yetu, huwezi ukaingalia filamu ambayo inaonyesha jinsi watoto wanavyokeketwa nchini. Sheria iko, tatizo ni nini? Tatizo linaonyesha ni sisi wanaume haturidhiki kumwona mtu hajakeketwa. Ni hilo tu! Hakuna lingine! Kama sisi hatujabadilika, basi suala la ukeketaji litaendelea. *Point* hii sitaki kuiendeleza zaidi kwa sababu mwenzangu aliniambia nimwachie yeye aizungumze kwa urefu kabisa, Mheshimiwa Fatma Maghimbi. Kwa hiyo baada ya kusema haya, namwachia Mheshimiwa Fatma Maghimbi azungumzie suala la ukeketaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mia kwa mia na ninaomba Serikali ilione kwa jicho la huruma suala la bajeti ya Wizara hii. Asanteni sana, naunga mkono hoja! (*Makofi*)

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nizungumzie kidogo juu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Wizara hii, maneno matatu yaliyomo, Jamii, Jinsia na Watoto vyote vina maana nzito sana kwa Wizara hii. Jamii, maana yake ni makundi ya aina moja yaliyo na amari moja yanayofanya shughuli moja. Kwa mfano, jamii ya wakulima, jamii ya wavuvi, jamii ya wanawake, jamii ya watoto. Kwa hiyo hii ndiyo maana yake. Jinsia



maana yake ni baba na mama na watoto, ni wale tunawaowazaa wakiwa wachanga mpaka wafikie kabla ya umri wa miaka 20, wale tunawaita watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Wizara hii kama inatakiwa ilete maendeleo ya makundi haya, ni Wizara kubwa sana. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri alinukuu usemi fulani wa Rais ambao uko katika *roman five* ya kitabu chake hiki na akaeleza kwamba Wizara hii ni nzito sana na ina majukumu mengi. Lakini nafikiri nukuu hii waliopewa Wizara hizi toka mwanzo hawajalifanyia kazi na hawaja-*realise* Mheshimiwa Rais kasema nini na kakusudia nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Rais alikusudia kuwa Wizara hii ni ngumu na nzito na ni kubwa kwa sababu inajumuisha jamii yote ya Watanzania. Kwa mfano, jamii nitazizungumzia makundi machache machache kwa sababu muda wenyewe ni mdogo, nitaanzia na makundi ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, makundi ya wakulima toka Wizara hii ianze naona haijachukua bado jukumu, inaachiwa Wizara yenyewe ndiyo iendeleze wakati inaeleza kwamba jamii ziendelezwe. Jumuiya ya wakulima hawajashughulikiwa, wana matatizo, kila siku wanazungumzia habari ya kupewa pembejeo, majembe ya kisasa mpaka leo watu wanalima kwa jembe la mkono na hata hivyo hawakati tamaa kulima. Wakishalima, kinachosikitisha zaidi ni kwamba wao hawashughulikiwi juu ya masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niko Pemba na Dar es salaam, huwa naona jinsi mazao kwa mfano ya mananasi, kipindi cha mananasi yanavyokuwa mengi. Je, Wizara hii ambayo inatakiwa isaidie, ilete maendeleo kwa jamii hii pia ya wakulima, mananasi yanakaa mpaka yanaoza, yanafika mpaka nanasi moja Sh.500 au S. 300: Je, Wizara hii imefanya nini kuendeleza wakulima? Hilo ni masikitiko makubwa sana. Wakati wa machungwa vile vile, basi hata viwanda vidogo vidogo au wakulima waimarishwe namna ya ku-*preserve* matunda kama haya na tuweze kuyapeleka nje au kutengeneza *juice* iweze kupeleka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoshangaza, huwa tunaona makopo ya *juice* au chupa za *juice* zinaandikwa, zinatoka Arabuni. Arabuni hakuna mchungwa wala hakuna nanasi wala hauoti. Lakini sisi kwetu yanakoota hatuwasaidii wakulima. Jamii hii imesahauliwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende haraka haraka. Siku moja nilikwenda Botswana, kuna Mhindi mmoja wanamwita Bwana Veg. Veg maana yake ni kifupisho cha *Vegetables*. Bwana huyu anachukua viazi hapo Gairo, anasafirisha anapeleka Botswana. Anachukua unga wa mhogo, anachukua mboga ya matembele, anachukua mboga ya kisamvu, anapeleka anakwenda kuuza Botswana. Basi siku anayofika pale, Watanzania wanapigania. Sasa huyu anaachiwa Mhindi mmoja anafanya biashara hii. Kwa nini Wizara hii isijaribu kuwaongoza wakulima na kununua vifaa vyao halafu Serikali ikapeleka, ikapata faida na wananchi wakawa na uhakika na soko lao?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye jamii ya wafugaji. Wafugaji pia wametupwa na Wizara hii pia inatakiwa ifanyie marekebisho mambo ya ufugaji. Tunasikia hapa kila siku wanalaumiwa wafugaji wanaambiwa wapunguze ng'ombe wao. Kwa nini? Sisi ni watu wa tatu, hao walio na ng'ombe wengi huko duniani mbona hawaambiwi wapunguze ng'ombe wao? Kupunguza ng'ombe, wasaidieni wapate viwanda vya kutayarishia nyama.

Mimi pia katika safari zangu nilizopita, nilishapita *Airport* moja wanauza nyama kavu za ng'ombe, wanauza nyama za kukausha, wanauza kila aina ya nyama. Sisi tuna ng'ombe wengi namna hiyo, Wizara hii kwa nini isifuatilie na Wizara hii tunaambiwa ni ya maendeleo ya jamii, jamii ni wakulima, wafugaji, wanawake na makundi yote. Kwa nini hawasaidiwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitakwenda kwenye jamii ya wavuvi. Wavuvi pia ni jamii ambayo ingawa ina Wizara, lakini tunaambiwa Wizara hii inasaidia jamii. Jamii ya wavuvi inahitaji sana kusaidiwa. Zamani kulikuwa na samaki wakavu, kulikuwa na samaki wanatiwa kwenye makopo. Lakini leo hakuna yote haya hayapo tena. Samaki wakavu hakuna tena ambapo tunao samaki wengi, badala yake tunamsikia Waziri Magufuli anawabana wavuvi, anawaumiza, wanataka kulia wavuvi. Anasema kuwa wavuvi sasa wasivue, wasivae viatu, wasichukue *oxygen* wakaenda chini kule, wasivae mawani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nani hapa aliye na mapafu ya kuweza kwenda chini futi mbili au tatu bila ya kuchukua *oxygen*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, mimi nilikuwa kwenye Kiti, hakusema hivyo! Alisema kwamba kila kitu, kama ni nyavu, kama ni viatu, kuna mazingira ambayo vinaweza kuvaliwa, kuna mazingira haviwezi kuvaliwa. Hiyo unayosema haikusemwa jana. Tuendele. (*Makofi*)

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hivyo ndivyo nilivyomwelewa kuwa nyavu zikachomwe na bahati nzuri basi, tulipata meseji nyingi kutoka kwa wananchi na wao ndivyo walivyoelewa kama nilivyoelewa mimi kuwa: “mwambieni Mheshimiwa Magufuli aje achome nyavu zetu.” Aje atuchome kila kitu cha uvuvi na sisi tuko tayari tutarudisha kadi zao za CCM.” Hili nililifurahia sana maana na sisi tutaongeza wanachama. Unaona! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Wizara hii mimi naonea huruma sana kwa sababu Wizara hii ina mambo mengi na hatuyaoni yakiendelezwa. Kwa hiyo, labda tungependekeza Rais achukue haya madaraka mengine kama watoto, aweke Wizara ya watoto au wakulima, maana jamii isiwe kabisa katika Wizara hii kwa sababu jamii ina *meaning* nyingine kabisa kuwa wote wanatakiwa wasahihishwe na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa wakati Mawaziri wanapopewa nafasi za Uwaziri, kama Mheshimiwa Magufuli, apelekwe akapate *training* ya uvuvi ni nini wa baharini kwa sababu yeye anasema, mimi namsamehe kwa sababu yeye ni Mnyamwezi

anatoka juu huko, hajui habari ya bahari wala haijui bahari. Sio ajabu hajapata kukanyaga hata maji ya bahari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, hebu ji-*address* kwa hoja hii, ya Magufuli ilikuwa jana! Naomba uendelee kuzungumzia Wizara hii. Usimzungumze Waziri mwingine.

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo Wizara hii, jamii maana yake ni hiyo!

**NAIBU SPIKA:** Sasa, Magufuli anaingiaje?

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naingia kwenye jinsia. *Message sent!* Jinsia maana yake ni wanawake na wanaume. Lakini bado sijaona kwamba wanawake na wanaume wanasaidiwa ili wapate maendeleo. Kwanza, nianze watu waliostaafu. Watu waliostaafu pia ni jamii ni jinsia hiyo. Kwa hiyo, wao wanahitaji kusaidiwa wapate kile wanachokitaka. Wanapostaafu, mafao yao wanakuwa hawayapati, wengine wanastaafu wakiwa kwenye umri wa kuweza kuwa na nguvu, lakini hawayapati mafao yao wala hawaajiri. Kwa nini watu kama hawa waliostaafu wakiwa na nguvu Wizara hii isiweze kuwasaidia?

*(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kukaribia kwisha)*

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Ya ngapi hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Ya kwanza!

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu hawa wanakuwa na watoto, wanataka kuwasomesha watoto wao, hawawezi. Mafao yao mwisho hayapatikani. Mwisho tumemsikia Naibu Waziri wa Fedha hapa anasema cheki zinakaa mpaka zinakuwa hazifai, zinapitwa na wakati. Sasa kwa nini hawapi habari kwa njia wanazokuwa na uhakika kwamba watapata habari? Huwezi kumtangazia mtu njoo uchukue cheki yako katika redio. Wengine hawana redio! Japokuwa wengine wanazo, kuna sehemu hapa Tanzania, Redio Tanzania haifiki. Wanapata Redio za Uganda, sasa watapataje pesa zao? Kuna sehemu nyingine wanapata Redio ya Kenya zaidi? Halafu isitoshe anasema anatangaza pia katika magazeti, nani aliye na uwezo wa kununua magazeti kila siku? Kwa hiyo, Wizara hii bado ina kazi kubwa ya kusaidia jamii ya jinsia. Jinsia, wanawake pia wana matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri angeweza kuwasaidia wanawake angalau kufundishwa namna ya kuvuna maji, tumepiga vibyongo wanawake kwa kuchota maji, vichwa vimekuwa sugu kwa kubeba ndoo. Kwa hiyo, hayo yote yanataka yaendelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kidogo kuzungumzia watoto. Watoto bado pia hawajafanyiwa kazi. Watoto hawafundishwi mashuleni namna kwa mfano ya kukimbia ngono zembe. Watoto wanapata mimba mashuleni na mimba siku hizi siyo tatizo. Nimeona mahali pameandikwa, “Mimba siyo tatizo, UKIMWI je, utaufanya

nini?” Kwa hiyo, pia Wizara hii isaidie kutizama *curriculum* za shule, ziandike nazo mafundisho namna gani watoto waweze kujisitiri au turudi kule *back to basic!* Sisi enzi zetu tukisoma, wanawake watupu na wanaume watupu. Kwa nini tusiende kule? Tulikuwa tunatishwa, mwanamme anatisha kiasi gani. Mimba zilikuwa enzi hiyo ni ajabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipata mimba ukiwa shule wakati huo ilikuwa ni maajabu makubwa! Lakini leo watoto hawaendelezwi wakaonyeshwa katika Wizara hii kwamba kuna ubaya kiasi gani wa mtoto kufanya ngono na mwanamme wakiwa shuleni kwa sababu anaweza kupata mimba akapoteza masomo yake. Kwa hiyo, maendeleo yake yakarudi nyuma. Anaweza pia kupata ugonjwa huu wa sasa akaweza kufariki. Lengo la Wizara hii mimi naamini bado halijatimizwa na ningependekeza kwa Mheshimiwa Rais kwamba Wizara hii ipunguziwe majukumu. Kila kitu hapa kipelekwe katika Wizara yake, ama sio hivyo wapewe pesa zote za Tanzania kwa kuendesha Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Asante sana! Hiyo kali!

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote kwa jinsi walivyoandaa vizuri. Lakini pia, niwape pole. Kwa sababu kazi waliyopewa ni kubwa sana na ni nzito na nitasema kwa nini. Kwanza, niseme kwa wazi kwamba naunga mkono hoja hii na nina sababu zangu tatu. La kwanza, ni umuhimu wa Wizara yenyewe na Wizara yenyewe ndio mhamasishaji mkuu wa maendeleo katika maeneo yetu, lakini pia ni chimbuko la maendeleo na nitatoa sababu zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimoja kimenisikitisha. Kwanza, ukiangalia muundo wa Wizara yenyewe, inaongozwa na akina mama na tunafanya makosa kuzani Wizara hii kwa kweli ni ya akina mama peke yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu pia upande wa Serikali tunafanya makosa kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, tunaona wote ni akina mama. Tatizo linaanzia hapo, ndio maana utaona hata wachangiaji leo walio wengi walikuwa ni wakina mama. Sisi wanaume tunaonekana wakorofi tu. Kwa nini tunaingia kwa mambo yasiyotuhusu? Hapana! Hii Wizara ni muhimu na nitasema kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, labda historia mjue, Wizara hii imeanza zamani. Afrika limekuwa ni Bara la wakimbizi, ni la wakimbizi kwa sababu tangu karne ya pili wakati wa vita vya Wakatago kule Afrika ya Kaskazini. Wakatago ni *Cathegenians* walikuwa wanagombana na Warumi. Wakawapiga Waswahili kuteremka chini, Warabu walipokuja Afrika Magharibi wakawapiga Waswahili na utumwa ukaingia. Kusini Makaburu wakaingilia Waswahili wetu wakawatandika, wakaja Kaskazini, wengine ndio hawa Wangoni walikuja mpaka Sumbawanga, wakatoroka wakarudi Songea, wengine tukawaoza. Ni historia ya wakimbizi! Waafrika wamekuwa ni Wakimbizi kutoka eneo moja hadi lingine, lakini, pia miongoni mwetu makabila kwa makabila tukaendelea kupigana.

Sasa baada ya uhuru, Baba wa Taifa kwa taarifa yenu, alisema tutaendelea kuwa wakimbizi ndani ya nchi yetu. Kwa muda gani? Kwa nini tuendeleo kuwa wakimbizi? Akasema hapana, lazima kuwe na Wizara itakayounganisha, kuwakusanya wananchi wote tutulie, tujiamini, tujiletee maendeleo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii ikaanza. Hivyo, shabaha na madhumuni yake yalikuwa ni kuwaunganisha wananchi wote wakae pamoja, wajiamini kuwa wanaweza kuleta maendeleo, waondokane na tabia ya kuwa wakimbizi kwa sababu wasiwasi ulianza kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkimbizi yeyote ana dalili kubwa tatu. Kwanza, makazi yake ya wasiwasi, nyumba siyo za kudumu maana anajua kesho atakuja afukuzwe. Angalia nyumba zetu za Waswahili, mpaka akiwa ndani unamwona mtu. Anaona saa yoyote anaweza kukimbia. Pili, mazao yake ya muda, haweki mazao ya kudumu. Nenda Tabora, utakuta miembe ni ya babu zetu, hawalimi na kupanda mahindi. Angalia minazi ya babu zetu. Mazao ya kudumu yakawa kwa kweli ni ya wasiwasi. Sasa katika msingi huo, tukaona kwamba lazima tuliangalie katika misingi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili mazao yake ni ya muda haweki mazao ya kudumu, nenda Tabora utakuta miembe ni ya babu zetu, hawalimi na kupanda miembe, angalia minazi mababu zetu ndiyo walipanda mazao ya kudumu kwa kweli ni ya wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msingi huo tukaona kwamba ni lazima tuliangalie katika misingi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani yapo mambo matatu ambayo ni lazima tuyaangalie, kwanza ni kuangalia uhuru tuliopata huu tunataka kufanya nini, nini shabaha na madhumuni ya Wizara hii. Ilipoamuliwa kuanzisha Wizara hii, Vyuo vya Maendeleo vya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vilianzishwa kwa nguvu na shabaha ilikuwa ni kuwafundisha wananchi ili waendeleo kujiletea maendeleo wao wenyewe. Leo vyuo hivyo ukiangalia vimechoka, vimekufa na vyuo vyenyewe hata vingine hata ruzuku havipati. Mheshimiwa Waziri ndiyo ameanza kutoa fedha kwa ajili kukarabati. Hivi kwa kweli malengo ya Wizara hii tutafikia kwa utaratibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasikia pia baadhi ya vyuo sasa hata vyeti vinafutwa wakati mlitaka vyuo hivi vitusaidie sasa tutoke hapa tulipo tuwasaidie wananchi wa ngazi zote ili walete maendeleo na nini kilikuwa kinafanyika. Enzi hizo nitawapeni mfano, Sumbawanga tulikuwa na Afisa Maendeleo ya Jamii alikuwa ndugu William Shellukindo na ndiye aliyem-*recruit* Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya kuwa Afisa Maendeleo na Mheshimiwa Mzindakaya alijifunza kuzungumza kutokana na Uafisa Maendeleo ya Jamii. Kwa sababu walikuwa wanafundisha mbinu za namna ya kuzungumza na wananchi ili kuwaimarisha waweze kufanya maendeleo yao wenyewe. Hiyo kazi ilikuwa ni ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya pili tukasema kwamba hii peke yake haitoshi yapo mambo ambayo ilikuwa sasa ni kupanga na kuangalia kila mwananchi katika eneo

lake apewe mafunzo maalum na Wizara zinazohusika zozote kama ni kilimo zitatoa utaalamu lakini mratibu Mkuu atakuwa Afisa Maendeleo ya Jamii. Hiyo kazi ndiyo ilikuwa ifanyike na Maafisa Maendeleo ya Jamii. Sasa wamekuwa ni wakusanyaji wa kodi, hawafanyi kazi iliyokusudiwa na tumewaacha waendele tu namna hiyo. Lakini wao walikuwa ndiyo msingi mkubwa kwa kila sera. Wanaitafsiri na kuwaambia wananchi nini shabaha na madhumuni ya sera hiyo, kama ni ya elimu kama ni ya kilimo, kama ni afya maafisa maendeleo walitufanyia kazi nzuri na nadhani hiyo kazi haijamalizika bado waendele maana bado umuhimu upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwafundisha maendeleo ni lazima tuwe na utaratibu ambao utakubalika. Sisi tunaamini ya kwamba Watanzania tuna bahati kubwa sana. Bahati ni ile tuliyopewa na Mwenyezi Mungu ya kuwa na ardhi nzuri, hatuna zaidi ya ardhi. Ndani ya ardhi tuna maji mazuri, ndani ya ardhi kuna madini, ndani ya ardhi kuna mafuta, ndani ya ardhi kuna petroli, ndani ya ardhi kuna kila aina na mifugo ndiyo iko juu ya ardhi, Mungu atupe nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilinachotakiwa ni kupata watu watakaotafsiri kwa uhakika hizi sera zetu na mimi nasema hakuna mtu mwingine ni kuimarisha Wizara hii ifanye majukumu yake na ninyi mtashangaa maendeleo yanaweza kuja haraka kuliko tunavyotegemea *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nasikitika wamepewa shilingi bilioni nne. Hakuna lolote pale, watabaki tu wanakarabati, wanazunguka hakuna kazi yoyote watafanya. Wizara hii bado ina jukumu kubwa sana katika kuleta maendeleo, nimejaribu kuangalia nini tatizo letu. Tatizo ni kila mtu anayekuja anakuja na sera zake, Waziri atakapoondoka hapo anakuja mwingine badala ya kusema nianzie mwenzangu alipoishia, anaweza kuanza na yake kabisa moja kwa moja. Leo nilikuwa namwambia Mheshimiwa John Malecela, kwamba ndani ya Bunge hili kwa taarifa yenu, wale ambao tuliwahi kushika nafasi kama Mawaziri wa Kilimo tuko tisa ndani ya Bunge hili, kuanzia Mheshimiwa Mzee John Malecela, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Jackson Makwetta na mimi tupo karibuni tisa ndani ya nyumba hii, kuna utaratibu tu wa kistaarabu. Nimeshukuru baadhi ya Wizara sasa zimeanza utaratibu wanapoondoka angalau wanawashukuru wenzake kwa kazi, lakini wengine akishaondoka fulani utadhani amefanya makosa gani, wanamwacha hivyo na yeye anaanza upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuendelea kama kila mtu anakuja na mambo yake mwenyewe. Ni lazima tufikie mahali fulani huyu ameishia hapa tumsaidie ili na huyu anayeingia aingie sasa kwa gia ya wapi mwenzangu alimalizia na alishindwa wapi na tufanye marekebisho gani ili tuendele ndiyo utaratibu unaotakiwa lakini kila mmoja anaendelea zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tatizo ni uchoyo na ubinafsi ndiyo unaotusumbua, ule ubinafsi utatumaliza. Hii kazi tunayoifanya ni kazi ya wananchi siyo kazi yetu, tuko hapa kuwasaidia wananchi ili kuwaletea maendeleo na maendeleo yenyewe hatutaki waendele kuwa wakimbizi ndani ya nchi yao, hakuna sababu yoyote

wananchi wetu wakaendelea kuwa wakimbizi, hakuna sababu yoyote msipokaa na kuambizana mipango tuliyoipanga, kama unahamisha watu kutoka kona fulani unawapeleka kwingine hakuna ubaya kukaa na kuzungumza jamani hapa tunawaondoeni kwa sababu moja, mbili na taratibu zitakazotumika ni hizi, maafisa maendeleo ya jamii ndiyo walikuwa wanafanya kazi hiyo. Siku hizi ukichukua mgambo huwa hana maelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo unaposema kwamba tuwapange wajasiriamali au tuwapange hawa vijana ambao wapo huko mitaani wanazunguka bila ya kuwa na utaratibu kuwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii, haitawezekana. Nataka kuonyesha uzito wa Maafisa Maendeleo ya Jamii ya kwamba kweli tutakuwa kila siku ni kusukumana na wote wataonekana ni wakimbizi ndani ya nchi yao, si vizuri hata kidogo ndiyo maana nataka niombe kabisa kwa dhati ya kwamba Wizara hii ipewe kipaumbele ili iweze kutekeleza majukumu yake yalivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu bahati mbaya labda tumechelewa lakini kweli mimi nitaiomba Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tukitaka kufanikiwa katika maendeleo ya maeneo yetu ni lazima tuwe na maafisa maendeleo wengi, tufungue vyyo vingi, mafunzo kwa wakulima wetu vijijini yaendeleo na kama inawezekana hata wajasiriamali wafundishwe mbinu mbalimbali kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la muhimu pia tuangalie namna ya kuhamasisha Maafisa Maendeleo ya Jamii. Zamani huwezi kupata nafasi ya kuwa Afisa Maendeleo ya Jamii au Afisa Kilimo bila kupata angalau *induction course*. Lazima wakuelewe kwamba wewe unaweza hiyo kazi, siyo mtu aende kwa ajili amekosa kazi. Tunafanya makosa wakati mwingine mtu anaingia kwenye kazi kwa sababu amekosa kwingine ni kosa kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipokuwa Bwana Shamba nilipoomba kazi ya Ubwana Shamba niliambiwa kwanza niende kufanya kazi za mikono kule Kasulu kwa muda wa miezi sita ili nithibitishwe kama nafaa kuwa Bwana Shamba. Walikuwa na utaratibu mzuri baada ya miezi sita ndiyo nika-*qualify* kwenda kwenye kazi, hapo unaonekana huyu anafaa na huyu hafai. Lakini sasa hivi tunaingiza watu tu bila hata kujaribiwa ili mradi amefaulu mitihani, hapana! Ni lazima tuangalie na mtu mwenyewe na uwezo wake kwa sababu tunapokwenda mbele ni lazima tuwe na watu ambao kweli wanajitolea kwa nia na madhumuni ya kutaka kusukuma maendeleo atakuwa nayo bila wasiwasi wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nini maendeleo, kwetu Sumbawanga ukisema nini maendeleo kule, Mfipa hata ukimwamsha usiku ukamwuuliza maendeleo ni nini atakuambia ni barabara ya lami. Unataka nini? Atakuambia barabara ya lami kabisa. Mwamshe hata usiku kwa sababu anaona bila barabara ya lami hatapata maendeleo mengine anayoyategemea ana sababu zake. Wanunuzi hawatakuja Sumbawanga ikiwa barabara ni mbaya, pembejeo hazitafika na hatapata fedha za kutosha za kuweza kununua vitu vingine na ndiyo maana utakuta suala la maendeleo ni mtambuka mzuri ni lazima

tukae na kujadili. Tunafanya nini ili kuondoa watu wetu hapa walipo waingie hatua ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho mimi nataka niombe tu kwamba kipindi tulichonacho ni kipindi kigumu kipindi ambacho kinataka watu wawe na elimu ya kutosha, na Maafisa wetu ni lazima tuwape elimu ya kutosha ili wapambane na mazingira haya tuliyonayo. Lakini tuwe na uratibu wa sera zote tulizonazo. Sera zote zilizopo ni lazima tuziratibu ili zisiwe zinaingiliana. Sera lazima ziwepo zile ambazo zinasaidia kututoa hapa tulipo na kuingia hatua ya pili, kama kuna matatizo basi tuweze kutafuta njia ya kutatua, hilo ni ombi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho yapo mambo mawili ambayo ni vizuri Mheshimiwa Waziri akaona, la kwanza nimepata taarifa ya kwamba Chuo cha Misungwi, nilikuwa nasoma si ajabu kisiendeleo tena kutoa cheti. Mimi nadhani tutafanya makosa, watu ambao tunataka siyo lazima wawe na *Diploma*, tunataka wa ngazi ya Cheti *very basic* ambaye atakwenda kijijini akazungumze na wananchi hatutaki digrii wala hatuendi kutafsiri maneno magumu. Tunataka ambaye ataweza kwenda kuchambua na kuzungumza na wananchi wetu kuhusiana na maendeleo yao *a common man form four* ama *form six* wanafahamu wanafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukianza mambo ya digrii hawa vijana hawatakwenda vijijini watataka wapate kazi za maana za ofisini na madhumuni na shabaha mliyokuwa nayo tutashindwa kuyafikia. Nisingependa hata kidogo tukashindwa kwa sababu mimi naiheshimu Wizara hii na ninaimani kabisa ya kwamba hata tutakapoanza kujadili kwenye vifungu mimi nitashangaa Wabunge kusimama naomba ufanye hivi. Hela ziko wapi, tungoje Waziri afanye kazi, tumsaidie mambo yake yaende vizuri ili mwaka kesho tupambane. Mimi nina imani kabisa Mheshimiwa Waziri Margaret Sitta, akisaidiwa na mama Lucy Nkya wanauwezo mkubwa sana tuwape kila aina ya msaada katika kipindi hiki ili mwaka kesho tuwasaidie wapate fedha zao na mimi na imani kabisa Wizara itafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya mwisho mwisho ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya hotuba ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Waziri kwamba naunga mkono hoja, sina mpango wa kuondoa shilingi na wala wakati wa Kamati ya Bunge Zima sitosimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kutoa tahadhari kwamba naweza kufanya mambo hayo mwaka kesho kama haya yanayofuata hapa hayatapatiwa majibu vizuri kama Mungu akitufikisha salama. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, mazingira ambayo huna fedha lakini unatakiwa kuleta maendeleo kwa wananchi, siyo jambo dogo ni jambo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni ya Maendeleo ya Jamii, maendeleo yanahitaji shughuli za kufanya, ili maendeleo yaonekane wananchi wanatakiwa kushiriki katika shughuli hizo, ili waweze kushiriki wanatakiwa kumiliki shughuli hizo na ili waweze kushiriki na kumiliki ni lazima wahamasishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii ni kubwa kabisa baada ya kutengeneza sera ni uhamasishaji, ili uweze kuhamasisha ni lazima uwe na taaluma ya kuhamasisha, taaluma ambayo unatakiwa kuisomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii inatakiwa kufanywa kwa wananchi wetu lakini kwa bahati mbaya sana wananchi wetu kule kwenye kata, vijijini watu hao hatunao hawa ambao wanataaluma hii, lakini tunategemea kwamba maendeleo tutayakuta kwenye vijiji na kata, kazi ambayo ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashangaa inakuwaje kazi hii ambayo ni ya taaluma imeachiwa maafisa watendaji wa vijiji ambao hawajasomea, kazi hii tumewaachia maafisa watendaji wa kata ambao hawajasomea, kwangu mimi naona hawa watu wanahitaji kwanza nao kuhamasishwa kwanza na watu ambao wamesomea kazi hiyo, lakini tumewaachia wahamasishwa na wasimamie kitu ambacho wenyewe hawajasomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri ndiyo maana maendeleo yanakuwa ya pole pole kidogo kwa sababu hatuna watu ambao wamesomea kazi hii .

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa sasa ndiyo nakuja kuongelea juu ya Bajeti ya Wizara hii, ukiangalia kazi za Wizara hii, malengo na umuhimu wake na Bajeti ya shilingi bilioni nne siyo fedha hiyo. Hapa ni kama mchezo tu mimi naomba sana mwakani fedha ya Wizara hii iongezwe, kama kweli tunataka kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hili kwa masikitiko sana kwa sababu kazi hii imeshindikana kabisa kufikisha kwa wananchi hasa wale ambao tunaowahitaji ni wale ambao wamesomea kazi hii kwa hiyo, ni lazima wasomeshe na nilikuwa najiuliza hivi inakuwaje kazi ya uhamasishaji tunawaachia watu ambao hawajasomea, inakuwaje Wizara ya Fedha itenge kiasi kidogo cha fedha kwa Wizara hii halafu itegemea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najiuliza hivi Mheshimiwa Waziri wa Fedha au Naibu Waziri wa Fedha akienda Hospitali anategemea kumkuta Daktari, akimkuta mganga wa kienyeji amekaa kwenye kiti cha Daktari akaanza kuhangaika kutaka

kumchoma sindano Mheshimiwa Waziri atasubiri apigwe sindano? Hivyo ndivyo kazi tuliyoifanya kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewaweka watendaji wa kata wahamasishe wananchi ambao wenyewe hawajasomea, hawa ni kama waganga wa kienyeji kwa shughuli za maendeleo, naomba sana tumwezeshe Waziri wa Wizara hii apeleke watu ambao wamesoma kazi ya maendeleo ili mambo ya elimu ya maendeleo iendelee. Matokeo yake watu wanaenda kuhamasishwa wajenge shule wanajenga wanaishia kutokuwapeleka wanafunzi shuleni, tunawahamasisha wajenge zahanati na vituo vya afya, wanajenga wanaishia kwa waganga wa kienyeji tunafanya kazi gani, tunahitaji uhamasishaji wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye Benki ya Wanawake, mimi naipongeza Serikali kwa kusaidia uamuzi huu ambao ni muhimu sana, ni muhimu sana kwa sababu hawa wanawake ni moja ya vikundi ambavyo vipo nyuma na njia pekee ya kuwasaidia ni kuwawezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono lakini naomba nitoe tahadhari kwamba Benki hii ni nzuri na kwanza imechelewa ilitakiwa kuanza mapema kwa kuwa tunaita ni Benki, Benki tunazifahamu na masharti yake tunayafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tumeshuhudia mamilioni ya JK yameishia wapi, yameishia kwa watu ambao wana uwezo na walio na uwezo wa kurudisha kama kweli tumekusudia kuwafaidisha akinamama ili waweze kuendelea vizuri kupitia Benki hii ni lazima masharti ya benki hii yaandaliwe vizuri sana, la sivyo tutakuwa na makundi mawili ya wanawake, wanawake wanaoweza walio na uwezo watakaonufaika na wanawake ambao wataendelea kuwa maskini pamoja na kuwepo kwa benki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu pamoja na kuanzishwa kwa benki hii ni vyema Wizara hii ianze kufikiria juu ya mfuko wa kusaidia wanawake, mfuko huu wa kusaidia wanawake hasa wale ambao hawana hata uwezo wa kwenda benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilifikiria mtu wa Jimbo langu mpaka akapate mkopo ataupata saa ngapi, nafikiria juu ya mtu wa Igumangobo atapataje mkopo wa fedha hii, kwanza mtu hajasoma na hata jinsi ya kurudisha fedha benki hajui, hata *writeup* hajui kuiandika, mimi naomba sana kama kuna masharti yaangaliwe vizuri sana lakini vile vile isambae haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langi ni kwamba si vyema benki hii mkaiweka Dar es Salaam, ije angalau Dodoma ili iwe rahisi kuwafikia hata watu wa Kwimba, kwa Dar es Salaam naona ni watu wachache tu watakaonufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumaliza juu ya benki naenda kwenye jina la Wizara, Wizara hii imeandikwa ni Wizara ya Wanawake Jinsia na Watoto. Maendeleo ya Jamii sawa lakini kuna Wanawake, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jaribuni kusoma hiki kitabu tatizo ni kwamba mtaona mengi yanaelezea juu ya wanawake, hakuna sehemu ambayo imetajwa juu ya mwanamume, sehemu yote inavyoelekea kwa Wizara hii Jinsia ni sawa sawa na Mwanamke, mwanamke ni sawasawa na jinsia. *(kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafahamu wanaposema jinsia wanataka tuamini kwamba ni wanawake na wanaume, wanataka tuamini hivyo lakini maelezo ambayo yamo kwenye kitabu hiki hayatuelekezi tuamini hivyo, inatia mashaka kwamba labda kuna ajenda fulani ya siri ambayo bado haijatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba Wizara hii ijaribu kuangalia ni kwa namna gani inaweza kumsaidia mwanaume ambaye ametelekeza familia yake kwa sababu ya nyumba ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara isaidie mwanamume ambaye anaogopa kwenda nyumbani mchana kwa sababu mke wake ni mkali sana. *(kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunaongea juu ya jinsia ni vyema tukaangalia vile vile siyo matatizo tu ya mwanamke vile vile muangalie na matatizo ya wanaume, yapo matatizo mengi, wapo wanaume wanapigwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye asilimia hamsini kwa hamsini naunga mkono, nayo imechelewa lakini ninachowaomba mkawe waangalifu jinsi ya kutumia ile hamsini kwa hamsini, tukiitumia vibaya haitotusaidia sana, ni jambo jema sana ni vizuri tukaliunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama nilivyosema naunga mkono hoja na ninaomba Wizara ya Fedha kwa mwaka kesho iongeze Bajeti ya Wizara hii ili wananchi wengi waweze kuhudumiwa na maafisa wa Wizara hii kiasi hiki hakitoshi kwa mwaka kesho kiongezwe. Safari hii wala sitatoa shilingi, mwaka kesho naweza kutoa shilingi kama wanaume wanaopata matatizo hawatapatiwa msaada. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii nzito sana na nyeti ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu naomba nitumie nafasi ya awali kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto Dada yangu Mheshimiwa Margaret Sitta, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Bajeti ni nzuri wamejitahidi kuainisha vipaumbele tumeona lakini tatizo la Wizara hii ni ufinyu wa Bajeti kama wenzangu walivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiojificha kwamba Bajeti hii kila mwaka ni ndogo sana, namhurumia sana Dada yangu Mheshimiwa Margaret Sitta, mwaka jana alikuwa kwenye Wizara ambayo alipitisha hapa trilioni 1.5, leo anapitisha Wizara yenye shilingi bilioni 14.6 mimi namhurumia sana, sijui zile hela atazifanyia kazi gani, kwa sababu ameshazoea kushika mafungu makubwa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kelele zetu mwaka kesho zitazaa matunda, ni lazima Wizara hii itazamwe kwa jicho la huruma kabisa, kwa sababu ni Wizara nyeti ina mambo mazito, ni Wizara inayoondoleza jamii, kwa nini isipewe kipaumbele kwa kupewa hela za kutosha, nina uhakika hata kama tukiendelea kubadilisha Mawaziri kwenye Wizara hii wataendelea kuchemka tu kwa sababu pesa ni ndogo. Naomba kama kweli tunataka kuwapima Mawaziri wanaopewa Wizara hii wapeni hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alianzia Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, ufanisi wake ulikuwa mdogo kwa sababu ya pesa, akaingia Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, leo dada yangu yupo humu ndani kwani ninaomba sana Wizara hii iongezewe pesa ili tuweze kuona ufanisi wa Mawaziri wetu katika Wizara hii ambayo tunaitegemea sana Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wenzangu wamesema kwamba Wizara hii inatazamwa kwa mtazamo hasi kwa sababu waliomo mle ndani katika nafasi za juu ni wanawake wote, Waziri ni mwanamke, Naibu Waziri mwanamke, Katibu Mkuu mwanamke, kwa kweli tunapata dhana potofu kuhusu Wizara hii, kama kweli Wizara hii inawalenga wanawake na wanaume ninaomba hata viongozi waingie katika mtindo ule ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waziri ni mwanamke, Naibu wake awe mwanamume, kama Naibu ni mwanamume basi Katibu Mkuu awe mwanamke, angalau tujue mtazamo wa Wizara hii uwe unafanana na Wizara zingine, nina hakika tukichanganya watendaji pamoja na Mawaziri, Wizara hii itakuwa na mtazamo tofauti kuliko ilivyo sasa. Wanaume mna tabia ya kututazama hivi hivi na ndiyo maana mnatupa hela ndogo tu ninaomba msituoneone tu, ninawaomba mtutazame kama ni wanawake tunaweza na tuna haki zote na tunastahili kupewa haki kama wanaume na mtu mwingine yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana mwaka kesho Wizara hii itazamwe kwa jicho tofauti, viongozi wachanganywe na pesa ziongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nizungumzie kuhusu maafisa maendeleo ya jamii, huko tulikotoka katika Halmashauri zetu tuna Mkuu wa Idara ambaye ni Afisa Maendeleo ya Jamii aliyeko katika Halmashauri, lakini Afisa huyu hapewi heshima kama wanavyopewa wakuu wengine wa idara, unamkuta Daktari wa

Wilaya ana gari, unamkuta Afisa Elimu wa Wilaya ana gari, unakuta Mhandisi ana usafiri, lakini Afisa maendeleo ya Jamii hana usafiri, unategemea huyu mtu atafanya kazi bila usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri peke yake ndiyo utakaompa ufanisi wa utendaji katika nafasi yake, tunaomba Maofisa Maendeleo ya Jamii waliopo kwenye Halmashauri zetu wapewe usafiri nina uhakika tukiwapa usafiri wataweza kusimamia nafasi zao, wataweza kuelimisha jamii na wataweza kufanya mambo mengi sana yanayolenga Wizara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo Wilaya tu vile vile hata maafisa wa maendeleo ya jamii walioko kwenye kata zetu hawa nao ni watu tunaowategemea sana katika kuhamasisha jamii kuleta maendeleo. Lakini unamkuta Afisa Maendeleo Jamii wa kata hata baiskeli hana, hata pikipiki hana. Hebu niambie watendaji walioko kwenye kata huyu Afisa Maendeleo kama hana hata baiskeli, hana pikipiki ana kata yenye vijiji saba atasafiri vipi kuvitembelea vile vijiji saba? Atafanyaje kazi ya kuhamasisha akinamama wale wajasiriamali, atafanyaje kazi ya kuangalia hata ukeketaji unavyoendeshwa huko ambao ni haramu kabisa? Tunaomba tutazame watendaji wetu tuwape usafiri. Nina hakika watendaji hawa wakipata usafiri wataweza kutimiza wajibu wao vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo naomba niongelee hawa wasichana wanaokatisha masomo kwa ajili ya kupata mimba. Wenzangu wamezungumzia na mimi nina wajibu wangu wa kuzungumza. Kwa kweli lazima tuwatazame hawa wasichana kwa jicho la huruma. Ni wasichana wanaopata mimba bila kudhamiria, wanalazimika, wanashawishiwa ukizingatia familia zetu ni maskini leo anapatikana mwanamume mmoja anamuonyesha fedha anadhani kwamba zile hela zitamsaidia kusoma, zile hela zitamsaidia kununua mavazi kumbe hela hiyo, inampeleka pabaya. Naomba sheria sasa itazamwe upya hawa wanafunzi wa kike wanaokatisha masomo kwa sababu ya mimba warudie kusoma baada ya kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama siyo hilo natoa *altenative* nyingine, kama mnaona hilo haliwezekani sasa naomba Serikali ibadili umri wa mtoto wa kike kuingia shule ya msingi, tumuingize mtoto wa kike miaka mitano ili aweze kumaliza shule ya msingi akiwa bado mdogo, akiwa bado hajavunja ungo nina hakika kama atakuwa hajavunja ungo basi matatizo kama haya ya kupata mimba uzembe yatakuwa hayapo. *(Makofi)*

Naomba watoto hawa wa kike waingie wakiwa na umri mdogo. Nina hakika atakapoingia sekondari bado atakuwa na umri ambao siyo mkubwa sana vile vile unapokuwa sekondari ile akili inapevuka unaweza ukapata akili yako ya kuona kwamba hiki ninachoshawishiwa na mwenzangu siyo kizuri. Uwezo wa kujitetea akiwa sekondari una nafuu kuliko shule ya msingi. Nilikuwa naomba mawazo haya mawili. Wanafunzi hawa wanapopata mimba warudie shule baada ya kujifungua ama waanza shule ya msingi wakiwa na miaka michache mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika tutakuwa tunawasaidia hawa watoto wa kike. Siyo hivyo tu hizi mimba hawanywi maji ama hawali kama chakula wanapewa na wanaume. Adhabu ya wanaume kufungwa jela mimi sioni kama adhabu inatosha. Naomba sheria imbane mwanamume anayemtia msichana wa kike mimba kuhakikisha anailea mimba, analea na mtoto na anamlea binti yule aliyemkatisha maisha yake kwa sababu wasichana hawa baada ya kupata mimba wanakosa thamani, wanakosa mwelekeo na aliyemharibia mwelekeo ni mwanamume.

Je, mwanamume huyu amewajibika vipi wakati yeye anaendelea na masomo mwenzie kakatishwa masomo? Naomba sana sheria iangalie namna ya kumbana mwanamume anayemtia mtoto wa shule mimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hilo naomba sasa nirudi kwangu Singida. Mkoa wa Singida nina Vyuvo vya Maendeleo ya Wananchi viwili. Naanza na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Singida Mjini. Napenda nitumie jukwaa hili kumpongeza sana Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida Mjini ndugu Mlade kwa kweli bwana Mlade anafanyakazi kubwa sana akishirikiana na walimu wenzake. Chuo kile amekibadili sura, kina sura nzuri, kina maendeleo makubwa, kina majengo ya kisasa hajapata hela ya Serikali, amefanya hayo kwa juhudi zake mwenyewe na walimu wenzake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ametafuta wahisani ndani ya nchi, nje ya nchi kwa hiyo, bidii yote hii lazima tumpongeze Mheshimiwa Mlade. Tumpongeze sana. Baada ya kumpongeza basi niombe Serikali muongezeeni OC Bwana Mlade ili kazi zake ziwe nyepesi. Chuo hicho kinamiliki wanafunzi 550, wanafunzi wa chuo 200 tena wako bweni, wanafunzi wa sekondari 350 mnapompa OC ndogo mnampa majaribu. Chuo hicho tunakitegemea kimkoa, hata viongozi wa Kitaifa wanakwenda pale. Juzi Mheshimiwa Rais amefika pale.

Naomba sana sana tumpe jicho la huruma huyu Bwana Mlade tumuongeze OC yake. Siyo hivyo tu chuo hicho kina gari, gari hilo la mwaka 1986 niambi ni Waziri gani hapa bado anaendesha gari la mwaka 1986, ni Waziri gani bado inatumia gari la mwaka 1986 gari ambalo lina umri wa miaka 22, OC inaishia kwenye matengenezo. Jamani ziko gari kwenye taasisi zetu za Serikali yanatumika yanafika mahali mpaka yanapigwa mnada, kuliko mpige mnada magari kama hayo, sasa nakupa *assignment* Mheshimiwa Waziri, tafuta gari za aina hiyo, mpelekee bwana Mledi imsaidie kuliko OC unayompelekea inaishia kutengeneza hii gari STG ya mwaka 1986 mpaka tunamhurumia sana huyu bwana. Gari haifanani kabisa na mandhari ya chuo. Nina hakika mkimpa gari bwana Mlade mtamtia moyo na ataendelea kuboresha chuo chake vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hicho tu bwana Mlade amejenga ukumbi wa kisasa, ukumbi huo ukikamilika utamuingizia fedha. Sasa hivi tumeanza kukitumia hivyo hivyo kwa kuibaiba lakini bado hakijakamilika. Kinahitaji *finishing* naomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na ufinyu wako wa Bajeti, nakujua wewe ni mbunifu, wewe una moyo wa huruma kama mama pamoja na Naibu wako tafuteni hela mahali popote hata nje ya Bajeti yako msaidie huyu bwana akamilishe ukumbi wake. Mkimpa hata milioni moja

ukumbi unakamilika huyo bwana, mtafutieni hela mahali popote akamilishe ukumbi huu ili uendelee sasa kumingizia fedha ambazo zitamsaidia kuboresha chuo chake kuendesha chuo chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongelea Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida Mjini sasa naenda Iramba Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msingi. Chuo hiki kiko mbali na Makao Makuu ya Wilaya, tarafa ya Kinyangili. Mahali kilipo chuo kiko chini kabisa ya mlima, ukitaka kwenda Wilayani au Mkoani mpaka upande mlima. Leo Mkuu wa Chuo yule ni mwanamke ana pikipiki. Hivi kweli mwanamke ataendesha pikipiki kupanda mlima wa Msingi, mlima ambao umezingirwa na pori la hifadhi? Bado tunazungumzia habari ya simba wapo huko huko, atapita huyu mwanamke na yeye mtazamieni gari mahali popote, yale mnayoyapiga mnada sisi kwetu yana thamani mpelekeeni ili limsaidie huyu mama.

Kwanza mwanamke kuendesha kupita pori hataweza, inawezekana hana mume ndio hapo mtakapomfanya anze kuolewa na mtu ambaye hakumtegemea kwa kupakiwa kuvushwa mlima. Mhurumieni huyu mama, msimtie majaribu mtafutieni gari hata kama limechakaa litamsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile chuo hicho hicho kina tatizo la umeme, Bunge hili hili lilishaahidi chuo hicho umeme miaka minne iliyopita. Sasa kuna kigugumizi gani ambacho kinafanya umeme usiende pale? Tunaomba chuo kipelekewe umeme kwa sababu Bunge lilishaahidi. Jamani likishatamkwa humu Waziri akitamka si tayari utekelezaji, kuna kigugumizi gani tena na bado chuo kile kile hakina maji, wanasafiri kilomita moja kufuata maji. Hivi kweli hawa wanachuo watafanyakazi, watasoma? Si watakalia kwenda kuchota maji tu? Naomba sana yanayowezekana jamani tuyafanye, vyuo vyetu vinafanyakazi kwa mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika tukivisaidia yale yanayowezekana tutakuwa tumefanya jambo jema na tutawarahisishia wenzetu waweze kufanya majukumu yao vizuri, kama wanavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hilo na mimi nizungumzie sasa kuhusu mfuko wa wanawake ndani ya Halmashauri. Nashukuru kwamba mpaka leo Halmashauri bado zinatenga asilimia 10 kwa ajili ya kukopesha akinamama wajasiriamali. Wizara nayo huwa inapeleka shilingi milioni nne kila mwaka kutunisha hiyo mifuko ambayo imetengwa na Halmashauri zetu. Kwa kuwa nimemuomba Mheshimiwa Waziri huyu na Bunge hili limemuomba Bajeti yake mwaka kesho iongezwe na yeye tunamuomba hii shilingi milioni nne akishaongezewa na yeye aongezee Halmashauri zetu aanze kupeleka hela nyingi kuliko hizo ili wajasiriamali wetu waweze kunufaika na hiyo asilimia 10 ambayo inawasaidia wanapata mikopo kirahisi, masharti siyo magumu kuliko mikopo mingine ya benki na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa kwa sababu mmemdai Waziri wa Fedha aongeze fedha sasa namuita Waziri wa Fedha azungumze anapewa dakika 15. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii. Lakini sitachangia kuhusu kuongeza fedha kwa sababu sina takwimu. Hili inabidi lipate watalaam ndiyo niweze kujua kwamba ni kiasi gani tunaweza kuongeza. *(Makofi)*

Mimi ningependa kuchangia Benki ya Wanawake. Kwenye kitabu hiki *page 24* kumeonyeshwa kwamba Serikali itatoa shilingi bilioni 2.2. Sasa nilitaka kutoa ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha benki ni kitu nyeti. Huwezi kuamka tu asubuhi ukaanzisha benki halafu ukasema kwamba Serikali itatoa fedha. Benki Kuu wana taratibu, kuna Kanuni 12 ambazo lazima uzitekeleze kabla hata Hazina haijatoa hizi fedha. Sasa kitu kimojawapo katika kanuni hizi ni kwamba benki yoyote ambayo inaanzishwa lazima iwe na *promoters*. Wale *promoters* ndiyo wanatakiwa waanzishe kiwango fulani cha fedha ambacho Benki Kuu itaridhika kwamba kwa kiasi hiki kweli hawa wanaweza wakaanzisha benki ndiyo mtu mwingine aweze kuongeza fedha. *(Makofi)*

Sasa kikubwa kabisa ambacho ni muhimu ambacho ningependa kushauri ni kwamba kwanza kabisa tuwe na hakika kwamba hawa wanaoanzisha Benki hii ya akinamama kuna *promoters*? Hawa *promoters* ni akina nani maana yake majina yao yote lazima yapelekwe Benki Kuu na hao *promoters* wako tayari kuchangia kiasi gani. Sasa baada ya kupeleka hiyo ndiyo mnaweza mkasema kwamba *okay* baada ya sisi kuchanga hizi lakini tuna mjomba pia ambaye anaweza kuchangia bilioni 2.1 vinginevyo Benki Kuu watakataa kwa sababu moja kwa moja *arbinital* itakuwa benki hii ni ya Serikali haitakuwa benki ya akinamama. *(Makofi)*

Kwa hiyo, moja ambalo ningependa kutoa ufafanuzi ni kwamba ni lazima tuwe waangalifu, tuhakikishe kwamba wapo *promoters* ndani ya akinamama ambao wanaweza wakatoa fedha zinazofika kiasi fulani, wenyewe wameeleza katika karatasi hizi kwamba lazima zifike kiwango fulani wale *promoters* wenyewe watoe ndiyo mtu mwingine aje aingie. *(Makofi)*

Sasa Serikali hatuna tatizo tunaweza tukasaidia kutoa hizo fedha, lakini lazima ikumbukwe kwamba Serikali yenyewe hii hii mmeshairuhusu ijitoe kwenye kufanya biashara sasa tukianza sasa tunajitoe kufanya biashara *NMB* lakini huku tunajiingiza kuunda benki nyingine na vijana watakuja na wazee watakuja na watu wengine watakuja. Mkisema kwamba tuliwapa akinamama lakini nyie hapana mnajitakia matatizo. *(Makofi)*

Sasa mimi nilitaka kushauri kwamba kwa kanuni za Benki Kuu kuweza kuanzisha Benki ya Kitaifa, benki hii ya akinamama watahitaji shilingi bilioni tano ili waweze kukubaliwa kupewa *license* ya kuanzisha Benki ya Kitaifa. Lakini nataka niwape mfano, *Akiba Commercial Bank* au *Azania Bank* ilianza na mtaji wa shilingi milioni 500 kama



*financial institution* baada ya miaka nane ikabadilishwa ikawa benki kamili na sasa hivi ina mabilioni ya shilingi. Kwa hiyo, kama kweli akinamama wenyewe wanaoanzisha benki hii hawataweza kuchangia shilingi bilioni tano, mimi ningeshauri tungeanzisha kwanza *financial institution*, *financial institution* ni benki ambayo inafanya mambo yote ya kibenki isipokuwa kutoa *cheque*. Kwa hiyo, benki inaweza kufanya yote ya kibenki, akinamama wakasaidiwa na kadhalika isipokuwa haiwezi kuruhusiwa kutoa *cheque*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaji unaotakiwa ni shilingi milioni 500. Kwa hiyo, kama uhakika kwamba hawa *promoters* hawapo na uhakika kwamba tunaweza tukawapata hawa *promoters* hakuna, mimi ningeshauri kabisa kwamba hebu tuanzishe *financial institution* na sisi Hazina tunaweza tukasaidia hiyo ikaanzishwa mara moja kwa sababu sasa hivi wanazo fedha ambazo ni zaidi ya shilingi milioni 500 tukahakikisha kwamba hiyo inaanzishwa mara moja. Sasa Hazina ikawakopesha hizo shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya kufanya mambo mengine ili benki hii iweze kufika mbali vinginevyo kwa taratibu hizi ambazo ziko za benki hapa kwa kupewa fedha na Hazina lakini benki ya wanawake, Benki Kuu watakataa. (Makofi)

Kwa hiyo, ningetaka nishauri hivyo na kama watakubali kwa kweli hata mkifika Dar es Salaam tuanze hata wiki ijayo mimi naweza nikawasaidieni Benki Kuu tukaanzisha *financial institution* ya akinamama ambayo ni benki lakini benki ambayo kwa sababu ya mtaji wake haiwezi kutoa *cheque*. Lakini inaweza kufanya mambo yote ya kibenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo naunga hoja mkono. (Makofi)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa maandalizi mazuri na uwasilishaji mzuri wa hotuba ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maoni, ushauri na maombi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ukarabati Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Kiwanda Muheza. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lengo la ukarabati wa vyuo vyake limeelezwa. Hata hivyo, vyuo vitakavyofanyiwa ukarabati vingeanishwa kwa kuwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Kiwanda, Muheza ni miongoni mwa vyuo ambavyo vinahitaji kuendelea kufanyiwa ukarabati.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo hicho amekuwa akiendesha vikao bila kuona umuhimu wa Mbunge, Mjumbe wa Bodi, kuhudhuria kufuatana na umuhimu wa kazi zake. Hali hii inafanya mambo mengi kudumaa kwa kukosa michango na msukumo wa Mbunge kwa mfano mradi wa umeme toka chanzo cha maji mto Ziggi kwa msaada wa Serikali ya Sweden.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mradi wa umeme kwa Chuo cha Kiwanda. Mwaka 2006/2007, Sweden walionyesha nia ya kusaidia kujenga mradi mdogo wa umeme kwa ajili ya chuo. Wahisani walihitaji andiko la uhifadhi wa Mazingira na kupata “Haki ya Matumizi ya Maji ya Mto Ziggi” hatimaye Wizara ilitoa fedha kwa andiko la Mazingira lakini haikufuatilia upatikanaji wa “Haki ya Matumizi ya Maji ya Mto Ziggi.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mjumbe wa Bodi, niliwasilisha maombi na ushauri wote kwa aliyekuwa Waziri wa Wizara hii na aliahidi kufuatilia. Hadi wiki iliyopita, Mkuu wa Chuo cha Kiwanda alikuwa bado hajapata hati hiyo na hivyo kushindwa kuendeleza mradi huo. Wanaohusika kutoa hati hiyo ni Wizara ya Maji na Umwagiliaji (sasa) na Ofisi yao ya Kanda iko Moshi. Mara kadhaa Mkuu wa Chuo, ameshindwa kufuatilia ombi hilo Moshi kwa ukosefu wa fedha (nauli)! Kwa hali hii, naomba Katibu Mkuu asaidie kwa kuiandikia Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kuwataka Maofisa wao waharakishe upatikanaji wa hati hiyo kwa manufaa ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Kiwanda kupata mradi wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, misaada kutoka Serikali ya Sweden. Serikali ya Sweden imekuwa tayari kutoa misaada katika Chuo cha Kiwanda na imesaidia kulipia gharama za mafunzo ya jamii katika vijiji vinavyozunguka Chuo. Kwa mfano, masomo ya utengenezaji wa matofali kwa ujenzi wa nyumba bora. Wizara husika ikajikita karibu na watoaji wa misaada toka Sweden na kusimamia utekelezaji wa mahitaji muhimu kama “andiko la Mazingira” upatikanaji na “hati za Matumizi ya Maji ya Mto Ziggi” basi wahisani wataona Wizara inajali Maendeleo ya chuo hivyo kuongeza misaada mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ukatili kwa watoto hapa nchini limekuwa likiongezeka siku baada ya siku. Matukio ya ubakaji kwa watoto wadogo na wale wa shule za msingi yamekuwa yanaongezeka badala ya kupungua. Tena mbaya zaidi siku hizi ili kupoteza ushahidi wakishawabaka wanawaua. Hili linasikitisha sana sana. Imefikia hatua sisi wazazi tunapokuwa mbali na watoto hatuna amani kabisa. Ni mikakati gani ya dharura imeandaliwa na Wizara kukabiliana na suala hili la hatari?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia suala hili likikemewa sana na *NGOs* zinazoangalia watoto mfano TAMWA lakini Serikali kwa kuona ukubwa wa tatizo hili inafanya nini? Karibu kila siku sasa yanaripotiwa matukio ya ubakaji! Watuhumiwa wanafanywa nini? Nashauri adhabu iongezwe na wahusika wote wahasiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi sana hapa nchini wamekuwa wananyanyaswa kijinsia, kimaslahi na hata kimajukumu. Cha kutisha, wengi wao hawajui haki zao za msingi na hata wale wanaozijua hawajui waitafutie wapi hiyo haki.

Wengine pia hawana uwezo wa kufuatilia hizo haki zao kwa sababu hiyo, wanabaki kuendelea kunyanyasika, kudhoofika na hata kupoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashirika yasiyo ya kiSerikali ndiyo yamekuwa mstari wa mbele kutetea haki za wanawake mfano TAMWA, LHCR na mengine. Mashirika hayo, kwa kutambua haki zinazoripotiwa, wamekuwa wanasaidia kutoa misaada ya kisheria ili waweze kufuatilia haki zao. Hili lilitakiwa kufanywa na Serikali yenye watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri alieleze Bunge hili, ni jinsi gani Serikali inawezesha mashirika haya kifedha ili waweze kuendelea na kufanikisha kazi wanayofanya ya kusaidia wanawake wanaonyanyasika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunapenda kuelezwa ni jinsi gani Wizara hii inasaidia Chama cha Madaktari Wanawake wanaofanya kazi kubwa ya kusaidia kuchunguza afya za wanawake kwa mfano ugonjwa Saratani kwa kinamama. Ni jukumu la Wizara hii kutupatia takwimu sahihi za kinamama wenye matatizo ya saratani na wangapi wamepatiwa huduma na wangapi wamekosa huduma. Ni msaada gani unatolewa kwa Madaktari hawa wanaofanya kazi kubwa ya kuokoa maisha ya Watanzania tena kwa kujitolea bure? Wataendelea kutegemea michango mpaka lini? Je, michango hiyo inakidhi mahitaji ya kazi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto yatima wapo wengi sana huko vijijini na hata misaada inayotolewa na TACAIDS haiwafikii kabisa. Fedha zinatumiwa kwenye semina na makongamano mijini. Wizara hii ina takwimu ya watoto yatima kwa nchi nzima? Wapo wapi na wanapata wapi huduma za msingi? Mgawanyo wa fedha zinazotolewa na wafadhili mbalimbali kwa ajili ya watoto hawa zinafanywa vipi? Nani anasimamia katika ngazi zote ili kuhakikisha kama kweli zinawafikia watoto hawa?

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo moja ambalo naiomba Serikali ilitolee maelezo na ufafanuzi ili Jamii ya Watanzania ielewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Elimu ya Tanzania haisemi chochote juu ya watoto chini ya umri wa miaka mitano (*under five*) ambapo shughuli za utoaji elimu kwa watoto hawa zimeachwa mikononi mwa sekta binafsi. Aidha, sekta hiyo pia sasa inafundisha Walimu kwa ajili ya kufundisha watoto hawa na viko vyuo vingi, kimojawapo ni Chuo cha Mtumba – Dodoma. Ninaomba ufafanuzi kwa maswala yafuatayo:-

Kwanza, je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kurasimisha utoaji wa elimu kwa watoto hawa, ili uwe wa kisheria na sio wa hiari usiotambuliwa na sera yetu ya elimu?

Pili, Serikali ina mpango gani wa kuvipa ruzuku vyuo hivi vya binafsi na Walimu ili watoe Walimu wenye viwango vya kitaifa kufundisha watoto hawa?

Tatu, Serikali itakubali kuwatambua Walimu waliomaliza kwenye vyuo hivi ili watumie kufundisha watoto hawa kwenye mfumo wa elimu rasmi ya kitaifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Simwanza Sitta, (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa hotuba yake nzuri sana ambayo ina maelezo ya kina kuhusu dhana ya maendeleo ya jamii na umuhimu wake katika maendeleo vijijini. Naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Lucy S. Nkya, (Mb), Naibu Waziri, Bibi Mariam J. Mwafisi, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo, kwa kufanya kazi kwa uaminifu, uadilifu na kutumia taaluma zao ipasavyo na kuiwezesha Wizara hiyo kuheshimika hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya, Wizara haipewi kipaumbele katika kugawiwa rasilimali hasa rasilimali watu ya kutosha, matatizo ya ukeketaji, unyanyapaa wa waathirika wa Ukimwi, uonevu wa Maalbino na kung'ang'ania desturi, tabia na mila ambazo ni vizuizi vya Maendeleo katika vijiji, yangepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ningetakiwa kuchagua wataalamu gani ningependa kuwa nao katika kata, ningesema nipatiwe wataalamu wa Maendeleo ya Jamii. Mnafanya kazi nzuri endeleeni na mimi nitashirikiana nanyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii tena kwa asilimia mia moja.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunijalia uzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie tena nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na wataalamu wote kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naipongeza Serikali kwa uamuzi wake mzuri wa kuwezesha na kuwaimarisha wanawake hususan katika utoaji wa mikopo kwa makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (*WDF*), kumehamasisha wanawake wengi zaidi kujiunga na vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo, ni vema Serikali ione umuhimu wa kuimarisha mfuko huu kwa kutenga fedha nyingi zaidi. Pia kuandaliwe mkakati utakaoweza kutoa elimu kwa ajili ya usimamizi na urejeshwaji wa fedha za mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sana, fedha za Mfuko wa Maendeleo (*WDF*), zilikuwa zikipelekwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya kuvipatia vikundi mbalimbali vya wanawake lakini utaratibu huo haukuwa na manufaa hata kidogo na kwa kuwa *SACCOS* nyingi zina uzoefu mkubwa, kwa nini fedha za Mfuko wa Maendeleo (*WDF*), zisipelekwe kwenye *SACCOS* zinazotambuliwa kuliko ilivyokuwa *SACCOS* nyingi zina uwezo wa kusimamia urejeshwaji wa fedha hizo na pia kupanua wigo wa wanawake wengi zaidi kunufaika na mfuko huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Maendeleo, kwa kuwa vyuo hivi vina umuhimu mkubwa kwa jamii na bado hatujaweza kuvitumia ipasavyo, kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuvijengea uwezo vyuo hivi ili viweze kujitegemea? Naomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya zoezi hilo ili vyuo hivi viweze kubuni na kuibua miradi itakayowawezesha kujitegemea kuliko kutegemea fedha kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vyuo hivi vipo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, kuna haja ya kuangalia uwezekano wa kuvitumia vyuo hivi ili viweze kujiendesha. Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Wizara ya Kazi, wakae pamoja kujadili kwa kina jinsi ya kubuni miradi na kuibua itakayoweza kusaidia na pia kufundisha stadi mbalimbali za ufundi na kazi zitakazowezesha wananchi kujijajiri na pia kuunga mkono juhudi za Rais wetu katika kuongeza ajira milioni moja ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wasichana wanaopata mimba shuleni kabla ya kumaliza darasa la saba. Tatizo hili ni kubwa sana hasa katika Mkoa wa Manyara na linatokana na tatizo la kutokuwa na shule za bweni. Mtoto wa kike hulazimika kutembea mwendo mrefu kwenda shule na kurudi jioni anakutana na hatari nyingi barabarani. Watoto huweza kubakwa na huweza kukutana na wanyama wakali. Naomba tuhimize shule kujenga shule za bweni za wasichana.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wanaopata mimba shuleni, wasiruhusiwe kurudi kuendelea na shule kamwe wajijunge na vituo vinavyofundisha stadi za kazi ili wapate ujuzi. Kwa wale ambao tayari wamekwishapata watoto, Serikali ione umuhimu wa kuhimiza ujenzi wa Vituo vya Ufundi (*VET*) katika kila Kata ili mama wadogo hawa wahimizwe kujiunga na stadi za kazi baada ya kujifungua ili hatimaye waweze kujijajiri wenyewe. Vituo vya *VET* vimesaidia sana hasa watoto wanaondolewa katika mazingira hatarishi. Kwa wale wanaopata mimba shuleni, waelekezwe kwenye *VET Centres* kuliko kuendelea na shule baada ya kujifungua. Hilo halitawezekana kabisa na kwa kufanya hivyo, tutakuza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifo vya wanawake na ugonjwa wa Fistula, ni vema Serikali iendelee kutoa elimu kwa wahusika, hasa ugonjwa wa Fistula wanawake wengi wanaogopa kwenda hospitali kwa kuwa wanaona aibu na hatimaye mume anamfukuza. Wahudumu wa afya waendeleo kutoa elimu ili akinamama hawa waweze kwenda kutibiwa na baadaye waweze kuhudumia familia zao.

Suala la Maalbino. Tatizo hili limekuwepo tokea siku nyingi lakini sasa tatizo limeshamiri. Tunaomba Serikali ivalie njuga kuhakikisha kuwa jamii inafichua wote wanaohusika na mauaji haya. Kila Kata iorodheshe idadi ya Maalbino ili tujue Tanzania tuna Albino wangapi? Hatuwezi kuwalinda ikiwa hatujui idadi yao. Tuna Albino wangapi Tanzania? Elimu itolewe kuondokana na mila potofu.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia siku ya leo kufika hapa hali nikiwa mzima. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake iliyojaa mategemeo kwa Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kutoa mchango wangu katika Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mimba kwa wanafunzi, kwa kuzingatia ukuaji wa tatizo hili, ni vema Serikali iweke sheria kali kwa mwanaume atakayempa mimba mwanafunzi, mara nyingi haya yanatokana na ghibla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watoto wa mitaani. Ongezeko la watoto wa mitaani wanaozururazurura, limeongezeka kila leo, ni vema Serikali ichukue hatua za makusudi za kuwadhibiti watoto hawa ili waweze kuwasomesha. Kufanya hivyo, ni kumuandaa na kumweka katika mazingira bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maalbino. Ni muda mrefu Maalbino wanaishi kwa wasiwasi mkubwa, hii inatokana na baadhi ya watu kuwaua eti kwa itikadi za kishirikina. Kwa nini, Serikali haiwezi kuondoa kero hii ili kumwezesha Mtanzania huyu kuishi kwa amani katika nchi yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria ya Ndoa na Mirathi, kwa kuzingatia sheria hii kuwepo, ni muhimu kwa kujua Watanzania tuna ndoa za kimila, pia kisheria kutokana na ndoa za kimila, kunachangia kwa kiasi kikubwa watoto wa kike kupata mimba za utotoni, Serikali iweke Sheria mahsusi ili imlinde mtoto huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, napenda kumpa hongera Mama Sitta na Naibu Waziri wake, kwa umahiri wake katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri. Naomba nichangie hoja hii ifuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya jinsia itolewe kwa viongozi wote wa Serikali na vyama. Ili kuleta utashi wa jinsia, kila Wizara, watendaji wapewe elimu ya jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamisheni ya Jinsia, kama inavyoleweka, umuhimu wa masuala ya jinsia, kuwe na Kamisheni ya Jinsia kama ilivyo kwa Ukimwi, Mazingira. Kamisheni hii ijikite katika kuelimisha kufuatilia na kuratibu suala la jinsia. *NGOs* nyingi zinafanya kazi nzuri kama wadau wengine wa Serikali. *NGOs* zipewe fedha na Serikali ili kutekeleza kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuho cha Maendeleo ya Jamii, Namtumbo, kina majengo mazuri Mputa, Serikali ichukue majengo yale iwe Chuo cha Maendeleo ya Jamii.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Watendaji wenzake, kwa kuandaa bajeti nzuri, pia na jinsi manavyoendesha Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa mitaani. Tatizo hili linazidi kujiimarisha. Hawa vijana wakikua bila malezi na wakakulia mitaani miaka ya mbele watakuwa ni hatari kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee na walemavu, njia itafutwe ya kuwasaida wazee na walemavu ili kuwapunguzia matatizo waliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mirathi, jamii iendelee kueleweshwa na kuelimishwa zaidi juu kuandika mirathi ili tatizo la yatima kunyang'anywa, kuzuiliwa mali lipungue na kuisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii, kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, pamoja na Naibu wake na watendaji wake wote wa Wizara kwa jinsi walivyoandaa na kuwasilisha hotuba yao ya bajeti, pamoja na udogo wa fedha waliyotengewa kwa matumizi ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mkakati madhubuti na uwepo wa Sheria ya Kujamiihana, bado tatizo hili linaonekana kuwa sugu kwa kuendelea kukua siku hadi siku. Ubakaji ni suala linalomdhalilisha mwanamke na hasa mtoto, jambo ambalo hupelekea sio kumvunjia haki tu bali pia kusababishia mwanamke kuendelea kumbebesha mzigo wa mimba ya pekee na malezi ya mtoto wa pekee. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa adhabu zipo lakini bado tatizo linakua basi labda sheria iangaliwe upya ili wahusika wa vitendo hivyo angalau waogope baada ya kuyaona marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto waishio katika mazingira magumu. Kama Serikali haikuwa makini katika kushughulikia tatizo hili basi mzigo mkubwa utaendelea

kuilemea Tanzania, kwani maambukizi ya Ukimwi yanaendelea, watoto wa mitaani wataendelea kuwepo na kuongezeka. Ushauri, Sheria za Ndoa ziangaliwe ama ziundwe na zizingatie mila na silka na tamaduni zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba wale watoto wanaobebeshwa mimba wakiwa wanafunzi basi wasimamiwe waweze kuendelea na masomo na pia wale waliowapa mimba walazimishwe kuwatunza watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa hotuba ya bajeti iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni mtambuka kwa maana ya kwamba watumishi wa Wizara wana wajibu wa kutafsiri sera mbalimbali na mipango yote inayopelekwa kwa wananchi. Watumishi hawa wana jukumu la kuraghibisha, kushauri jamii kutambua matatizo yanayowakabili na pia kutoa mafunzo ya kuandaa mipango ya kutatua matatizo na namna ya kuyatekeleza. Jukumu hili linaonekana kutoweka kutokana na kutokuwepo watumishi wa kutosha na wale waliopo hawana nyenzo za kazi na wanaonekana kukata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwaendeleza wanawake, utaratibu wa mafunzo kwa viongozi wa vikundi vya wanawake urejeshwe. Hivi sasa kuna vikundi vingi vya wanawake lakina havina mwongozo wowote. Chuo cha Rungemba katika miaka ya 70 kilitoa mafunzo kwa viongozi wanawake lakini hivi sasa kinatoa mafunzo kwa watumishi. Ni muhimu sana kiwepo chuo maalum kwa ajili ya mafunzo kwa wanawake ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza Wizara, Waziri, Naibu na Katibu Kuu, kwa kuandaa mpango mzuri na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, “*Convention on the Rights of the Child*” itafsiriwe kwa Kiswahili na iwe *popularized* nchini kote ili jamii ifahamu na kulinda haki za mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni dhidi ya ukeketaji na dhuluma dhidi ya wanawake, iweke mkazo katika kufanya kazi na “*social institutions*” ili kupenya zaidi ndani ya jamii na kupiga vita ‘*patriarchy*’ mfumo dume na kuboresha mahusiano ya kijinsia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pesa kidogo kwenye bajeti, Wizara ijaribu kuibua aina ya maendeleo ambayo jamii ya Kitanzania inahitaji. Jamii inaitazama Wizara



hii kama ndio dhamira ya Jamii kama mfano *conscience of the society in Tanzania*. Vision ya Maendeleo ya Jamii, ndio itakayotuongoza tuweze ku-integrate social and cultural value zetu katika shughuli za maendeleo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta, (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Lucy Nkya, (Mb), Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii mahiri yenye mwelekeo wa kuboresha sekta zote zilizoko ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, napenda kutamka rasmi kuwa ninaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Ninawaomba Mungu awape afya njema ili waweze kutekeleza azma yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hii, sasa naanza kutoa mchango wangu kama ifuatavyo ukiambatana na mapendekezo au ushauri wangu. Hivyo ninayo matumaini kuwa Mheshimiwa Waziri wakati akifanya majumuisho atatoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Wizara hii ni ndogo sana, ni ukweli usiyojificha kuwa Wizara hii ni nyeti sana na ina majukumu makubwa sana katika kuendeleza jami, jinsia na watoto lakini inasikitisha sana kuona kila mwaka bajeti yake inakuwa ndogo sana. Ninapenda kufahamu Serikali inatumia kigezo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Margaret Sitta, alipokuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, alikuwa napitisha bajeti yenye trilioni moja na nusu leo anapitisha bilioni 14.5, je, hii ni kumtendea haki au kumfifisha ari ya kazi? Naiomba Serikali ijitahidi sana kuongeza bejeti ya Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kuongozwa na wanawake tu, napenda kuonyesha furaha yangu pale ninapooa wanawake wenzangu wanakumbukwa kushika nafasi za juu katika kuongoza. Mfano Waziri wa Wizara hii ni mwanamke, Naibu Waziri mwanamke na Katibu Mkuu ni mwanamke na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi inanipa taabu sana na wasiwasi kuwa Wizara hii wanaitazama kwa sura ya wanawake kumbe ni ya maendeleo ya jamii. Kwa nini viongozi wasiwe mchanganyiko kama zilivyo Wizara zingine ili kufuta dhana potofu kwa baadhi ya watu kuwa ni ya wanawake tu. Ninapenda ijulikane kuwa ni Wizara ya watu wote kama ilivyojieleza kuwa ni ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasichana wanaokatisha masomo kwa kupata mimba shule za msingi au sekondari. Ninatoa masikitiko yangu kwa wale wasichana wanaokatisha masomo kwa kupata mimba wakiwa shule za msingi au sekondari. Ninatoa wito kwa Serikali kuwa wasichana wanaopata ujauzito kuwa suala hili, iwe changamoto kwa Watanzania na Serikali pia lakini la msingi ni kuangalia njia za kupunguza mimba mashuleni na sio kuwafukuza wasichana hao wanaopata mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, msichana anapopata mimba kisha akafukuzwa na mwisho wake kielimu inaishia hapo, sio jambo zuri. Ninaiomba Serikali itazame upya Sheria hii na iletwe hapa Bungeni ili ifanyiwe marekebisho ili msichana akishajifungua arudi shuleni kuendelea na masomo ili aweze kupanga maisha yake ya baadaye vema kwa maslahi yake, familia yake na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ushauri huo, napenda pia kutoa ushauri mwingine wa mtoto wa kike kuanza masomo mapema mfano miaka mitano (5) ili amalize elimu ya msingi kabla hajavunja ungo (balehe). Hii itasaidia balehe kumkuta akiwa sekondari kidogo atakuwa na uwezo wa kujitetea pale anapopata kishawishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijana anayempa msichana mimba, inasikitisha sana kijana wa kume anayebainika kumpa msichana mimba adhabu anayopata haimsaidii msichana huyo. Ninaiomba Serikali kuwa kijana anayebainika kumtia msichana mimba kwa njia yoyote ile pamoja na adhabu anazopewa pia alazimike kutunza mimba hiyo, baadaye mtoto huyo na mama mwenye mtoto kwani yeye ndiye chanzo cha yote yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Singida. Napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Singida, Ndugu Mlade pamoja na timu yake yote kwa jinsi wanavyojitahidi kukiendeleza chuo hiki kwa mbinu zao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali kukiongezea nguvu Chuo hiki ambacho sasa hivi ni kikubwa sana kina wanachuo wa bweni 160 na kutwa 20 na wanafunzi wa sekondari wa kutwa 150,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali kuongeza *OC* ya Chuo hiki, ili iweze kusaidia kuendesha chuo hiki kikubwa na kinachotegemewa sana na Mkoa kwani hata Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alifika hapo mwaka huu 2008 Mei.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia chuo kipewe gari jipya, lile ambalo wanalo ni la tangu 1986 (STG), limechakaa sana, linamaliza fedha kwa matengenezo. Vilevile chuo kimejenga ukumbi mkubwa sana ambao utawaingizia fedha nyingi sana ukikamilika. Ninaomba Wizara iwasaidie fedha za kumaliza ukumbi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia chuo hiki kina-hitaji kompyuta za kufundishia kwa sasa tuko karne ya teknolojia mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Msingi – Iramba. Ninashukuru kusikia kuwa Chuo hiki kimepewa pikipiki mpya baada ya ile ya zamani kuchakaa sana. Lakini napenda kuishauri Serikali kuwa chuo hiki kiko chini ya mlima hivyo matumizi ya pikipiki kwa Mkuu wa Chuo mwanamke ni magumu sana. Ninaishauri Serikali kukipa chuo hiki gari, litasaidia kupanda mlima ambao umetanda msitu wa hifadhi, usalama wa pikipiki ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia chuo hiki kimeomba umeme na kiliahidiwa sasa ni miaka minne lakini hakijapata na diseli imepanda kwa jenereta ambalo wanalo na limechakaa pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile chuo kinakabiliwa na tatizo la maji ninamuomba Waziri aende ajionee kero hizi mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afisa Maendeleo wa Wilaya na Kata, napenda kuikumbusha Serikali kuwa mtendaji yeyote wa Serikali ili aweze kutekeleza wajibu wake ni kumpa vitendea kazi. Inasikitisha sana Serikali inapowabagua Wakuu wa Idara mfano Daktari wa Wilaya anapewe gari, Afisa Elimu wa Wilaya anapewa gari na kadhalika lakini Afisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hapewi gari, je, hii ni haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, kupewa gari ili aweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo mfano kuelimisha wajasiriamali vijijini, elimu juu ya ukeketaji, watoto waliotokea kwenye mazingira magumu na kadhalika. Vile vile wale Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata wapewe pikipiki ili zivasaidie kuzifikia jamii kwa kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasikitika kueleza Serikali kuwa tatizo la ukeketaji bado ni tatizo kubwa katika jamii kwa wasichana Mkoa mingi ukiwemo na Mkoa wa Singida. Napenda kulipongeza shirika lisilokuwa na kiSerikali la *AFNET*, kwa kazi kubwa lililofanya kwa kupambana na mila mbaya ya ukeketaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali kuliunga mkono shirika hili kwani sasa hivi limesimamisha huduma kwa kuishiwa na fedha. Aidha Wizara iweke mikakati yake bayana ya kupambana na mila hii mbaya ya ukeketaji wa wasichana, tatizo ambalo linawaathiri sana wasichana kiafya na kupoteza maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake, ninaishukuru sana Serikali kutekeleza ahadi yake ya kuchangia benki ya wanawake bilioni mbili za mwaka jana. Hivyo basi, ninaomba fedha hizi zitolewe haraka ili benki hii iweze kuanzishwa kwani wanawake wanaisubiri kwa shauku kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali ipeleke elimu hii kwa wanawake wote nchini ili waweze kujiunga na benki ambayo itakuwa mkombozi sana kwao na jamii kwa ujumla kwani tunaamini ukimwezesha mwanamke, umewezesha familia na jamii kwa ujumla. Vile vile wanaume wahamasishwe kujiunga na benki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kumi kwenye mfuko wa wanawake, ninaipongeza sana Serikali kwa kuendelea mfuko huu wa wanawake katika Halmashauri zetu za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji katika nchi nzima. Ninasikitika kuijulisha Serikali kuwa sio Halmashauri zote zinatenga asilimia hii kumi. Ziko Halmashauri ambazo hazitengi ipasavyo, ninaitaka Serikali itoe msisitizo mkali Halmashauri ambazo hazitekelezi sasa zitekeleze ili wanawake waendeleo kukopeshwa mikopo midogo midogo ambayo inaendeleza wajasiriamali wanawake na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali huwa inatenga shilingi milioni nne (4,000,000), kutunisha mfuko huo wa wanawake kila mwaka, ninaendelea kuikumbusha Serikali kuongeza bajeti ili Wizara nayo iweze kuongeza kiwango cha fedha katika mfuko huo wa wanawake katika Halmashauri zetu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha watoto wa Mazingira Magumu cha Kititimo Singida Manispaa, napenda kuijulisha Serikali kuwa Kituo cha Watoto waliotokea kwenye mazingira magumu cha Kititimo kilichopo Manispaa ya Singida, aliyekuwa anakihudumia alikwishaondoka kurudi kwao Ulaya ama amekitelekeza. Hivyo, ninaiomba Serikali ibebe mzigo huu kwa asilimia kwani sasa kinaombaomba tu kwa watu mbalimbali mfano Wabunge, Wafanyabiashara, watu wa Mungu, viongozi wa Serikali na kadhalika jambo ambalo linawapa taabu sana wanaokihudumia kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyeti wa kituo hiki cha Kititimo, ninamwomba Waziri kabla Bunge hili la bajeti halijamalizika, tuongozane, aende ajionee watoto hao wanaohitaji huruma yake kwa niaba ya Serikali yetu. Nina matumaini kuwa akienda, atapata jambo la kusema kwa maslahi ya watoto hao ambao wanaishi kwa neema tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninarudia tena kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na niwatakie utekelezaji mwema.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunduru tuna chuo kimoja cha Maendeleo cha Nandembo. Chuo hiki hakijapata fedha za ukarabati kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia jedwali la mgao wa fedha za maendeleo, inaonesha dhahiri jinsi chuo hiki kilivyotelekezwa. Chuo kiko umbali wa km 16 toka Tunduru mjini, hakina usafiri (gari lililopo liko juu ya mawe), genereta halipati kasma ya mafuta, majengo yanashambuliwa na mchwa pamoja na nyufa. Hali ya chuo ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie, mwaka huu chuo hiki kimekumbukwa? Jibu kama ndiyo, ni fedha kiasi gani zimetengwa mwaka huu kwa ajili ya ukarabati wa chuo hicho? Jibu kama siyo, kuna sababu gani za msingi zinazoisukuma Serikali kukitelekeza chuo hiki? Serikali inatoa ahadi gani kwa wananchi wa Tunduru kwa suala la ukarabari wa chuo hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke kwamba chuo hiki kinahudumia takriban wananchi wa Wilaya ya Tunduru na Wilaya ya jirani za Namtumbo na Nanyumbu. Naisihi sana Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha kuendeshea chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuvo vya Maendeleo ya Wananchi, napenda kuishukuru sana Serikali kwa kukitengea fedha shilingi milioni hamsini na nne (Sh. 54,000,000) kwa ajili ya ukarabari wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi wa Chisalu Wilaya ya Mpwapwa. Ukarabati unaendelea vizuri. Hata hivvyo, chuo hicho kinakabiliwa na matatizo yafuatayo:-

- Upungufu wa Walimu;
- Hawana gari (usafiri) gari lililopo lipo juu ya mawe. Serikali iliahidi ukarabati wa gari hilo lakini Serikali haijapeleka fedha hizo hadi leo. *Tractor* ni bovu linahitaji matengenezo makubwa;
- Chuo kipelekewe umeme wa Taifa kutoka Mpwapwa ili Chuo kiwe na umeme wa uhakika;
- Nashauri Chuo hiki kibandilishwe ili kiwe Chuo cha Maendeleo ya Jamii na wafundishwe Maafisa Maendeleo ya Jamii – *Diploma* na vyeti ili kuongeza idadi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kuwa ni wachache na wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa kukosa vitendea kazi, vyombo vya usafiri na kutoendelezwa kitaaluma; na
- Chuo hiki kipanuliwe ili kichukue wanafunzi na wachaguliwe moja kwa moja kutoka shule za sekondari *Form IV* na *VI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Margareth Sitta (mb) Waziri na Naibu Waziri Mheshimiwa Lucy Nkya kwa hotuba nzuri yenye matumaini juu ya Jamii, jinsia na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha Wizara hii kuangaliwa kama Kitengo cha wanawake. Sio Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Watu wengi wanapotosha kuwa hii Wizara ni ya wanawake tu, ukizingatia hii Wizara ni ya wanaume na wanawake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunataka mabadiliko Wizara yenyewe irekebishwe kwa mfano leo Waziri ni Mwanamke, Naibu Waziri ni mwanamke, Katibu Mkuu ni

wanamke, Aliyewasilisha maoni ya Kamati ni mwanamke, aliyewasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani ni mwanamke na wachangiaji wanne wa mwanzoni ni wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya yanasababisha mambo yafuatayo:-

Kwanza, Wizara kupewa pesa kidogo za Bajeti; Wizara hii ionekane ya wanawake kama kitengo cha Serikali; naomba iangaliwe 50/50 katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuishukuru Wizara kutengea shilingi 156,620,000/= katika Chuo cha Maendeleo cha Malya. Pia naishukuru Kamati ya Bunge kukitembelea Chuo hiki. Nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Malya kitakapokamilika, kitasaidia wananchi wengi na mafunzo ya ufundi wa kutengeneza mikokoteni, ambayo itawasaidia wanawake na wanaume sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kuona umuhimu wa Chuo cha Maendeleo cha Misungwi kupewa hadhi ya kufundisha *Diploma* ila nitaomba masomo ya cheti yasifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aje na tamko rasmi la kukemea mavazi ya chupi kwenye miziki yote. Hili lazima Wizara na wanawake wote tukatae kuona wanaume wamevaa vizuri, wanawake wanava chupi. Hii ni kumdhalilisha mwanamke. Hapa hakuna usawa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mitaa inayofuga omba omba na wanasababisha watoto kuzaliwa bila malengo na kuongezeka kwa watoto na wengi wanakosa fursa ya kusoma. Aidha, mijini wale watoto omba omba watafutwe wazazi wao, wawajibishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maneno kubadilishwa. Mara watoto wa Mtaani, mtoto wa mazingira magumu, hapa duniani hakuna watoto wa aina hii. Hii tabia ikomeshwe, watu wawe na malengo ya kuzaa na wawahudumie watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mambo yafutayo yazingatiwe:-

- Mikopo ya *WDF* iwafikie wanawake wa Geita, Ilemela, Nyamagana, Magu, Misungwi na Ukerewe. Naungana na maoni ya Kamati kuwa fedha hizi zipelekwe katika *SACCOS* ili wanufaike wanawake wengi;
- Mafunzo ya wajasiriamali yawafikie hata kwa wanawake wa Mkoa wa Mwanza ukizingatia huko kuna wavuvi na wafanyabiashara ni wengi;
- Asasi ya wanawake wa Maendeleo, Mheshimiwa Waziri awaombe watembelee Mkoa wa Mwanza ili nao wanufaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha tunakwenda vizuri 50/50 ifikapo mwaka 2010, wanawake wengi waingie katika uongozi na utendaji.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa wanawake katika ngazi ya uongozi wa kisiasa, kiutendaji na maamuzi.

Nakubaliana na pendekezo hili kwa sababu kwanza, limo katika Ilani ya Chama chetu cha CCM, lakini Tanzania imeridhia mikataba ya kimafaifa na kikanda ya haki na ustawi wa wanawake. Lakini ili lengo hili liweze kufikiwa, tukazanie elimu ya mtoto wa kike. Pia katika nafasi za uteuzi unaofanywa na Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa madaraka aliyopewa kikatiba, afanye uteuzi kutoka makabila yote (makubwa na madogo, yaliyosoma na yenye elimu ndogo) na kutoka Mikoa yote ili kupata uwakilishi wa utendaji mpana.

Napendekeza chama Chama cha Wanasheria Tanzania (*TAWLA*) kishughulikie masuala yote ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kama vile:- mauaji, ubakaji, vipigo, kuumizwa, (udhalilishaji wa kijinsia) na kadhalika. Lakini kubwa zaidi ishughulikie mimba za wanafunzi wa kike wanayopewa na vijogoo vya kiume mashuleni au majumbani wawapo likizoni. Mahakama za kawaida zinawaachia wahalifu baada ya kutoa hongo/rushwa.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na Watendaji wake wote wa Wizara hiyo kwa hotuba yao nzuri yenye kueleweka ilivyo murua na ufasaha.

Nashukuru pamoja na Wizara hii kuonekana kwamba ndio duni, lakini angalau bajeti yake imeongezwa. Tunashukuru, mwakani izidi kuongezwa kwani Wizara hii imebeba mambo yote ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kimaendeleo. Hivyo basi, iachwe kuonekana kwamba haima umuhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi Wizara inasisitiza kufanya ukarabati wa vyuo vyake vya Maendeleo ya wananchi, kuviongeza nyenzo, vifaa wataalamu na kadhalika. Pia vyuo hivyo viwezeshe kubuni mambo mbalimbali ya kiuchumi na Maendeleo ya kuweza kumkomboa mwananchi kufikia maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mikataba yote pamoja na Miswada ya Sheria inayowahusu wanawake na watoto iletwe haraka Bungeni ili ifanyiwe kazi ipasavyo na sera pia ziboreshwe. Naitakia Wizara utekelezaji mwema.

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta,

Naibu Waziri Dr. Lucy Nkya na Katibu Mkuu Bibi Mariam Mwafisi kwa kazi nzuri kwa kukabiliana na changamoto zinazowakabili katika Wizara yao.

Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Wizara hii ni Wizara mtambuka na ina umuhimu mkubwa sana kwa maendeleo. Lakini bajeti iliyotengwa ni ndogo. Jumla ya Shilingi bilioni 14 kwa ajili ya mambo mtambuka ya nchi hazitoshi, ni vyema mkakati uanze kuanzia Wizarani ili bajeti ijayo iongezwe kwa manufaa ya Taifa.

Pili, Maafisa Maendeleo ya Jamii kwenye Halmashauri zetu ndio viraka vya majukumu mengi. Ataongoza Idara ya Maendeleo ya Jamii, kilimo, ushirika, afya (Ukimwi) na kadhalika. Hivyo, wamekuwa wakisaidia kuziba mapengo ya nafasi mbalimbali na hii ni kwa sababu ya asili (*nature*) ya taaluma zao. Katika hali hiyo, tafadhali Wizara iongeze udahili kwa wanafunzi wanaoingia katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii.

Tatu, Wizara ianzishe mkakati wa kubadilisha sheria zenye *lacunae* kama vile sheria ndogo ya 1971, *the marriage act 1971 (act No. 5 of 1971)* ambayo inaruhusu ndoa chini ya miaka 18 kinyume na katiba iliyotamka umri wa *soundmind* kuwa miaka 18.

Nne, sheria za *affiliation ordinance na adaptation ordinance* zimepitwa sana na wakati kwa watoto waliozaliwa nje ya ndoa na fedha ndogo kwa *putative father* wanazowajibika kuwasaidia watoto hao. Ni aibu kuendelea kusitasita kufanya uamuzi wa msingi bila kujali wakati uliopo. Wizara isaidie kuleta sheria mbadala zenye msaada kwa watoto hao.

Tano, liko tatizo la mirathi kwa wajane na watoto kiasi cha wanaje na watoto kudhulumiwa na baadhi ya ndugu wenye roho mbaya. Sasa tuanzishe utaratibu uliowazi wa kugawa mali za Marehemu kwa wajane na watoto na pia *division of maltimonial assets*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Pia nampongeza mtoa hoja, naipongeze Wizara hii kwa uandaaji mzuri wa kitabu cha hotuba na ni wa makini na kisayansi. Nawaombea Mwenyezi Mungu awawezeshe kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara na Serikali kwa ujumla, kujitahidi kuieleimisha Jamii juu ya usawa wa jinsia. Tatizo kubwa bado lipo katika Jamii hata wanawake wenyewe hawatambui nafasi yao wala wanawake wenzao na hivyo Jamii imeendelea kubeza nafasi ya mwanamke na mwanamke mwenyewe kujibeza. Kwa hiyo, Jamii inatakiwa ibadilike na kuielewa dhana ya jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kuikomboa jamii kifikra, utachukua muda mrefu sana kuwakomboa wanawake.



Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya mkakati wa kufikia 50% ya ushiriki wa wanawake inataka nguvu ya zaidi. Msingi wangu katika hoja hii inatokana na ukweli ukale uliojikita katika Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi ya mwanamke ienziwe, ipendwe, ionekane na kima mwanamke atakayefanya vizuri katika eneo lolote ikijulikana atangazwe ili ionekane tunavyojali na kuthamini mwanamke mmoja akisonga mbele. Pale alipo mwanamke, sisi wanawake wenzie tuunge mkono sana na kumtia moyo, badala ya kucharura au kufedhehesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yetu iendelee kijivunia mwanamke Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro - Naibu Katibu Mkuu, Umoja wa Mataifa. Ukweli ametuletea sifa, wanawake, Taifa na Bara letu zima la Afrika. Naipongeza Serikali yetu.

Aidha, naiomba Serikali, ijitahidi sasa kuendelea kuwainua wanawake wengine ili wawe wengi katika nafasi mbalimbali za nafasi za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba pia Serikali itusaidie katika kufanikisha suala zima la 50/50.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa maandishi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri Katibu Mkuu na wataalam wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Maendeleo kwa kweli viangaliwe kwa jicho la huruma vitengenezwe na kuboreshwa na kupatiwa vitendea kazi, viwe na hadhi inayostahili.

Chuo cha Tengeru kumekuwa na malalamiko kuwa Wizara haipokei cheti cha *Diploma* cha Chuo cha Tengeru na hakitambuliwi na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kama mtu anapomba kazi Wizara hiyo. Kama ni kweli, ni sababu zipi ziinazopelekea kukataliwa kwa cheti hicho? Wananchi waelewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukeketaji unaendelea kwa baadhi ya Mikoja, watoto wadogo amboa hawana uwezo wa kukataa, maoni yangu katika jambo hili ni vyema sasa Serikali ipeleke wahudumu na wataalam wa afya Wilayani na Vijijini na gari la matangazo wakishirikiana na watendaji kama mfumo wa kiliniki na watoto wote wa kike wenye umri mdogo kukagauliwa kujua kama wamekeketwa au la. Njia hii inaweza kusaidia na kupunguza kitendo hiki, potofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili wa wanawake na watoto kumekuwa na ukatili mkubwa kwa kudhalilisha na ubakaji. Serikali iendelee kuelimisha jamii kutokomeza hali hii.

Kuhusu ajira kwa watoto, hivi ni kwanini hapa Dodoma, sokoni kuna watoto wengi wadogo wanaobeba mizigo? Naomba Serikali ifuatilie ili wapelekwe shule wakasome ili wapate haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia ni 17, jambo la kusikitisha bado haijaletwa Bungeni kuridhwa ili iwe sheria na Bunge kupitia na sheria mbalimbali ambazo zinahitaji kurekebishwa na kupewa baraka na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea talaka wakati wa kesi ya kuachana na inapotokea mama kupeleka malalamiko ya kutotunzwa watoto: Je, Serikali haioni kwamba sasa wakati umefika wa kuweka Mahakama maalum ya kushughulikia kesi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na vifo vingi sana vya wajawazito. Hili naomba liangaliwe kwa makini, elimu itolewe ili akina mama hawa wajijue ni mambo gani ya msingi wanatakiwa kuyazingatia wanapokuwa wajawazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nimesikia maiti imefukuliwa ya albino mwanamke na kuchukuliwa viungo vyake. Naomba Serikali itumie vyombo vya usalama kuchunguza zaidi hasa Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaunga mkono hoja mia kwa mia. Baada ya hapo, ninaomba kutoa pongezi kuwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa juhudi zao za kila siku na nia nzuri ya kuleta usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi majuzi tu hapa Bungeni wengi walipata fursa ya kuweka sainsi katika kijarida cha “Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake.”

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa wengi wanazungumizia ule ukatili wa maguvu “*physical*” lakini mimi naomba uonekane wazi pia ule ukatili wa mawazo na fursa sawa kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninaomba kuelimishwa, ni lini Wizara yako itashirikishwa kwenye uteuzi wa Bodi mbalimbali? Ziko bodi ambazo hazina hata mwanamke mmoja, ikiwemo ile ya Tumbaku. Hivi huu sio ukatili? Ina maana wanawake hawawezi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa zoezi zima linasuasua sana na haliendi kwa *speed* tuliyotarajia, ninaomba Waziri atakapokuwa anajumuisha, atueleze endapo hela tunazoendelea kuchangia mafungu zinawekwa *Bank* kuzalisha faida. Pia tungependa kupatiwa *report* kila mwezi. Je, jambo hili linawezekana?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza kabisa natoa pole kwa familia ya aliyekuwa Mbunge wa Tarime - Mheshimiwa Chacha Zakaria Wangwe, Mungu awape subira. Vile vile natoa pole kwa wanachana wote wa CHADEMA Mungu ailaze roho ya Marehemu mahala pema Peponi. Vile vile natoa pole kwa Mheshimiwa Severina Mwijage kwa kufiwa na mtoto, dereva na mjukuu wake. Mungu ampe moyo wa subira na azilaze roho za Marehemu pema Peponi.

Baada ya pole hizo, naomba niende kwenye dira na dhima ya Wizara. Wizara hii inalenga kuiwezesha jamii kuwa yenye mwamko, kujiamimi, kujituma na kuwa na utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii katika kujiletea maisha bora kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na haki za watoto.

Dira na dhima ya Wizara hii imelenga mambo ya msingi kabisa lakini utekelezaji wake ni duni kwani bajeti yake ni ndogo. Vile vile baadhi ya majukumu yametawanywa kwenye Wizara nyingine kama ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na ya Afya na Ustawi wa Jamii. Naomba kujua kuna tofauti gani kati ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Jamii? Kwa nini majukumu yanayofanana yatenganishwe? Vilevile Wizara itupe tofauti ya majukumu yake na yaliyopo kwenye Wizara nyingine zinazoshughulikia masuala ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza na ninasisitiza vita ya kukataa ukatili dhidi ya wanawake na watoto iendelezwe kwa juhudi kubwa. Mila potofu vile vile zipigwe vita, mfano ukeketaji, kurithiwa, Kuna watu wenye ulemavu Jamii nyingine zinadai ni mkosi, kutumia viungo vya walemavu wakiwemo maalbino, vita hii iendelezwe ili amani katika jamii iendelee kuwepo. Sababu watu wenye ulemavu wa viungo na hasa ngozi huishi bila amani. Kwa hiyo, Serikali iwachukulie hatua wote watakaobainika kutenda vitendo vya mauaji ya walemavu ili iwe fundisho kwa wale wote wenye tabia hiyo mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa wa ukimwi unaitesa sana jamii, kwakuwa kuna mkakati wa kupima na kuanza matumizi ya dawa za kupunguza makali ya gonjwa hilo, ninaomba Serikali iangalie au ifuatilie wale wagonjwa waliokwishaandikisha kuchukua dawa wanaendeleaje. Maana kuna taarifa kuwa wengi wao hawaendi tena kufuata dawa. Sasa kuna mawili, aidha, wamezidiwa sana hawawezi kufata dawa au wameshakufa na kuacha mayatima. Tatizo lingine ni lishe, dawa ni kali sana, zinawashinda watumiaji.

Vile vile katika vijiji vyetu hakuna washauri nasaha kwani wengi waliopimwa hukata tamaa na kufa haraka. Sasa Serikali inapohamasisha kupima itawanye na washauri wenye fani hiyo, wawe wamesoma *sociology* na *psychology*.

Mwisho, kwa suala hili, Serikali itoe dawa za magonjwa nyemelezi kwa wenye virusi vya Ukimwi kabla hawajaanza kutoa dawa za ARVs. Dawa hizo zitolewe bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu asilimia 50 kwa 50, nashauri wanawake wajengewe uwezo wa kielimu katika fani mbalimbali ili waweze kujiamini na kujiwezesha kufanya shughuli mbalimbali. Vile vile itakuwa rahisi wanawake kujiamini na kugombea nafasi mbalimbali. Kwa hiyo, mpango mkakati wa kufikia asilimia hiyo 50 itakuwa rahisi kuanzia ngazi ya vijiji mpaka Taifa. Kwani wanawake watakuwa wameelimika na watajitambua hali itakayopelekea kujiamini na kufikia hatua ya kushika wadhifa mbalimbali. Kwa hiyo, yafanyike maandalizi kwanza kabla ya kwenda kwenye hatua hiyo ili kazi ya ushawishi iwe rahisi au mkakati wa 50% - 50% uende sambamba na ujangaji uwezo kwa wanawake. Serikali ituambie imefikia hatua zipi bado miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuwa watoto wa shule za Msingi wanakatisha masomo yao kwa tatizo hilo sugu la ujauzito. Elimu itolewe kwa Jamii kama ilivyo katika mapambano dhidi ya Ukimwi.

Nafikiri ni vizuri elimu au mapambano ya kuzuia Ukimwi yaende sambamba na kuzuia mimba za utotoni. Kwani aweza kupata mimba na Ukimwi juu. Hivyo tatizo la mimba sio pekee, linaambatana na Ukimwi.

Ushauri wangu ni kwamba, ili watoto wa kike wapate elimu, inabidi wote waliopata mimba warudi mashuleni, kwani Taifa litapoteza wasomi wa fani mbalimbali wa kike. Mfano kuna taarifa kuwa mwaka uliopita watoto 18,000 walipata mimba na kusitisha masomo yao. Hii ni hatari, tuchukue hatua haraka na wale akina baba wanaowapa mimba watoto waendeleo kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndoa za umri mdogo, haitofautiani na mimba za utotoni, kwani watoto wakiotelewa hupata watoto wakiwa wadogo na vile vile masomo yao hukatishwa, hivyo haki ya mtoto inavunjwa. Sheria ya ndoa ya mwaka 1971, inaruhusu mtoto wa miaka 15 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi wake. Sheria hii inamnyanyapaa mtoto. Mheshimiwa Rais kila mara anasihiti tuache watoto wa kike wasome. Vipi sheria hii haibadilishwi? Imepitwa na wakati na inamnyima mtoto haki yake ya msingi ya kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Mataifa unamtambua mtoto ni mtu wa chini ya miaka 18. Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) wanaweza kuhamasisha dunia kupiga vita ajira za watoto kutoka umri chini ya miaka 18. *ILO* imesaidia kuokoa maisha ya watoto 35,000 waliokuwa katika ajira mbaya. Hali ya uchumi ya mwaka 2007 inaonyesha kuwa watoto 22,731 ndio ambao tayari wameshajiingiza kwenye ajira mbaya katika Wilaya 11 nchini. Watoto hao wameacha shule na sababu kuu ni umasikini. Wengi wao hutumwa na wazazi na walezi wao, wengine ndio walezi wa familia zao baada ya kuachwa mayatima. Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maadili mema kwa jamii ni jambo la msingi sana. Hapa wazazi, walezi, wanatakiwa wawe makini sana katika malezi ya watoto. Ili kuepusha watoto wasiingie kwenye tabia za ulevi na kuvuta sigara, waache kuwatuma watoto wawashie sigara zao, wasiwape pombe wakiwa wadogo na wasiwatume watoto kwenye vilabu vya pombe na bar. Vile vile watoto wasitumwe mahali popote palipo na

mambo yasiyolingana nao, kama kupeleka ujumbe kwenye ma-bar na ma-*guest houses*. Watoto wapangiwe magazeti na vipindi vya TV vinavyowafaa. Watoto wakilelewa katika maadili mazuri, jamii itakua na maadili mazuri. Hili ni suala la jamii nzima. Kila mtu mahali pake ahakikishe maadili yanatawala watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, niungana na wenzangu katika kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri pamoja na uandaaji mzuri wa bajeti na uwasilishaji mzuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha uliopita, Wizara hii ilitueleza kuhusu kuanzishwa kwa benki ya wanawake katika kipindi hicho na baadhi ya wananchi walinunua hisa. Naomba kufahamu mchakato wa kuanzisha benki hiyo umefikia wapi? Mpaka sasa mtaji umefikia kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina jukumu la kuangalia pia Maendeleo ya watoto wote wa kike na wa kiume, lakini naona imeegemea sana na kuangalia watoto wa kike tu bila kujali athari na matatizo yanayowakumba watoto wa kiume.

Mfano, mtoto wa kike akibakwa adhabu kali hutolewa kama vile aliyebaka kufungwa miaka 30. Lakini mtoto wa kiume akilawitiwa kwa nguvu, (kubakwa) mtuhumiwa hupewa dhamana tofauti na aliyebaka mtoto wa kike na mwishowe mtuhumiwa huyo aliyelawiti mtoto wa kiume huachiwa huru au kifungo cha miaka 2 – 7 tu. Kwa nini Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria na katiba isifanyie marekebisho sheria hii ya kubaka ili watoto wa kiume atendewe haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la jamii ya albino ambayo hivi sasa inaandamwa na mauaji. Ni vyema Wizara hii ikasimama imara kukomesha mauaji hayo kwa kutoa elimu ya kutosha juu ya imani za kishirikina ambazo baadhi ya mauaji wanaziamini, hivyo kuendelea kuwaua ndugu zetu hawa albino. Watoto wadogo Albino wanafungiwa nyumbani na wazazi wao kuogopa wasiuawe, hivyo kuwafanya wakose elimu. Ni jukumu la Wizara hii kuhakikisha kuwa watoto hawa wanapata elimu bora. Naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kunipa nguvu na kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na wale wote waliotoa ushirikiano kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke ni mtu ambaye ana majukumu makubwa ndani ya Jamii. Mfano uzazi, malezi ya mtoto, uzalishaji wa kilimo, utunzaji wa familia, usafi wa mazingira na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majukumu, wanawake wengi wanashindwa kutekeleza majukumu ya maendeleo kutokana na kukosa haki zao za msingi kama elimu. Tunaiomba Serikali iharakishe kuunda Mabaraza ya Watoto kila Mkoa ili wapate kukaa pamoja na kutoa mawazo yao. Vile vile tunaiomba Serikali kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali zinazohusu mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Wizara mama inabeba Wizara tofauti na ina majukumu mengi makubwa lakini bado inapewa bajeti ndogo. Tunaiomba Serikali pamoja na mara hii kuongezewa bajeti, lakini mwaka kesho iongeze kutoka shilingi bilioni 14 – 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaume wapunguze kuwapiga wake zao na kuwanyanyasa na kuwanyonga au kuwaua kwa kupigwa mapanga, wanaume tunaomba wapunguze wivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba wazazi wapunguze hasira watoto. Wanapokosea tuwape adhabu ndogo ndogo, tusiwapige mpaka wakapoteza maisha wala tusiwapige mpaka kuwapelekea kupata ulemavu, tuwe na upendo na sisi turudi utoto mara ya pili watupe upendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwombea kila la kheri Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na awape maisha marefu na afya njema ili walitumikie Taifa letu.

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ruangwa inaongoza nchini kwa akina mama wengi kufa wakati wa kujifungua au mara tu baada ya kujifungua. Pia watoto wengi hufa kabla ya mwaka. Tunaomba tusaidiwe kutibu ugonjwa huu.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara kwa hotuba nzuri yenye kutia matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitalenga kwenye uwezesaji wa wanawake kiuchumi ambapo ni pamoja na uanzishwaji wa Benki ya wanawake Tanzania. Wananchi wengi hawajaelewa kabisa mikakati iliyowekwa katika uanzishwaji wa Benki ya wanawake hali ambayo inarudisha nyuma zoezi la ununuzi wa hisa.

Serikali iweke wazi namna itakavyosaidia benki ya wanawake. Serikali itoe fedha za kulipia gharama za uanzishwaji na kuona umuhimu wa kutoa fedha za uwezesaji wa kiuchumi kwa wananchi (Mfuko wa JK) kupelekwa katika Benki ya Wanawake Tanzania pale itakapoanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, langu ni hilo tu, naomba lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Wizara hii chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Margaret Simwanza Sitta kwa kazi nzuri zinazofanywa kwa ushirikiano na Naibu Waziri wake pamoja na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya bajeti ya mwaka 2008/2009 ni ndogo sana na haitoshi lakini naomba Serikali hiki tulichopewa kitumike vizuri katika mambo muhimu yatakayo shughulikiwa na Wizara hasa uwekezaji wa uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na kijamii kwa nguvu zote, pia kutoa elimu kujenga majengo na miundombinu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kwa makusudi kuzingatia maadili mazuri kwa wananchi wa kiume kwa yanayowahusu, vile vile kwa wanawake wote au jinsi kwa wakubwa na wadogo, watoto na wakubwa kwamba yote hadi kizazi ili kuwa na nchi kama Taifa lenye kuendelea na kuwa na maadili mema.

Kwa niaba ya wananchi wa Magogoni na mimi mwenyewe naunga mkono hoja.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo pekee katika Mkoa wa Manyara kwa miaka hii yote hakijakarabatiwa. Hakuna gari, trekta limeharibika; japokuwa tumekitengea Chuo cha Ardhi ya kutosha.

Naomba tuangaliwe Mkoa wa Manyara kwa jicho la huruma.

**MHE. MARGRETH AGNES MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kuanzia Waziri, Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba nzuri ya kueleweka na yenye matumanini ya kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfuko wa Maendeleo wa wanawake kupitia Halmashauri. Ni vizuri Wizara imeelekeza kuwa mikopoo yake sasa itapitia kwenye SACCOS. Je, utaratibu huu mpya walengwa wameelimishwa utakavyokuwa? Kama sio hivyo fedha hizo zinaweza kuwafaidisha wajanja wachache tu. Zaidi, nashauri fedha za mfuko huu zitumike kutunisha amana za Benki ya Wanawake inayotarajiwa kuanza ili baadaye benki hii iwe na manufaa kwa wanawake wa ngazi zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi wa jinsi watoto wenye ulemavu wanavyoshughulikiwa na Wizara hii kwa sababu ninachokifahamu naona uzito huwekwa kwa watoto yatima, mitaani na wanaoishi kwenye mazingira magumu isipokuwa hivi karibuni kuna msukumo wa kuwaangalia pia watoto albino kwa vile kuna hili janga la mauaji wa albino.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa wanawake kwenye maonyesho ya biashara inatia moyo kwamba Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imedhamira kuongeza idadi ya washiriki hata hivyo nashauri katika kuandaa washiriki hao wanawake wenye ulemavu ambao wanakidhi vigezo vya maonyesho nao washiriki kikamilifu wakielekezwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii, Ustawi, Ushirika katika Wilaya, Mikoa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu sasa sheria mbalimbali zinazomgandamiza mwanamke zinasemekana marekibisho ya kuendelea kuandaliwa. Lakini ikumbukwe kwamba jinsi marekebisho hayo yanavyokawia kuletwa Bungeni ndiyo ukatili na unyanyasaji wa wanawake unavyozidi hasa vijijini. Pia itakuwa vigumu kwa wanawake kufikia asilimia 50 katika ngazi za maamuzi kisiasa, kiuchumi na kadhalika endapo ukatili huo hautakomeshwa kwa kutumia sheria kali zilizo wazi kwa jamii. Kwa msingi huo, nashauri Wizara iharakishe mchakato wa marekebisho ya sheria za ukandamizaji mbalimbali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo, uzima wa kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ukeketaji nchini bado ni mbaya maana bado yapo maeneneo ndani ya nchi hii wanaendelea kwa kasi kubwa tendo hili la ukeketaji. Hivi Serikali pamoja na jitihada yote inayochukuliwa, inasemaje kuhusu hali ilivyo sasa na inayo mikakati gani itatupelekea siku moja tukasema kwamba hali hii imeondoka kabisa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli watoto wa Mitaani, kwa kweli imekuwa ni kero kubwa sana hapa nchini. Ni aibu kwa kiasi fulani kama inapoingia katika miji yote nchini. Watoto wameacha masomo, kukimbilia mijini na kwa bahati mbaya wengine hawana hata jamaa kule mjini walikokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo, wengi wao huwa ombaomba, kufanya kazi ambazo ni aibu hata kuzitaja. Je, Serikali inao mpango gani ambao utalifanya Taifa hili kuondokana na tatizo la watoto wa Mitaani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya wanawake hasa vijijini, kwa kweli kama kweli Serikali imejipanga kuleta Maendeleo ya wanawake wa nchi hii na hasa wale wanaoishi vijijini- ambao mimi nawaita ni *Disadvantaged* kwanza ni kuwapatia elimu ya kujitambua kwamba na wao ni watu sawa na wengine na kwa hiyo, wanao wajibu wakujitafutia maendeleo yao wenyewe na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Serikali ina mpango gani wa kuwaendeleza wanawake na hasa wale wanaoishi Vijijini?



Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mimba za wasichana, ni tatizo ambalo imekuwa sugu sana hapa nchini, kwa maana kwa kweli juhudi kubwa imechukuliwa na Serikali lakini bado hali haijabadilika. Sasa ni vyema tutafute kinga kuliko tiba. Lakini je, hiyo tiba ipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wale wanaobebesha wasichana mimba wanashughulikiwa, basi naamini hali ingepungua kwa kiasi Fulani. Lakini bado wanaofanya hivyo hawajachukuliwa hatua inayofaa. Naomba Wizara ichukuehatua kukabili hali hii. Ahsante nawasilisha.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Napongeza kwa usimamizi mzuri wa Wizara pamoja na changamoto zilizopo Wizarani. Najua Mheshimiwa Waziri na Naibu ni wapya, lakini sio wapya kiutendaji, ni wazoe fu walioboea.

Nasema ni watendaji walioboea kwani mara tu walipoingia ofisini walianza kazi kama askari wa miavuli kwa kufuatilia hasa vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kikiwemo na Chuo cha Malya ambacho kinatakiwa kiendeleze jamii inayoizunguka ambayo kwa mwaka huu wa fedha 2008/2009 kama ni kweli kimepangiwa zaidi ya shilingi milioni 159 kwa ajili ya shughuli mbali mbali ikiwemo ukarabati wa mabweni yaliyo katika hali duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo hicho kilikuwa na gari lake, lakini gari hilo liliharibika hadi leo halijulikani lilipo. Kama liliuzwa, naomba Wizara inipe majibu, nini mbadala wa gari hilo kwa chuo hicho? Gari hilo lilikuwa moja ya vitendea kazi vilivyokuwa vikisaidia kurahisisha shughuli za chuo.

Wizara inafahamu matatizo mengi yaliyopo chuoni hapo mbali ya gari, tatizo kubwa ni la walimu, vitanda, magodoro na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa eneo la chuo ili kuepusha migogoro ya ardhi ambapo hapo awali zipo tetesi kuwa baadhi ya eneo lilimegwa na kuuziwa mfanyabiashara aliyetaka kujenga kiwanda cha kuchambulia pamba. Naomba Wizara imwombe Mkurugenzi ili upimaji wa eneo la Chuo ufanyike haraka ili kuepusha migogoro kama nilivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili wananchi wa Malya wafaidike na Chuo hicho, naiomba Serikali kupitia Wizara hii ifanye utaratibu wa kuwapata walimu wanaoweza kutoa elimu ya malezi bora ya watoto ili kupunguza idadi ya watoto wa Mitaani. Chuo hicho Wizara yako ielekeze semina zote zinazohusu Ukimwi zifanyike Malya ili Chuo hicho kiweze kupata mapato pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Malya endapo kitakuwa na vifaa, walimu wa kutosha pamoja na mgao mdogo na kupata vijana wengi katika maeneo hayo watapata ujuzi wa kupelekea kujiajiri hivyo, kupunguza ukali wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Mji wa Malya utapata umeme mwaka huu, tunaiomba Wizara iandae pesa za kuweza kufanya *wiring* ili kukiwezesha Chuo hicho kuwa na umeme ili kuongeza ufanisi wa shughuli zinazoendelea na zitakazofanywa hapo hasa za ufundi.

Mwisho, napenda kuiomba Wizara katika utaratibu wa utoaji mafunzo ya rejea kwa watalaam ngazi za Kata siyo vizuri kutenga maeneo au Mikoa yenye maendeleo. Nashauri rejea ya mafunzo haya yafanyike vijijini kwenye Kata kama zile za Malya, Lyoma, Walla, Mahigisu katika Wilaya ya Kwimba kuliko kupeleka rejea hizo Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na kadhalika. Pelekeni semina/rejea kule kwa wahitaji. “Yesu alikuja kuwaponya wenye dhambi siyo wazima.” Naunga mkono.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa kweli kazi wanayoifanya ni ya mfano. Naomba waendeleo hivyo hivyo kwa manufaa ya kuendeleza jamii na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo la Iramba Mashariki kuna Chuo cha Maendeleo ya Msingi. Awali ya yote naipongeza sana Wizara kwa kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa chuo chetu. Ukarabati umefanyika vizuri sana na sasa chuo kinapendeza mno, mmonyoko wa ardhi uliokuwa hapo mwanzo umekwisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza sana Mkuu wa Chuo na Wasaidizi wake kwa kazi nzuri wanazofanya hapo chuoni. Pia niwapongeza sana kwa kutunza mazingira na wameanzisha na kuutunza msitu mkubwa wa asili kwa faida ya chuo kama kuna kuondoa mmomonyoko wa udongo na hatimaye wana mpango wa kufuga nyuki. Naomba Wizara iwasaidie kupata mizinga ya nyuki wanaouma na wasiouma na wapate mtaalamu wa kufanya kazi ya kuweka mizinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Msingi bado kina matatizo makubwa matatu. Umeme huu ni mwaka wa nne toka Serikali iahidi kupeleka umeme toka Kinampanda ambapo ni kilomita nne tu kutoka chuoni. Gharama yake wakati huo ilikuwa ni hilingi milioni 83.4. Wizara ya Nishati na Madini walishaahidi kufanya hiyo kazi, naomba Mheshimiwa Waziri asaidie kumkumbusha Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la muda mrefu ambalo lipo kwenye chuo chetu ni usafiri (gari). Chuo chetu kipo karibu kilomita 50 toka Singida na kilomita 30 toka Kiomboi ambako ndiko mishahara na mahitaji mengine hupatikana na pia chakula na mahitaji mengine hupatikana Singida. Narudia kuomba chuo hiki kipatiwe gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado chuo kinakabiliwa na matatizo ya maji. Naomba sana Wizara isaidie kupata maji ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba chuo kiongezewe fedha za matumizi ya kawaida. Naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya. Hongereni sana.

Sera ya Taifa kuhusu wasichana wanaopata mimba wakiwa shuleni. Suala la mimba shuleni ni changamoto yetu kuhakikisha kuwa inadhibitiwa, ipungue kama siyo kukomesha kabisa. Kwa kuwa mpaka sasa hakuna sera ya Taifa kuhusu suala hili, utaratibu uliopo ni kumfukuza shule msichana aliyepata mimba hii siyo sawa! Siyo sawa kumfukuza shule jumla kwa sababu tunamnyima haki ya msingi ya kupata elimu, tunaendelea kujenga kundi la watu wasiosoma, licha ya azma yetu na dunia nzima kuwa kila mmoja apate elimu, msichana husika anakosa fursa ya kuwa mama bora kwa maisha ya baadaye na watoto wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, anayempa ujauzito hawajibiki kumtunza msichana na mtoto atakayezaliwa. Pia, kama ni mwanafunzi anaendelea na shule, tunawalaani milele, wanaoathirika zaidi ni watoto wa wananchi vijijini, maskini na wafugaji. Hivyo, napendekeza tuweke mipango madhubuti ya kuwakinga wasichana wasipate mimba shuleni, wako watakaopata mimba, kwa bahati mbaya waruhusiwe kurudi shuleni baada ya kujifungua. Anayehusika na ujauzito wa mtoto wa shule, awajibike katika malezi, siyo kumfunga jela, bali amhudumie msichana na mtoto atakayezaliwa. Mapendekezo haya, na mengine muhimu katika suala hili, yawekwe kwenye sera ya Taifa kuwalinda watoto (wasichana) hao. Ni wakati muafaka sasa kuwa na sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwakilishi wa asilimia 50 kwa 50, suala hili si tu la kisiasa, bali pia ni la jamii nzima ya Tanzania. Uamuzi wa kuwa na uwakilishi wa asilimia 50/50 utagusa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ambayo inawahusu Watanzania wote. Hivyo suala hili ni muhimu kujadiliwa Kitaifa kabla ya kulifanyia uamuzi wa mwisho. Ikumbukwe, hata uwakilishi wa sasa wa jinsia Bungeni, kwa mfano, ni suala la Kikatiba pia. Tusiamue kisiasa, bali kwa kuzingatia hali halisi tukishirikisha maoni mahususi ya jamii nzima.

Mheshimiwa Naibu spika, naipongeza Wizara kwa kupigania kupata Bajeti kwa ajili ya ukarabati wa majengo katika vyuo vya maendeleo hususani kile cha Buhangija, ambacho bado mazingira hayaridhishi. Naomba pesa zilizotengwa shilingi 95,376,700/= ziwahi kutolewa kwa kazi zilizopangwa. Bado kunahitajika pesa zaidi kwa Bajeti zijazo ili kuboresha Chuo cha Buhangija katika maana ya majengo, vifaa vya kufundishia, mazingira ya chuo (ikijumuisha upandaji wa miti) na mengineyo bila ya kusahau kupeleka wakufunzi wa kutosha wenye sifa. Nawatakia kila la kheri.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa iwapo Wizara hii kama itatumika vizuri ndiyo injini ya maendeleo kwa kuwa inayo watumishi wenye utaalim mtambuka, wamesambaa nchi nzima lakini inaeleza, Wizara hii haipewi kipaumbele kabisa kwa kuwa mambo mengi ya maendeleo ya jamii yanafanyika katika Wizara nyingine na matokeo yake ni kuwa maendeleo ya jamii inaonekana kama mratibu wa mambo ya maendeleo na jinsia lakini bila kuwa na majukumu yaliyo wazi. Maofisa Maendeleo ya Jamii waliotapakaa nchi nzima hawapewi nyenzo za kufanyia kazi, hawana Bajeti ya kutosha, hawana usafiri sasa wanategemewa vipi kufanya na kutekeleza majukumu yao.

Hivyo basi, Serikali iko tayari kufanya tathmini ya kina ili kubaini malengo, majukumu mahususi yanayotakiwa kutekelezwa na Wizara hii, pamoja na maofisa wake walioko hadi ngazi ya kata na pengine vijijini? Kufanya tathmini ya kina ya nyenzo na rasilimali zinazotakiwa ili Wizara hii iweze kufanya kazi yake kama injini ya maendeleo. Kufanya tathmini ya kina kuhusu majukumu ya maendeleo ya jamii yanayoweza kutekelezwa vizuri zaidi (*effectively and efficiently*) na Wizara hii kuliko Wizara zingine na kuyaondoa kwenye Wizara hizo ili yaweze kusimamiwa na kutekelezwa kikamilifu kuliko Wizara hii kuonekana kama mirathi wakati kazi ya uratibu inafanywa na ofisi ya Waziri Mkuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo hatutafanya *restructuring* ya msingi na ku-*streamline* shughuli za Wizara hii naogopa na ninachelea kusema kuwa Wizara hii itaendelea kuonekana. Si muhimu, haina kazi zinazoeleweka na hivyo kuendelea kupewa ruzuku au fedha kidogo sana kama Bajeti. Nashauri Mheshimiwa Rais ashauriwe kufanya tathmini zilizotajwa na *restructuring* ili Wizara hii iweze kufanya kazi zake za msingi, yaani kukuza, kutekeleza na kusimamia masuala yote yanayogusa moja kwa moja maendeleo ya jamii, jinsia na watoto, pamoja na kuwa mambo haya bado yatabaki kuwa mtambuka. Lakini bado tunaweza kuweka wazi mambo yanayopaswa kusimamiwa na kutekelezwa na Wizara kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, uwaji wa maalbino. Ni jambo la kusikitisha jinsi binadamu wenzetu wanavyoawa kikatili sababu ya watu wachache wenye kutaka utajiri wa haraka hasa kwenye madini wenye kuamini ushirikina. Ni wajibu wa Serikali sasa kutumia njia kama alivyotumia mtangazaji wa *BBC Ms. Vicky Mtetema* ili kuwakamata waganga wote na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria na sheria uchukue mkondo wake. Vile vile nina hakika kabisa wanakijiji wakitumika kwa kupewa elimu na kupewa zawadi kwa atakayefichua waganga hawa itakuwa ni rahisi kuwapata sababu hawa watu wanaishi katika vijiji hivi hivi vya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ndogo ya mwaka 1971, pamoja na Serikali mara nyingi kujibu baadhi ya maswali hapa Bungeni kwamba wanashughulikia suala hili sababu linaingilia imani za watu. Ni kitu cha kusikitisha kuanzia mtoto wa miaka 15 anaruhusiwa kuolewa kwa ridhaa ya wazazi wake. Lakini hapo hapo Tanzania hii tunaupungufu wa wataalam na vile vile tunajitahidi kumwezesha mwanamke kielimu na hatimaye apate nafasi katika uongozi. Ikiwa sheria hii haitarekebishwa na watoto hawa

wa kike wakaolewa wakiwa na miaka 15, je, tutaweza kufikia azma yetu ya *fifty fifty* hapa Tanzania?

Kuhusu watoto yatima na mashirika yasiyo ya KiSerikali, Mashirika haya yamekuwa yakipokea misaada mingi ya fedha, vyakula, mavazi, dawa na kadhalika. Lakini sina uhakika kama misaada hii inawafikia walengwa, ningetaka kujua, je, Serikali inafuatilia kwa njia gani kuhakikisha misaada inawafikia walengwa? Kila kukicha zinafunguliwa *NGO's* nyingi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, vyuo vilivyopo kwa sasa hivi vipo kwenye hali mbaya majengo ni ya kukarabati havina walimu wa kutosha.

Nashauri, Serikali badala ya kujenga vyuo vipya vikarabati vilivyopo, waandae walimu wa kutosha na wataalam hawa wakilitumiwa elimu iende mpaka kwenye vitongoji na vijiji. Nina hakika kabisa vyuo hivi vikiboreshwa lazima tutapata wanafunzi wengi watakaojiunga.

Mwisho kabisa naomba iangalie sehemu ya kufanya biashara kwa wanawake wajasiriamali isiwe tu katika Jiji la Dar es salaam pia ianze katika mkoa yote ya Tanzania sababu hata huku kuna wanawake. Ni matumaini yangu Wizara hii itaendelea kwa nguvu zote kuhakikisha inatekeleza mpango wake wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto hususan wakati wa mirathi kunakuwepo na dhuluma nyingi sana dhidi ya wajane na watoto wao.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi kutoa mchango wangu. Nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa umahili wao katika kusimamia shughuli za Wizara vizuri. Hii yote inanifanya kwa niaba ya wananchi wa Misungwi niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri kukubali ombi la siku nyingi la Chuo cha Maendeleo ya Jamii kuanza kutoa stahada na shahada kwa mwaka 2008/2009 naipongeza sana Serikali, pamoja na mazuri hayo ipo tetesi ya kuacha kutoa mafunzo ya ngazi ya cheti kwa chuo hicho kitendo ambacho si kizuri, kitakatisha tamaa wananchi wa Kanda ya Ziwa ambao tegemeo lao ni chuo hicho na mwamko wa kuanza kukitumia umeanza kuonekana. Mfano kilichokuwa Chuo cha Ushirika Moshi baada ya kuwa Chuo Kikuu hakijaacha kazi/kozi ya kutoa mafunzo kwa ngazi ya cheti katika Chuo Kikuu hicho. Pamoja kuwa na chuo kingine Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tunaipongeza kufanya ukarabati mkubwa kwa chuo chetu hasa ujenzi wa ukumbi wa chakula, mabweni na vyumba vya madarasa tunashukuru sana. Leo hii nimeona taarifa ikionyesha maendeleo ya ununuzi wa samani kitu ambacho tunazidi kukubaliana na juhudi za Serikali kuwa zina nia nzuri kwa Watanzania kupitia chuo hicho cha Misungwi.

Ombi, nyumba za watumishi ni haba na hazijafanyiwa ukarabati naiomba sana Serikali ilione suala hili kuwa ni tatizo linalohitaji ufumbuzi wa haraka hii itawafanya walimu wetu watoe mafunzo kwa ufanisi bila hofu ya mahala pa kuishi. Suala lingine ni

hali ya maslahi si nzuri sana, Serikali itoe motisha kwa walimu ili wafanye kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikafanya utaratibu wa kuwasiliana na Wizara ya TAMISEMI juu ya kuwaajiri moja kwa moja wahitimu wanaomaliza kozi katika vyuo vya maendeleo ya jamii ili wananchi vijijini wawe wataalam wenye taaluma nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho sisitizo ni mafunzo ya cheti kuendelea kutolewa Chuo cha Misungwi si vinginevyo kuepuka kuuwa msingi ulioanza kujengeka. Serikali yetu ni sikivu nategemea majibu mazuri kuepusha kusimama na kutaka ufafanuzi wakati wa vifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuunga mkono mia kwa mia.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu spika, nami pia napenda kuungana na Wabunge wenzangu katika kuchangia Bajeti ya Wizara hii. Kwanza napenda kuongelea tatizo la watoto wa mitaani. Watoto hawa wanazidi kuongoezeka kwa kasi katika Jiji la Mwanza, watoto hao imekuwa kero na hata kufikia kuwa tishio la wananchi ambao hutembea kwa miguu zaidi ya saa moja usiku. Pia imekuwa tatizo kwa wenye magari kwa kuibiwa vioo na hata lebo za magari yao, na suala hili hufanyika hata nyakati za mchana. Hivyo naiomba Serikali kushirikiana na wahisani, kutafuta eneo nje kidogo ya jiji la Mwanza kwa ajili ya matunzo ya watoto hawa wasiweze kuja mjini kwa urahisi. Kama ilivyo sasa ambapo wahisani wa *Kuleana* wanawalelea watoto hawa katikati ya jiji na kama mtoto wa mtaani ataonekana mjini basi akamatwe na achukuliwe hatua.

Pia kama ushauri utakubaliwa watoto hawa wajengewe shule huko huko na waweze soma, hata wale ambao wamezidi umri, wafundishwe ufundi. Tunaomba wahisani (*Kuleana*) waombwe hilo, kama tutaongea nao na watakubali tutaondokana na tatizo.

Pia kufuatilia watu ambao husema wanalea watoto yatima na wanapopata ufadhili misaada hiyo haifiki kwa watoto yatima. Vitendo vya kuanzisha vituo vya kulea watoto yatima kwa sasa vimekuwa vingi sana kwa hiyo, tunaiomba Wizara ihakikishe vituo hivi ili kuchunguza malezi ya watoto hawa kama yanakidhi haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naiomba Wizara iwatupie macho ya huruma akinamama wajane na wale wanaoishi na virusi vya UKIMWI, kwa kuwapatia mikopo ili waweze kujiendesha na kupunguza kundi la ombaomba. Na wale wanaoishi na virusi vya UKIMWI ambao wanatumia dawa, waweze kujihudumia na kuweza kujinunulia lishe.

Pia naomba Wizara ifuatilie suala la watoto yatima ambao waliorodheshwa na wanapatiwa huduma za sare za shule na daftari kwani wengi wao hawapati mahitaji yao wakati muafaka na hata kusuasua katika masomo yao. Lakini cha muhimu naomba kundi hili la watoto yatima waweze kusamehewa ada kwa umoja toka elimu ya msingi hadi

sekondari, kwani wengi wao hushindwa kuendelea na masomo yao kwa ajili ya kuchangia ada, majengo na madawati. Pia michango mingine ambayo hawana uwezo wa kulipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara hii itetee zaidi unyanyasaji wa wanawake. Pia itoe elimu ya ufahamu kwa akinamama, kupitia makongamano na kadhalika, kwani wanawake wengi ni waoga na hawajui haki zao na ujasiri wao ni mdogo. Wizara iwahamashe watoto wa kike na kutoa tahadhali kwa mabinti katika ubebaji mimba na kuacha masomo. Wajue kusema hapana. Makongamano ya watoto wa kike yafanyike mara kwa mara ili waweze kujua nini wanatakiwa kufanya. Kama sio mimba wanaweza pata hata UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaombeeni kazi njema ili tupate Taifa lenye watu waadilifu. Ahsante.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na watendaji wa Wizara kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba nzuri napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare kilipanda daraja mwaka jana na kuanza kutoa *Diploma*, tunaishukuru Serikali kwa uamuzi huo. Lakini yapo matatizo mengi katika chuo hicho ambayo ni pamoja na upungufu wa walimu, miundombinu mibovu na hii ni pamoja na chuo kutokuwa na uzio ambao ni hatari kwa usalama wa mali na watoto wa kike walioko chuoni hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufahamu Wizara imejiandaajie kupunguza matatizo hayo yanayokikabili chuo kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Chuo cha Maendeleo ya Jamii *FDC* kinalo tatizo kubwa la fidia ya wananchi waliopo katika kiwanja cha chuo hicho. Wizara inalijua tatizo hilo la muda mrefu na iliahidi kulishughulikia kwa kulipa fidia, sasa napenda kufahamu Serikali imefikia wapi kulipa fidia kwa wananchi ili chuo kiweze kufanya uendelezaji wa chuo hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kushirikiana na Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote kwa kuendeleza Wizara hii na jamii kwa ujumla. Pamoja na kwamba Bajeti ya Wizara kila mwaka inakuwa ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa mwaka huu imeongezeka kidogo lakini bado haitoshi. Nashauri Serikali iiongezee fedha Wizara hii nyeti mwaka huu. Naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia yafuatayo, kwanza ni kuhusu sheria zinazowakandamiza wanawake na watoto. Kuna baadhi ya sheria mpaka sasa zinawakandamiza wanawake kwa hiyo, naiomba Serikali ilete Bungeni Miswada hiyo ili irekebishwe na kupatikana sheria zinazowalinda wanawake na vile vile watoto kwa ujumla. Pia elimu kwa wanawake, elimu ni msingi wa maisha na unapomueleimisha mwanamke umeelimisha jamii. Naishauri Serikali itoe elimu zaidi kwa wanawake juu ya kuendeleza miradi yao ya maendeleo na jinsi ya kutafuta soko la uhakika kwa bidhaa zao.

Kuhusu Benki ya Wanawake. Kwa nini mpaka leo benki ya wanawake hajaanza kazi ili kuwakomboa wanawake? Bajeti ya mwaka 2007/2008 Serikali iliahidi kuanzisha benki hii lakini mpaka leo haijaanza kazi, kitendo ambacho kinadhihirisha kwamba wanawake bado wanawekwa nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri benki hii ya wanawake ianzishwe ili wanawake wawe na sehemu yao ya kutatua matatizo yao ya upatikanaji wa mikopo maana benki nyingine ni vigumu kupata mikopo kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ichangie moja kwa moja katika uanzishaji wa benki hii. Mikopo kwa wanawake wajasiriamali (*SACCOs*), naomba kujua kwa nini mikopo huwa haiwafikii wanawake vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa JK haijulikani kama unawanufaisha wanawake, bali unawanufaisha wafanyabiashara wakubwa kwa maeneo mengi ya Tanzania. Serikali iliona hili na iwasaidie wanawake wajasiriamali maana ndio wanaoleta maendeleo ya nchi hii, kwa sababu wao ndio wakulima na wafanyakazi wazuri kwa uadilifu wao mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikitoa mikopo kwa wanawake wanakuwa na uhakika wa fedha zao kurejeshwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa ya ngono. Nasikitishwa sana kwa tatizo hili linalowadhhalilisha wanawake walio wengi pale wanapojitahidi kutaka kujikwamua kiuchumi kwa kuomba kazi, sehemu tofauti na hasa zile kazi za sekta binafsi (ngono) hotelini, viwandani na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi huombwa rushwa ya ngono ili kupatiwa kazi. Hii si haki ya binadamu, nashauri Serikali ifuatilie sana.

Suala la ukeketaji wa watoto ni kinyume cha haki za binadamu. Ipo mikoa inayoongoza kwa unyanyasaji huo kwa watoto. Tatizo hili ni kubwa sana na inadhalilisha watoto wa kike, na inaonekana baadhi wazazi wanafurahia ukeketaji wa watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itoe elimu zaidi kwa wazazi dhidi ya ukeketaji wa watoto. Kuhusu watoto yatima, watoto yatima ni wetu wote lakini kuna baadhi ya koo (familia) wananyanyasa sana watoto yatima.



Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itoe elimu juu ya suala hili la kutowanyanyasa watoto yatima na badala yake wawalee kama wanavyolea watoto wao wanao wazaa. Kama jamii haijawalea watoto yatima watalelewa na nani? Naishauri Serikali ifuatilie watoto hawa hasa vijijini na kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanawake wajane, wananyimwa haki zao za msingi pale mume anapofariki, wajane hunyang'anywa hata nyumba, shamba, vifaa na hata watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ifuatilie sana dhidi ya vitendo hivi kwa wanawake wajane ambao hawana hatia. Pia elimu itolewe na sheria zifuatwe na ndio maana nasisitiza kuwa na sheria zisizowakandamiza wanawake na wajane.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kupewa Wizara hii muhimu kwa jamii ya Watanzania. Napenda kupongeza kwa usimamizi wa vyuo vya elimu zinazosimamiwa na Wizara yake. Kwa vile tumeanzisha shule nyingi za sekondari ingependeza Wizara iongeze nafasi za shule kwa wanafunzi ili waweze kupata elimu ya kujenga uwezo wa wanawake na wanaume ili waendeleze miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la unyanyasaji wa wazee vikongwe wanaouawa na watu wenye imani potofu eti vikongwe hao wanaloga pamoja na mauaji ya albino ambao hawana hatia. Serikali wachukue hatua kali ya adhabu kwa wale watakaopatikana na makosa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watoto wengi wanaozurura mijini kuombaomba wengine wanatumwa na wazazi wakaombe fedha barabarani, ningeshauri watoto hao wapelekwe kwa wazazi wao na wazazi wapewe adhabu kutokana na kuwakataza watoto kwenda shule na kuwapotosha kuwa ombaomba jambo ambalo linawapoteza watoto hao.

Kuhusu mikopo kwa wanawake, Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Longido ni wilaya mpya. Napenda kueleza kwamba mikopo yote iliyotolewa kabla ya wilaya kugawanywa na Monduli hawajawahi kupata mikopo. Kwa kuwa sasa Longido ni Wilaya yenye halmashauri yake naomba tupatiwe mikopo kwa wanawake wa wilaya hii mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kwenye jimbo la Longido tuna shule ya wanafunzi wasioona. Naomba shule hiyo Wizara yako ichukue suala la shule hiyo kuwapatia vifaa muhimu kwao.

Mwisho naunga mkono hoja, bali kumbuka kuwapa wanawake wa jimbo la Longido mkopo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Margret Sitta, kwa kuwasilisha vyema hotuba yake. Napenda pia kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, kwa kazi nzuri anayofanya kwa ushirikiano na Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru kwa kuboresha kilichokuwa Chuo cha Mafunzo ya Maendeleo Vijijini Mlale na kuwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii kilichopo mkoani Ruvuma. Lakini ningependa pia kuiomba Wizara kuja Wilayani Namtumbo, Kata ya Kitanda, kijiji cha Mputa tuna majengo imara yaliyokuwa Makao Makuu ya kambi ya wakimbizi wa Msumbiji na sasa yapo hayana shughuli *productive* kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna majengo ambayo yanaweza kuwa nyumba za wakufunzi na mengine kuwaka madarasa na shughuli zingine zitakazopangwa. Majengo hayo yapo katika eneo zuri, ningependa Wizara ifike kuona kwani wanakijiji wenyewe katika mkutano wa hadhara wa kijiji ndio waliniomba tuone jinsi ya kuleta chuo chochote kwa ajili ya kuendeleza jamii. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima na afya kamili na kuweza kushika kalamu na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia kwa kuiomba Serikali ifanye haraka kwa kuleta sheria ya ndoa na mirathi ili tuepushe balaa la kuwaozesha watoto wangani wadogo na vile watu hasa wanawake wapate mirathi bila ya matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi wanateseka sana na kupata mateso kwa sababu hakuna sheria madhubuti au sheria zilizokuwa zimeshapitwa na wakati hasa ukizingatia watoto wanaozaliwa nje ya ndoa mpaka leo wanalipwa shilingi 100/= ya kujikimu je, hii kweli ni haki? Vile vile naiomba Serikali iweke sheria kali zaidi hasa ukizingatia bado wanaume wamekuwa sugu sana katika kuwabaka watoto wa shule na kuwapa mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakusikitisha zaidi juzi katika vyombo vya habari ameoneshwa mtoto wa shule mwenye umri wa miaka 11 tu amebakwa na amepata mimba je, Serikali inasemaje katika kadhia hii je, hatuoni hapa panataka juhudi za maksudi kuhusu watoto wetu na hawa wanaume ambao hawana imani na watoto wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhalifu huu wa kuwabaka watoto na kuwapa mimba za utoto ndio unaochangia vifo vingi vya wanawake wenye mimba na wale wanaojifungua, naisisitiza Serikali iwachukulie hatua kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu albino Serikali ina mkono mrefu, la kusikitisha ni kwa nini mambo haya ya kuwaua albino bado yanaendelea na watu wanaofanya hivyo wanajulikana, kwani naamini kama Serikali ifanye ushirikiano na raia pamoja na kuwapa motisha vile vile na kuwahakikishia usalama wa maisha yao basi naamini kuwa watakuwa mstari wa mbele katika kuwafichua wahalifu hao ambao hawaitakii mema nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipange mipango madhubuti ya kuwasaidia watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu wawajengee makazi maalum ya kuwasaidia, wasiwaachie *NGO's* peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ahsante.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Waziri Mheshimiwa Margaret Sitta na Naibu wake kwa uwezo wao mkubwa wa kuongoza Wizara hii.

Nashauri pamoja na kuwa kuna vyuo vitano vitakavyokarabatiwa mwaka huu, Wizara iwe karibu na makandarasi watakaoifanya kazi hiyo. Pia akinamama na vijana wasomi wahamasishwe ili kuwa wakufunzi katika vyuo vyetu vya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii ili kazi ya Wizara hii iweze kuonekana na kuleta ufanisi katika maendeleo ya watu wetu. Inasikitisha kuona Wizara hii ndiyo ya mwisho katika kupewa fedha. Serikali ifanye juhudi za makusudi kutoa pesa ili kuanzisha benki ya wanawake. Ikumbukwe kuwa wanawake ndiyo wajasiriamali wakubwa katika nchi yetu. Kuanzishwa kwa benki hii kutamkomboa mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, witi wangu ni kuwa ukimwelimisha mwanamke umelielimisha Taifa zima, tuwasaidie wanawake. *It can be done play your party.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni mtambuka kwa maana ya kwamba inaingiliana na Wizara nyingine kama ya Afya na Ustawi wa Jamii, Elimu, TAMISEMI na nyingine nyingi lakini ufinyu wa Bajeti hii unatokana na muingiliano huo. Lakini kuna mambo ya msingi ambayo Wizara hii inapaswa kusimamia ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wanawake kiuchumi, kielimu na kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina jukumu kubwa la kusimamia, maendeleo ya watoto. Kwa kuwa kibailoia mtoto tangu akiwa tumboni mwa mama yake (mimba) hadi anapozaliwa na kufikia umri wa miaka mitano, ubongo wake hukua kwa 70% hadi 80%. Hivyo hiki ni kipindi muhimu sana kwa watoto hawa kwa makuzi yao na hivyo wanapaswa kupata lishe bora na malezi mazuri ili wakue wananchi wema na hivyo kutohatarisha si tu maisha yao lakini pia kwa wananchi wengine. *Child Development Theory*, inasema kwamba mtoto wa *under five years* akitunzwa vyema, basi mtoto huyu ataleta tija kwake binafsi na kwa Taifa kwa ujumla.

Kwa kuwa dira ya Wizara hii ni kuwawezesha Watanzania kuwa na mwanamke na kujiamini ili kujiletea maisha bora kwa kuzingatia usawa na kijinsia na haki za watoto na kwa kuwa Wizara hii ina Bajeti ndogo sana. Je, Wizara inategemea nini katika

utekelezaji wa dira yake hii hasa ikizingatiwa kuwa dira hii inalenga kwa watu milion 34 na zaidi? Wizara ina mikakati gani kuhakikisha lengo lao hilo linafikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali Wizara hii imekuwa na mwingiliano mkubwa sana kwa mfano kuna idara ya maendeleo ya jamii na idara ya ustawi wa jamii na idara hizo zipo chini ya Wizara mbili. Hili ni tatizo kubwa sana kwa ufanisi kwani kwa vyovyote vile kutakuwa na kukwepa majukumu na hivyo kutupiana lawama. Vyuvo vya maendeleo na vituo vya maendeleo vilitumika huko nyuma kama sehemu nyeti sana kwa jamii kushirikiana, kuelimishana na kutiana shime katika maendeleo, cha kushangaza vituo vile havipo tena. Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii havipati fedha za maendeleo ili kukarabati vyuo hivyo na kuongeza idadi ya wanafunzi. Ni muhimu basi kama Serikali inashindwa kuipa Bajeti ya vyuo hivi, wavikabidhi kwa Wizara ya Elimu na mafunzo ili viboreshwe kwani Wizara hii ndiyo iliyopewa kipaumbele na utaendelea kuwa kipaumbele.

Kuhusu mila potofu, Tanzania kama nchi nyingine Kusini mwa Jangwa la Sahara, limekumbwa na imani za kuamini kuwa akinamama wazee wenye macho mekundu *Red Eyes* ni wachawi. Mila hii imeshasababisha vifo vingi na wamama hawa wanaendelea kuuawa. Ukweli ni kwamba kibaioljia wazee wale wanakuwa na wekundu kwenye macho kutokana na kuathirika na moshi hasa ikizingiwa nyumba zao hazina sehemu ya kupitishia moshi wanapopika. Hivyo Wizara hii ina jukumu la kutoa elimu hususan kwa maeneo yale yaliyoathirika kwa kiasi kikubwa na mauaji haya ili jamii hizo ziweze kuishi kwa uelewano na usalama. Lakini pia kwa kuwa Wizara hii inahusika na mashirika yasiyo ya Kiserikali, basi wasaidie zile *NGOs* zenye lengo la kuelimisha jamii ili waweze kuisaidia jamii kwani mitandao yao ni mipana sana.

Kwa kuwa wanawake wamekuwa wakifanya kazi nyingi tena ngumu sana kama kukata na kubeba kuni, kuinga maji kwa umbali mrefu, kulima, kukata majani na kadhalika. Naamini Wizara ikiwawezesha akinamama hawa na kuwapatia vifaa vya kisanyansi kama jembe la kukokotwa na ng'ombe, *tractors* na kadhalika kuwa na teknolojia hii kutawafanya wanaume wafanye kazi hizi na hivyo kuwasaidia wake zao.

Mwisho, suala la benki ya wanawake sidhani kama litakuwa na tija kwa wanawake kwani wanawake hawa ni wadau katika benki nyingine. Je, benki hii itakuwa na utaratibu mwingine tofauti na benki nyingine? Wanawake watafaidika vipi?

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu pamoja na watendaji kwa hotuba nzuri ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza wanawake kwa kazi kubwa wanazozifanya kwenye uongozi mbalimbali na wafanyabiashara ndogo ndogo na kati pia na kwa asilimia kubwa wanawake wakulima vijijini. Wanawake wanafanya kazi kubwa ndani ya nchi yetu na kukuza uchumi wa Taifa letu na pia kutunza na kukuza familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake ni wafanyakazi wakubwa ndani ya nchi yetu kwa kuwa sheria zinahitaji kutizamwa upya ili ziwaondolee matatizo na ziweze

kuwapa raha na haki pale wanapoachika au kufiwa na waume wao nayo ni sheria ya ndoa na mirathi, sheria hizi hebu ziangaliwe upya kwani kuna mambo yanamnyanyasa mwanamke na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya watoto yatapatikana kwa kuwa na watoto ambao watazaliwa ndani ya ndoa na si kuwa na watoto wengi wa mitaani ambao hawana mbele wala nyuma hawana maadili kwa kukosa mapenzi na mafunzo ya baba na mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ichukue juhudi za makusudi za kisheria kuhakikisha wale wote wanaowapa mimba vijana wetu wadogo mimba za utotoni hasa wanapokuwa shule na kwa kuwa vijana hawa wanakuwa wadogo wanapozaa wanakuwa hawawezi kutunza watoto hawa na ndipo ongezeko kwa watoto wa mitaani kuongezeka, je, Serikali ina mkakati gani kutoa elimu kupitia Wizara hii. Kutafuta vikundi vya michezo ya kuigiza inayohusiana na athari za mimba za utotoni na vikaweza kusika kwenye redio na kuonekana kwenye luninga ili vijana wetu wa kike na kiume wakaweza kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naunga mkono hotuba hii. Ahsante sana.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na pongezi hizo nina maoni yafuatayo:-

Kumekuwa na tabia ya baadhi ya wanawake (watu wazima), wenye uwezo kifedha, kuchukua vijana wadogo wa kiume na kufanya nao mapenzi kwa kuwarubuni kwa fedha na kuwapa magari na wengine kuwalipia ada za shule. Hali hii inawaharibu vijana wengi kutopenda kufanya kazi na kujitegemea na baadhi yao huambukizwa maradhi. Je, serikali inatoa tamko gani kuhusiana na tabia hiyo mbaya? Kwa wale ambao wanajijua wameathirika lakini wanaendelea kuwarubuni vijana wetu wa kiume ambao ni nguvu kazi ya taifa; na jamii inaona inabaki kulalamika bila kuchukua hatua yoyote; je, serikali itachukua hatua gani za kukomesha tabia hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Taasisi ya WAMA kwa jitihada za kukomesha mimba mashuleni.

Naishauri Wizara iandae Programu Maalumu kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake na pia jinsi ya kupanga uzazi wa mpango kwa wanawake hapa nchini. Vilevile iwe na mpango wa kujenga kituo cha wanawake kwa kila mkoa ili kuwaweka wanawake pamoja kwa lengo la kuwaendeleza kufikra na kiuchumi (*centre for Women*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia uhai na uzima na kunijalia kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wake kwa ushirikiano wao, utendaji wao na uwakilishaji wa hotuba yao leo katika Bunge lako Tukufu. Hotuba ambayo imejitosheleza kabisa, inayojali kufanya kazi kwa bidii katika kujiletea maisha bora kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na haki za watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza hayo ni lazima kuwa na elimu ya kutosha kwa jinsia zote, pamoja na watoto. Kwa kuwa Wizara inavyo vyuo vya maendeleo ya jamii, ninaiomba ichukue juhudi hiyo kwa kushirikiana na Halmashauri viliko vyuo hivyo, kuwakusanya vijana na kuwapeleka katika vyuo vyetu vya maendeleo ya jamii kujifunza stadi zilizoko; ndipo tutafikia lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ndiyo sumu ya ujinga; dawa ya masikini juhudi ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uazishwaji wa benki ya wanawake unasua sua; hii ni kwa sababu bado wananchi wengi hawajaelimishwa mikakati ya uwazishwaji kwake, pia namna ya zoezi la ununuzi wa hisa. Kwa hiyo, serikali iweke wazi jinsi itakavyoisaidia benki ya wanawake, namna itakavyotoa fedha kulipia gharama za uwazishwaji na namna itakavyosaidia kutoa fedha za kulipia gharama za uwezeshaji kwa wanawake, ili benki hiyo ianze kazi mara moja. Pia mafunzo yatolewe hasa ya umuhimu wa uanzishwaji wa benki na kuhamasisha wateja waje wawekeze katika benki hiyo mara tu itakapoanzishwa rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KANALI FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nina heshima kubwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya, pamoja na hotuba nzuri iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuipokea hotuba hiyo nzuri, nimeona nami upande wangu niunge mkono hotuba hii kwa kuchangia mambo machache yafuatayo:-

1. Ninaunga mkono bidii ya Wizara pamoja na wanaharakati wote wanaopiga vita na kupinga kwa nguvu zao zote; unyanyasaji, upigaji wa wanawake na watoto wadogo.
2. Ninaunga mkono na kupiga vita maharamia wanaowatesa na kuwauwa ndugu zetu Maalbino.
3. Ninaungana na Wizara katika kupiga vita ukeketaji wa wasichana.

4. Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Wizara ipigane sheria ya kupewa haki mjane na kusimamia mirathi ya mayatima ili kuepuka mateso ya mali za marehemu kudhibitiwa na upande wa familia ya marehemu.

5. Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Wizara kuendeleza bidii kubwa katika kuelimisha umma katika kupambana na maovu haya yote niliyoyaeleza hapo juu na mengi mengineyo ambayo Wizara wanayaelewa.

6. Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza serikali kuanzishwa “benki ya wanawake” ninaishauri serikali iharakishwe na kuanza haraka benki hiyo, kuharakisha maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu, kwa heshima kubwa sasa ninaomba kuunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia Hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kabla sijaendelea, kwanza niunge mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naanza kuchangia hoja kwa kulaani vitendo vya wanaume ambao wanawadhalilisha wanawake kwa vitendo vibaya kama vile ubakaji na kuwapiga hadi kuwapa vilema vya kudumu. Vitendo kama hivi vikemewe vikali sana, kwa sababu ni ukiukaji wa haki za binadamu na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa watoto siku hizi limekuwa jambo la kawaida na wengine wanafikia kuwatupa watoto na hata kuwauwa na kuwanyima haki ya kuishi kikatiba. Watu kama hawa wakigundulika wapewe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi limekuwa jambo la kawaida kwa wasichana na hasa wasichana wa shule kupewa ujauzito. Mtindo huwo umekuwa ukiwaathiri watoto kwa kukosa masomo na kukatisha masomo yao. Sasa wakati umefika kwa wasichana wadogo kupatiwa elimu ya kutofanya ngono zembe wakiwa bado shuleni. Pia watu ambao wanawapa ujauzito (mimba), wasichana wa shuleni na hata waliokuwa si wa shuleni, watu hao wapate adhabu kali na wakati wa kesi wasipate dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wazee ambao wanawakatisha watoto wao shule kwa kuwapa waume (kuolewa), bila watoto wenyewe kukubali ndoa hizo. Nadhani sasa wakati umefika wa kuwashughulikia wazee hao na hata hao wanaume ambao wanafunga ndoa na wasichana hao wapate adhabu kali ili kuondoa tatizo hilo na iwe funzo kwa wengine,

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nchi yetu imekabiliwa na uigaji wa mambo ya nchi za nje na kuacha utamaduni wetu wa Tanzania. Watoto wetu, hasa wasichana kuiga mavazi yasiyo na heshima, akina mama hao wanajidhalilisha wenyewe kwa kuvaa nguo fupi ambazo si za heshima au kuvaa suruali zinazowabana sana, jambo ambalo hata

msichana aliyevaa huwa hana raha nayo kwa jinsi lilivyombana. Sijui hili Waziri anasema nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wanawake ambao ni wajane wanabeba ujauzito (mimba) bila mpango na kushindwa kuwatunza watoto hao na wengine kuvitupa vichanga baada tu ya kuzaa. Naiomba Wizara hii isimamie kutoa elimu ya uzazi wa mpango au hata kutozaa kwa sababu wanawauwa na kutekeleza watoto hao bila hatia. Watu hao wakipatikana, wapate adhabu kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi khoja mia kwa mia.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ya jinsi Wizara hii itakavyosaidia kuhakikisha kuwa vikundi vya akina mama wajasiriamali wanaojishughulisha na ufinyanzi wa vyungu katika Kata ya Lumbila, Wilayani Ludewa, wanashiriki katika Maonyesho ya Biashara yatakayofanyika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wanawake wengi waliojiunga na Mlangali SACCOs iliyoko Wilayani Ludewa na kwa kupitia SACCOs hii wanawake hao wangeweza kusaidiwa kupata mikopo nafuu kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa; je, Wizara hii itasaidiaje kufikia azma hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jedwali Na.6 ni Wilaya chache sana zilipata mikopo ya fedha katika Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (WDF) mwaka 2007/2008. Je, Wizara inatoa ahadi gani kuhakikisha kuwa wanawake wachache kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa wanafuzu kupata mikopo kutoka Mfuko huo?

Katika jedwali Na.7 ni wanawake kumi tu ndio waliopata mafunzo ya ujasiriamali mwaka 2007/2008 kutoka Iringa na Njombe Mkoani Iringa. Je, Wizara itakubali kuhakikisha kuwa katika mwaka 2008/2009, wanawake wachache kutoka Ludewa wanapata fursa ya mafunzo hayo ya ujasiriamali?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na ambayo inatoa mwelekeo wa matumaini katika jamii yetu. Yafuatayo ni baaldhi ya mwono wangu:-

1. Katika utoaji mafunzo mbalimbali, Wizara imependelea sana kutoa huduma hiyo kwa wanawake kuliko wanaume. Hali hii haionyeshi ushiriki wa jinsia zote.

2. Katika jitihada za utoaji mafunzo katika vyuo hapa nchini, Wilayani Chunya hakuna hata mtu mmoja aliyehudhuria mafunzo hayo kulikoni?

3. Wizara hii bado haijaleweka fasaha kwenye Wilaya ya Chunya. Nashauri hatua zichukuliwe kutoa elimu ya uelewa Wilayani humo.



4. Wizara iangalie jinsi inavyoweza kusaidia vijana wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STALLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margret Simwanza Sitta, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Lucy Sawere Nkya, pamoja na Katibu Mkuu, Bibi M. Mwaffisi kwa jitihada mbalimbali zinazoongeza ustawi wa wanawake.

Aidha, napenda kuchangia kama ifuatavyo: Wanawake wenzetu waishio vijijini wana kiu ya kuelewa kinachoendelea. Wanawake wa mijini wengi wameshastarabika na kufahamu zaidi juu ya ongezeko la familia na elimu ya UKIMWI. Kwa hiyo, naiomba Wizara yako ituwezeshe kuandaa kongamano moja la vijijini katika Mkoa wa Ruvuma.

Pili, tunawapongeza juu ya *50/50 percent* ya ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi. Hili si suala jepesi na linataka maamuzi na nguvu ya ziada katika kulisukuma. Tumefahamu ugumu uliopo, lakini kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ana dhamira ya dhati ya kuliwezesha suala hili, basi suala hili linahitaji kushughulikiwa mapema ili kuweza kuwahi ratiba ya uchaguzi.

Tunashauri pia kuwezesha vikundi vya wanawake kwa kuwa *link* na wahisani mbalimbali wanaopitia Wizara yenu.

Mimi ni Mwenyekiti wa *NGO - Better Life Tanzania*, ambayo inawezesha masuala ya ujasiriamali Ruvuma na tumefanikiwa sana katika suala la kilimo cha uyoga. Nawakaribisha siku mkipata nafasi mje kututembelea. Bila kusahau kuwa Mheshimiwa Waziri, Mama Sitta, uliwahi kututembelea na tunashukuru sana kwa *support* yako ya shilingi laki moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo muhimu sana kuhusu haki za akina mama na watoto. Sheria ya Mirathi, Sheria ya Pesa za Kumkimu Mtoto na Sheria ya Ndoa umri chini ya miaka 18, zinaletwa lini Bungeni? Hivi kikwazo ni nini? Naomba muwasiliane na TAMWA kwani najua wana *draft* ambayo inaweza kutoa mwanga kwa kuanzia.

Mwisho; ni muhimu kuwashirikisha wanaume kwani maamuzi yetu mengi yamekwamishwa na kukosa *column* kwa kuwa wengi wao ni wanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara hii kwa kuleta hotuba nzuri. Ninaomba suala la maalbino lishughulikiwe kwa makini, ikiwezekana yaundwe makambi maalumu yenye kuwekewa ulinzi wa kutosha. Hao maalbino washauriwe kutembea wakiwa wengi si mmoja mmoja.

Vifaa vinunuliwe kwa wingi kwa walemavu hasa wale viziwi na vyombo mbalimbali vya habari washauriwe kuwa wanaweka watu wa kuonyesha ishara kwa viziwi hasa kwenye televisheni wakati wa taarifa ya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijiaalia siku ya leo kufika hapa Bungeni bila ya kukamatwa mkono. Hii inaashiria kuwa niko mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa taarifa yake iliyojaa matumaini kwa jamii ya kitanzania. Wizara husika ni eneo la wananchi wetu kihaki pia kimaendeleo ambayo sura yake ni kukuza jamii yenye mwamko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa nimzungumzie wanafunzi wa kike mashuleni. Ongezeko la wanafunzi kutiwa mimba mashuleni linazidi siku hadi siku. Tatizo hili limekuwa tata, kwa mtazamo wa juu unaweza kujiuliza ni nani mhusika wa tatizo hili kati ya Wizara hii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimba za wanafunzi mimi nasema bado serikali haijawa tayari kulikomesha tatizo hili. Kutotoa sheria juu ya mwanafunzi akajua, kutaweza kupunguza tatizo. Sheria ya mwanafunzi anapochukua mimba ili ajue amevunja sheria ni kumfukuza shule tu. Kufanya hivi kutasaidia kupunguza tatizo, mfanya kosa kuhukumiwa. Tukimuwekea sheria ya kurejea shuleni baada ya kuzaa, kutachangia kukua kwa tatizo na kuzidi serikali kubebeshwa mizigo ya watoto wasio na baba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaelewe maalbino wapo sawa kama walivyo Watanzania wenzao. Kwa maana hiyo, wanahaki sawa na wenzao. La kusikitisha, mauwaji ya maalbino yanaongezeka kila leo. Tuitazame serikali; serikali ni eneo pana, siamini kama serikali itajipanga kuweza kuwanusuru wenzetu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la watoto mitani ni mzigo mkubwa wa serikali. Ukiangalia serikali ilivyoipa bajeti Wizara hii, utaona bajeti yake ni ndogo mno. Wizara hii inayoongozwa na Waziri mwenye uwezo, imani, imebeshwa mzigo mkubwa na dhahiri bajeti yao ni ndogo. Naiomba serikali imsaidie Mama Sitta ili aweze kufanikisha azma yake ya huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria za Ndoa na Mirathi; kwa kuwa haki za mirathi na ndoa zimetokana na andiko takatifu kama vile Qurani, Injili na kadhalika, napata wasi wasi serikali itaweza kuacha sheria hizi na kuwa na nyingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza serikali kutambua umahiri wa wanaume hapa nchini. Hivyo, yapaswa serikali iwawezeshe wanaume ili waweze kuzimudu familia zao. Kumwezesha baba kutapunguza mzigo kwa serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi leo mtoto wa Mtanzania aliyefiwa na wazazi ama mwenye umaskini uliokithiri, bado anaishi katika mazingira magumu. Ni vyema serikali ipange mikakati mahususi ili iwanusuru watoto hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vifo vya wanawake wakati wa kujifungua ni tatizo kubwa sana. Pamoja na uhaba wa elimu vijijini, tatizo sugu ni upungufu wa hospitali. Wizara inapaswa ishirikiane na Wizara ya Afya ili inusuru maisha ya wenzetu hawa.

Baada ya maelezo yangu hayo, napenda kumpongeza Mama Sitta na Naibu wake, kwa umahiri wao. Mwenyezi Mungu, awawezeshe katika nia yao. Ahsante.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuipongeza hotuba nzuri iliyosomwa na Waziri mbele ya Bunge lako Tukufu la Bajeti kwa mwaka 2008/2009, yenye mwelekeo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005. Pamoja na pongezi hizi, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Ingawa kwa muda mrefu tatizo la vitendo vya ukatili wanaofanyiwa wanawake na watoto, limekuwa likipigiwa kelele na jamii lakini vitendo hivyo vya ukatili vinaendelea; inaonyesha ukatili huu umegawanyika katika maeneo mawili makubwa, ambayo ni mila na desturi kwa baadhi ya makabila, pia sheria zinazotumika ambao ingefaa zifanyiwe marekebisho.

Baadhi ya makabila kuona suala la kuwakeketa wanawake ni lazima, vinginevyo hawaolewi au kutengwa na jamii. Wengi wa wanawake hao hupatwa na madhara makubwa na wengine hupoteza maisha. Pamoja na kwamba Wizara inajitahidi kupiga vita ni vyema elimu hii iwafikie sana wanaume ambao kwa mfumo dume uliowatawala, wakielimika wanaweza kusaidia kukomesha tatizo hili.

Ili kukomesha vitendo vya ukatili vlya kuwabaka wanawake na watoto, ingefaa sheria ya ubakaji ifanyiwe marekebisho, hasa Sheria za Bodi ya Parole. Wapo wafungwa wanaohukumiwa kwa makosa ya ubakaji, baadaye wafungwa hao wanaachiwa huru chini ya Sheria ya Bodi hiyo ya Parole. Hayo ni makosa makubwa sana, hii imetokea; jambo ambalo linaondoa imani kwa wananchi na serikali yao. Katika gereza moja, aliwahi kuachiwa huru mfungwa aliyehukumiwa miaka kumi na tanokwa kosa la kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka mitano; ukatili gani huu?

Wizara hii ni nyeti sana, lakini inasikitisha sana kuona inapewa fedha kidogo sana; kama bajeti ya mwaka 2008/2009 imepewa shilingi bilioni 14.6. Kiasi hiki ni kidogo sana, kulinganisha na majukumu mazito yanayoshughulikiwa na Wizara hii. Nashauri kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara hii ifikiriwe na kupewa kipaumbele kuongezewa bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Waziri mwenye dhamana na Wizara hii, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa maandalizi mazuri ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na majukumu ya Wizara hii ni dhahiri Wizara hii ndiyo kiungo cha wananchi hasa kwa kutoa elimu ili wananchi ambao ni jamii kwa ujumla, kuelewa haki zao ili kujisimamia wao wenyewe kimaendeleo. Inashangaza kuona Wizara hii inafanya shughuli zake mwisho wilayani. Pamoja na maofisa maendeleo ya jamii kuwepo wilayani bado utendaji wao haueleweki ni upi kwani mara nyingi watendaji hawa wameonekana kufanya kazi nyingine kabisa kama vile kwenye idara ya elimu na kadhalika. Hatujaona mpango kazi wa Afisa Maendeleo wa Wilaya anumia vipi nafasi yake katika kutoa elimu kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala hili ni wajibu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii wawepo hadi ngazi ya Kata, watoe mafunzo mbalimbali yakiwepo yale ya ujasiriamali ili wananchi washiriki katika shughuli za maendeleo kwa nia ya kujiondolea umaskini. Kadhalika vifaa kama gari na pikipiki vitolewe kila wilaya ili kurahisisha utendaji kazi kwa Maafisa Maendeleo.

Juhudi za kuchochea maendeleo ya wananchi kupitia Wizara hii bado hazijaonekana; hivyo juhudi zianzie Wizarani kwa kumtaka Waziri na Naibu wake kutembelea Wilaya zote na ikiwezekana hata kwenda ngazi za Kata hasa vijijini kwa nia ya kuchochea shughuli za maendeleo ya wananchi.

Kwa ngazi nilizozitaja kwamba zinahitaji zipewe kipaumbele, pia bado Wizara haijatoa utaratibu wa namna wanayoitumia katika kuwajengea uwezo wanawake na wanaume katika kushiriki katika utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo na kufaidika sawa katika maendeleo. Utaratibu unaotumika katika kupata wanafunzi wanaotakiwa kujiunga na vyo vya maendeleo ya jamii haueleweki, Wizara iweke wazi badala ya utaratibu huu ambao ni wa kificho.

*Women Development Fund (WFD)* kwa nini Mfuko huu uhudumie Halmashauri za Wilaya 23 pekee na kiwango cha fedha kilichokopeshwa ni shilingi milioni 152; kiwango hiki ni kidogo sana, sawa na wastani wa Sh. 666 kwa kila Wilaya. Huu ni mzaha na ukichunguza sana fedha hizi hazijawafikia walengwa halisi, nyingi zitakuwa zimeishia kwenye semina na usafiri ama posho kwa wawezeshaji. Wizara ibuni utaratibu muafaka ili mikopo hiyo iwe ya tija itakayowaendeleza wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri jamii inaongezeka siku hadi siku, idadi kubwa ya watoto inaongezeka siku hadi siku, lakini katika kuongezeka huku tumejionea jinsi gani watoto wadogo wanavyoingia katika hali mbaya ya mazingira kutokana na kukosa wazazi wote na hata ndugu tumejionea watoto katika mazingira magumu; watoto kufanya kazi kwa umri mdogo; na unyanyasaji katika masuala mbalimbali yakiwemo ya ngono na kadhalika. Kupitia mazingira hayo, lazima ongezeko la watoto wasiokwenda shule (elimu ya msingi), inawezekana kabisa. Naomba Wizara ifanye utaratibu wa watoto

wa aina hii kwa nchi nzima ili kutafuta namna bora ya kukabiliana na hali hiyo. Kadhalika, Wizara izifuatilie kwa kariabu *NGOs* zinazojishughulisha na malezi ya watoto, kwa maana baadhi ya *NGOs* zinaweza zikawa zinafanya kazi hii kwa maslahi yake binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kazi inayofanywa na Asasi hizi (*NGOs*), ambazo sio za kiserikali, lakini naomba Wizara izifuatilie kwa karibu; zipo zinazoendeshwa kifamilia, kiurafiki na kadhalika. Naomba Wizara ikague mahesabu ya *NGOs* hizi kila mwaka na pia ifahamu mahali zinapofanyia kazi (ofisi). Kwa kufanya hivyo, tutakuwa na *NGOs* zinazoendeshwa kwa ukweli na hivyo kuepokana na *NGOs* za mifukoni.

Nashukuru taarifa ya Waziri kwamba, sasa serikali itatoa fedha ya dhamana katika uanzishaji wa benki ya wanawake. Naamini benki hii ndiyo mkombozi wa mwanamke. Naomba mara baada ya benki hii kuanzishwa, basi lazima iwe na matawi sehemu mbalimbali mikoani ili kumfanya mwanamke wa kila sehemu kushiriki katika huduma ya benki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la kuwa na sheria inayomhusu mtoto, kama Protokali nyingi za kimataifa zinaitaka nchi kuwa na sheria hii; je, serikali (Wizara) baada ya kusikia hivyo; ina maandalizi gani hata kama suala zima litaridhiwa? Naomba maelezo wakati Waziri atakapotoa majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa kike wanaendelea kupata mimba hivyo kushindwa kumaliza masomo. Naiuliza Wizara ina mikakati gani ya haraka kudhibiti, kwa maana ya kutoa adhabu kwa wanaume wanaosababisha tatizo hili? Naishauri serikali kuunda sheria itakayoweza kumbana kijana wa kiume atakayebainika kusababisha tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuweza kuandaa hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwepo na usawa wa kijinsia na upatikanaji wa fursa sawa kwa wote ni vizuri wanawake wakapewa nafasi zaidi ya kushiriki katika mafunzo au semina zinazotolewa katika nchi yetu ili kuweza kuwapa wanawake uelewa zaidi na hii itawaondolea woga na kutojiamini ambao wanawake wengi hasa vijijini wanao na hili lilisababishwa na suala la mfumo dume. Kama tutafanya hayo, ninaamini tutafikia azma ya serikali ya kufikia asilimia 50 kwa 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi wamepoteza haki zao nyingi za msingi hasa pale waume zao wanapofariki au wanapoachana na wenzi wao, mwanamke anaonekana kama mpita njia katika familia hiyo na hivyo kumsababishia matatizo mengi ambayo hushindwa kuyatatua hasa suala la watoto na hii husababisha tatizo kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia sahihi ya kumlinda mwanamke huyu ni kuhakikisha kuna sheria za kumlinda na kumsaidia kupiga vita na mila potofu zinazomdhalilisha mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto wa kike naye amekuwa akipata matatizo mengi ambayo yanasababisha mtoto huyu kushindwa kuendelea na masomo pale wazazi wake wanaporidhia mtoto wao kuolewa akiwa na umri wa miaka kumi na tano na hii ni sheria ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka 15 kwa mtoto awe wa kike au wa kiume bado ni watoto ambao wanahitaji elimu na matunzo toka kwa wazazi na siyo mtoto huyo kwenda kuanza maisha ambayo ni hatari kwake. Hivyo, tunaiomba serikali ilete mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ambayo inaruhusu mtoto wa miaka 15 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi wake. Kama sheria hizi zenye upungufu hazitafanyiwa marekebisho, basi suala la kufikia asilimia 50 kwa 50 litakuwa ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza serikali kwa ahadi yake ya kutoa shilingi bilion 2.1 ili kupata leseni itakayoweza benki kuanza. Mwaka 2007, Wabunge tulihamasishwa umuhimu wa benki hiyo na wengi tulinunua hisa za benki hiyo; sasa tungependa kujua nini kinaendelea kwa kina na wale waliokwisha kutoa fedha zao; je, fedha hizo ziko wapi na zinafanya kazi gani? Kama zinafanya kazi; je, walionunua hisa hizo watapata gawio toka mwaka walionunua?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii.

**MHE. DR. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Kwanza, nampa pongezi Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwa maandishi kuwa Wizara hii ni muhimu na ni mtambuka, maana yake inashughulikia mambo mengi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu haki za mtoto ni jambo muhimu sana kwa taifa letu, hasa kwa kuleta maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa mitaani ni jambo la kusikitisha mno. Wimbi hili la watoto wadogo mpaka vijana (nguvu kazi), lifanyiwe kazi. Ikiibidi, watoto hawa wapelekwe kwenye shule maalum au vituo maalum au warudishwe majumbani kwao. Wizara hii iwe kinara kwa jambo hili, pamoja na kusaidiana na wadau wengine wanaohusika. Sio jambo zuri kuona watoto wanaendelea kuteseka mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa mitaani, wimbi hili ni kubwa mno hasa kwenye miji mikubwa. Matatizo yanayosababisha kuwa watoto wa mitaani yanafahamika. Kwa hiyo, naomba kwanza tukabiliane na wimbi hili tulionalo la watoto wa mitaani mijini, kwa kulitafutia mahali pa kwenda au kuwaweka kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutoe elimu huko vijijini na mijini ili wawe tayari kukabiliana na tatizo hili. Jamaa na familia wote wawe karibu sana na watoto wao ili kupiga vita tatizo hili la kuruhusu nafasi ya watoto kukimbilia mijini na kuwa watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashukuru na kuwatakia kazi nzuri Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Naibu wake na Wafanyakazi wote wa Wizara hii.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa taarifa yake. Vilevile Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wataalam mbalimbali wa Wizara, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kukamilisha taarifa hii hadi kuwasilishwa kwetu leo.

Nianze na uanzishwaji wa mabaraza ya watoto nchini. Naiomba serikali iandae mikakati ya muda mrefu kuhusu uanzishwaji mabaraza haya ili kumkomboa mtoto kutoka katika fikra potofu zilizotawala nchini. Mabaraza haya yanawaamsha watoto kuweza kujua haki zao na kuzitetea ipasavyo, kuwaamsha watoto kiuchumi, kiuongozi, kiafya na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nimuulize Mheshimiwa Waziri kuwa, tokea kuanzishwa kwa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ni Idara ngapi ambazo zimeundwa katika maeneo husika ili kuwaendeleza watoto nchini?

Serikali inachukua hatua gani za ziada kukomesha upatikanaji wa mimba za watoto wa kike wakiwa shuleni kuweza kuendelea na masomo na tukiangalia kuwa kila mwaka idadi ya wanafunzi wa kike wanaopata mimba inaendelea kuongezeka?

Kwa kuwa mara nyingi baadhi ya walimu huwa ndio chanzo cha upatikanaji wa mimba hizo; je, serikali inaweka mikakati gani ya ziada kwa walimu watakaohusika kumpa mimba mwanafunzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, serikali inaweka mikakati gani kwa wanafunzi waliojifungua ambao wamekatisha masomo na hawana mpango wa kujiendeleza kimasomo kutokana na hali zao za maisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi wanawake ni wenye kufanya kazi ngumu katika jamii, wakiwa viongozi wa familia kutokana na kutelekezwa kwao kifamilia au kijamii. Serikali ni vyema kuwaendeleza wanawake hawa pale wanapojitokeza kujiunga na SACCOs, iwape kipaumbele wanapoomba mikopo ya kujiendeleza kibiashara. Iweke mikakati ya kuwahudumia pale wanapopata magonjwa ya aina mbalimbali na kuweka

mikakati maalumu ya kuwasidia wajane na kuwaorodhesha katika kila Halmashauri husika ili kujua idadi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ueleweshwaji wa wanawake wajasiriamali kuhusu huduma za bure zinazotakiwa kutolewa na vituo vya afya; naiomba Wizara ichukue juhudi za kuielimisha jamii kuhusu huduma hizi. Mara nyingi wanawake wanakuwa hawaelewi suala hili na kushindwa kufika katika vituo vya afya kwa kuogopa gharama zitolewazo na vituo vya afya.

Wapo watoto ambao wana watoto na kutokana na kutokujua huduma za mtoto kuanzia umri wa miaka 0 – 5 anatakiwa afanye nini, kumpatia chanjo na mengineyo, anashindwa kufika kituoni kwa kuona aibu au hata elimu duni aliyonayo inachangia. Ni vyema serikali au Wizara iweke utaratibu wa kuwaelimisha wanawake hawa kwa kuweka Mabaraza ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la mauaji ya maalbino nchini yanaendelea siku hadi siku kwa mbinu za kishirikina; na kwa kuwa jamii hizi nazo zinahitaji kupata elimu, afya na mengineyo; je, serikali inaandaa mikakati gani ya kuwasaidia jamii hizi ili waweze kujiendeleza na wao kiuchumi na wasiendeleo kudhalilika nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji wangu wameisha na nadhani Waziri waliochangia hawa anaweza kuwajibu na kama tu kasema kitu mna majibu mtajibu. Kwa hiyo, namuita Mheshimiwa Naibu Waziri dakika 30 na Mheshimiwa Waziri dakika 45. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa nilipo nikiwa na afya njema na uwezo wa kuchangia katika hoja ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mheshimiwa Waziri kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Aidha, pia nampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Nampongeza Waziri wangu Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Vile vile napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili wamsaidie na kumshauri katika kazi zake. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa sana namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuiteua kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto baada ya mabadiliko ya mwezi Februari, 2008. Ninathamini heshima aliyonipa na ninaahidi kufanya kazi kwa nidhamu, uadilifu na nguvu zangu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwashukuru wanawake na wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro kwa kuniamini na kunituma niwawakilishe katika Bunge lako Tukufu. Ninaahidi kuwawakilisha na kuwatumikia kwa upendo na uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru familia yangu nikianza na mume wangu mpendwa Profesa Nkya na watoto wetu Febby, Jonas, Theresa, Petro na ndugu zangu wote pamoja na marafiki kwa upendo wao na maombi yao kwa Mwenyezi Mungu ambaye yanaisaidia sana katika utendaji wa shughuli za kulitumikia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Mariam Mwaffisi, kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Ushirikiano wao mzuri unanirahisishia sana utendaji wa kazi zangu katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii na Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu kwa michango yao ambayo mingi imetusaidia na inatusaidia sana kuboresha mikakati ya kutoa huduma za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na bila kusahau naomba nichukue fursa hii nimshukuru sana Mheshimiwa Spika na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, kwa kazi nzuri wanayoifanya kuliongoza Bunge hili Tukufu hasa wanapotuongoza asubuhi katika kujibu maswali yetu ambao ni wajibu wetu mkubwa kwa wananchi na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa, naomba nirudi kwenye kuchangia hoja ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa naomba nitamke kwamba ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia muda mfupi nitajibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge hasa zilizoелеkezwa kwa Idara ya Watoto na Idara ya NGOs na zilizobaki zitajibiwa na kutolewa maelezo na Mheshimiwa Waziri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wameelekeza maswali yao kwenye haki za watoto pamoja na sheria na sera ambazo zinalenga maendeleo na haki za mtoto. Wengi wameuliza na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii imeuliza mikakati ya kurekebisha sheria zinazohusu haki za wanawake na watoto. Kifungu cha kwanza walichouliza kwa kuwa sheria nyingi zinazohusu haki za wanawake na watoto zimepitwa na wakati, Serikali iweke mikakati ya kujadili Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Sheria ya Mirathi ili marekebisho ya sheria hizo yaweze kufanyika haraka iwezekanavyo kabla ya Bunge hili kumalizika mwaka 2010. Kwa kuwa protokali na itifaki za nyongeza zinazohusu haki za watoto na wanawake na kutungiwa sheria za kutekeleza, Kamati inaishauri Serikali kuwa mikakati ya kutoa elimu na mafunzo ya protokali na itifaki hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya hoja hii ni kuwa nakubaliana na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii kuhusu kuweka mikakati ya kujadili Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi. Aidha, hivi sasa Serikali chini ya uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria inaandaa mchakato wa kuwa na Waraka wa Serikali yaani *White Paper* utakaowezesha wananchi kujadili na kutoa maoni ya namna ya kurekebisha Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Sheria za Mirathi na Urithi na wakati utakapofika wananchi watapatiwa fursa hiyo. (*Makofi*)

Hali kadhalika sheria zinazohusu watoto hivi sasa zinapitiwa na kufanyiwa marekebisho ili ziende na wakati na Maazimio ya Kimataifa yanayohusu Haki na Ustawi wa Mtoto. Wizara ya Katiba na Sheria inashughulikia Sheria hizo na zitaletwa katika Bunge hili Tukufu mwezi Oktoba, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kukubaliana na ushauri wa Kamati ya kuwa mikakati ya kutoa elimu na mafunzo ya Mikataba ya itifaki za nyongeza za haki za wanawake na watoto. Wizara yangu imekuwa ikitoa elimu na mafunzo ya aina hiyo kupitia Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Halmashauri kwa lengo la kusambaza elimu hiyo kwa makundi mengine ya jamii na Wizara yangu itaendelea kutoa elimu na mafunzo hayo kwa kuanzia na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. Mafunzo hayo yatatolewa katika kipindi hiki cha Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi, wamezungumzia sera ya Taifa kuhusu wasichana wanaopata mimba wakiwa shuleni. Chini ya hayo kuna vipengele vitatu (a), (b) na(c). Kipengele (a), suala la mimba ni changamoto yetu kuhakikisha kuwa inadhibitiwa ipungue kama siyo kukomesha kabisa na kipengele (b), kwa kuwa mpaka sasa hakuna sera ya Taifa kuhusu suala hili utaratibu uliopo ni kuwafukuza shule wasichana waliopata mimba hii siyo sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele (c), watoto wanaobebeshwa mimba wakiwa wanafunzi warudishwe shuleni baada ya kujifungua. Hizo ni hoja tatu ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wafuatao:- Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa

Jenista Mhagama, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya na Mheshimiwa Grace Kiwelu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya hoja nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala la watoto wanaopata mimba shuleni pamoja na ugumu wa tatizo hili bado lipo mikononi mwa wananchi hususan familia kwani linawanyima haki wasichana ya kupata elimu na kuweza kuwa na maisha bora na kutoa mchango wao katika maendeleo ya Taifa hili. Hivyo, ni wajibu wa kila familia kukaa na kutunza wanafamilia wakiwemo wasichana kwa kuwapa maadili, mila na desturi njema na zenye kuleta maendeleo. Aidha, kila familia ijitahidi kuzalisha mali ili kusaidia wasichana wasipate vishawishi kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana kwamba watoto walio wengi wanajiingiza kwenye vishawishi vya ngono ili wapate fedha za kukidhi mahitaji yao hususan siku hizi ambapo inabidi watoto wengi wa shule waweze kulipa nauli za daladala na waweze kwenda shule na wazazi wanakuwa na kipato kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba mjadala unaoendelea ndani ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wa kuangalia uwezekano wa kuweza kuwarejesha hao watoto mashuleni kwa kufuatana na mawazo na mchango wa jamii yatafikia tamati ili hili suala la kuwarejesha hao watoto ambao wamepata mimba wakiwa shuleni waweze kurudi na kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba kutokuwapa fursa hao wasichana kuendelea kusoma ni kuendelea kuwaambia kwamba nyie sasa hamfai kuwa raia wema kwa hiyo, muendele katika mambo ambayo hayafai na tafiti zinaonyesha kwamba machangundoa wengi wanatokana na watoto waliopata mimba shuleni na wakakosa mtu wa kuwapokea ndani ya familia zao na ndani ya jamii. Kwa hiyo, wanaamua kuhamia Mijini na kujitafutia kipato kwa kufanya shughuli za kichangundoa ili waweze kujikimu katika maisha yao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naamini kwamba mjadala unaoendelea sasa kutokana na wataalam ambao wameteuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi utafikia tamati yenye kuleta kheri kwa wasichana hao walioathiriwa na hilo janga la kupata mimba wakiwa shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limepigwiwa kelele kubwa sana ni suala la watoto wanaoishi mitaani. Suala hili limezungumziwa sana na Waheshimiwa Wabunge wafuatao, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis na Mheshimiwa Diana Chilolo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa wametoa mawazo yafuatayo, kwamba watoto wanaoishi mitaani wapelekwe kwa wazazi wao. Sasa suala linakuja ni kwamba unaweza ukawakamata ukawarudisha kule lakini sijui utakapowarudisha watabakia huko tuendele

kuangalia. Wazazi wanaoshindwa kulea watoto hao kuwafanya waishi mitaani wapewe adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kama basi tunaweza tukawabainisha, lakini wengi watoto hawa Waheshimiwa Wabunge ni watoto yatima, hawana wazazi sasa sijui tutamwajibisha nani hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ongezeko la watoto wanaoishi mitaani katika Jiji la Mwanza, hili limezungumziwa na Wabunge wawili. Lingine mawazo waliyotoa hoja ni kutoa elimu vijijini na mijini kuhusu tatizo la watoto wa mitaani na kipengele (d), kutoa watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika kituo cha Kititimo kilichoko Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili tunakubaliana kwamba suala la watoto wanaoishi mitaani ni tatizo la kitaifa na ni aibu kwa Taifa letu. Lakini tunakubali kwamba lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwamba kila familia ina wajibu wa kuwajibika kuhakikisha kwamba watoto wanapata chakula, watoto wanapata mahitaji muhimu na tunaamini kwamba wale watoto ambao hawatakuwa na wazazi ni kwamba zamani katika jamii zetu tulikuwa na utamaduni wa kuwalea kuwalea watoto kijamii (*collective responsibility*), lakini kwa bahati mbaya kutokana na hali ya maisha kuwa ngumu sasa hivi hata ndugu wanashindwa kuongeza mzigo ndani ya familia zao ndiyo sababu hawa watoto wanakwenda mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine ni kwamba watoto wengine yatima wanakuwa wananyang'anywa kile kidogo walichoachiwa na wazazi wao hata nyumba na mashamba na watu wasiokuwa na aibu mbele ya Mwenyezi Mungu.

Kwa hiyo, tatizo linakuwa kubwa kunakuwa na matatizo ya kisheria, kunakuwa na matatizo ya maadili ya kuheshimu watoto yatima na kuheshimu maadili ya dini zetu kwa hiyo, inakuwa ni kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ikishirikiana na shirika la *consortium* la Uingereza limepanga kwenye kipindi hiki cha mwaka 2008/2009 tutafanya utafiti mkubwa wa nchi nzima kuangalia ukubwa wa hili tatizo, maana yake tuweze kupata angalau idadi ya watoto ni wangapi, kwa nini wako mitaani, ni matatizo gani waliyonayo kwa watoto wenyewe kwa sababu sisi kama Wizara tunazungumzia ushirikishwaji wa watoto katika maamuzi. (*Makofi*)

Sasa sisi tukisema kwamba, tutoe maamuzi tuwakamate watu wazima tuwapeleke sijui kwenye vituo gani, tutakuwa hatujawasaidia. Kwa hiyo, ndiyo sababu tumeona kwamba, tuwashirikishe watoto wa mitaani katika utafiti huu, watuambie kwa nini wapo mitaani na wanafikiri kwamba jamii ifanye nini iwasaidie na kama wao wenyewe wapo tayari kushirikiana katika hilo ambalo wanasema kwamba, likifanyika wataacha kukaa mitaani. Tutakapoweza kubaini hili, tunaweza sasa kupanga mikakati ya kuangalia

namna ya kuwatoa hawa watoto na ikawa ni mkakati endelevu, sio wa kwenda kuwakamata watoto tu kama tunakamata kuku, halafu tunawapeleka tunasema ni wazururaji, baada ya siku mbili/tatu wanarudi mitaani. Ndiyo sababu tumesema kwamba ni vyema tukafanya utafiti, tubaini ukubwa wa tatizo na kwa nini hilo tatizo lipo. Wadau muhimu kwenye hili ni hawa watoto, watatuambia kwamba ni kitu gani ambacho kikifanyika watatoka mitaani na watoto wengine hawatakwenda mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine kubwa iliyojitokeza ni ukeketaji wa watoto na Waheshimiwa Wabunge wanasema kwamba, hiki ni kinyume na haki za binadamu. Wamezungumza kwamba, ipo mikoa inayoongoza kwa unyanyasaji huo kwa watoto. Wakaendelea kuongeza kwamba, tatizo hili ni kubwa sana na linadhalilisha watoto wa kike na inaonekana baadhi ya wazazi/jamii wanafurahia ukeketaji kwa watoto wao na ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Suala hili la ukeketaji pia linaashiria kiwango cha ukatili dhidi ya wanawake na watoto; wakauliza Serikali ina mkakati gani wa kuondoa tatizo la ukeketaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge waliochangia katika hoja hii ni Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Idd Azzan na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja hii, tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wameleta michango yao baada ya sisi kuandika majina. Naomba niwatambue Wabunge wengine wasiopungua kumi ambao wamechangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kuwa, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali, zitashughulikia kuondoa ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike nchini. Serikali inafanya juhudi kubwa ya kuhamasisha na kushawishi jamii kuacha mila hii potofu. Serikali imeandaa Mpango wa Taifa wa Kuondoa Ukeketaji wa 2001 - 2015. Mpango huu unatekelezwa na Serikali yenyewe, ikishirikiana na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, baadhi yao yakiwa ni TAMWA, TAWLA, *Inter-African Committee on Traditional Practices* na matawi yake yaliyoko Mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Tanga na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika mengine ni *Women's Research and Documentation Project* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *Anti Female Genital Mutilations Network* ya Dodoma na *Women's Wakeup* ya Dodoma. Hata hivyo, kutokana na utafiti wa *DHS* wa mwaka 2004/2005, ukeketaji umepungua kwa asilimia tatu kutoka asilimia 18 mwaka 1996 hadi asilimia 15 mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ukeketaji ni suala ambalo lipo ndani ya mila na desturi za makabila yetu. Hata tukisema kwamba tutoe elimu kwa walengwa; walengwa wengine sasa hivi wamekuwa ni watoto wa siku mbili au tatu. Ninachoomba ni kwamba, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, mkishirikiana na Waheshimiwa Madiwani na Viongozi wetu wa Dini, muwahamasishe wananchi kwamba, ukeketaji una

madhara makubwa na mateso makubwa kwa watoto wa kike, pamoja na wanawake na kwamba, unavunja haki za binadamu kwa watoto wa kike. (*Makofi*)

Mimi ninaamini tukifanya hii ni ajenda mojawapo katika kunadi sera za vyama vyetu, basi tutaondoa hili tatizo na litapungua kwa kiwango kikubwa. Wengine wamezungumzia kuhusu Sheria ya Kujamiiana na watoto wanaobakwa. Mheshimiwa Idd Azzan amezungumzia kwamba, kuna watoto wa kiume wanaobakwa, wanalawitiwa. Inaelekea kwamba, Sheria ya makosa ya kujamiiana ya mwaka 1998 inawalinda zaidi wanawake kuliko wanaume. Mimi naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hii Sheria ya Kujamiiana haibagui jinsia ya mwathirika au mhanga wa uvunjaji wa Sheria hii. Tatizo linakuja kutokana na mitazamo tofauti ya Mahakimu kwenye Mahakama zetu. Bila kuficha, kwa sababu ni enzi za uwazi na ukweli; kunakuwepo na tatizo la rushwa. Ndiyo sababu unaona kwamba, wale ambao wamekamatwa kwa kulawiti watoto wanapewa dhamana.

Kisheria ni kwamba, wanasema kuna haki ya kupewa dhamana. Sasa inategemea na mtazamo wa Hakimu, anavyoona ukubwa wa hili tatizo, kwa jinsi mtoto ambavyo amethirika kiafya na kisaikolojia na jinsi ambavyo yule ambaye ni mtuhumiwa, atakavyoweza kuingilia upelelezi wa hiyo kesi. Ninapenda kushauri kwamba ni vyema na ndugu zetu Mahakimu sasa wakaona kwamba, utendaji mzuri na utawala bora ndani ya majukumu yao ya kazi utatusaidia sana katika kuwaadhibu hawa watuhumiwa na kupunguza kwa kiwango kikubwa hili tatizo la ubakaji wa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imejitokeza kwa wingi sana ni ya watoto yatima. Hoja hii imegawanyika katika vifungu vine; Wamezungumzia elimu itolewe juu ya suala hili na wale wanaowatunza wawalee kama watoto waliowazaa; na watoto wafuatiliwe vijijini kuweza kusaidiwa. Wanachokizungumzia hapa ni kwamba, watoto yatima wanaopata huduma walio wengi ni wale wanaoishi mijini sio wa vijijini.

Jamii iendelee kuelimishwa kuhusu miradi na urithi kwa hao watoto yatima. Wengine wakazungumzia juu ya sheria zinazolinda haki za urithi na mirathi kwa watoto yatima. Wengine wakaongeza kwamba, kati ya hao watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu, kuna watoto walemavu na kuna *albino*. *Albino* tatizo kubwa linalowakumba ni kule kuuawa kwa ajili ya imani za kishirikina. Waheshimiwa Wabunge, waliochangia katika eneo hili ni Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Maulidah Komu Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Khadija Ally Al-Qassmy na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wameleta michango yao kwa maandishi, muda mfupi kabla sijaja kuchangia hapa. Naomba niwatambue Wabunge hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kuhusu kutoa elimu kwa jamii, kutoa huduma na malezi ya kijamii kwa watoto yatima. Tatizo hili pia ni la kijamii na kwamba jukumu la kuwalea watoto ni la jamii yote. Aidha, Serikali inafuatilia masuala ya watoto wakiwemo yatima kwa kuweka Sera na Programu mbalimbali za kuwasaidia watoto yatima.

Kwa suala hili, Wizara yangu inashirikiana kwa karibu na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, katika kufuatilia maendeleo na ufumbuzi wa watoto yatima kwa lengo la kuweka mikakati ya kitaifa kwa ujumla na utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto, ambayo sasa imeshapitishwa kwenye Bazara la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua inayofuata kwenye kipindi hiki cha mwaka 2008/2009 ni kutengeneza mikakati ya utekelezaji, pamoja na usambazaji wa hiyo Sera ya Watoto. Ndani ya Sera ya Watoto, jambo ambalo limetiliwa mkazo sana ni watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu wakiwepo watoto yatima, walemavu, *albino*, pamoja na haki ya watoto ya kuishi. Hiyo ina maana ya kwamba, tuangalie namna ya kutoa huduma.

Elimu kwa wasichana wetu na akina mama wengine ambao wanapata mimba, wanaamua kuzaa, wananyonga watoto na wanawaua au wanawatelekeza bila kujali kwamba hawa watoto ni binadamu wanaostahili. Hapa mimi naomba nitoe wito kwa taasisi yetu ya dini; hili ni suala ambalo linakwenda kinyume na Misahafu yetu ambayo tunaiheshimu sote. Kuuu mtoto mchanga ni kutenda dhambi. Kwa hiyo, naomba wajaribu kutusaidia sana kwenye suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Sera ya Elimu ya Taifa. Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Elietta Switi na Wabunge wengine wamesema kwamba, Sera ya Elimu ya Tanzania haisemi chochote kuhusu watoto chini ya umri wa miaka mitano. Aidha, shughuli za utoaji elimu kwa watoto hawa zimeachwa mikononi mwa sekta binafsi. Swali; je, Serikali ina mipango gani na dhamira gani ya kurahisisha utoaji wa elimu ya watoto hawa? Serikali ina mpango gani wa kuvipa ruzuku vyuo vinavyotoa elimu ya mafunzo kwa walimu wa shule za awali, pamoja na kuwatambua walimu wa shule za awali?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona hili ni changamoto. Ningependa kusema kwamba, Wizara yetu inaratibu utekelezaji na uandaaji wa Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto wenye umri wa miaka sifuri mpaka miaka minane kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya. Ningependa kusema kwamba, hili suala naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tukija mwaka kesho tutakuja na hiyo Sera mtaiona. Utekelezaji wa hiyo Sera, nafikiri utakuwa umeangalia suala zima la kutoa elimu kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo limejitokeza ni Mabaraza ya Watoto, limezungumziwa na Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Wizara imetenga kiasi cha fedha ambacho kwa kipindi hiki cha mwaka 2008/2009, tutahakikisha kwamba, tunaanzisha Mabaraza ya Watoto katika Wilaya 20 na tutaendelea awamu kwa awamu mpaka tutakapokuwa tumemaliza Wilaya zote tukishirikiana na *UNICEF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine imejitokeza kwenye *NGOs*. Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, imezungumzia kwamba, tuangalie utendaji na migongano katika utekelezaji wa Kanuni na Sheria za *NGOs*. Pili, Kamati ya Bunge ya Maendeleo

ya Jamii ikaendelea kusema kwamba, pia tuangalie mfumo wa kukusanya na kuchambua takwimu za utekelezaji zinazoendeshwa na *NGOs* kwa kuwa Sheria ya *NGO* inataka kila *NGO* kutoa taarifa ya utendaji wa kazi. Je, hizi ambazo hazifanyi hivyo Wizara ina mkakati gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGO* katika kikao chake cha dharura cha tarehe 12 Aprili, 2008, kimejadili Kanuni za Maadili na zimeshapelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, tunasubiri zitawekwa kwenye Gazeti la Serikali ili ziweze kuanza kutumika rasmi. Pia Wizara yangu inakamilisha uanzishwaji wa tovuti itakayotumika kuingiza takwimu na taarifa za *NGOs* zilizosajiliwa nchini na Sheria ya Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali kuanzia uchambuzi wa takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile hoja ambazo hatujazijibu hapa, naahidi kwamba tutazitoe kwa maandishi kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa vile zimebakia hoja chache tu kuhusu *NGOs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita mtoa hoja, dakika zake ni 45.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nachukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yetu jioni ya leo. Ni wazi kwamba, wachangiaji wa hoja yetu walikuwa wengi sana na hivyo ni kudhihirisha jinsi gani suala la maendeleo ya jamii linavyowagusa wengi. Napenda kuwashukuru wote kwa michango yao mizuri ambayo nataka niwahakikishie tutaifanyia kazi ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwatambua na kuwashukuru wachangiaji wote. Kwanza, namshukuru Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, aliyesoma na kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya mwaka jana, yaani mwaka uliopita, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka huu wa fedha 2008/2009. Aidha, namshukuru pia Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa hotuba yake nzuri. Vilevile nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, walioweza kuchangia katika hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa majibu ya hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, napenda kutoa ufafanuzi wa jumla hasa kuhusu majukumu ya Wizara, wajibu na kazi za Wataalamu na tofauti iliyopo kati ya maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama zilivyo Wizara nyingine, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ina jukumu la kuandaa Sera ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii; Sera ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake; Sera ya Maendeleo ya Mtoto; Sera ya



Maendeleo ya Familia; na Sera ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Wizara pia inalo jukumu la kuandaa Mikakati, Programu, Miongozo mbalimbali na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya NGOs na kuratibu utekelezaji wa Sera hizo unaofanywa na wadau mbalimbali, wakiwemo jamii zenyewe, Serikali za Mitaa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na hata Wizara nyingine. Aidha, Wizara ina jukumu la kusimamia na kuendesha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hasa kuwashukuru Wabunge wengi na hususan hawa waliochangia jioni hii; Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Paul Kimiti. Wamesisitiza umuhimu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii. Pia nashukuru wamewataja baadhi ya Wabunge; kwa mfano, Mheshimiwa Dr. Mzindakaya na mimi nataka niongezee kwenye orodha ya Wabunge ambao wameshakuwa Maafisa Maendeleo wa Mikoa. Nikitaja majina yao utaona kweli jinsi wanavyojua kutoa hoja zao kutokana na kazi nzuri walizozifanya katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Mmojawapo ni Mheshimiwa Stephen Wasira; mnaonaje anavyojibu maswali hapa? (*Makofi/Kicheko*)

Wengine ni Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, lakini pia mnamkumbuka aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Cleopa Msuya na wengine wengi ambao wameshapitia Sekta hii ya Maendeleo ya Jamii, ambao wamefanya kazi nzuri. Mimi ningependa niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, kama mtakumbuka miaka ya nyuma; uzuri wa Serikali yetu ni kwamba, tunapona jambo limelegea tunalirudisha tena, tunaliwekea mkazo zaidi. Kama mnakumbuka miaka ya nyuma, ninyi wenyewe m sema na ni mashahidi kwamba, kuna majengo ya maendeleo yale ambayo walikuwa wanayaita *welfare*. Majengo ambayo yalikuwa ya kufundishia wananchi mambo mbalimbali ya kimaendeleo.

Mnakumbuka zamani kulikuwa na magari ya sinema, ambapo Maafisa Maendeleo ya Jamii walikuwa wakipita kuelezea mambo mbalimbali ya kimaendeleo. Wanasimamisha magari katika uwanja wa mpira, wanatoa mada nyingi ambazo zinasaidia wananchi kujiletea maendeleo. Kwa hiyo, msisahau yale mambo mazuri yaliyokuwa yakifanyika zamani, sasa hivi tuseme ukweli yale majumba ya maendeleo yaliyokuwa yakitumika kuelimisha wananchi wengine wamegeuza kwa bahati mbaya sana Halmashauri nyingine zimebadilisha zimekuwa baa na kuzifanyia mambo mengine kabisa, ambayo sio kusudio lake enzi za zamani. Majengo yale yaliwekwa kwa ajili ya kusaidia wananchi kujua mambo, ujuzi na stadi mbalimbali. Kwa kutumia hao Maafisa Maendeleo ya Jamii na Serikali imeona umuhimu wa kurudisha kazi nzuri waliyokuwa wanaifanya na unaona sasa hivi tunaamini kabisa yataimarishwa.

Nachukua nafasi hii, kutoa wito kwa Halmashauri kuangalia uwezekano wa kurudisha yale majengo yaliyokuwa yakitumika na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kuwafundisha wananchi mambo mbalimbali ya kujiletea maendeleo katika maeneo yao. Hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii, wamejifunza stadi na maarifa mbalimbali ya kumwelewa binadamu katika maeneo yake, ambayo kwa Kizungu naweza kusema *sociology*.

Wamejifunza jinsi ya kuelewa mazingira ya watu; jinsi ya kuelewa mila na desturi za watu; utaratibu na mbinu za kuhamasisha. Kwa hiyo, wao ndiyo maana tunasema kwamba, Wizara yetu ni mtambuka, kwa sababu wanashughulikia maeneo yote yanayoleta maendeleo nchini.

Kwa hiyo, ukihamasisha kijiji, kujichimbia visima ni maendeleo. Ukihamasisha watu kujiunga na kisomo cha elimu ya watu wazima ni maendeleo. Ilimradi masuala yote yale yanayoleta maendeleo, yanahamasishwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyodhihirika katika michango ya Waheshimiwa Wabunge, Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii wanao wajibu wa kuwaandaa wananchi kushiriki katika utekelezaji wa Sera mbalimbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Sote tunafahamu, wataalam hao walivyoshiriki na kufanikisha utekelezaji wa Programu na Miradi mbalimbali. Baadhi ya hizo Programu kama tunavyokumbuka ya uhai, ulinzi na maendeleo ya watoto; *HESAWA*, *TASAF* na Programu Shirikishi za Kilimo. Ni dhahiri kuwa, wataalamu hawa ambao wamesomea sayansi ya jamii na uhamasishaji, huwezesha utekelezaji wa Sera za Wizara hii na Wizara nyingine. Hivyo, wataalamu hao huhusika na utekelezaji wa Miradi katika sekta karibu zote na kufanya hivyo si kwenda nje ya maeneo ya kazi. Baadhi ya maeneo ambayo wataalamu wa sekta hii hushiriki sana ni pamoja na mapambano dhidi ya UKIMWI, hifadhi ya mazingira na kuwezesha wananchi katika ujasiriamali.

Kutokana na umuhimu wao, nachukua nafasi hii kutoa wito kwa Halmashauri, kuwawezesha wataalamu kifedha na kinyenzo ili waweze kutekeleza majukumu yao ambayo ni mengi na muhimu. Kama nilivyosema asubuhi, mwaka huu naishukuru Serikali imeanza kutoa shilingi milioni 3.6 kwa Halmashauri zote ili kuwawezesha hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii, wafanye kazi zao kufuatana na majukumu ya Wizara. Kwa hiyo, nawaomba sana Wiongozi wote wa Halmashauri, wahakikishe kwamba wanawapa fedha hizo ili waweze kufanya kazi zao kikamilifu. Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri katika jukumu la kuwaendeleza Wataalamu hao kitaaluma. Aidha, nawaombeni Waheshimiwa Wabunge, kwa nafasi zenu kama Wajumbe wa Halmashauri, mhakikishe kuwa Halmashauri zinawapatia fedha zilizotengwa maalum kwa wataalamu hao. Ni matumaini yangu pia kuwa, Wizara ya Fedha itaendelea kuongeza fedha katika kifungu hicho ili kuwawezesha wataalamu hao kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Wakati kazi za wataalamu hao wa Maendeleo ya Jamii ni kuwezesha ushiriki wa wananchi katika maendeleo, wataalamu wa ustawi wa jamii wana wajibu wa kuhudumia makundi ya watu wenye mahitaji maalum ili kuwawezesha wananchi hao kushiriki katika mchakato wa maendeleo. Makundi hayo ni pamoja na watu wenye ulemavu, wazee na familia zenye matatizo ya kutoelewana, watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kadhalika. Aidha, ustawi wa jamii wanao wajibu wa kurekebisha tabia ambazo haziendani na maadili ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, limejitokeza pia suala la Wizara hii kuonekana kuwa ya wanawake, kutokana na viongozi wake wa juu kuwa wanawake. Mimi sioni tatizo hata kidogo, ilimradi wale viongozi waliopo wanafanya kazi kikamilifu. Uzoefu

unaonyesha kuwa, ngazi ya uongozi hubadilika mara kwa mara; kwa mfano, tangu Wizara hii imeundwa, uongozi umebadilika zaidi ya mara tatu lakini watendaji wamebakia karibu wale wale. Wengi wa watendaji hao ni wanaume. (*Makofi*)

Kwa mfano, katika Idara ya Maendeleo ya Jamii, inao viongozi watano lakini mwanamke ni mmoja tu. Idara ya Watoto inao viongozi watatu wote ni wanaume. Idara ya Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali inao Viongozi watatu, ambao wote ni wanaume. Vivyo hivyo kwa Sera na Mipango. Aidha, zaidi ya asilimia 80 ya Wakuu wa Vyuo ni wanaume. Kwa hiyo, mimi sioni tatizo lolote pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, napenda kama ilivyo kawaida, niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba yangu. Jumla ya Wabunge waliochangia hoja ya Wizara yangu ni 69, wakiwemo tisa waliochangia kwa kauli na 60 waliochangia kwa maandishi. Nawashukuru sana wote mliochangia. Aidha, Waheshimiwa Wabunge sita walichangia wakati Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilipowasilishwa. Naomba niwatambue kama ifuatavyo; nikiamini kwamba muda nitakaoutumia hautahesabiwa. Waliochangia kwa maandishi ni wafuatao:-

Kwanza ni Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mlingwa, Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir na Mheshimiwa Feteah Saad Mgeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Samuel Mchele Chitalilo, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma, Mheshimiwa Maida Hamadi Abdallah, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene, Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mheshimiwa

Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Philip Sang'ka Marmo, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu, Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir na Mheshimiwa Vuai Abdallah KHamis. (*Makofi*)

Waliochangia kwa kauli ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Elietta Namdumpe Switi, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo na Mheshimiwa Dr. Lucy Sawere Nkya, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkulo umemwacha.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Oooh! Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, waliochangia kupitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mheshimiwa Martha Mosses Mlata, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel na Mheshimiwa Masoud Mohamed Masoud. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali kwamba, kulikuwa na wachangiaji wengi na siyo rahisi kuweza kujibu hoja zao zote kwa muda nilionao. Hata hivyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, tutajibu hoja zote zilizotolewa kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nianze kutoa majibu kwa baadhi ya hoja kama ifuatavyo:-

Nimeona kwamba, kwa muda nilionao na hoja zilizotolewa ni nyingi, ningeomba kwanza nipitie haraka haraka yale ambayo naona nisiache kuyapitia, halafu baadaye nirudi kwenye hoja. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, iwapo nitarudia baadhi ya hoja mnisamehe tu kwa sababu lengo langu ni kutaka kujibu mengi kwa kadiri nitakavyoweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna yale ya msingi ambayo yametajwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, mimi kwanza ningeenda kuzungumzia juu ya hoja ya *fifty fifty*. Hoja hii sisi kama Wizara tumeichukulia kwa aina mbili au kwa utaratibu wa aina mbili. Kwanza, tumechukua *fifty fifty* kwa kuangalia uwakilishi wa wanawake katika ngazi za utendaji, ngazi za maamuzi, lakini hasa ngazi za utendaji. Kwa hiyo, sisi kama Wizara, tuliandaa mkakati wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, kuangalia jinsi ambavyo tunaweza kupata uwakilishi wa *fifty fifty* hasa katika ngazi za maamuzi, lakini pia za utendaji. Kwa msingi huo, tukawa tumeandika mkakati wetu ambao sasa hivi upo katika ngazi ya kujadiliana na wadau halafu baadaye upelekwe kwenye ngazi za maamuzi

ya juu. Tumechukulia pia upande wa pili huu wa sualal la *fifty fifty* kwa lengo la kuingiza akina mama kwa 50% Bungeni. Hili suala sasa linakwenda hata nje ya Wizara yetu, kwa kushirikisha chama na serikali kwa ujumla. Kwa hiyo, kwa msingi huo, haya masuala yanakwenda kwa pamoja lakini kwa utaratibu tofauti. Jambo la msingi ni kwamba, uwakilishi wa akina mama wa 50% kwa 50% Bungeni na katika nafasi za utendaji unafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ningependa kuizungumzia ni suala la ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ambalo limetajwa na Wabunge wengi. Suala hili kama mnavyokumbuka, nimelitaja pia kwenye hotuba asubuhi kwamba, ukatili dhidi ya wanawake na watoto si suala la Wizara tu; ni suala la kushirikisha jamii yote ya Tanzania kwa ujumla. Kwa msingi huo, sisi tumeenda hata nje ya Wizara; sisi kama Wizara, tuliandaa mkakati na mpango kazi wa tangu 2001 mpaka 2015 na sasa hivi tunauangalia ili kuona kama baadhi ya maeneo pengine yamepitwa na wakati. Tumeona kwamba, kuna umuhimu wa kushirikisha wadau wengine. Kwa hiyo, sasa hivi mimi nina furaha kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, juzi tulikuwa na mazungumzo na Mheshimiwa IGP Said Mwema, kuangalia jinsi gani ambavyo Wizara yetu sisi inaweza kushirikiana na Jeshi la Polisi ili tuone jinsi linavyoweza kushughulikia hili suala la ukatili dhidi ya wanawake, kwa sababu tumeona bila kushirikisha vyombo vya usalama hatuwezi. Pia tumeshirikisha wadau wengine ambao ni *NGOs* na wakati huo huo tumeshirikiana na taasisi isiyo ya Kiserikali ya *Hans Seidel Foundation* ya Kijerumani, ambayo imekubali kutusaidia sisi katika Kampeni hii ya *Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto*. Mpaka sasa hivi tunaangalia uwezekano hata wa kupata *Cinema Vans* ambazo zinaweza kusaidia kutembea huku na kule kujaribu kuelimisha wananchi ili waache mambo ya ajabu yanayofanywa sasa hivi ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto na pia hata wanawake, wazee na *albinos* kama mnavyosikia.

Kwa hiyo, hili suala tunalishughulikia lakini si peke yetu tunashirikiana na wadau. Nachukua nafasi hii pia kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, ninyi mkiwa wawakilishi wa wananchi; mtusaidie katika maeneo yenu kutusaidia katika Kampeni hii ya *Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto*. Ninawashukuru kwa kuwa mmetia saina katika vijarida ambavyo vile vikonyo vinapelekwa Umoja wa Mataifa, majina yenu yakaonekane kule kwamba, mnatuunga mkono katika kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Kwa hiyo, nawaomba sana wote Halmashauri na Wananchi wote kwa ujumla, tusaidiane katika vita hii ya kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine kubwa sana iliyojitokeza ni kusaidia watoto wa mitaani. Kama alivyosema Naibu Waziri, alipokuwa naye akijadili hoja za Wabunge na mimi ningependa kurudia. Suala hili la watoto wa mitaani ni kubwa sana na linakuja katika sura ya ajabu sana. Wapo baadhi ya wazazi kutokana na utafiti mdogo uliofanywa na watu wengine, wazazi wengine wanajificha kando, wanawatuma watoto kuja kuomba. Ninyi mnawaona ni watoto wa mitaani, kumbe wana wazazi wao wamebana sehemu fulani. Wakati huo huo kweli wapo watoto wa mitaani wanaotokana na mazingira magumu, waliofiwa na wazazi wao. Kwa hiyo, sisi kama Wizara, tumeona ni vizuri tushirikiane na wadau. Kwa hiyo, tumeushirikisha Ubalozzi wa Uingereza ambao unatuunganisha na *International Consortium of Street Children*, ambao wamekubali kuja

kufanya kazi na sisi ili kufanya utafiti wa kina, kuona chanzo cha watoto wa mitaani na wakati huo huo kupata mikakati ya jinsi ya kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tumeliona ni kubwa sana ni suala la sheria zinazowakandamiza watoto na wanawake, hasa zilizopitwa na wakati, zenye matatizo kama vile Sheria ya Ndoa, Sheria ya Watoto na Sheria ya Uasili ya Watoto na nyingine nyingi. Tumejadiliana na Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba, ambaye amenihakikishia kwamba, ataleta Bungeni mwezi Oktoba ili baadhi ya Sheria hizi ili ziangaliwe na kufanyiwa marekebisho hasa kwa kushughulikia maeneo ambayo yanawakandamiza au kuwanyima haki watoto na wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kulikuwa na suala la mimba za watoto kama alivyoelezea Naibu Waziri, mimi nimeona pia nilizungumzie. Hili la mimba za watoto, mimi kwa bahati nzuri nimeanza kulishughulikia nikiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Hili ni suala gumu ambalo linahitaji kushirikiana sisi sote, kuhakikisha kwamba watoto wetu wa kike hawaendelei kupoteza masomo yao. Kwa misingi hiyo, naamini kinachoendelea sasa hivi ndani ya Wizara kuna mjadala ambao unaangalia jinsi ya kushughulikia suala hili, lakini pia na kuangalia uwezekano wa kurudisha watoto shuleni ili waendeleo na masomo kama ilivyo katika nchi nyingine kama Malawi, Zambia, Ghana na Nigeria, wanawapa nafasi.

Hii itategemea jinsi ambavyo wananchi watakuwa wamechangia katika mjadala huo na tunao Wabunge wanaofuatilia ambao ni Wajumbe wa Kamati hiyo; tuna Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Zainab Vulu, ambao wote wanahudhuria vikao hivyo vya kuamua hatima ya suala la watoto kukatizwa masomo kutokana na mimba. Mimi nikiwa Waziri ambaye ninasimamia haki za watoto, ningechukua nafasi hii, kuomba wazazi wote na jamii yote kwa ujumla, tujitahidi kukemea wanaume wote wanaojihusisha na watoto wadogo. Wakati huo huo pia tuangalie ni jinsi gani ambavyo tunaweza kushawishi wazazi kuwa karibu na watoto wao zaidi, kuwapa maadili mema na kuwafundisha ili wachukue tahadhari zozote zinazowafanya watoto kuishia kukosa masomo na hivyo kupunguza idadi ya wanawake waliosoma na hivyo kuwa na ushiriki mdogo katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja nyingine ambayo ni muhimu sana; suala la Vyuo vya Maendeleo na Vyuo vya Wananchi. Vyuo hivi (*FDCs*) ni vyuo vya maana sana. Kwa muda mfupi niliokaa katika Wizara hii, kwanza mimi nilipokuwa Waziri wa Elimu, nilikuwa hata nafikiria kuvichukua vyuo hivi, lakini baada ya kukaa na kuviona sasa hivi nasema visichukuliwe viendeleo kukaa chini ya Wizara hiyo hiyo viimarishwe, kwa sababu nimeona kazi nzuri sana inayofanywa na vyuo hivyo. Kama alivyosema Mheshimiwa Diana Chilolo, ni kweli Singida Mjini wanafunzi wanaokwenda kuchukua mafunzo ya ujasiriamali mbalimbali, ufundi stadi mbalimbali wapo 200 wanaolala pale; ni faida kubwa sana. Tulikuwa tunaangalia kama tunaweza kuongeza idadi hii, sasa fikiria sisi tuna vyuo 53 kama kila chuo kitachukua wanafunzi wengi kuwapa ufundi wa useremala, *welding* na wengine umakenika, stadi zile ambazo zinaweza kuwasaidia kujajiri au kuajiriwa; tutakuwa tumechangia sana katika kupata ajira zaidi ambazo lengo letu ni kuzidi hata 1,000,000. Kwa hivyo, vyuo hivi vina maana sana.

Ninachukua nafasi hii kumshukuru Waziri wa fedha, ambaye baada ya sisi kuandika andiko la umuhimu wa vyuo hivyo, alikubali kutoa shilingi bilioni 1.5 mwaka huu wa fedha. Tunaamini kabisa hizo shilingi bilioni 1.5 kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge kwamba, tusifanye ukarabati mdogomdongo tuchukue vyuo vichache tufanye kazi nzuri sana na majedwali yameonyesha, tutachukua vyuo vichache tuvifanyie ukarabati wa kutosha ili kweli vifanye kazi. Ninaamini kabisa Wizara ya Fedha, kutokana na jinsi mliyochangia humu ndani, mwaka kesho naamini kutokana pia na uwezo wa fedha wataongeza fedha za matengenezo ili vyuo hivi vifanye kazi iliyokusudiwa. Uzuri wa vyuo hivi tofauti na vyuo vingine, wale walimu wa vyuo vya hasa vya Maendeleo ya Wananchi, wanakwenda kufundisha wakulima nje. Wanakwenda kuwafundisha ufugaji wa nyuki, yaani ambao kwa Kizungu unaitwa *out reach*. Wanatoka chuoni wanawafuata wananchi kule waliko. Kazi ambayo hakuna vyuo vingine vinavyoifanya. Kwa hiyo, mimi nasimama mbele ya Bunge lako kusema hivi Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 53 ni vya maana sana viendelee na virekebishwe ili vizalishe ajira. Vyuo vya Maendeleo ya Jamii pia ndiyo vinavyotufundishia Maafisa Maendeleo wa Jamii ambao tunawahitaji sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba tumetaja kwamba, Maafisa Maendeleo wa Jamii ambao ni muhimu sana, wanaoshuka mpaka kuwafikia wananchi ni Maafisa Maendeleo wa Wilaya na Maafisa Maendeleo wa Kata. Sasa fikiria katika Kata nadhani 2,579 nchini ni 39% katika nchi hii ambazo zina Maafisa Maendeleo wa Kata, ambao ndio wa maana. Wanajua kuhamasisha, wao hata ukiwapa baiskeli wanakwenda. Nami ningependa kuchukua nafasi hii, kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, tutafanya jitihada kwa kadiri iwezekanavyo na kuongeza hata na ubunifu ili kushirikiana na Halmashauri, kuwapa angalau vitendea kazi ili waweze kufanya kazi yao muhimu sana wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la muhimu ambalo limezungumzwa ni Sera ya Watoto. Sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, tunachotakiwa kuangalia ni kwamba mtoto apate haki zake tano; ya kwanza kabisa ni haki ya kuishi, haki ya kutunzwa, haki ya kulindwa, haki ya kuendelezwa, haki ya kutokubaguliwa na haki ya kushirikishwa. Kwa hiyo, sisi tunapokuja kwenye Sera, kwa mfano, Waheshimiwa Wabunge wengi tu wamezungumzia elimu ya awali inayotolewa kwamba sisi tuiingilie, lakini katika kuangalia zile haki tano za mtoto, lazima tushirikiane na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa sababu wao ndio wanaojua kati ya umri wa sifuri mpaka miaka minane ni aina gani ya kinga na matunzo gani wanapaswa kupata. Halafu pia Wizara ya Elimu yenyewe ndiyo inayopaswa kujua masuala ya elimu. Uzuri wake tulishafanya kikao cha pamoja na maafisa wetu wanashughulikia hivi sasa.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ndiyo inayopaswa kusema mtoto wa umri labda wa miaka miwili mpaka mitatu anapaswa kupata elimu ya namna gani, kwa sababu utakuta mtoto wa umri wa miaka mitano tayari ameshaanza kujifundisha mambo makubwa ya kumpita kimo. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ndio inayopaswa kuelezea aina gani ya elimu hawa watoto wapate. Sisi Wizara zote tatu, tunashirikiana ili tupate Sera moja ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine sasa ningependa kujibu kutokana na hoja zilivyotolewa, lakini niliona haya ya awali ni vizuri niyatoe kabla nisije nikagongewa kengele kabla sijayatoa. Ningependa nilitaje hapa jambo moja ambalo nimeliacha kulizungumzia kuhusu hivyo hivyo vyuo ninavyovipenda. Hivi vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Wananchi, tumeanza kuzungumza na Wizara husika, yenyewe ipo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ili tuone kama VETA inasaidia vyuo binafsi, tuangalie basi jinsi gani ambavyo hii VETA inaweza kusaidia vyuo vyetu vya wananchi. Sisi wakitusaidia basi tunaweza kwenda kufanya kazi vizuri tu. Suala la kuongezewa bajeti, hili limezungumziwa sana hata na Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama amelizungumzia sana kwa niaba ya Kamati nzima. Nadhani na Waheshimiwa wote mmesikia, naamini kabisa Serikali ina masikio itaangalia jinsi ya kutekeleza kutokana na uwezo wa kifedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye hoja ambazo naamini kabisa sitafika mwisho, lakini nyingine nizitaje haraka haraka. Kamati ya Kudumu ndiyo hiyo imezungumzia suala la bajeti ambalo tumelizungumzia kwamba, tayari Serikali imesikia italifanyia kazi. Wizara ijenge hoja ya kuongezewa bajeti yake, tayari wameshalizungumzia pia Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Dokta Slaa. Sisi tunasema kwamba, Serikali imesikia; naamini itaangalia jinsi ya kuwezesha. Mheshimiwa Dokta Slaa, alizungumzia Maafisa Maendeleo ya Jamii kutokuwa na nyenzo na bajeti ya kutosha kufanyia kazi; ni kweli hii ndiyo sehemu ambayo tutaifanyia kazi ili tuwawezeshe hawa wafanyakazi kutokana na umuhimu wao. Pia Kamati ya Kudumu ilizungumzia suala la ushauri wa Kamati kuwa Serikali iweke mikakati ya kutekeleza mkataba wa huduma kwa Mteja, hasa kwa kutoa mafunzo na elimu kwa wahusika.

Aidha, Wizara ichapishe majarida ya kutosha na kugawiwa wahusika; huu ni ushauri ambao tutauzingatia. Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ilizungumzia suala la jengo, hoja ambayo iliyochangiwa pia na Mheshimiwa Elietta Namdumpe Switi kuwa Jengo halionyeshi hadhi ya kuwa Makao Makuu ya Wizara. Napenda kuchukua nafasi hii, kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mheshimiwa akipata nafasi ya kufika Dar es Salaam, aangalie tu nyuma ya jengo letu lile chakavu kuna jengo kubwa ambalo linajengwa la ghorofa sita kama sikosei, ambalo sasa hivi tayari tumeshamaliza ghorofa tatu, tunangojea awamu ya mwisho kumalizia ghorofa ya sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wasemaji wa Kambi, walizungumzia juu ya kuangalia suala zima la muundo wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na ikiwezekana Wizara hii iwe na jukumu moja la kuangalia maendeleo ya jamii kwa ujumla na Wizara nyingine yoyote isipewe majukumu hayo. Nadhani nimeshalizungumzia vizuri kwamba, sisi tunaangalia sera zetu ili kuhakikisha kwamba, zinafanyiwa kazi katika maeneo mengine. Ninaamini kabisa kwamba, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani amenisikiliza na Kambi ya Upinzani pia imesikia. Nisingependa kurudia majukumu ya Wizara kwa sababu nimeyaeleza vizuri sana katika kitabu cha hotuba pale mwanzoni kabisa.



Kambi ya Upinzani pia ilizungumzia upungufu wa wakufunzi katika Vyuo na Wizara ni kweli sasa hivi Afisa Utumishi wetu, yaani wa Wizara , anaandaa orodha ya upungufu wa watumishi na amekwishaandika barua kuomba kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Mwaka huu tumepewa watumishi 98 ambao tayari wameajiriwa, lakini tunaamini tukiomba tena tutaongezewa ili tukidhi mahitaji ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *fifty fifty* lilizungumziwa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, lakini tayari nimeshalizungumzia. Mchakato wa Uwezesaji wa Benki ya Wanawake tumeshauzungumzia, ambao ulizungumziwa na Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar na Mheshimiwa Captain John Komba, wote wamezungumzia suala hilo. Nilitaka kusema tu kwamba, mchakato unaendelea na tunaamini kabisa kwamba, mwaka huu wa fedha, Benki itakuwa imeshaanza kazi yake. Mheshimiwa Janet Kahama alizungumzia wanawake washirikishwe katika kuunda benki. Wizara itahamasisha wanawake ili wajiunge, lakini si wanawake tu tunaamini pia kina baba watajiunga. Ningechukua pia nafasi hii kuzungumzia suala alilolizungumzia Mheshimiwa Bujiku Sakila kwamba, hii Wizara inaonekana inajali wanawake tu. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Bujiku Sakila, Wizara hii inaitwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, sasa pale kwenye jinsia ndio akina baba wapo. Ukiangalia kwenye kitabu ndani hata kwenye majedwali, karibu watu 31,000 waliopata mafunzo wanaume ndiyo wengi zaidi karibu 24,000 na 17,000 tu ndio wanawake. Kwa hiyo na wanaume nao wanafaidika.

Tulipokuwa tunazindua ile Kampeni ya Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto kwenye risala yetu mbele ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, tulimwambia kwamba, ukatili dhidi ya wanawake na watoto; tunawataja tu wanawake na watoto kwa sababu idadi ni kubwa zaidi, lakini ni kweli wapo wanaume wanaofanyiwa ukatili dhidi yao. Nami ningechukua nafasi hii, kuwalaani wanaume wanaofanya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na pia kuwalaani wanawake wanaofanya ukatili dhidi ya wanaume. Tatizo tu ni kwamba, wanaume ndio mmezidi sana. Nashukuru kwamba, mliweka sahihi zenu kwenye kijarida cha kukataa, tunaomba muwahamasishe wanaume wenzenu. Mheshimiwa Spika, aliwatahadharisha kwamba, ndani mle kuna kipengele kinasema mtawasaidia akina mama kazi za jikoni, mmeshakubali nawashukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetekelezaje Sheria za Ndoa? Nimekwishasema zitaletwa na Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba. Hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid na Mheshimiwa Stella Manyanya. Hiyo tumeshasema, inafanyiwa kazi mwezi wa Oktoba baadhi ya Sheria zitakuja. Suala la uwezesaji wa wanawake alilizungumzia Mheshimiwa Komu. Mimi ningetaka kusema hivi, maana ya *Gender Mainstreaming* ni nini? Maana ya *Gender Mainstreaming* na *Gender Budgeting* ni kwamba, suala la maji, kutengeneza matunda, ndio maana ya *Gender Mainstreaming*. Alizungumzia hata Mheshimiwa Maghimbi. Mwaka jana, yaani mwaka wa fedha uliopita, tulikuwa tumeandaa kikao na Makatibu Wakuu wa Wizara zote na ninaamini Katibu Mkuu Mama

Mwaffisi, ataandaa tena kikao kingine na Makatibu Wakuu. Maana ya *Gender Mainstreaming* ni kwamba, katika kuangalia bajeti hasa *Gender Budgeting*, muangalie ni jinsi gani mtakavyotenga fedha ili wanawake washiriki vizuri katika sekta husika. Kwa hiyo, kama ni Wizara ya Maji; ni jinsi gani ambavyo watatenga fedha ili zisaidie wanawake kupata maji kwa utaratibu ambao watauweka wao wenyewe. Ndio maana utakuta kila Wizara ina *gender focal person* pale, maana yake ni kwamba, aangalie masuala kama hayo.

Kama ni Wizara ya Kilimo watafanyaje; watatenga kiasi gani; na kwa utaratibu gani ili wanawake waweze kulima vizuri zaidi au waweze kupata nyenzo za kuwasaidia kulima zaidi; ndio maana ya *Gender Mainstreaming*. Kwa hiyo, sio mimi tu ni Wizara zote kuangalia katika Sekta zao, watakavyoweza kuweka bajeti ya kuwasaidia akina mama ili waweze kushiriki katika Sekta husika. Kwa hiyo, yote aliyokuwa anayazungumzia Mheshimiwa Komu, ndio ya Mheshimiwa Dokta Nagu pale Viwanda. Katika Sekta yake yeye anaweza kufanyaje ili wanawake waweze kunufaika. Kwa hiyo, inagusa Wizara zote, ndiyo maana ya *Gender Mainstreaming* na kuwaweka wale wawakilishi katika Wizara zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi tumejikakamua, tumetaja wazi kwamba, sisi kama Wizara kwa kushirikiana na *ILO* na wadau wengine, tunatafuta eneo moja Dar es Salaam la kuweza kuwapatia wanawake wa nchi nzima, soko walete bidhaa zao ili zionekane. Kwa hiyo na sisi tumejikakamua kwa njia mojawapo ya kushiriki katika suala hilo na pia kusaidiana na *Equal Opportunity* kuleta akina mama wajasiriamali kuja kuangalia na kuweka bidhaa zao zionekane na ziweze kununuliwa.

Kwa hiyo, wamesema kutafuta maeneo mapya ya bidhaa za wanawake, ambayo amechangia Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Batenga, Mheshimiwa Janeth Massaburi. Haya yote tunayafanyia kazi. Halafu kulikuwa na suala lingine; utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa fedha za *WDF*, yaani *Women Development Fund*. Huu Mfuko wa kuwaendeleza akina mama unapitia kwenye Halmashauri, kwa hiyo, Halmashauri ikichangamka, ikikopa Sh. 4,000,000 ikifanya vizuri inapewa Sh. 8,000,000. Kwa hiyo ni kuchangamka tu kwa Halmashauri. Ningechukua nafasi hii kutoa wito kwa Halmashauri, ziendeleo kuwasiliana na Wizara yetu wakope zile fedha, wakirudisha wanapata tena. Nina furaha sana, mfano mzuri niliouona Mafinga, nimekuta akina mama wamefuga nguruwe, kuku, ng'ombe na mbuzi. Wakasema mama twende tukakuonyeshe samani tulizonunua. Wakanipeleka mpaka kwenye nyumba ya mwanachama mmojawapo wa ile *SACCOS* nione fedha walizopata kutokana na kikundi chao kwa kutumia Mfuko wa Maendeleo ya akina mama kununua samani. Anasema mume wake anamheshimu sana kutokana na alivyochangia maendeleo ndani ya nyumba ile. Kwa hiyo, Mfuko huu ni wa maana, Halmashauri ziendeleo kuwasiliana na sisi ili wapate.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mimi ninaamini kabisa tutafanya mengi tu tukishirikiana na wao. Suala hili limezungumziwa sana na Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Mhonga Ruhanywa, Mheshimiwa Hemed

Mohamed Hemed, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Kanali Feteah Saad Mgeni, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Florence Kyendesya na Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro. *TACAIDS* ina utaratibu wake kwa kushirikiana na Halmashauri; inawapeleka fedha Halmashauri zenyewe zinashughulika. Sisi hatufiki kwenye vijiji kwa suala la *UKIMWI* ila ni Halmashauri zenyewe wanashirikiana na *TACAIDS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maswali mengine mengi tu yaliyoulizwa ambayo tumeyachukua, kama nilivyosema, nimeahidi kwamba tutayafanyia kazi. Kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare kwamba, kina matatizo mengi kama alivyosema Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Herbert Mntangi na Mheshimiwa Switi kwamba, kweli vipo vyo vyo vinavyohitaji miundombinu kutengenezwa na kadhalika, yote tutayafanyia kazi. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Musoma pia kina matatizo; haya yote tutayafanyia kazi. Nami nilitaka kusema tu kwamba, kama nilivyoahidi hapo awali, maswali mengi ni ya uchakavu wa majengo, lakini tutayafanyia kazi. Halafu pia kama nilivyosema, Chuo cha Misungwi, nyumba za watumishi wa vyo vya maendeleo ya jamii, yote hayo yamezungumzwa. Naona ni vizuri sisi kama Wizara tujipange. Kama nilivyoahidi, kuandika andiko zuri zaidi ili kuwasiliana na wenzetu wa Hazina ili watusaidie kupata fedha za kuendelea kutengeneza vyo hivi ambavyo tunavitegemea sana.

Ombi la Wizara kwenda Wilayani Namtumbo; kama ulivyosema Mheshimiwa Vita Kawawa, yote hayo tutaona tu jinsi ya kufanya. Halafu Mheshimiwa Charles Mlingwa, naye amezungumzia fedha zilizotengwa (Sh. 95,376,700), kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Wananchi Buhangija ziwahi kutolewa; ni kweli mara tu zitakapotolewa na sisi tutazileta huko.

Wizara kuchukua juhudi kushirikiana na Halmashauri zilizoko, kukusanya vijana na kuwapeleka katika Vyo vya Maendeleo ya Wananchi kupata stadi, yote haya tunayafanyia kazi. Cheti cha Diploma Tengeru kukataliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Nilitaka kusema tu kwamba, hivi vyo vilivyokuwa vikitoa cheti vitaendelea kutoa cheti. Kwa hiyo, naomba niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tumeona cheti ni kitu cha msingi sana na Watendaji wengi hasa wanaokwenda kwenye Kata ni wale ambao wana elimu hiyo.

Mikakati ya kuboresha Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Malya, alizungumzia Mheshimiwa Esther Nyawazwa na mimi nataka kusema tu kwamba, hata mwaka huu wa fedha, Chuo cha Malya kimetengewa fedha na kitaendelea kutengewa fedha kutokana na uwezo wa serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema tu kwamba, maswali tuliyoulizwa ni mengi na wengi wamezungumzia hata pengine Wizara ibadilishwe. Mimi naona Wizara ibaki hivyo hivyo ila sisi tu tuendeleo kufanya kazi kwa bidii na kuratibu haki za wanawake, haki za wanaume kama binadamu wenzetu na haki za watoto, ilimradi sisi sote tuhakikishe kwamba, haki zile zinalindwa. Wanaoweza kutusaidia kulinda hizi haki

ni wananchi kwa kufichua maovu; ni sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge kwa kuongea na wale watu tunaowawakilisha katika maeneo yetu. Mimi naamini kwamba, Waheshimiwa Wabunge wanaweza sana kwa sababu wanaelewa mila na desturi za watu wanaowawakilisha. Kwa hiyo, wao wanaweza kutusaidia sana. Kwa mfano, masuala ya ukeketaji, nadhani Waheshimiwa Wabunge wanaotoka maeneo hayo, wanaweza kutusaidia sana lakini sisi peke yetu hatuwezi, inabidi lazima tushirikiane na wadau; wadau ni *NGOs*. Sisi kama alivyosema Naibu Waziri, tumeweka sheria nzuri tu Namba 24 ya Mwaka 2002, ambayo itatusaidia kufanya kazi kwa karibu sana na *NGOs*. Kwa hiyo, tukishirikiana sisi sote pamoja na *NGOs*, tunaamini kana kwamba, masuala kama hayo ya ukeketaji, ukatili na mengineyo mengi yatawezekana tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono na kwa mujibu wa kanuni ya 104(1), naongeza muda wa dakika 30.

#### **KAMATI YA MATUMIZI**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

Kif. 1001 - *Administration and General*.... .... Sh. 1,618,386,003

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza.

Sina haja ya mshahara wa Waziri wala nini, ninachoomba ni ufafanuzi. Nimefurahishwa kwamba, Wizara imesema inaandaa Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Watoto. Sasa ninapenda tu kufahamu kwamba; je, Wizara itazingatia vipi katika Sera hiyo mpya, yaliyosemwa kwenye Sera ya Watu wenye Ulemavu nchini na yaliyosemwa kwenye Mkataba wa Haki na Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu Duniani ili Sera hiyo iwe kamilifu, iwazingatie vizuri zaidi na hilo kundi la watoto wenye ulemavu?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kumjibu Mheshimiwa Margreth Mkanga, kufuatana na swali lake aliloliuliza kama ifuatavyo:-

Ametaka ufafanuzi kwamba, kwa jinsi gani Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto itakavyozingatia suala la walemavu. Kwanza, ninataka kusema kwamba, tunapotengeneza Sera yoyote ni vizuri sana kushirikisha wadau. Suala la walemavu ni muhimu sana, hata kwenye kitabu changu cha bajeti nimesema. Kwa hiyo, naamini katika kundi la watu watakaoshirikishwa pia ni kundi la walemavu ili tuone jinsi

gani ambavyo wanashirikishwa kikamilifu ndani ya Sera, yaani Sera itamke jinsi ambavyo watahughulikiwa.

Kama nilivyosema tangu awali kwamba, Sera itatengenezwa na Wizara tatu kwa sababu tunapozungumzia hii Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Awali ni kuanzia mwaka 0 – 8. Kwa msingi huo, tutahusisha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ambao wataangalia mtoto mlemavu na wa kawaida anapaswa kupata kitu gani. Kwa upande wa elimu nayo itaangalia watoto wakiwemo walemavu wanapaswa kupata nini katika umri huo kati ya 0 - 8 kufuatana na Sera ya Elimu itakavyokuwa. Sisi tutaangalia kama mtoto anapata haki zake tano katika Sera hiyo. Kwa hiyo, mimi naamini tukiwashirikisha na wadau wengine, basi tutapata tu jambo zuri au utaratibu mzuri wa kuwashughulikia watoto wenye ulemavu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima Mdee karibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mshahara wa Waziri, kwa hiyo, mambo ya Vote hakuna siku hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yetu ukurasa wa 11, tumezungumzia suala zima la tatizo la umeme katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Rugemba. Nampongeza Waziri alivyosema kwamba, wanavithamini sana Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii. Katika maelezo yake hajatoa majibu, inawezekana anaweza akatuambia kwamba yeye siyo Waziri wa Nishati na Madini, kwa hiyo hahusiki na umeme.

Ninataka atupe programu, kuna programu gani kuhusiana na umeme katika chuo hiki ambacho taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba, tokea mwaka 1973 hakuna Umeme? Vilevile tufahamu kwamba, Mheshimiwa Rais katika kampeni zake alisema kwamba by 2010 kila nyumba itakuwa na umeme. Sasa hapa tunazungumzia Chuo. Naomba uniambie kuna programu gani katika kuwezesha hiki chuo kiweze kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima kweli kila nyumba? Haya Mheshimiwa Waziri! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa ufafanuzi kuhusu hoja aliyotoa Mheshimiwa Halima Mdee. Kwanza, karibu sana. Ninataka kusema tu kwamba, kama ataangalia jedwali la matengenezo ya vyuo; kuna vyuo ambavyo mwaka huu vinapata umeme wa *solar* na ndivyo tulivyoweka kwamba, kila mwaka kutakuwa na vyuo ambavyo tunavipa umeme wa *solar*.

Kwa hiyo, napenda nimhakikishie kwamba, pamoja na kufuatilia umeme wa *TANESCO*, lakini pia tutaweka kwenye utaratibu wa *solar* ambao kila mwaka tunachukua vyuo kama tulivyoonyesha kwenye jedwali. Asiwe na wasiwasi; kwanza chuo cha Rugemba sasa hivi kinafanyiwa matengenezo makubwa sana. Mimi mwenyewe

nimefika pale katika vyuo vinavyofanyiwa ukarabati mkubwa, hicho ni kimojawapo na ukitaka hata kutembelea huko utafurahi, kuna maktaba nzuri sana, kwa hiyo haiwezi kuwa maktaba bila umeme. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Kwa kuwa dira na dhima ya Wizara hii ni kuwezesha jamii kuwa na mwamko wa kujiamini, kujituma na kuwa na utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii katika kujiletea maisha bora kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na haki za watoto. Hii itakuwa zaidi kwenye suala zima la haki za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi watoto yatima wameongezeka sana na wengi kati ya hao wamekuwa pia ni waathirika wa Virusi vya UKIMIWI na UKIMWI. Tukiangalia unakuta mashirika ya watu binafsi ndiyo wamekuwa wanajenga vituo, kwa mfano, kuna hiki Kituo cha Tumaini hapa Dodoma. Ninaomba kujua kwa kuwa Serikali inajua kabisa kwamba, kuna watoto wengi sana waathirika wa UKIMWI. Je, kuna kituo hata kimoja ambacho Serikali imetenga au imejenga kwa ajili ya watoto hawa; na kama hakuna Wizara hii ambayo nina hakika ndiyo inahusika; ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba watoto hawa walau wanapata makazi ya kudumu ambayo yatakuwa yanahudumiwa na Serikali?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nifafanue swali alilouliza Mheshimiwa Susan Lyimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka tu kusema kwamba, sisi jukumu la Wizara yetu kama nilivyoeleza kwenye Kitabu chetu cha Bajeti ni kwamba, tunaratibu, kusimamia au kuhakikisha kwamba, haki za mtoto zinalindwa. Kuhusu kuwatunza watoto kwenye eneo moja, sisi hatushughuliki nalo moja kwa moja. Mimi naamini lipo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Ninavyofahamu mimi, hakuna anayeanzisha mahali pa kutunzia watoto yatima au wa aina yoyote, bila kupata kibali cha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa misingi hiyo, sisi tupo tayari kusaidiana nao lakini jukumu hasa lipo kwenye Wizara inayohusika.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu nilielezea jinsi gani ambavyo akina mama wengi wananyanyasika hapa nchini na wengi wao hawajui haki zao za msingi. Nilipenda kujua kwa kuwa kuna *NGOs* ambazo zinasaidia kutoa elimu ya ufahamu kwa akina mama, pamoja na kutambua haki zao msingi na kutoa msaada wa kisheria kwa mfano *TAWLA*, *TAMWA*, *Human Rights Centre* wanasaidia sana akina mama kuweza kujua haki zao na wanafanya hivyo kwa kujitolea. Ninapenda kujua; je, Serikali inatoa mchango gani kwa vyama hivi ili viweze kusaidia akina mama wengi zaidi kuweza kutambua haki zao na kuweza kuzifuatilia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilielezea pia matukio mengi ambayo yamekuwa yanaongezeka na masuala ya ubakaji wa watoto ambayo kwa sasa hivi karibu kila leo kwenye vyombo vya habari matukio yanaongezeka badala ya kupungua. Kwa hiyo, ninapenda kujua kwamba Wizara au Serikali kwa ujumla inachukua hatua gani za dhati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu inayotolewa kwa wanaume ambao wanawabaka watoto ni ndogo kiasi kwamba, badala ya kupunguza matatizo; matatizo yanaongezeka. Mimi ninapenda Serikali itamke kwamba, wanaume wote wanaowabaka watoto wahasiwe ili tihakikishe kwamba, tatizo hili linaondoka kwa ajili ya kutetea haki za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe ufafanuzi wa maswali au hoja alizozitoa Mheshimiwa Sakaya.

Kwanza, kuhusu mchango gani tunaowapa *NGOs* zinazojishughulisha na watoto. Mimi ninataka kusema kwamba, *NGOs* ni Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali na kwa misingi hiyo, yana utaratibu wake wa kupata fedha. Sisi tunachotoa ni ushirikiano. Tunawahitaji sana kama nilivyosema kwenye bajeti yetu. Tunaweka sasa hivi utaratibu wa kupata taarifa zao ili tushirikiane kwa karibu kwa sababu tunahitaji sana kushirikiana nao.

Kwa hiyo, nataka kusema kwamba, sisi hatutoi mchango wowote kwenye *NGO* ila mchango tunaotoa ni kuwashirikisha katika mipango yetu na katika utengenezaji wa Sera ili waweze kutupa mawazo zaidi.

Nilipofafanua hapa sasa hivi nilipokuwa nikijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge nilisema kwamba, tuna hii Kampeni ya Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto siyo maneno tu. Nilisema mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, nafurahi kutangaza kwamba, juzi tulikuwa na Mheshimiwa IGP Said Mwema hapa hapa Dodoma, tukafanya kikao na maafisa wa ngazi ya juu wa Jeshi la Polisi ili tuunde Kamati ya pamoja, kwa sababu tumeona sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, suala la ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto hatuliwezi peke yetu. Kwa hiyo, wao wamekubali sasa hivi tutaunda Kamati ndogo ambayo itawahusisha pia wadau wengine na wadau ambao tunategemea kuwahusisha ni hawa hawa *NGOs* ambao tumeshaona kwamba, watatusaidia sana; watu kama TAWLA, TAMWA na Waandishi wa Habari wa Kiume pia kwa kupitia umoja wao watakavyotushauri. Tumeona kwamba, tukiwa na Waandishi wa Habari, *NGOs* na Jeshi la Polisi, tunaweza kusaidia kukabiliana na hili suala na TAWLA kwa mfano, wale wenye utaalumu wa Sheria, tunawahitaji sana.

Tumesema kwamba, mwanamke au mwanaume anaweza kufanyiwa ukatili mbaya sana kijijini akabaki hajui mahali pa kwenda kupata ushauri wa kisheria. Kwa hiyo, tunadhani tutakavyokubaliana, ninavyoamini mimi kwenye kikao chetu, tutaona pia maeneo ambayo TAWLA hawana matawi labda tusaidiane nao tupate matawi maeneo

yale ili watu waweze kupata ushauri wa kisheria. Mimi nashukuru sana kama nilivyosema, *HANS Foundation* wameshakubali kufanya kazi na sisi.

Ninaamini kabisa tumeshaongea na *EU*, yaani Umoja wa Nchi za Ulaya, nao wameonyesha kutaka kutusaidia na wametuletea kabisa barua ya kutuhakikishia wapo tayari kufanya kazi na sisi kwa utaratibu ambao tutauweka. Kwa hiyo, mimi naamini yote hayo; tukichanganya huu ukatili dhidi ya wanawake na watoto, pamoja na hayo masuala ya kubakwa tutayaibua, kwa sababu kitu kikubwa ni kuyaibua watu waone aibu, wachukuliwe hatua na ninaamini tutafika mbali.

Hili suala sasa la kuhasi sijui kama Mheshimiwa Chikawe ameshawasilisha bajeti yake, nadhani hili suala ndiyo linamfaa sana. Kama anaweza kupitisha Sheria ya namna hiyo na sisi Wabunge si zinapita humu humu, kwa hiyo, tutalionga hilo suala. Waheshimiwa Wabunge ndiyo wengi sana, nadhani watatusaidia sana kwenye suala hili, lakini kwa leo tuliahirishe.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kupata ufafanuzi.

Kabla sijapata ufafanuzi, naomba nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa mambo mengi aliyoyatolea ufafanuzi. Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, katika mchango wangu wa maandishi na wa kuzungumza hapa Bungeni, nimezungumzia kwa huzuni kabisa jinsi tatizo la usafiri linavyokera Vyuo vya Maendeleo vya Wananchi Singida. Nikaeleza baada yakutambua Wizara hii haina pesa, sikutaka ku-*complicate* tatizo; nikasema kwa sababu tuna shida tulateeni hata magari yale yanayopigwa mnada kwa shilingi milioni nne hizo hizo sisi yatatufaa kwa sababu pale mjini wana gari la mwaka 1986. Chuo cha Msingi, Mkuu wake wa Chuo ana pikipiki anapanda mlima wa Msingi wenye kuzingirwa na msitu wa hifadhi. Ndugu zangu, naomba mvihurumie hivi vyuo viwili, tunataka *reconditions* zinazouzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe ufafanuzi uliohitajika na Mheshimiwa Diana Chilolo kama ifuatavyo:-

Tuna vyuo 53 mpaka sasa hivi, yaani vya maendeleo ya wananchi na kati hivyo; vyuo 29 tu ndiyo vina magari tena magari yenyewe ni ya zamani. Kwa hiyo, yeye mwenyewe ni shahidi; siku ya leo katika kuchangia Waheshimiwa Wabunge wengi wameonyesha kwamba, bajeti yetu ni finyu. Ninachomwomba ni kwamba, atuvumilie mara tutakapopata uwezo tutamsaidia. Pia ni kweli Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinahitaji magari na mama anayeendesha pikipiki, namwomba tu aendelee wakati Serikali inatafuta fedha.



**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilikuwa nimeuliza swali ambalo nilikuwa naomba nipate ufafanuzi. Kuna hii Tume Maalumu ambayo imeundwa kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati wa kuhusu *fifty fifty* ya Wanawake. Sasa nilikuwa naomba nipate hadidu za rejea za kikao cha hiyo Tume halafu pia nipatiwe au niambiwe Wajumbe ni akina nani na watashikishaje wadau katika hilo?

Lingine, nakushukuru sana kwa kunijibu kuhusu Rugemba, hasa Mheshimiwa Halima Mdee alivyoliuliza. Ninashangaa mimi siyo fundi, lakini *solar* ninavyoijua Mufindi kuna baridi kali sana; sasa *solar* itakuwaje? Halafu kuna *computer* ambazo tulizipitia kwenye vikao vya maendeleo ya jamii tukaona kwamba, *computer* nyingi zinanunuliwa. Ningeomba pia unihakikishie kwamba, angalau *computer* moja watapata huko Lungemba.

**MWENYEKITI:** Sasa ni *solar* au nini? Naomba ujibu la *solar*.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *solar* mimi nadhani ni kheri kuwa na nusu shari kuliko kuwa na shari kamili. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri tuanze na *solar* halafu baadaye uwezo utakapopatikana wa umeme wa gridi, basi tuendelee nao. Kwa kuanzia, naomba tuanzie na *solar*. Kuhusu *computer*, watapata zipo kwenye bajeti yetu ambayo tayari imeshaandaliwa katika bajeti ya mwaka huu.

**MWENYEKITI:** Huyu anazungumzia Rugemba lakini sasa kulikuwa na Waziri wa Nishati hapa alitaka kusimama.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru akinisaidia.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI :** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninataka kuongezea kwenye majibu ya nyongeza ya Mheshimiwa Waziri juu ya suala ambalo limeulizwa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu umeme kwenye Chuo cha Rugemba. Naomba kuahidi tu kwamba, tunashirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto hapa, pamoja na Wananchi wa Rugemba na Wananchi kwa ujumla, kuona kwamba ni jinsi gani huduma ya umeme itawafikia. Ninaahidi kwamba, tunalifanyia kazi kwa pamoja. (*Makofi*)

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia suala la Benki ya Wanawake na baada ya ufafanuzi uliotolewa na Waziri wa Fedha, ninaona Benki hii kuanzishwa kuna tatizo kubwa.

Ninapenda kujua, tulihamasishwa na tukatoa pesa kwa ajili uanzishwaji wa Benki hiyo; je, fedha zetu ziko wapi na zinafanya nini; na je, tutapata gawio kutokana na fedha hizo?

**MWENYEKITI:** Mimi nilivyoelewa, Waziri wa Fedha, alikuwa anasema tu utaratibu lakini najua Benki ile imekwenda mbali zaidi ya hapo, hata hao wanaosema wapo. Hebu sema Waziri wa Maendeleo ya Jamii.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kuhusu fedha zilizochangwa na Waheshimiwa Wabunge, nawahakikishia kupitia Bunge hili Tukufu kwamba, sisi tuna zaidi ya shilingi milioni 876 ambazo zipo *Escrow Bank*, ambazo zimeshaka tayari kusubiri hizo shilingi bilioni 2.1 tuanze kutangaza hisa zinunuliwe zaidi. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi fedha zipo.

**MWENYEKITI:** Alichotaka kusema, yaani maelezo aliyotoa Waziri wale wahamasishaji wapo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wahamasishaji wapo.

Sisi tuna Kamati ambayo Mwenyekiti ni Mheshimiwa Simba na Wajumbe wengine ambao ni akina Mama Lupembe, ambao wameboba kwenye masuala ya Benki, wanafanya kazi kubwa sana. Vilevile tuna mtaalamu ambaye tumempata anatusaidia, uanzishwaji wa Benki kwa kweli tumefikia hatua ya mbali sana.

Mimi namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na imani kwamba, hii Benki itaanzishwa. Oodha ya Wabunge wote waliochangia ninayo, kiasi walichochangia, tarehe waliyochangia na tuna mtaalamu aliyeshughulikia yupo hapa, kama kuna tatizo lolote tunaomba tuonane nao, tuna orodha kamili hii hapa.

**MWENYEKITI:** Ninachosema ni kwamba, wasiwasi aliutoa Mheshimiwa Waziri wa Fedha; hii Benki maandalizi yake yamekuwa *advanced*, yote aliyosema mmeyafanya?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yote yaliyotakiwa na benki yamefanyika, kinachosubiriwa ni hiyo shilingi bilioni 2.1 tu. Tumefikia hatu nzuri jengo limeshapatikana, leseni ya kuendeshea imeshapatikana, *Tin Number* tumeshaipata na kweli tumefikia hatua ya mbali sana katika uanzishwaji wa benki na hata hayo ya kusema watakaonunua tumefikia hatua ya mbali sana.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi ninaomba maswali mawili Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Moja tu linatosha.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kanuni inaniruhusu?

**MWENYEKITI:** Naomba unisikilize; uliza moja tu kwa sababu ya *time*, nina-*manage* kikao.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa nitasema hili moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikizungumzia Chuo cha Maendeleo ya Jamii ya Msingi. Chuo hiki ni cha muda mrefu na ni miongoni mwa vyuo viwili ambavyo vipo Mkoani Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo moja ambalo limenisimamisha mpaka kutaka Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi ni juu ya ahadi iliyotolewa mwaka 2005 ndani ya Bunge hili Tukufu, juu ya chuo kile kupatiwa umeme, siyo wa *solar* bali ni umeme wa gridi kabisa kutoka pale Kinampanda ili uje pale chuoni. Sasa ni miaka minne; sijui Mheshimiwa Waziri ataniambia nini ili wale watu wa Msingi wapate umeme?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza, napenda kumpa pole Mheshimiwa Killimbah kama kweli tangu mwaka ule aliahidiwa hajapata. Mimi naomba aendelee kuvuta subira tu na kwa kuwa tayari amenikumbusha, naomba nilichukue nikalifanyie kazi. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1002 - <i>Finance And Accounts..</i> ... ..	Sh. 323,042,180
Kif.1003 - <i>Policy and Planning..</i> ... ..	Sh. 361,027,040
Kif.2001 - <i>Training and Folk Dev. Colleges...</i> ... ..	Sh. 2,930,400,622
Kif.2002 - <i>Community Development...</i> ... ..	Sh. 1,382,421,850
Kif.2003 - <i>Community Development College – Tengeru</i> ... ..	Sh. 0
Kif.3001 - <i>Gender Development</i> ... ..	Sh. 551,015,985
Kif.3002 - <i>Children Development...</i> ... ..	Sh.397,439,300
Kif.4001 - <i>NGOs Coordination...</i> ... ..	Sh. 256,660,020

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> ... ..	Sh. 1,200,800,000
--	-------------------

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho nikisome labda ni hiyo *Sub-vote* 1001 - *Public Buildings*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwa sababu nikiangalia ile *Sub-vote* 2002, kuna kifungu kidogo cha 6229 ambacho pia kinahusu *Public Buildings*. Kwa hiyo, naomba kujua ni nini; yaani hiyo *Public Building* maana yake ni nini; ni Makao Makuu ya Wizara au ni pamoja na vyuo; na kwa nini ina-appear katika sehemu mbili na kwa amount tofauti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umeipata; kuna shilingi 1,200,800,000 ni kwa ajili ya nini?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Zile za kwanza shilingi bilioni 1.2 ni kwa ajili ya kumaliza Jengo la Makao Makuu pale Wizarani na hizi za pili alizokuwa anazitungumzia ni za ukarabati wa vyuo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning*... .. Sh. 1,151,040,000  
Kif. 2001 - *Training and Folk Dev. Colleges*... .. Sh. 2,455,777,000  
Kif. 2002 - *Community Development* ... .. Sh. 758,830,000  
Kif. 2003 - *Community Development College – Tengeru*... .. Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Gender Development* ... .. Sh. 426,965,000

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba tu kujua katika kifungu kidogo cha 6259 *kinachohusu Advocacy and Gender Development Program*. Nilivyokuwa najua, siku za nyuma katika Wizara hii kulikuwa na kitengo ambacho kilikuwa kinasaidia sana Wanawake katika kusoma, yaani kilikuwa kinawapa *scholarship and sponsorship*. Ninaomba kujua kama kifungu hiki ndicho kinachohusika na kama sasa hivi bado kitengo kile kipo na kinasomesha Wanawake?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu kilichokuwa kikitumika kufundisha au kutoa mafunzo kwa ajili ya Wanawake, kilikuwa ni cha Mradi na ulikwisha. Sasa hivi ndiyo tunaanza kuhangaika kutafuta ni nani anaweza kutusaidia kukirudisha. Kwa kweli kilikuwa ni kifungu kilichosaidia akina mama wengi kusoma. Kifungu hiki tunachozungumzia sasa hivi ni cha *Gender Budgeting*, kama tulivyokuwa tunasema, tunajaribu kama nilivyozungumza, tutawaita Wakurugenzi wa Halmashauri na wengine wengi tu ambao tunaona watatusaidia kuhusu *Gender Budgeting* niliyokuwa

naizungumza hapa. Kwa sababu kama wale wanaopanga fedha kwenye bajeti hawakuchukulia maanani suala la kuangalia uwezeshaji wa Wanawake ndani ya bajeti zao haisaidii. Kwa hiyo, hii ina lengo maalum la kusaidia suala la *Gender Budgeting*.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hii haihusiani na yale aliyoyasema?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haihusiani na *training* ya Wanawake.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 - *Children Development* ... .. Sh. 828,245,000

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hizi fedha zinaombwa au tunapata msaada?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, hapa tunasema kifungu gani na *item* gani siyo jumla?

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *Vote 3002, sub-items* zote kwa sababu ...

**MWENYEKITI:** Hapana!

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, twende *sub-vote 5415*.

**MWENYEKITI:** Sasa hii inaitwa *Child Protection and Participation*.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenyewe kama Serikali, hatuchangii chochote kwa hifadhi ya vijana wetu, naona kila kitu ni msaada kutoka nje; kwa nini?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Huu ni mpango ambao tunashirikiana na *UNICEF*, lakini hata na sisi wenyewe tukiangalia kwenye vifungu hapa hasa kule tulikotoka, kuna kifungu ambacho tumeweka cha kusaidia uundwaji wa Mabaraza ya Watoto. Kwa hiyo na sisi tunachangia pia kwenye Wilaya 20 kuanzia mwaka huu wa fedha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *NGOs Coordination*... .. Sh. 23,820,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa mwaka 2008/2009, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuna dakika zetu chache, napenda kusema kwamba, kesho tunaingia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, tunao mchango wa siku mbili; kwa hiyo, wanaotaka kujiandaa wajiandae kama kawaida yetu tuna tatizo la *time*. Nawashukuru sana, kwa kazi nzuri mliyoifanya siku ya leo na ninawashukuru sana kwa michango ambayo imeonyesha kabisa kwamba, watu wameanza kuielewa Wizara hii. Nadhani tuendeleo hivyo hivyo kwa sababu ni Wizara ambayo inatuhusu sisi sote; siyo ya wanawake na wala siyo ya watoto peke yao, bali ni ya watu wote.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa uelewa huo, niwatakie jioni njema na mapumziko mazuri mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge lilihirishwa mpaka Siku ya Jumatano,  
Tarehe 06 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*